# Kiswahili

## kwa

## Shule za Rwanda

## Mchepuo wa Lugha

## Kidato cha 6

## Mwongozo wa Mwalimu


**Sylvain Ntawiyanga**
**Jacqueline M. Kinya**
**Ali Muhamud**
**Sanja Leonard**



LONGHORN
PUBLISHERSLIMITED
expanding minds

Kimechapishwa na:

Longhorn Publishers (Rwanda) Ltd.,
Remera mkabala na Benki ya COGE
S.L.P 5910
Kigali, Rwanda.

Longhorn Publishers (Kenya) Ltd.,
Barabara ya Funzi, Eneo la Viwandani
S.L.P. 18033–00500
Nairobi, Kenya

Longhorn Publishers (Uganda) Ltd.,
Ploti 4, Eneo la Vubyabirenge, Ntinda,
S.L.P 24745
Kampala, Uganda.

Longhorn Publishers (Tanzania) Ltd.
Barabara Mpya ya Bagamoyo/Garden,
Mikocheni B, Ploti Namba: MKC/MCB/81
S.L.P 1237, Dar es Salaam, Tanzania

© S. Ntawiyanga, J. M. Kinya, A. Muhamud, S. Leonard 2017

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupigisha chapa, kutafsiri au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote ile bila idhini, kwa maandishi ya Longhorn Publishers Ltd.

Chapa ya kwanza 2017

**ISBN 978 9997 77 133 9**

Kimepigwa chapa na Ramco Printing Works Ltd,
Unit 2, Ramco Industrial Complex,
Barabara ya Mombasa, Eneo la Viwandani,
S. L. P. 27750 - 00506, Nairobi.

# Yaliyomo

Ramani ya yaliyomo........................................................................................xiii
Utangulizi ........................................................................................................ xviii
Ratiba ya mafunzo ........................................................................................ xxiii
Andalio la somo ............................................................................................. xxv

**SURA YA KWANZA ............................................................ 1**

**Mada Kuu 1:** Fasihi katika Kiswahili ................................................................ 1

**Mada Ndogo:** Ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili........... 1

**Somo la 1: Fasihi andishi..................................................................5**

**Vipindi 1-2: Kusoma ufahamu ..........................................................5**

1.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu tanzu za fasihi andishi.................. 6

**Vipindi 3-4: Kujifunza msamiati .......................................................7**

1.2 Kujifunza msamiati kuhusu tanzu za fasihi andishi ........................................ 8

**Vipindi 5-6: Matumizi ya lugha........................................................9**

1.3 Majadiliano kuhusu umuhimu wa fasihi andishi........................................... 10

**Vipindi vya 7-8: Kusikiliza na kuzungumza ...................................11**

1.4 Majadiliano ..................................................................................................... 12

**Vipindi vya 9-10: Sarufi (Sentensi ya Kiswahili)..............................12**

1.5 Maana ya sentensi ........................................................................................... 13

1.6 Sehemu kuu za sentensi .................................................................................. 14

1.7 Mazoezi ya ziada.............................................................................................. 17

1.8 Majibu.............................................................................................................. 18

**Somo la 2: Utanzu wa hadithi fupi................................25**

**Vipindi 11-13: Kusoma ufahamu ..................................................25**

2.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira ......... 26

**Vipindi 14 -15: Kujifunza msamiati.................................................27**

2.2 Kujifunza msamiati wa hadithi kuhusu uhifadhi wa mazingira ......................28

**Vipindi 16-18: Matumizi ya lugha...................................................29**

2.3 Majadiliano kuhusu uhifadhi wa mazingira ..............................................30

**Vipindi vya 19-21: Kusikiliza na kuzungumza..................................30**

2.4 Majadiliano kuhusu sifa bainifu za hadithi fupi ........................................ 31

**Vipindi vya 22-25: Sarufi (Virai) ......................................................33**

2.5 Maana ya kirai ................................................................................ 34

2.6 Mazoezi ya ziada .............................................................................. 37

2.7 Majibu ............................................................................................. 38

**Somo la 3: Utanzu wa riwaya ........................................................43**

**Vipindi vya 26-28: Kusoma ufahamu ..............................................43**

3.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Sura moja ya riwaya kuhusu uchaguzi wa viongozi ................................................................ 44

**Vipindi vya 29-30: Kujifunza msamiati ..........................................45**

3.2 Kujifunza msamiati kutokana na sura moja ya riwaya husika............... 46

**Vipindi vya 31-33: Matumizi ya lugha ..........................................47**

3.3 Majadiliano kuhusu sifa bainifu za riwaya.............................................. 48

**Vipindi vya 34-36: Kusikiliza na kuzungumza.................................50**

3.4 Majadiliano kuhusu maudhui .................................................................. 51

**Vipindi vya 37-40: Sarufi (Kirai kivumishi) ....................................52**

3.5 Kirai kivumishi ................................................................................... 53

3.6 Mazoezi ya ziada ............................................................................... 56

3.7 Majibu ............................................................................................... 57

**Somo la 4: Utanzu wa tamthilia ...................................................62**

**Vipindi 41-43: Kusoma ufahamu...................................................62**

4.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Sura moja ya tamthilia ..................................... 64

**Vipindi 44-45: Kujifunza msamiati ................................................64**

4.2 Kujifunza msamiati kutokana na sura ya tamthilia husika...................... 66

**Vipindi 46-48: Matumizi ya lugha...................................................67**

4.3 Majadiliano kuhusu sifa bainifu za utanzu wa tamthilia......................... 67

**Vipindi vya 49-51: Kusikiliza na kuzungumza.................................69**

4.4 Maigizo ya sura ya tamthilia ................................................................ 70

**Vipindi 52-55: Sarufi (Kirai kitenzi) ...............................................71**

4.5 Kirai kitenzi ........ 72

4.6 Mazoezi ya ziada ........ 74

4.7 Majibu ........ 76

**Somo la 5: Utanzu wa ushairi ........ 82**

**Vipindi 56-57: Kusoma shairi ........ 82**

5.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Shairi kuhusu kuyalinda mazingira ........ 83

**Vipindi 58-59: Kujifunza msamiati ........ 84**

5.2 Kujifunza msamiati wa shairi kuhusu kuyalinda mazingira ........ 85

**Vipindi 60-61: Matumizi ya lugha ........ 86**

5.3 Majadiliano kuhusu sifa bainifu za utanzu wa ushairi ........ 87

**Vipindi vya 62-63: Kusikiliza na kuzungumza ........ 88**

5.4 Kukariri shairi ........ 89

**Vipindi vya 64-65: Sarufi (Vishazi) ........ 90**

5.5 Maana ya kishazi ........ 91

5.6 Mazoezi ya ziada ........ 94

5.7 Majibu ........ 95

**SURA YA PILI ........ 105**

**Mada Kuu 2:** Fasihi katika Kiswahili ........ 105

**Mada Ndogo:** Uhakiki wa tanzu za fasihi andishi ........ 105

**Somo la 6: Uhakiki wa fasihi ........ 109**

**Vipindi 1-2: Kusoma ufahamu ........ 109**

6.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Kifungu kuhusu fasihi katika Kiswahili ........ 111

**Vipindi 3-4: Kujifunza msamiati ........ 112**

6.2 Kujifunza msamiati kuhusu fasihi katika Kiswahili ........ 113

**Vipindi 5-6: Matumizi ya lugha ........ 114**

6.3 Matumizi ya lugha: Maudhui na fani katika fasihi ........ 115

**Vipindi vya 7-8: Kusikiliza na kuzungumza ........ 116**

6.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano ........ 117

**Vipindi 9-10: Sarufi (Maana ya kitenzi) ........................................ 118**

6.5 Maana ya kitenzi ........................................................................ 120

6.6 Mazoezi ya ziada ........................................................................ 123

6.7 Majibu ........................................................................................ 124

**Somo la 7: Wahusika katika fasihi andishi .................. 129**

**Vipindi 11-13: Kusoma ufahamu................................................ 129**

7.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Hadithi fupi kuhusu suala la urithi .............. 130

**Vipindi 14 -15: Kujifunza msamiati............................................. 131**

7.2 Kujifunza msamiati wa hadithi kuhusu suala la urithi .......................... 132

**Vipindi 16-18: Matumizi ya lugha................................................ 133**

7.3 Majadiliano kuhusu aina mbalimbali za wahusika................................ 134

**Vipindi vya 19-21: Kusikiliza na kuzungumza............................... 136**

7.4 Majadiliano kuhusu tabia na sifa za wahusika...................................... 137

**Vipindi vya 22-25: Sarufi (Kauli ya kufanyiwa na kufanyika) ........ 139**

7.5 Kauli ya kufanyiwa/kutendewa .............................................................. 140

7.6 Mazoezi ya ziada ................................................................................ 144

7.7 Majibu ................................................................................................ 145

**Somo la 8: Maudhui na dhamira katika fasihi andishi .................. 152**

**Vipindi 26-27: Kusoma shairi...................................................... 152**

8.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Shairi kuhusu ukulima .................................. 153

**Vipindi vya 28-29: Kujifunza msamiati ......................................... 154**

8.2 Kujifunza msamiati wa shairi kuhusu ukulima ..................................... 155

**Vipindi 30-31: Matumizi ya lugha................................................ 156**

8.3 Majadiliano kuhusu maudhui na dhamira ya shairi............................. 157

**Vipindi vya 32-33: Kusikiliza na kuzungumza............................... 158**

8.4 Majadiliano.......................................................................................... 159

**Vipindi vya 34-35: Sarufi (Kauli ya kufanyisha/kutendesha)......... 160**

8.5 Kauli ya kufanyisha/kutendesha............................................................ 162

8.6 Mazoezi ya ziada ................................................................................ 165

8.7 Majibu ................................................................................................ 166

**Somo la 9: Mandhari katika fasihi andishi .................................. 170**

**Vipindi 36-38: Kusoma ufahamu.................................................. 170**

9.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Sura moja ya tamthilia yenye mandhari mbalimbali ..................................................... 172

**Vipindi vya 39-40: Kujifunza msamiati ........................................ 173**

9.2 Kujifunza msamiati kutokana na maonyesho ya tamthilia husika...... 174

**Vipindi 41-43: Matumizi ya lugha................................................. 175**

9.3 Majadiliano kuhusu mandhari ................................................. 176

**Vipindi vya 44-46: Kusikiliza na kuzungumza............................... 177**

9.4 Majadiliano.......................................................................... 178

**Vipindi 47-50: Sarufi (Kauli ya kufanywa/kutendwa) .................. 179**

9.5 Kauli ya kufanywa/kutendwa ................................................. 180

9.6 Mazoezi ya ziada ................................................................. 183

9.7 Majibu ................................................................................. 184

**Somo la 10: Uhakiki wa mbinu za lugha katika fasihi andishi....... 188**

**Vipindi vya 51-53: Kusoma ufahamu ........................................... 188**

10.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Sura ya riwaya yenye mbinu za lugha....... 189

**Vipindi vya 54-55: Kujifunza msamiati ........................................ 190**

10.2 Kujifunza msamiati kutokana na sura ya riwaya husika ................... 191

**Vipindi vya 56-58: Matumizi ya lugha ........................................ 192**

10.3 Majadiliano kuhusu mbinu za lugha ...................................... 193

**Vipindi vya 59-61: Kusikiliza na kuzungumza............................... 196**

10.4 Majadiliano kuhusu mbinu za lugha ..................................... 197

**Vipindi vya 62-65: Sarufi (Kauli ya kufanyua/kutendua)............. 198**

10.5 Kauli ya kufanyua/kutendua ................................................ 199

10.6 Mazoezi ya ziada ................................................................ 202

10.7 Majibu ................................................................................ 203

**SURA YA TATU ..................................................... 212**

**Mada Kuu 3:** Ubunaji ..................................................... 212

**Mada Ndogo:** Hotuba na Ufupisho ..................................................... 212

**Somo la 11: Sehemu kuu za hotuba ..................................................... 216**

**Vipindi 1-3: Kusoma ufahamu ..................................................... 216**

11.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Hotuba kuhusu usafi ..................................................... 218

**Vipindi cha 4-5: Kujifunza msamiati ..................................................... 219**

11.2 Ujifunzaji wa msamiati wa hotuba kuhusu usafi ..................................................... 220

**Vipindi 6-8: Matumizi ya lugha ..................................................... 221**

11.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano ..................................................... 222

**Vipindi vya 9-10: Kusikiliza na kuzungumza ..................................................... 223**

11.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga hotuba ..................................................... 224

**Vipindi 10-11: Sarufi (Uambishaji wa vitenzi) ..................................................... 225**

11.5 Uambishaji wa vitenzi ..................................................... 226

11.6 Mazoezi ya ziada ..................................................... 230

11.7 Majibu ..................................................... 231

**Somo la 12: Sifa za hotuba ..................................................... 236**

**Vipindi 13-15: Kusoma ufahamu ..................................................... 236**

12.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Hotuba kuhusu ushirikiano wa kijinsia ..................................................... 237

**Vipindi 16-17: Kujifunza msamiati ..................................................... 238**

12.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na hotuba ya ushirikiano ..................................................... 239

**Vipindi 18-20: Matumizi ya lugha ..................................................... 239**

12.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu sifa za hotuba ..................................................... 240

**Vipindi vya 21-22: Kusikiliza na kuzungumza ..................................................... 241**

12.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano ..................................................... 242

**Vipindi 23-25: Sarufi (Uambishaji wa vitenzi) ..................................................... 243**

12.5 Viambishi awali na viambishi tamati ..................................................... 244

12.6 Mazoezi ya ziada ..................................................... 246

12.7 Majibu ..................................................... 249

**Somo la 13: Hotuba na insha ....... 255**

**Vipindi 26-28: Kusoma ufahamu ....... 255**

13.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Hotuba kuhusu kupigana na umaskini ....... 256

**Vipindi 29-30: Kujifunza msamiati ....... 257**

13.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na hotuba husika ....... 258

**Vipindi 31-33: Matumizi ya lugha ....... 258**

13.3 Matumizi ya lugha: Tofauti kati ya hotuba na insha ....... 259

**Vipindi 34-35: Kusikiliza na kuzungumza ....... 261**

13.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga hotuba ....... 262

**Vipindi 36-37: Sarufi (Viambishi tamati) ....... 263**

13.5 Sarufi: Viambishi tamati ....... 264

13.6 Mazoezi ya ziada ....... 266

13.7 Majibu ....... 267

**Somo la 14: Ufupisho ....... 275**

**Vipindi 38-40: Kusoma ufahamu ....... 275**

14.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Hotuba kuhusu umuhimu wa maadili ....... 276

**Vipindi 41-42: Kujifunza msamiati ....... 277**

14.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na hotuba ya umuhimu wa maadili ....... 278

**Vipindi 43-45: Matumizi ya lugha ....... 279**

14.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu sifa za ufupisho ....... 280

**Vipindi 46-47: Kusikiliza na kuzungumza ....... 281**

14.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kufupisha hotuba ....... 282

**Vipindi 48-50: Sarufi (Uundaji wa nomino kutokana na vitenzi) ....... 283**

14.5 Uundaji wa nomino kutokana na vitenzi ....... 284

14.6 Mazoezi ya ziada ....... 287

14.7 Majibu ....... 288

**Somo la 15: Mwongozo wa kuandika ufupisho............................292**

**Vipindi 51-53: Kusoma ufahamu.................................................292**

15.1 Kusoma na kufahamu: Hotuba kuhusu manufaa ya elimu ................293

**Vipindi 54-55: Kujifunza msamiati ..............................................294**

15.2 Ujifunzaji wa msamiati wa hotuba kuhusu manufaa ya elimu ...........294

**Vipindi 56-58: Matumizi ya lugha...............................................295**

15.3 ***Matumizi ya lugha:*** Majadiliano kuhusu mwongozo wa kuandika ufupisho ....................................................................................296

**Vipindi 59-60: Kusikiliza na kuzungumza ....................................297**

15.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kufupisha hotuba ...................................298

**Vipindi 61-62: Sarufi (Uundaji wa vitenzi jina).............................299**

15.5 Uundaji wa vitenzi jina ...............................................................300

15.6 Mazoezi ya ziada .........................................................................302

15.7 Majibu .......................................................................................303

**SURA YA NNE .........................................................308**

**Mada Kuu 4:** Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo ..................308

**Mada Ndogo:** Midahalo na mijadala...........................................................308

**Somo la 16: Sifa za mdahalo.........................................................314**

**Vipindi 1-3: Kusoma ufahamu .....................................................314**

16.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mdahalo kuhusu athari za mavazi ya kisasa .......................................................316

**Vipindi 4-6: Kujifunza msamiati ..................................................317**

16.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na mdahalo husika .......................317

**Vipindi 7-9: Matumizi ya lugha....................................318**

16.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za mdahalo .......................................319

**Vipindi 10-12: Kusikiliza na kuzungumza ....................................320**

16.4 Kusikiliza na kuzungumza: Mdahalo ..................................................321

**Vipindi 13-16: Sarufi (Maana ya nomino)......................322**

16.5 Uundaji wa nomino....................................................................323

16.6 Mazoezi ya ziada ........ 326
16.7 Majibu ........ 327
**Somo la 17: Mwongozo wa kuandika mdahalo........ 331**
**Vipindi 17-19: Kusoma ufahamu........ 331**
17.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mdahalo kuhusu athari za rushwa........ 333
**Vipindi 20-22: Kujifunza msamiati ........ 333**
17.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na mdahalo husika ........ 334
**Vipindi 23-25: Matumizi ya lugha........ 335**
17.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano ........ 336
**Vipindi 26-28: Kusikiliza na kuzungumza ........ 337**
17.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga mdahalo........ 338
**Vipindi 29-32: Sarufi (Maana ya kivumishi) ........ 339**
17.5 Maana ya kivumishi pamoja na uundaji wake........ 340
17.6 Mazoezi ya ziada ........ 342
17.7 Majibu ........ 343
**Somo la 18: Mjadala........ 348**
**Vipindi 33-35: Kusoma ufahamu ........ 348**
18.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo ........ 349
**Vipindi 36-38: Kujifunza msamiati ........ 350**
18.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na mjadala husika ........ 351
**Vipindi 39-41: Matumizi ya lugha........ 351**
18.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za mjadala ........ 352
**Vipindi 42-44: Kusikiliza na kuzungumza ........ 353**
18.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo ........ 354
**Vipindi 45-47: Sarufi (Uundaji wa vitenzi) ........ 355**
18.5 Maana ya kitenzi pamoja na uundaji wake........ 356
18.6 Mazoezi la ziada ........ 360
18.7 Majibu ........ 361
**Vipindi 48-50: Kusoma ufahamu ........ 365**
19.1 ***Kusoma na kufahamu:*** Mjadala kuhusu ugonjwa wa Ukimwi ........ 366

**Vipindi 51-53: Kujifunza msamiati ................................................ 367**

19.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na mjadala husika ......................... 368

**Vipindi 54-56: Matumizi ya lugha................................................. 369**

19.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano ............................................................ 370

**Vipindi 57-59: Kusikiliza na kuzungumza ...................................... 371**

19.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga mjadala ..................................... 372

**Vipindi 60-62: Sarufi (Maana ya kiwakilishi) ................................. 373**

19.5 Sarufi: Maana ya kiwakilishi pamoja na uundaji wake....................... 374

19.6 Mazoezi ya ziada ........................................................................................ 376

19.7 Majibu ........................................................................................................ 377

Vitabu vya Rejea ......................................................................................... 383

## Ramani ya Yaliyomo

| | MADA 1: FASIHI KATIKA KISWAHILI | MADA 2: FASIHI KATIKA KISWAHILI | MADA 3: UBUNAJI | MADA 4: UKUZAJI WA MATUMIZI YA LUGHA KIMAANDISHI |
|---|---|---|---|---|
| **IDADI YA VIPINDI** | **65** | **65** | **62** | **62** |
| **UWEZO WA MSINGI UPATIKANAO KATIKA MADA** | Mwanafunzi aweze kuelewa tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani. | Mwanafunzi aweze kuelewa na kufuata mtindo wa kuchambua kazi za fasihi (vitabu, mashairi, nyimbo…) kwa minajili ya kukuza uelewa wa undani wa lugha na kutambua ujumbe unaojidhihirisha katika maendeleo ya fikira na utamaduni wa wananchi; kujua jinsi ya kunyambua kitenzi cha Kiswahili. | Mwanafunzi ataweza kuelewa mtindo wa hotuba na kuuzingatia katika mazoezi ya utungaji pamoja na ufupisho; kujua kuchambua kitenzi kwa njia ya uambishaji | Mwanafunzi aweze kuelewa mwongozo wa midahalo na mijadala na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa; kujua jinsi ya kuchambua maneno ya Kiswahili kwa kutumia njia ya uambishaji. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **IDADI YA MASOMO** | 5 | 5 | 5 | 5 |
| **VIFAA VYA KUJIFUNZIA** | - Vitabu<br>- Majarida<br>- Rekoda<br>- Vinasa sauti<br>- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati<br>- Mtandao wa intaneti<br>- Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wazito kuelewa | - Vitabu<br>- Majarida<br>- Rekoda<br>- Vinasa sauti<br>- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati<br>- Mtandao wa intaneti<br>- Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wazito kuelewa | - Vitabu<br>- Majarida<br>- Rekoda<br>- Vinasa sauti<br>- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati<br>- Mtandao wa intaneti<br>- Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wazito kuelewa | - Redio<br>- Runinga<br>- Taarifa zilizorekodiwa<br>- Vifaa vya kunasia sauti<br>- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati<br>- Mtandao wa intaneti |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MBINU ZA KUJIFUNZIA NA KAZI** | - Kuwapa wanafunzimaandishi tofauti (vitabu, habari zilizorekodiwa, majarida n.k.) yanayobeba ndani yake tanzu za fasihi andishi za Kiswahili na kuyaelezea.<br>- Kuigiza jukwani tamthilia itakayochaguliwa na mwalimu au wanafunzi wenyewe.<br>- Kulikariri shairi fulani na kulighani darasani.<br>- Kujadili athari za tamthilia za Kinyarwanda (k.m. Urunana) katika kuimarisha hatua za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa ukimwi (HIV/AIDS). | - Kuwapa wanafunzi (katika makundi) maandishi tofauti, vitabu, habari zilizorekodiwa, majarida n.k.) yanayobeba tanzu za fasihi andishi za Kiswahili na kutoa uchambuzi wake kwa kufuata mwongozo wa uchambuzi uliotolewa.<br>- Kujadili tamthilia mbalimbali wakisisitiza juu ya wahusika na tabia zao katika harakati za kuboresha umoja na maridhiano ya Wanyarwanda. | - Kutunga hotuba kutokana na mada tofautitofauti kama vile: umoja wa Wanyarwanda, unyanyasaji wa kijinsia, kazi za *Umuganda*, usafi wa mazingira, n.k.)<br>- Kuchagua hotuba tofauti zilizotungwa na watu wengine na kuzitolea ufupisho.<br>- Kutambua vitenzi mbalimbali vilivyotumiwa katika hotuba, insha na vifungu vya ufupisho na kuviambisha katika hali tofauti. | Kujadiliana mada kuhusu masuala ya jamii kama vile: rushwa, dawa za kulevya, unyanyasaji wa kijinsia, desturi ya kujitegemea, kazi za *Umuganda* katika maendeleo ya nchi, ndoa nchini Rwanda, malezi ya jana na ya leo na ugonjwa wa Ukimwi.<br>- Kusikiliza mijadala kwenye redio au kwenye runinga au vipindi vingine vya habari katika Kiswahili na kutoa ripoti kwa njia ya mazungumzo kufuatia pande mbili zilizohusika. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | - Kuchambua tungo mbalimbali kwa kuzitolea vifungu vyake. | - Kunyambua vitenzi tofauti katika kauli husika. | | - Kuchambua vifungu tofauti vya taarifa vyenye maneno yalioambishwa. |
| **UWEZO WA JUMLA** | - Stadi za utafiti<br>- Ubunifu na ugunduzi<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu<br>- Ushirikiano na stadi za maisha<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Tafakuri tanduizi | - Stadi za utafiti<br>- Ubunifu na ugunduzi<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu<br>- Ushirikiano na stadi za maisha<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Tafakuri tanduizi | - Usuluhishaji wa matatizo<br>- Tafakuri tanduizi<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu<br>- Utawala binafsi na stadi za maisha<br>- Ubunifu na ugunduzi | - Tafakuri tanduizi<br>- Ubunifu na ugunduzi<br>- Ujifunzaji wa muda mrefu<br>- Ushirikiano, utawala na stadi za maisha<br>- Mawasiliano katika lugha rasmi<br>- Stadi za utafiti |
| **MASUALA MTAMBUKA** | - Usawa wa kijinsia<br>- Elimu ya pamoja<br>- Mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa pamoja na mwendelezo wake | - Amani na maadili mema<br>- Elimu ya pamoja<br>- Usawa wa kijinsia | - Amani na maadili mema<br>- Usawa wa kijinsia | - Amani na maadili mema<br>- Mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | - Amani na maadili mema | - Mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake | - Mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake<br>- Elimu ya pamoja | - Elimu kuhusu fedha<br>- Usawa wa kijinsia<br>- Elimu ya pamoja |
| **VIGEZO VYA TATHMINI NA UPIMAJI WA UWEZO WA MSINGI UPATIKANAO KATIKA MADA** | - Uwezo wa kutofautisha aina mbalimbali za fasihi andishi kutokana na muundo wake.<br>- Ujasiri wa kujieleza kwa ufasaha mbele ya wanafunzi wengine.<br>- Ujuzi wa kuchambua tungo mbalimbali. | - Uwezo wa kuchambua tanzu za fasihi andishi kulingana na mwongozo wa uchambuzi aliojifunza.<br>- Uwezo wa kunyambua vitenzi katika kauli husika.<br>- Ujasiri wa kujieleza kwa ufasaha mbele ya wanafuzi wengine. | - Uwezo wa kutunga na kufupisha hotuba au tanzu nyingine za fasihi andishi ya Kiswahili.<br>- Ujuzi wa kutambua vitenzi katika hotuba na kuviambisha kwa namna mbalimbali. | - Uwezo wa kuzungumza, kusikiliza, kusoma na kufanya mawasiliano kwa njia ya maandishi kwa kujieleza.<br>- Uwezo wa kushiriki kwenye mdahalo au mjadala na kutoa hoja akimheshimu mpinzani wake. |

# UTANGULIZI

## Nafasi ya Kiswahili katika jamii na mfumo wa elimu

Lugha ya Kiswahili imepewa hadhi kubwa kwa kuteuliwa kuwa mojawapo katika lugha rasmi za Jumuiya ya Afrika. Nchini Kenya na katika nchi ya Tanzania, Kiswahili ni lugha ya taifa na pia lugha rasmi. Nchi za Uganda na Burundi nazo hazijaachwa nyuma kwani lugha ya Kiswahili imeanza kukita mizizi huko na kufunzwa kikamilifu. Nchini Rwanda, Kiswahili ni lugha rasmi.

Nchi nyingine kama Marekani, Ujerumani na mataifa mengi ya Ulaya yameanza kufunza lugha ya Kiswahili katika vyuo vikuu. Wanaelewa kuwa Kiswahili ndiyo lugha inayoweza kuunganisha nchi za ng'ambo na Afrika. Lugha hii huwafaa sana watalii wanaozuru Afrika.

Mipango imefanywa ili kuhakikisha kuwa lugha ya Kiswahili inawekwa katika programu za tarakilishi na kwenye mtandao duniani kote. Ni wazi kuwa Kiswahili kinapiga hatua kwa kasi sana ili kuweza kwenda na wakati.

**Kiswahili katika mfumo wa elimu nchini Rwanda**

Somo la Kiswahili limekuwa likifundishwa katika viwango vya elimu vya sekondari nchini Rwanda. Kwa sasa, somo hili linatathminiwa kitaifa kwa wanafunzi wanaosoma Kiingereza, Kiswahili na Kinyarwanda.

Lugha ya Kiswahili imepewa nguvu zaidi hasa tukizingatia kuwa wanafunzi wengi hulichukua somo hili katika sekondari na vyuo vikuu na kupata mafunzo katika fasihi na isimu na kufuzu katika somo hili. Tukitilia maanani mambo haya yote, tutaona kuwa wizara ya elimu imeipa lugha ya Kiswahili heshima inayostahili na kuhakikisha kuwa lugha hii inakuzwa.

**Mbinu za kufundisha mada mbalimbali**

**a) Ufahamu**

Ufahamu ni kipengele muhimu katika lugha ya Kiswahili. Ufahamu umebeba stadi zote zinazoweza kushughulikiwa kama vipengele tofauti tofauti.

Katika kufundisha hatua hii, mwalimu anaweza kuwachangamsha wanafunzi kwa kuwaagiza watazame michoro ya vitabuni na kutaja majina ya wanayoyaona. Pili, wanafunzi waeleze matukio mbalimbali katika michoro hiyo. Kwa mfano: *msichana akiketi chini ya mti, watu wakijadiliana, basi lililoanguka n.k.*

Kuwaruhusu wanafunzi kusoma kwa sauti huku wakipokezana kwa zamu ni muhimu. Mwalimu wa Kiswahili anashauriwa awe ameteua kifungu kabla ya kipindi kuwadia. Auchambue msamiati mpya na kuupigia mistari ama kuuandika kwenye daftari la kumbukumbu. Angalau kila mwanafunzi apate fursa ya kusoma sentensi kadhaa. Mwalimu ayakosoe makosa yoyote ya matamshi.

Wanafunzi wasome tena habari hiyo kwa kimya. Watafakari juu ya habari hiyo kisha wajibu maswali kwa kusema kisha kwa kuandika. Katika kiwango hiki cha wanafunzi, mwalimu azingatie na kusisitiza majibu ya sentensi nzima.
*Kwa mfano*:
Basi limefanya nini? Limeanguka. (ni kosa)
Basi limeanguka. (sahihi)

Mwalimu awaelekeze na kuwaongoza wanafunzi jinsi ya kutunga sentensi fupifupi wakitumia msamiati mpya baada ya kuyafafanua na kuelezea maana na matumizi ya maneno hayo.

Wanafunzi katika kiwango hiki wanapaswa kuwa wanajua kusoma kwa ufasaha. Wanaposoma, mwalimu anapaswa kuwa macho kwa sababu wanafunzi wengine huenda wakawa na mbinu mbaya ya usomaji. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi hawasogezi kitabu karibu sana na macho na pia hawatumii vidole kuelekeza macho.

Mwalimu anapaswa kusoma taarifa ambayo anawatarajia wanafunzi kusoma. Achambue maneno magumu ambayo yametumika na kuelewa maana. Awaambie wanafunzi wasome mmoja mmoja kwa sauti huku akisikiliza kwa makini ili kukosoa makosa yote ya matamshi. Ni bora zaidi mwalimu ayaandike maneno magumu ubaoni. Awaelekeze wanafunzi ili wapate maana ya maneno magumu kutokana na makala waliyoisoma.

**b) Msamiati**

Katika kufunza msamiati, ni jambo la busara endapo mwalimu atatumia vifaa halisi katika kueleza maana na matumizi ya msamiati. Endapo vifaa vingine ni vigumu kuvipata, basi mwalimu anaweza kutumia picha au aandae chati nzuri ili kulifanya funzo hili kueleweka kwa urahisi na pia kulifanya kuwa la kusisimua zaidi. Aidha, mwalimu anaweza kuunda au kubuni vifaa vya kufundisha. Kwa mfano: matumizi ya katoni kuunda mfano wa tarakilishi pale ambapo si rahisi kuipata tarakilishi na kuileta darasani ili kuizungumzia.

Mwalimu anaweza kufunza msamiati kwa njia ya ufahamu. Hapa itambidi mwalimu awaongoze wanafunzi kupata maana kutokana na habari yenyewe. Katika funzo la msamiati, ni bora mwalimu awaambie wanafunzi watunge sentensi wakitumia msamiati waliojifunza.

### ch) Kusikiliza na kuzungumza

Kusikiliza na kuzungumza ni kipengele muhimu sana katika kujifunza lugha yoyote ile. Ni wazi kuwa mtu ambaye hajapata kusikia neno lolote, yaani alizaliwa kiziwi, kamwe hawezi kuongea. Ataongea akisema nini? Binadamu yeyote alijifunza kuongea kupitia kwa kuwasikiliza watu wengine wakiongea na maneno ya kwanza aliyoyazungumza ni yale aliyoyasikia.

Ni sharti mwalimu akuze stadi hii muhimu ya kujifunza lugha. Wanafunzi wanaweza kujifunza funzo la kusikiliza na kuzungumza kwa kuigiza mchezo wa kuigiza. Kila mwanafunzi apewe sehemu yake ya kuigiza. Mwalimu ajitayarishe kwa kutunga (endapo ana uwezo) au kuteua mchezo wa kuigiza unaofaa kwa kuzingatia maudhui na kiwango cha wanafunzi. Somo hili huwajenga wanafunzi kuwa na uwezo wa kuongea mbele ya wengine kwa ufasaha bila matatizo yoyote.

Hali kadhalika, wanafunzi wanaweza kujadiliana na wenzao kuhusu mada tofauti tofauti. Wanaweza kuendeleza mijadala kwa kutoa hoja mbalimbali kuhusu mada watakayoteua.

Tathmini katika funzo hili huwa ni maswali ambayo humhitaji mwanafunzi kuyajibu kwa kuongea ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wamepata fursa ya kuongea na kuwasikiliza wengine wakiongea. Itakuwa bora endapo mwalimu ataandaa mara kwa mara vipindi kabambe vya michezo ya kuigiza, midahalo na masimulizi. Aidha, wanafunzi wapewe fursa ya kusikiliza vipindi vya redio na hata inapowezekana, kutazama runinga na kanda za video.

### d) Sarufi

Sarufi ni mpangilio maalum wa maneno kwa ufasaha kulingana na kanuni zake au kupanga na kutumia maneno vizuri kulingana na mipango au taratibu zilizokubaliwa kuwa ni sahihi. Sehemu muhimu katika sarufi ni ngeli. Mtu yeyote asiyejua na kuzitawala ngeli kamwe hawezi kusema kuwa anaielewa lugha ya Kiswahili. Atakuwa akituhadaa. Sarufi pia hujumuisha sehemu muhimu kama vile: matamshi, majina, vielezi, vitenzi, viambishi, uakifishaji, nyakati, vivumishi na mnyambuliko wa vitenzi.

Mwalimu atumie mbinu mbalimbali katika kuwafunza wanafunzi sarufi. Mwalimu atafute nyenzo zinazofaa na rahisi kupata. Mwalimu asitafute nyenzo ambazo zitagharimu kiasi kikubwa cha pesa. Pia, aunde vifaa vyake ili kuepuka matumizi ya pesa kwa minajili ya kuvinunua.

Mwalimu awatathmini wanafunzi wake ili kutambua iwapo wameelewa yale yote waliyojifunza. Endapo watatokea wanafunzi ambao hawajaelewa, basi mwalimu achukue jukumu la kuwasaidia wanafunzi wake mmoja mmoja kibinafsi kutegemea matatizo yao.

**e) Kuandika**

Katika kuandika, mwalimu asisitize kuhusu hati nadhifu na inayosomeka kwa urahisi. Kila herufi iandikwe vizuri. Mwalimu aziandike herufi ubaoni na kuwaonyesha wanafunzi jinsi zinavyoandikwa. Mwalimu azungumzie uakifishaji bora. Mwalimu awape zoezi la kuandika na kuhakikisha kuwa wanafunzi wamefuata maagizo.

Mwalimu anaweza kuandaa funzo la imla ambapo anapaswa kuteua sentensi nzuri zenye maneno ambayo huwatatiza wanafunzi wake kisha ayaandike ubaoni na kuwaongoza wanafunzi kuyasoma kwa ufasaha. Mwalimu ayafute kisha awaambie wanafunzi wayaandike jinsi atakavyoyasoma. Njia hii itamwezesha mwalimu kuelewa iwapo wanafunzi wake wameelewa au la. Vilevile, mwalimu anaweza kuyasoma maneno (kwa matamshi sahihi) na kuwaagiza wanafunzi wayaandike.

**Tathmini**

Hii ndiyo sehemu muhimu sana kwa sababu hiki ndicho kigezo kinachomwezesha mwanafunzi na mwalimu kutambua kama malengo ya funzo lake yalitimia.

Mwalimu huwatathmini wanafunzi wake ili:

(a) Kumwezesha kuelewa hatua walizozipiga wanafunzi.
(b) Kuwatia wanafunzi moyo wa kuendelea kujifunza.
(ch) Kuelewa maendeleo yake katika kufunza.
(d) Kumwezesha kuelewa kama ametimiza malengo yake vizuri ili aweze kulirudia funzo inapobidi.
(e) Kumwezesha kutambua kama malengo ya funzo lake yalifaulu na kwa kiasi gani.

**Aina za tathmini**

1. Kuandika muhtasari wa yale wanafunzi walisoma.
2. Kutahini usahihi wa sentensi zilizoandikwa kwenye madaftari.
3. Kuhakiki matamshi kwa kusoma sentensi au vifungu mbalimbali.
4. Kutunga sentensi zilizoendelezwa vizuri.
5. Kuambatanisha maelezo na maneno kwa usahihi.
6. Mazoezi na marudio ya mitihani ya wiki.
7. Maswali ya chemshabongo darasani ambayo humwezesha mwanafunzi kuelewa na kukumbuka aliyoyasoma hapo awali.
8. Mitihani ya kila mwisho wa muhula.

Ni muhimu mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi ili aelewe matatizo ambayo yanawakabili wanafunzi na awafunze upya sehemu yenye matatizo. Mwalimu asisitize kuhusu kufanya masahihisho.

Mwalimu awatambue wanafunzi wenye matatizo na kuwapa msaada maalum. Atumie mbinu mbalimbali ili kumwezesha mwanafunzi kuelewa vyema. Mwalimu

awe makini sana anaposhughulikia wanafunzi dhaifu ili wasikate tamaa. Daima awatie motisha.

**Nyenzo za kufunzia**

Nyenzo ni muhimu katika somo lolote likiwamo Kiswahili. Mwalimu anatarajiwa kuwa mbunifu na kutumia nyenzo ambazo zinapatikana kwa urahisi. Ni muhimu mwalimu kuhakikisha kuwa hamna gharama inayoweza kuepukika katika funzo lolote lile. Ni vyema mwalimu abuni baadhi ya nyenzo zake.

Mwalimu yeyote ni lazima aende na wakati. Wakati huu ambapo teknolojia imekua sana hasa katika mawasiliano, ni muhimu mwalimu kutumia vifaa vya kisasa. Kwa mfano, ni muhimu mwalimu kutumia vifaa halisi kama rununu na kutumia picha za baadhi ya vyombo ambavyo ama havipatikani katika mazingira ya shuleni au mwalimu hawezi kuvibeba na kwenda navyo darasani kama vile: tarakilishi, runinga, kipepesi n.k.

Ni vyema kwa mwalimu kuyafahamu mazingira ya mwanafunzi wake. Anapofunza kuhusu baruapepe, mtandao, wavuti n.k., somo hili litakuwa rahisi kwa wanafunzi wa mjini na kuwaelezea wanafunzi hao ni rahisi sana. Wanafunzi wale ambao hawajawahi kuona wala kusikia mambo hayo, kwao huenda ikawa ni kioja. Hapo mwalimu anatakiwa awe na nyenzo za kutosha ili kuwafaa wanafunzi wake. Vifaa vingine vinapatikana kwa urahisi na mwalimu anaweza kuwaambia wanafunzi wake walete baadhi ya vifaa hivyo.

Mwalimu asichukulie funzo lolote kuwa rahisi. Utashangaa kugundua kwamba unapofunza kuhusu mimea, wanafunzi wengi hasa wa mijini hawajapata kuiona mimea mingi. Ni bora kwa mwalimu kutumia picha au mimea yenyewe kama inaweza kupatikana.

Mwisho kabisa, ni vyema kwa mwalimu kuelewa kuwa kufaulu au kutofaulu kwa funzo lolote kunamtegemea mwalimu. Ukiwaona wanafunzi wako wakilipenda somo la Kiswahili ujue kuwa aliyefaulu ni wewe. Ukiwaona wanafunzi wakilalamika kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu na inayosinya basi ujue tatizo ni wewe. Ni jukumu la mwalimu yeyote aliyehitimu kuona kuwa wanafunzi wake watakuwa wakilitarajia somo lake na kutaka asitoke darasani. Hapo utakuwa umefaulu. Wewe ndiwe unayewafanya wanafunzi wakuchukie na wewe ndiwe unayeweza kuwafanya wanafunzi wakupende.

**Namna ya kuwashughulikia wanafunzi wa aina mbalimbali**

Mwalimu anapaswa kwenda darasani akifahamu jambo moja kuwa wanafunzi wote wanaweza kufunzwa na kuelewa. Mwalimu ajiepushe kabisa na tabia ya kuwapa wanafunzi wengine majina kuwa ni wajinga. Wanafunzi wote wameletwa shuleni kuondoa ujinga. Unapomwita mwanafunzi mjinga uelewe kuwa wewe ndiwe uliyeshindwa kuondoa ujinga huo.

Jinsi wanafunzi walivyotoka katika mazingira tofauti ndivyo wanavyotofautiana na ndivyo walivyo tofauti katika kuelewa somo au funzo lolote. Utawapata

wanafunzi wenye akili tambuzi kiasi kwamba wakiambiwa kitu huelewa haraka ajabu. Wakipewa zoezi wao hulifanya haraka.

Mwalimu anapaswa kuwa macho na kuwashughulikia vizuri kwa sababu wanaweza kupotoka kwa urahisi. Wanapomaliza zoezi huishia kupiga kelele na kuwasumbua wenzao. Mwalimu anapaswa kuwaandalia mazoezi ya kutosha ili wakimaliza waendelee na mengine.

Mwalimu anapaswa kuwashughulikia barabara wanafunzi wanaochukua muda kuelewa. Akishawapa wengine zoezi, achukue muda huo kuwasaidia wanafunzi dhaifu. Ahakikishe kuwa japo watachukua muda kuelewa, mwishowe watawafikia wale wanaoelewa haraka.

Mwalimu hupata sifa chungu nzima anapowasaidia wanafunzi dhaifu kuwa bora. Kufaulu kwa darasa lolote kunategemea wanafunzi wote. Ni bora kwa mwalimu yeyote kujikwamua katika kutoa sababu kuwa wanafunzi wake ni dhaifu. Swali bado litamrudia, "Umefanya nini kuondoa udhaifu wao?" Umepewa jukumu. Mustakabali wa wanafunzi unakutegemea wewe. Itakuwa ni fahari kubwa utakapowaona wanafunzi wako wakifanikiwa. Wanafunzi pia watamwonea fahari mwalimu wao.

Mwalimu atenge muda wake ili kuwashughulikia wanafunzi wenye matatizo mbalimbali hasa wale ambao si wepesi wa kuelewa. Hali kadhalika, mwalimu anapaswa kuchukua tahadhari ili asiwakere wanafunzi wengine. *Kwa mfano:* katika kusimulia hadithi, anapaswa kutoa hadithi ambazo hazitawadunisha wanafunzi wenye upungufu fulani.

Mwalimu ahakikishe kuwa katika mafunzo yake ameshughulikia usawa wa jinsia. Pasiwe na ubaguzi wa aina yoyote.

**Ratiba ya mafunzo**

Ratiba ni muhimu kwa mwalimu yeyote aliyehitimu. Ni sharti mwalimu awe na mwongozo na taratibu za kufuata ili asisahau mambo muhimu.

Mwalimu aandae ratiba kutokana na silabasi ambayo ndiyo mwongozo unaotoa mwelekeo wa kufundisha. Mwalimu avitumie vitabu bora vilivyoidhinishwa na wizara ya elimu.
Ufuatao ni mfano wa ratiba ya mafunzo katika somo la Kiswahili.

| WIKI | KIPINDI | MADA KUU | MADA NDOGO | MALENGO | NYENZO | ASILIA | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 1- 2 | FASIHI KATIKA KISWAHILI | Ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili<br>i) Kusoma ufahamu | - Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;<br>- Kutambua maana ya fasihi ya Kiswahili;<br>- Kuelewa umuhimu wa fasihi andishi katika Kiswahili;<br>- Kufahamu tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili. | - Vitabu vya fasihi<br>- Majarida<br>- Rekoda<br>- Vinasa sauti<br>- Simu zenye uwezo wa kuhifadhi hati<br>- Mtandao wa intaneti<br>- Vifaa au zana kwa wanafunzi wasiojiweza au wazito kuelewa | Kitabu cha mwanafunzi ukurasa wa 1-4 | |
| 2 | 3- 4 | | ii) Kujifunza msamiati | - Kubaini msamiati unaotumika katika fasihi;<br>- Kutaja tanzu za fasihi andishi;<br>- Kutumia msamiati wa fasihi kwa usahihi katika sentensi na maongezi. | - Kazi za fasihi za waandishi mbalimbali;<br>- Majarida kuhusu fasihi;<br>- Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21;<br>- Mtandao wa intaneti. | Kitabu cha wanafunzi ukurasa wa 4-5 | |

## Andalio la somo

Huu ni utaratibu anaouandaa mwalimu ili kuliendesha vyema somo lake kuanzia mwanzo hadi tamati. Utaratibu huo humwezesha mwalimu kufuata hatua baada ya nyingine na kuweza kupata picha ya somo lake mapema. Humwezesha mwalimu kushughulikia masuala yote muhimu katika somo. Kufikia mwisho wa somo, mwalimu huweza kutathmini ili kuelewa kama somo lake limefaulu.

**Mfano wa andalio la somo**

**Jina la shule**: NYUNGWE **Jina la mwalimu :** JULIA NYIRANEZA

| **Muhula** | **Tarehe** | **Somo** | **Kidato** | **Mada** | **Idadi ya masomo** | **Muda** | **Idadi ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| wa kwanza | 10.05.2017 | Kiswahili | cha sita | ya 1 | 1 kwa 5 | Dakika 40 | 38 |

| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu pamoja na idadi yao: 1**<br>Mwanafunzi mwenye matatizo ya kusikia. | |
|---|---|
| **Mada Kuu:** | **Fasihi katika Kiswahili** |
| **Uwezo upatikanao katika mada:** | Mwanafunzi aweze kuelewa tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani. |
| **Kichwa cha somo:** | Kifungu kuhusu tanzu za fasihi andishi |
| **Malengo ya kujifunza:** | • Kutokana na kifungu cha habari, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kutofautisha kwa usahihi tanzu za fasihi andishi.<br>• Kutokana na kifungu, mwanafunzi atakuwa na uwezo wa kutambua kwa urahisi maana ya msamiati unaohusiana na tanzu za fasihi andishi. |
| **Mpangilio wa darasa** | **Mandhari:** Somo linatokea darasani. |
| **Zana / Vifaa** | • Kitabu cha mwanafunzi<br>• Vitabu vya kazi za fasihi andishi<br>• Majarida mbalimbali kuhusu fasihi<br>• Mtandao wa intaneti |
| **Marejeleo** | Kitabu cha *Kiswahili kwa shule za Rwanda*, kidato cha 6; 2017, *Kamusi ya karne ya 21*, Longhorn Kenya, *Kitabu cha Kiswahili*, kidato cha 6, MK. |

<table>
<tr><td rowspan="2">Muda na hatua</td><td colspan="2">Mbinu za kufundishia na kujifunzia:<br>Kwa njia ya maigizo katika makundi au kati ya wanafunzi watatu watatu, wanafunzi watatazama mchoro kisha wasome kifungu cha habari kuhusu tanzu za fasihi andishi.</td><td rowspan="2">Uwezo wa jumla, masuala mtambuka na maelezo mafupi</td></tr>
<tr><td>Wajibu wa mwalimu</td><td>Wajibu wa wanafunzi</td></tr>
</table>

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Utangulizi**<br>Dakika 5 | - Mwalimu awaamkie wanafunzi wake, kisha awaulize maswali mepesi kuhusu maarifa yoyote waliyo nayo kuhusiana na fasihi ya Kiswahili.<br>- Mwalimu atangulize somo kwa kuwagawa wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awachangamshe kwa kuwauliza maswali mepesi kuhusu mchoro ulio katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 1. Mwalimu ahakikishe kuwa mwanafunzi mwenye matatizo ya kusikia ameketi karibu naye na mwalimu amsomee kwa sauti ya juu. | - Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu.<br>- Wanafunzi wajadiliane kile wanachokiona kwenye michoro kwa sentensi kamili za Kiswahili. | **Uwezo wa jumla:**<br>i) ***Kupata stadi za utafiti:*** Wanafunzi wahimizwe kufanya utafiti kuhusiana na tanzu za fasihi katika Kiswahili.<br>ii) ***Kuwa na tafakuri tanduizi:*** Wanafunzi wataweza kufikiri kwa undani kuhusiana na fasihi watakayofundishwa katika somo hili.<br>iii) ***Kuwa na uwezo wa kushiriki katika mawasiliano kwa lugha rasmi:*** Kupitia kwa mazoezi ya kuigiza tamthilia na kukariri mashairi mbalimbali, uwezo huu utapatikana. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Somo lenyewe**<br>Dakika 30 | - Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kifungu cha habari kuhusu fasihi andishi.<br>- Mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wanasoma kama ipasavyo huku wakizingatia kanuni zifaazo za kisarufi, utamkaji sahihi na kiimbo kinachotakiwa.<br>- Mwalimu aendelee kwa kuwauliza wanafunzi wajadiliane kuhusiana na tofauti zilizopo kati ya tanzu mbalimbali za fasihi andishi.<br>- Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kujibu maswali ya ufahamu kwa kuandika majibu sahihi kwenye madaftari yao. | - Wanafunzi jipange katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wasome kifungu cha habari.<br>- Wanafunzi wasome kifungu cha habari kwa ufasaha na kwa kutamka maneno kama inavyostahili.<br>- Wanafunzi washiriki katika kutunga majadiliano kwa kuwasikiliza wenzao na pia kutoa hoja zao.<br>- Wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu. | **Masuala mtambuka:**<br>i) ***Usawa wa kijinsia:*** Wanafunzi wafahamu kuwa kazi za tanzu mbalimbali za fasihi zinaweza kuandikwa na waandishi wa kike na hata wa kiume.<br>ii) ***Mafunzo kuhusu uzalishajimali***: Wanafunzi watambue kuwa kazi za kifasihi zilizoandikwa na kuchapishwa zinaweza kuuzwa na kuwapatia waandishi pesa za kujikimu maishani. |
| **Hitimisho**<br>Dakika 5 | - Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kusahihisha maswali ya ufahamu kwa kuwashirikisha kwenye shughuli hiyo. Pia, atilie mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika katika ujifunzaji wao. | - Wanafunzi washiriki katika usahihishaji wa zoezi la ufahamu na baadaye wafanye marudio. | |
| **Tathmini ya mwalimu** | Mwalimu achunguze iwapo ameyatimiza malengo ya somo hili au la. | | |

Sura ya **Kwanza**

**Mada Kuu 1:** Fasihi katika Kiswahili

**Mada Ndogo:** Ufafanuzi wa tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili

## Uwezo upatikanao katika mada hii:

Mwanafunzi aweze kuelewa tanzu tofauti za fasihi andishi katika Kiswahili kwa madhumuni ya kuimarisha sanaa na kuitumia kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani.

## Malengo ya kujifunza

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema |
|---|---|---|
| • Kutaja tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili.<br>• Kufafanua maana ya kila utanzu wa fasihi andishi.<br>• Kueleza mchango wa kila utanzu katika maendeleo ya kiutamaduni na kiuchumi ndani ya nchi.<br>• Kubainisha mtindo wa tanzu za fasihi andishi kwa kuzingatia fani yake.<br>• Kueleza vifungu vya sentensi. | • Kuigiza tanzu za fasihi andishi zinazohusika.<br>• Kulinganisha tanzu mbalimbali za fasihi andishi kutokana na muundo wa kila utanzu.<br>• Kujadili mchango wa fasihi andishi katika maendeleo ya kiutamaduni, kijamii na kiuchumi katika nchi.<br>• Kusoma au kusikiliza kazi za fasihi kutoka tanzu za fasihi andishi.<br>• Kutafsiri tabia za wahusika katika tanzu husika.<br>• Kuhalalisha uhusiano uliopo baina ya kichwa cha utanzu na yaliyomo.<br>• Kuchambua sentensi za Kiswahili kwa kuonyesha vifungu vyake. | Mwanafunzi atapata mabadiliko ya:<br>• Kuuhifadhi utamaduni wa nchi na kuukuza zaidi kutokana na tabia za wahusika zilizojitokeza katika tanzu husika.<br>• Kuimarisha kazi za sanaa kama mojawapo ya njia za kujitegemea maishani.<br>• Kutoa mchango wake binafsi katika mabadiliko ya maendeleo ya utamaduni wa uchumi wa raia. |

## Maelezo kwa mwalimu

Mada hii inahusiana na masomo ya sanaa, kujenga uhusiano mwema, kujenga tabia njema, umoja na ushirikiano, umoja na maridhiano, upendo, adabu n.k.

Fasihi katika Kiswahili itashughulikiwa katika mada hii. Fasihi ni somo muhimu katika jamii kwani huhusisha matukio mbalimbali kuhusiana na jamii zetu na maisha yetu ya kila siku. Fasihi imegawika kuwili ambapo kuna fasihi andishi na fasihi simulizi. Katika mada hii, tutajikita hasa katika fasihi andishi pamoja na kuzichunguza tanzu zake. Tanzu za fasihi andishi ni: *riwaya, hadithi fupi, ushairi* na *tamthilia*. Maana za tanzu hizi za fasihi andishi zitafafanuliwa pamoja na kutajiwa mifano. Fasihi hutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiutamaduni na kiuchumi katika nchi. Pia, watu huweza kujitegemea kupitia kwa sanaa katika fasihi andishi.

Mada hii pia inahusisha kuelezea vifungu vya sentensi kwa mtindo wa virai na vishazi.

## Masuala mtambuka

Baadhi ya masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni elimu ya pamoja, usawa wa kijinsia, amani na maadili pamoja na mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake.

Amani na maadili yatashughulikiwa kupitia kwa kazi za fasihi za waandishi mbalimbali ambazo wanafunzi watazisoma. Katika usomaji huu, umoja na amani unaweza kuhimizwa kupitia kwa wahusika mbalimbali, matukio mbalimbali pamoja na maudhui yanayojenga ushirikiano wa wanajamii. Wanafunzi waelekezwe kutangamana kwa amani na upendo. Usawa wa kijinsia utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasichana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao licha ya jinsia zao tofauti. Elimu ya pamoja itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma pamoja kwa kuwashirikisha hata wanafunzi wenye ulemavu na matatizo mbalimbali. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi wote kukubali na kushirikiana kwa pamoja na wenzao kutoka katika matabaka mbalimbali ya kijamii. Wanafunzi pia watafundishwa umuhimu wa mazingira yao na namna ya kuyahifadhi.

## Uwezo wa jumla

Katika ufundishaji wa somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanapata uwezo wa kuwa na tafakuri tanduizi, stadi za utafiti, usuluhishaji wa matatizo,

mawasiliano katika lugha rasmi, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu.

Mwalimu awaelekeze na awashirikishe wanafunzi wote katika kuwa na tafakuri tanduizi kwa kufikiri kwa undani zaidi kuhusiana na fasihi watakayofundishwa katika somo hili. Ujuzi huu utawawezesha kuyajibu maswali katika somo hili kuhusiana na fasihi katika Kiswahili.

Kupitia kwa mazoezi ya kuigiza tamthilia na kukariri mashairi mbalimbali watakayokumbana nayo, wanafunzi watahimizwa kuwasiliana kwa lugha rasmi, kuwa na utawala binafsi pamoja na kuzifahamu stadi mbalimbali za maisha. Stadi za utafiti zitakuzwa kupitia kwa wanafunzi kufanya utafiti kuhusiana na tanzu za fasihi katika Kiswahili. Ujifunzaji wa muda mrefu uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na fasihi katika Kiswahili watakayotumia nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku.

## Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kama vile:

| | **Msamiati** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1. | **fasihi** | taaluma inayohusu tungo za kisanaa za simulizi na andishi |
| 2. | **utanzu** | tawi mojawapo la kitu. Kwa mfano: fasihi |
| 3. | **riwaya** | hadithi ndefu ya kubuni yenye wahusika na mtiririko wa matukio mengi yaliyoandikwa kwa lugha ya nathari |
| 4. | **tamthilia** | hadithi ambayo imeandikwa kama mazungumzo kati ya watu |
| 5. | **hadhira** | jumla ya wasikilizaji au watazamaji wa kazi maalum |
| 6. | **sentensi** | neno au kifungu cha maneno kinachojitosheleza kimaana |
| 7. | **kiima** | neno linaloonyesha mtenda katika sentensi na huja baada ya kitenzi |
| 8. | **kiarifu** | sehemu ya sentensi yenye kitenzi pamoja na vijalizo vyake |
| 9. | **sanaa** | uhodari wa kuwasilisha hisia za binadamu kwa maandishi |
| 10. | **mwandishi** | mtu anayeshughulika na uandikaji wa kitabu au makala |

## Usuluhishaji wa tatizo

Katika sehemu hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kulingana na zoezi husika kisha awaombe wachunguze kwa makini mchoro ulio katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 1 kuhusiana na fasihi katika Kiswahili

pamoja na tanzu zake mbalimbali. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika shughuli hii. Wanafunzi wachunguze mchoro huo na mwalimu awaulize maswali kama vile: *Fasihi andishi ina tanzu zipi*? Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu maswali hayo na kuelewa tanzu za fasihi katika Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu achochee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tanduizi kwa kuchunguza na kujibu maswali kuhusu fasihi ya Kiswahili.

## Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali katika ujifundishaji wao. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, mwalimu ahusishe matumizi ya breli pamoja na vifaa vya kunasia sauti.

Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kusikia, mwalimu anaweza kuhusisha matumizi ya lugha ya ishara. Pia, mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri wa lugha ya ishara. Haya yatawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wanafunzi wenzao bila vikwazo vyovyote.

Nafasi ya wanawake na walemavu katika fasihi ya Kiswahili itiliwe maanani kupitia kwa kazi mbalimbali za fasihi ambazo wanafunzi watasoma zikiwemo zilizo katika *Kitabu cha Mwanafunzi* 19-22 ili kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja. Hili litadumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi na kuwafanya kuwa wazalendo kamili katika umri wao.

## Orodha ya masomo na vipindi

| **Mada ya somo** | | **Idadi ya vipindi** |
|---|---|---|
| Somo la 1: | Tanzu za Fasihi Andishi | 10 |
| Somo la 2: | Utanzu wa Hadithi Fupi | 15 |
| Somo la 3: | Utanzu wa Riwaya | 15 |
| Somo la 4: | Utanzu wa Tamthilia | 15 |
| Somo la 5: | Utanzu wa Ushairi | 10 |
| | | **JUMLA: 65** |

# Somo la 1: Fasihi andishi

## Vipindi 1-2: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutambua maana ya fasihi ya Kiswahili;
- Kuelewa umuhimu wa fasihi andishi katika Kiswahili;
- Kufahamu tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Vitabu vya fasihi;
- Majarida mbalimbali kuhusu fasihi;
- Kazi za fasihi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 1-4;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu kifungu cha habari kuhusu fasihi andishi, dhana ya fasihi andishi, tanzu za fasihi andishi na umuhimu wa fasihi katika kuendeleza jamii kwa ujumla. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu maana ya fasihi ya Kiswahili pamoja na tanzu za fasihi andishi. Mwalimu anaweza kuandaa masimulizi yaliyorekodiwa au kuandikwa ili wanafunzi wayasikilize au wayasome darasani. Masimulizi haya yanaweza kuhusu fasihi ya Kiswahili kwa ujumla zikiwemo tanzu mbalimbali za fasihi andishi. Ni vyema mwalimu alete vifaa vingine vinavyoweza kurahisisha uelewa wa mada hii kama vile vitabu vya hadithi, tamthilia na mashairi mbalimbali.

Hivyo basi, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza

kuelewa somo hili kwa kuhusisha vifaa alivyovileta na kueleza michoro iliyopo kwa kutamka huku maelezo mengine yakiandikwa ubaoni au kwenye breli. Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali mepesi kuhusu maarifa yoyote waliyo nayo kuhusiana na fasihi ya Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu.

Mwalimu atangulize somo kwa kuwagawa wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awachangamshe kwa kuwauliza maswali mepesi kuhusu mchoro ulio katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 1. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuelewa maana ya fasihi, matawi yake pamoja na tanzu mbalimbali za fasihi andishi. Mwalimu awaulize maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye mchoro huu?* Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa na mwalimu. Kwa mfano: *Mimi ninaona mchoro wa matawi ya fasihi. Mimi ninaona tanzu za fasihi andishi* na kadhalika.

Mwalimu atumie mchoro ulio katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 1 kufafanua maana ya fasihi, matawi yake pamoja na tanzu za fasihi andishi. Kupitia kwa majadiliano ya mwalimu na wanafunzi, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa umuhimu wa fasihi katika jamii. Aidha, mwalimu aulize maswali kwa kuwataka wanafunzi waweze kugundua kile kinachowasilishwa na mchoro uliopo ili wakuze uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi na kuwasaidia kupata ujuzi katika ubunifu na ugunduzi, tafakuri tanduizi, usawa wa kijinsia kupitia kwa masimulizi watakayosikiliza au kusoma. Hivyo basi, ni lazima mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kuelewa maana ya fasihi ya Kiswahili.

## 1.1 Kusoma na kufahamu

### Kifungu kuhusu tanzu za fasihi andishi

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya kifungu cha habari kuhusu fasihi andishi kilicho katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 1-3. Wanafunzi wasome kama wanavyoelekezwa na mwalimu. Katika shughuli hii, mwalimu

achunguze iwapo wanafunzi wanasoma ipasavyo huku wakizingatia kanuni zifaazo za kisarufi, utamkaji sahihi na kiimbo kinachotakiwa. Baadaye, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wote wamekielewa kifungu walichosoma kwa kuwauliza maswali kama vile: *Fasihi ina matawi mangapi? Tanzu za fasihi andishi ni zipi?* na kadhalika. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu na watoe hoja zao kuhusu maana na tanzu za fasihi andishi.

Mwalimu aendelee kwa kuwauliza wanafunzi wajadiliane kuhusiana na tofauti zilizopo kati ya tanzu mbalimbali za fasihi andishi. Shughuli hii itawawezesha wanafunzi kuweza kwenda maktabani na kutafuta vitabu vya fasihi na kujisomea kwa kurejelea utanzu wowote wa fasihi andishi.

Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kujadiliana maswali ya ufahamu waliyopewa na baadaye wayasahihishe maswali hayo huku mwalimu akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

## Tathmini ya vipindi 1-2

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kufafanua maana ya fasihi, maana ya fasihi andishi pamoja na kuzitaja na kuzifafanua tanzu mbalimbali za fasihi andishi. Vilevile, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wanaweza kueleza tofauti zilizopo kati ya tanzu mbalimbali za fasihi andishi.

## Vipindi 3-4: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati unaotumika katika fasihi;
- Kutaja tanzu za fasihi andishi;
- Kutumia msamiati wa fasihi kwa usahihi katika sentensi na maongezi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za fasihi za waandishi mbalimbali;
- Majarida mbalimbali kuhusu fasihi;
- *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21;*
- Mtandao wa intaneti;

- *Kitabu cha Mwanafunzi,* ukurasa 4-5;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu msamiati unaotumika katika ufafanuzi wa fasihi ya Kiswahili kupitia kwa kifungu watakachokisoma katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 1-3. Kwa kuwa kifungu kinahusu tanzu mbalimbali za fasihi andishi, ni vyema mwalimu alete vitabu mbalimbali vya fasihi vinavyoweza kurahisisha uelewa wa msamiati katika mada hii.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza kuelewa somo hili aidha kwa kutumia lugha ya ishara au breli huku maelezo mengine yakiandikwa ubaoni. Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa shughuli hii ya wanafunzi ya kutambua na kuufafanua msamiati unaohusu tanzu za fasihi andishi.

## 1.2 Kujifunza msamiati kuhusu tanzu za fasihi andishi

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wajadiliane kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao. Mwalimu anaweza kuwaruhusu wanafunzi kutumia kamusi pale inapohitajika. Ili kuwaelekeza wanafunzi kupata uelewa wa msamiati huo, mwalimu awaongoze katika kuchunguza matumizi ya msamiati huo katika kifungu cha habari kuhusu tanzu za fasihi andishi walichokisoma hapo awali. Wanafunzi wajadiliane na mwalimu azunguke darasani akitoa maelekezo kwa wanafunzi wanaotatizika. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu zoezi la 1 la msamiati na ahakikishe kuwa wanafunzi wote wamejibu maswali yaliyopo. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatunga sentensi zao wenyewe zilizo sahihi kwa kutumia msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika vitabu vyao. Mwalimu awaongoze wanafunzi kutunga sentensi zenye kuimarisha maadili mema katika maisha ya kila siku, kuchukia tabia zote zinazozuia maendeleo, kujiamini, kuwaamini wengine na kuunga

mkono umoja kwa minajili ya ushirikiano. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 2.

## Tathmini ya vipindi 3-4

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kwa kurejelea msamiati mahususi waliopatana nao katika kifungu cha habari kuhusu tanzu za fasihi andishi walichokisoma hapo awali kama vile: *riwaya, tamthilia, shairi* na kadhalika. Kwa hivyo, vifaa vilivyotumiwa kujifundishia somo hili vinaweza kutumiwa kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kurejelea tanzu mbalimbali za fasihi andishi.

## Vipindi 5-6: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kufafanua tanzu za fasihi andishi;
- Kueleza umuhimu wa fasihi andishi kwa jamii.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Kazi za fasihi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 5;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Masimulizi yaliyoandaliwa na mwalimu kwa kurekodiwa au kuandikwa yatumiwe kuwaongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kujadili umuhimu wa fasihi andishi katika jamii. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu umuhimu wa fasihi andishi kwake binafsi na kwa jamii yake.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi katika makundi yao.

**d) Utaratibu wa somo**

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

## 1.3 Majadiliano kuhusu umuhimu wa fasihi andishi

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watano watano wajadiliane kuhusu mambo matano yanayofafanua umuhimu wa fasihi andishi ya Kiswahili katika jamii.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili swali lililo hapo juu. Wanafunzi wanaweza kurejelea kazi zozote za fasihi andishi ambazo wanazifahamu.

Wanafunzi wanaweza kutoa majibu kama vile:

*a) Kufundisha maadili mema kwa watu katika jamii.*

Wanafunzi wanaweza kutoa mfano wa kazi ya kifasihi inayofundisha maadili kwa watu katika jamii.

*b) Kuonya, kushauri au kutahadharisha kuhusu mambo fulani katika jamii.*

Wanafunzi wanaweza kutoa mfano wa kazi ya kifasihi inayowaonya wanajamii dhidi ya shughuli au mambo fulani yaliyo na madhara katika jamii.

Wanafunzi wanaweza kurejelea kazi mbalimbali za kifasihi ambazo wamewahi kuzisoma ili kujadiliana kuhusu swali walilopewa katika sehemu hii. Baadaye, mwalimu aombe kila kundi la wanafunzi lijitokeze mbele ya darasa na kuwaeleza wenzao matokeo ya majadiliano yake. Katika hatua hii, mwalimu arekebishe makosa ya kimatamshi pindi yanapotokea.

Ni vyema mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanaweza kujibu swali hili kwa kiwango cha kuridhisha na kuonyesha kwamba wamefahamu umuhimu wa fasihi andishi katika jamii. Mwalimu azunguke darasani na kutoa maelezo pale yanapotakiwa ili kuelekeza makundi ya wanafunzi wanaotatizika.

## Tathmini ya vipindi 5-6

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea umuhimu wa fasihi andishi katika jamii na katika maisha yao binafsi huku wakirejelea kazi mbalimbali za kifasihi ambazo wamewahi kuzisoma. Kwa hivyo, vifaa

vilivyotumiwa kujifunzia somo hili vinaweza kutumiwa kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa somo hili.

## Vipindi vya 7-8: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kujadili umuhimu wa fasihi andishi;
- Kujadili tanzu za fasihi andishi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za fasihi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 5-6;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Masimulizi yaliyoandaliwa na mwalimu kwa kurekodiwa au kuandikwa yatumiwe kuwaongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kujadili umuhimu wa fasihi andishi kwao binafsi. Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu umuhimu wa fasihi andishi kwake binafsi.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi katika kujadili kuhusu namna fasihi andishi imemfaidi yeye kama mtu binafsi.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa.

## 1.4 Majadiliano

Sehemu hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni yake binafsi kuhusu umuhimu wa fasihi andishi kwa maisha yake binafsi. Kila mwanafunzi ataombwa kuwaeleza wanafunzi wenzake katika makundi yao kuhusu kazi yoyote ya kifashi aliyowahi kuisoma na namna ilivyokuwa na umuhimu kwake binafsi. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili kujadili kuhusu kazi ya utanzu wowote wa fasihi andishi ambao amewahi kuusoma na namna kazi hiyo ilivyokuwa na umuhimu kwa maisha yake binafsi.

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao. Baadaye, mwalimu aombe kila kundi la wanafunzi lijitokeze mbele ya darasa na kuwaeleza wanafunzi wenzao kuhusu matokeo ya majadiliano yao. Mwalimu naye achukue muda wake kwa kusahihisha makosa ya wanafunzi hasa ya kimatamshi pindi yanapotokea na awapongeze pale wanapofanikiwa huku akiomba makundi mengine kuwaiga wenzao na kusahihisha makosa waliyofanya ili waboreshe mawasilisho yao.

Vilevile, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wanatunga sentensi kamili zisizo na makosa ya kisarufi ili wapate uwezo wa kuwasiliana katika lugha fasaha. Aidha, ni vyema pia mwalimu awasaidie wanafunzi kupata ujuzi katika tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha, elimu kuhusu fedha na kadhalika kupitia kwa kazi mbalimbali za kifasihi walizowahi kuzisoma.

## Tathmini ya vipindi 7-8

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kundi. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kueleza umuhimu wa fasihi andishi kwa maisha yao binafsi.

## Vipindi vya 9-10: Sarufi (Sentensi ya Kiswahili)

### a) Malengo ya somo

- Kufafanua maana ya sentensi ya Kiswahili;
- Kutambua sehemu kuu za sentensi ya Kiswahili;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kuonyesha sehemu zake kuu.

**b) Vifaa vya kujifundishia**

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 6-10;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ambayo itawawezesha wanafunzi kutambua maana ya sentensi ya Kiswahili. Mwalimu anaweza kuandika mifano kadhaa ya sentensi mbalimbali za Kiswahili ambazo atawapa wanafunzi katika makundi yao ili wazijadili.

**d) Utaratibu wa somo**

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu maneno mbalimbali ambayo hutumika kuunda sentensi katika Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi wajikumbushe kuhusu maneno mbalimbali ambayo hutumika kuunda sentensi katika Kiswahili kama vile: *nomino, vitenzi, vivumishi* n.k.

## 1.5 Maana ya sentensi

Katika sehemu ya 1 ya sarufi, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wapange maneno waliyopewa kwa usahihi ili kuunda sentensi kamili na sahihi ya Kiswahili.

Wanafunzi katika makundi yao wapange maneno waliyopewa kama walivyoelekezwa na mawalimu. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua maneno yaliyotumika kuunda sentensi walizopewa. Baada ya hapa, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutambua maana ya sentensi kamili ya Kiswahili. Awaeleze kuwa *sentensi ni kundi la maneno au neno moja lililo na maana kamili*. Wanafunzi wafahamishwe kuwa *maana katika sentensi huonyeshwa na kitenzi*. Kwa mfano:

1. Njoo!

2. Mwalimu anaandika ubaoni.
3. Mama amepika chakula kingi.
4. Amelala.
5. Sitarudi.

Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 kwa kutunga sentensi kumi sahihi katika tungo yakinishi na tungo kanushi. Pia, wanafunzi waeleze aina za maneno yaliyotumika kuunda sentensi ambazo watatunga. Wanafunzi wajibu zoezi hilo na mwalimu awaombe wachunguze maelezo muhimu yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi ili wapate kuelewa maana ya sentensi ya Kiswahili. Swali katika zoezi la 4 litumiwe na mwalimu kama njia ya kuchunguza iwapo wanafunzi wameshafahamu maana ya sentensi kamili ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu awaongoze wanafunzi katika kujibu swali hilo na awaombe walisahihishe kwa pamoja huku akiwashirikisha wanafunzi wote kutambua makosa ya wenzao na kuyasahihisha.

## 1.6 Sehemu kuu za sentensi

Katika sehemu ya pili ya ujifunzaji wa sarufi, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili wachunguze jedwali lililo na sentensi zilizoainishwa kwa kuzingatia sehemu zao kuu.

Wanafunzi wachunguze sentensi hizo na mwalimu awaelekeze kuelewa sehemu kuu za sentensi ya Kiswahili ambazo ni *kiima* na *kiarifu*. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kufahamu kuwa kiima ni sehemu ya sentensi ambayo hueleza mtenda wa kitendo fulani katika sentensi husika ilhali kiarifu huhusisha kitenzi katika sentensi husika. Kwa mfano:

1. Mwanafunzi anafagia darasa. (*Katika sentensi hii, 'mwanafunzi' ni kiima kwa sababu ndio mtenda na 'anafagia darasa' ni kiarifu kwa sababu imebeba kitenzi*)
2. Mimi nitaandika insha. (*Katika sentensi hii, 'mimi' ni kiima kwa sababu ndio mtenda na 'nitaandika insha' ni kiarifu kwa sababu imebeba kitenzi*)
3. Ninasoma. (*Katika sentensi hii, 'ninasoma' ni kiarifu kwa sababu imebeba kitenzi*)

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujadili zaidi kuhusu sehemu kuu za sentensi ambazo ni kiima na kiarifu. Kwa mfano:

| Tungo | Ubainishaji |
|---|---|
| Mtoto alianguka chini. | Mtoto mdogo (Kiima)<br>aliangusha ndoo chini (Kiarifu) |
| Mwalimu hodari atafundisha fasihi andishi. | Mwalimu hodari (Kiima)<br>atafundisha fasihi andishi (Kiarifu) |
| Mwali mrembo atashinda mtihani. | Mwali mrembo (Kiima)<br>atashinda mtihani (Kiarifu) |
| Tamthilia yake imeigizwa jana. | Tamthilia yake (Kiima)<br>imeigizwa jana (Kiarifu) |

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi wajadili tofauti kati ya sentensi kamili na sentensi isiyo kamili.

Kwa mfano:

| Sentensi kamili | Sentensi pungufu (kundi la maneno) |
|---|---|
| 1. Walifunga mlango mapema. | Nyumba na mlango wake mzuri sana. |
| 2. Kaka ameondoka. | Mama, dada, nyanya, babu na wewe. |

Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wameelewa fundisho hili, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali katika zoezi la makundi kisha hapo baadaye wajibu maswali ya zoezi la 6 na la 7. Maelezo muhimu yaliyoandikwa katika kitabu cha mwanafunzi yatumiwe kuwaelekeza wanafunzi kutambua muundo kamili wa sentensi ya Kiswahili.

Katika fundisho hili, mwalimu pia awashirikishe wanafunzi katika kutambua maana na mifano ya shamirisho na chagizo katika sentensi za Kiswahili.

## Tathmini ya vipindi 9-10

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha katika somo hili. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa mwalimu wa kubainisha iwapo wanafunzi wamepata uelewa wa kutosha kuhusiana na sehemu kuu za sentensi ya Kiswahili.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

- ***Sentensi*** ni kundi la maneno au neno moja lenye kuwa na maana kamili. Maana katika sentensi huonyeshwa na kitenzi. Kundi la maneno lisilohusisha kitenzi si sentensi na neno moja ambalo si kitenzi kikuu nalo haliwezi kuwa sentensi.

***Mifano:***

1. Mwalimu alifundisha tanzu za fasihi.
2. Uwera amenunua vitabu vizuri.
3. Uwera hapendi kusoma vitabu vya fasihi.
4. Kamana atafungua akaunti katika benki yetu.
5. Akaunti yake itafungwa kesho.

- Sehemu kuu za sentensi ni mbili tu: ***Kiima (K)*** na ***Kiarifu (A)***.

Kiima huhusisha ***nomino, viwakilishi*** na ***vivumishi*** ilhali kiarifu huhusisha ***kitenzi, nomino, vivumishi*** pamoja na ***vielezi***.

**Kwa mfano:** *Mtoto mdogo ameangusha sahani vibaya.*

Sehemu ya kiima itakuwa: *mtoto mdogo* (Nomino + Kivumishi)

Sehemu ya Kiarifu itakuwa: *ameangusha mkate vibaya* (Kitenzi + Nomino + Kielezi)

- Sehemu kuu za sentensi ni mbili: ***Kiima*** na ***Kiarifu***.
- ***Kiima*** ni neno au kundi la maneno yanayoonyesha mtenda na huja kabla ya kitenzi.

  **Mfano:** <u>*Kaka yangu*</u> *anafyeka nyasi vizuri*. (Sehemu iliyopigiwa mstari ni ***Kiima***)
- ***Kiarifu*** ni sehemu ya sentensi inayoanzia kwenye kitenzi pamoja na maneno yanayofuata kitenzi hicho.

  **Mfano:** *Kaka yangu* <u>*anafyeka nyasi vizuri.*</u> (Sehemu iliyopigiwa mstari ni ***Kiarifu***)
- Maneno yanayofuata kitenzi huwa ni ***shamirisho*** na ***chagizo***.

  **Mfano:** *Kaka yangu anafyeka nyasi vizuri*. (Neno 'nyasi' ni nomino inayokuja baada ya kitenzi hivyo inaitwa ***shamirisho***.)

  **Mfano:** *Kaka yangu anafyeka nyasi vizuri*. (Neno 'vizuri' ni kielezi kinachofafanua kitendo cha kufyeka hivyo kinaitwa ***chagizo***)

## 1.7 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe kusoma tena kifungu cha mazungumzo kuhusu '***Elimu ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi kuliko biashara***' kisha waandike sentensi tano zenye vitenzi katika wakati uliotimilika.

### Majibu ya zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi wataandika. Sharti zihusishe vitenzi vilivyotumika katika wakati uliotimilika katika kifungu cha mdahalo walichosoma hapo awali. Kwa mfano:

1. *Wasemaji na wasikilizaji ambao m**me**kuja hapa leo, hamjambo!*
2. *Watu wa**me**elimishwa ili waweze kuwa na uelewa wa mahitaji ya jamii zao.*
3. *Kupitia elimu tu**me**weza kupata teknolojia ya kuboresha maisha yetu.*
4. *Rwanda i**me**wekeza katika elimu.*
5. *Mpango wa elimu ya msingi ya miaka kumi na miwili u**me**anza kuzaa matunda mema.*

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi kumi sahihi katika wakati uliotimilika tungo kanushi na tungo yakinishi.

***Kwa mfano:***

1. *Chakula kimeiva.* – *Chakula hakijaiva.*
2. *Mtoto amelala sana.* – *Mtoto hajalala sana.*
3. *Mwalimu ameandika ubaoni.* – *Mwalimu hajaandika ubaoni.*

## 1.8 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 3-4

1. Fasihi andishi ni aina ya sanaa ambayo msanii au mtungaji hutumia maneno ambayo huandikwa kwa lengo la kupitisha ujumbe.
2. Dunia ya leo imekuwa kama kijiji kimoja kutokana na maendeleo ya fasihi andishi yaliyoenea kote duniani kupitia kwa uandishi na usomaji kwenye mtandao.
3. Riwaya, hadithi fupi, tamthilia na ushairi.
4. Huwa na wahusika wengi wa kubuni na huandikwa kwa aya na kwa mfululizo wa matukio mengi.
5. Beti, mishororo na mizani.
6. Hadithi fupi na huwa na wahusika wachache sana ilhali riwaya huwa na wahusika wengi. Hadithi fupi huhusisha visa vifupi vifupi ilhali riwaya huhusisha usimulizi wa matukio marefu.
7. Tamthilia huandikwa kwa mtindo wa maneno kuandikwa mbele ya mhusika anayeyazungumza ilhali shairi huandikwa kwa kutumia beti zenye mishororo.
8. Fasihi andishi huchangia katika ukuzaji wa lugha kwa sababu watu wanaweza kuhifadhi msamiati wao wa kale kupitia kwa kazi ya uandishi. Fasihi andishi hukusanya matukio ya dunia na kuyaleta karibu na msomaji hivyo basi kurahisisha ufahamu wa historia ya wengi. Huchangia katika maendeleo ya utamaduni wa nchi kupitia kwa maandishi ambayo huzingatia elimu kuhusu utamaduni. Fasihi andishi ni sanaa inayomsaidia binadamu kujiendeleza na kuelimika kuhusu historia ya mtu tangu kale na pia kutabiri kisayansi mambo yatakayoathiri binadamu siku zijazo.
9. Msanii hutunga kazi za fasihi akilenga kupitisha ujumbe kwa hadhira yake.
10. La. Kazi ya fasihi andishi ni mali ya mtu binafsi hivyo basi mtu yeyote hawezi kuibadilisha kazi ya mwingine.

### Zoezi la msamiati, ukurasa 4

Mwalimu atathmini maelezo ambayo yatatolewa na wanafunzi. Sharti maelezo hayo yahusishe msamiati waliopatana nao katika kifungu cha habari walichokisoma.

**Kwa mfano:**

***Hadhira*** - jumla ya wasikilizaji au wasomaji wa kazi maalumu

**Zoezi la 1 A, ukurasa 4**

Mwalimu atathmini maelezo ambayo yatatolewa na wanafunzi. Sharti maelezo hayo yahusishe msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

***Kwa mfano:***

1. ***Tamthilia*** - hadithi ambayo imeandikwa kama mazungumzo kati ya watu; mchezo wa kuigiza
2. ***Riwaya*** - hadithi ndefu ya kubuni yenye wahusika na mtiririko wa visa iliyoandikwa kwa lugha ya mfululizo
3. ***Shairi*** - mtungo wenye muundo na lugha ya kisanii unaofuata utaratibu wa vina na mizani, hisi au tukio juu ya jambo au maisha
4. ***Hadithi fupi*** - ni utungo wa kinathari ambao unazungukia tukio moja kuu na unaosimulia kisa kinachomhusu mhusika mmoja au wahusika wachache sana na unaozungumzia kipindi maalumu kwa mtindo wa kibanifu.
5. ***Ishara*** - alama au tendo linalowasilisha kitu halisi
6. ***Mizimu*** - vivuli vya watu waliokufa zamani vinavyowatokea watu kwenye ndoto
7. ***Mtandao*** - mfumo wa mawasiliano wa kielektroniki unaopitia katika kompyuta ambao watu huutumia kupata taarifa za aina mbalimbali au kuwasiliana
8. ***Wahusika*** – mtu, mnyama au kiumbe yeyote katika hadithi ya kubuni anayetenda mambo kadhaa kulingana na atakavyo mtunzi ili kuijenga hadithi yake
9. ***Sanaa*** - uhodari wa kuwasilisha hisia za mwanadamu kwa maandishi. Kwa mfano: kupitia kwa riwaya, tamthilia, hadithi fupi na mashairi andishi
10. ***Wasanii*** - watu walio na ujuzi wa kuchora, kutunga au kuchonga

**Zoezi la 1A, sentensi katika tungo yakinishi, ukurasa 4**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi, ziwe katika hali yakinishi na zihusishe msamiati walioueleza hapo awali.

***Kwa mfano:***

1. ***Tamthilia*** niliyoisoma inasisimua.
2. Sisi husoma ***riwaya*** kila muhula.
3. Nitatunga ***shairi*** lenye beti sita.
4. ***Hadithi fupi*** nzuri huwa na wahusika wachache.
5. Lugha ya ***ishara*** hutumiwa sana na wasanii wengi.
6. Mtoto aliota akikimbizwa na ***mizimu***.
7. Nitasakura kwenye ***mtandao*** ili kupata habari kamili.
8. Nimezoea kusoma vitabu vyenye ***wahusika*** wengi.
9. ***Sanaa*** ya uandishi inapendwa na wengi.
10. ***Wasanii*** wengi hutunga kazi zao wenyewe.

**Zoezi la 1B, sentensi katika tungo kanushi, ukurasa 4-5**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi kisarufi, zihusishe ukanusho wa sentensi katika hali yakinishi zilizo hapo juu.

***Kwa mfano:***

1. Tamthilia niliyoisoma haisisimui.
2. Sisi hatusomi riwaya kila muhula.
3. Sitatunga shairi lenye beti sita.
4. Hadithi fupi nzuri haiwi na wahusika wachache.
5. Lugha ya ishara haitumiwi sana na wasanii wengi.
6. Mtoto hakuota akikimbizwa na mizimu.
7. Sitasakura kwenye mtandao ili kupata habari kamili.
8. Sijazoea kusoma vitabu vyenye wahusika wengi.
9. Sanaa ya uandishi haipendwi na wengi.
10. Wasanii wengi hawatungi kazi zao wenyewe.

### Zoezi la 2, ukurasa 5

1. Fasihi andishi
2. lengo
3. hadhira
4. mali
5. wachache
6. Riwaya
7. mishororo

### Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 5

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi. Sharti hoja hizo zihusishe umuhimu wa fasihi andishi ya Kiswahili katika jamii.

***Kwa mfano:***

1. ***Kuiongoza na kuielekeza jamii:*** fasihi andishi ni nyenzo muhimu ya kuwaelekeza watu na kuwakanya dhidi ya kufanya jambo fulani. Kwa mfano, kupitia kwa mashairi andishi, tabia ambazo hazikubaliki katika jamii huweza kukejeliwa.
2. ***Fasihi andishi huhifadhi historia ya jamii fulani:*** kwa kusoma hadithi zinazohusu matukio halisi ya kihistoria katika jamii na pia kuhusu mila na tamaduni za jamii husika, historia ya jamii hiyo huhifadhiwa.
3. Huakisi na kuonyesha imani, itikadi na msimamo wa jamii fulani kuhusu mambo mbalimbali.
4. ***Huburudisha wanajamii:*** mashairi mengi husomwa kwa ajili ya burudani. Halikadhalika, riwaya na hadithi fupi pia husomwa kama njia ya kujiburudisha.
5. ***Hukuza na kuendeleza stadi za lugha miongoni mwa wanajamii:*** Kutokana na mbinu mbalimbali za uandishi ambazo hutumiwa na wasanii wengi, ukuzaji wa stadi ya utungaji na uandishi hukuzwa.
6. Hukuza na kuimarisha uhusiano kati ya wanajamii mbalimbali.

### Zoezi la sarufi, ukurasa 6

1. Wewe huenda shuleni kila siku.
2. Mimi ni mwanafunzi wa kidato cha sita.

3. Mwalimu wetu anafundisha somo la Fasihi.
4. Kwa nini unakariri shairi hilo polepole?
5. Riwaya huwa na wahusika wengi walio wa kubuni kuliko hadithi fupi.
6. Tamthilia ni utanzu mmojawapo katika tanzu za fasihi andishi ya Kiswahili.

**Zoezi la 3A, ukurasa 6**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu maana ya sentensi kisha watunge sentensi zao wenyewe. Sharti sentensi watakazotunga ziwe sahihi kisarufi na zihusishe nyakati tofautitofauti katika tungo yakinishi.

***Kwa mfano:***

1. Mimi nimeamka mapema.
2. Mama atakuja kesho.
3. Wewe ulisoma riwaya yangu.
4. Kalisa anaandika shairi.
5. Tamthilia mbili zitasomwa muhula huu.

**Zoezi la 3B, ukurasa 6**

1. *Mimi nimeamka mapema*. (Kiwakilishi, kitenzi, kielezi)
2. *Mama atakuja kesho.* (Nomino, kitenzi, kielezi)
3. *Wewe ulisoma riwaya yangu. (*Kiwakilishi, kitenzi, nomino, kivumishi)
4. *Kalisa anaandika shairi.* (Nomino, kitenzi, nomino)
5. *Tamthilia mbili zitasomwa muhula huu.* (Nomino, kivumishi, kitenzi, nomino, kivumishi)

**Zoezi la 3CH, ukurasa 6**

1. Mimi sijaamka mapema.
2. Mama hatakuja kesho.
3. Wewe hukusoma riwaya yangu.
4. Kalisa haandiki shairi.
5. Tamthilia mbili hazitasomwa muhula huu.

**Zoezi la 4, ukurasa 7**

Sentensi kamili ya Kiswahili:

1. Huwa na ujumbe uliokamilika na unaoeleweka.
2. Huwa na mpangilio maalumu wa maneno. Yaani: kiima na kiarifu (KN+KT).
3. Huwa na kauli ya vitenzi. Kwa mfano: tendwa, tendeka, tendea n.k.
4. Huhusisha hali ya vitenzi katika sentensi husika. Kwa mfano: yakinishi, kanushi, amrishi n.k.
5. Huwa na nyakati za vitenzi katika sentensi. Kwa mfano: uliopo, uliopita, ujao n.k.

**Zoezi la 5, ukurasa 7**

Sentensi zisizo kamili ni: 1, 4, 5 na 10. Sentensi hizi hazina vitenzi.

**Zoezi la 6, ukurasa 8**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi na jinsi watakavyozibainisha.

***Kwa mfano:***

1. Mwanafunzi hodari ametunga shairi refu.

    ***Sehemu ya kiima***: Mwanafunzi hodari

    ***Sehemu ya kiarifu:*** ametunga shairi refu

2. Riwaya niliyosoma ilikuwa ya kuvutia.

    ***Sehemu ya kiima:*** Riwaya

    ***Sehemu ya kiarifu:*** niliyosoma ilikuwa ya kuvutia

**Zoezi la makundi 1A, ukurasa 8**

1. Kiima (nomino), kiarifu (kitenzi, nomino, kivumishi).
2. Kiima (kiwakilishi), kiarifu (kitenzi, nomino, kivumishi).
3. Kiima (kiwakilishi), kiarifu (kitenzi, kielezi).
4. Kiima (nomino), kiarifu (kitenzi, kielezi, kielezi).
5. Kiima (nomino), kiarifu (kitenzi, nomino).

**Zoezi la makundi 1B, ukurasa 8**

1. ***Kitenzi:*** neno linaloarifu kuhusu jambo linalofanywa na nomino au linalofanyiwa nomino au kiwakilishi chake.
2. ***Nomino:*** neno linalotaja mtu, kitu, jambo, hali au mahali.
3. ***Kivumishi:*** neno linaloeleza zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi chake.
4. ***Kielezi:*** neno linaloeleza zaidi kuhusu vitenzi, vivumishi na hata vielezi vingine.

**Zoezi la 7, ukurasa 10**

| Sentensi | Kiima | Kiarifu |
|---|---|---|
| 1. *Kamana alitunga hadithi fupi sana.* | *Kamana* (nomino) | *alitunga* + *hadithi* + *fupi* + *sana*<br>(kitenzi, nomino, kivumishi, kielezi) |
| 2. *Mutoni ataigiza tamthilia jukwaani.* | *Mutoni* (nomino) | *ataigiza* + *tamthilia* + *jukwaani*<br>(kitenzi, nomino, kielezi) |
| 3. *Abayo na Mukunzi waliandika riwaya mwaka jana.* | *Abayo na Mukunzi* (nomino, kiunganishi, nomino) | *waliandika* + *riwaya* + *mwaka* + *jana*<br>(kitenzi, nomino, nomino, kielezi) |
| 4. *Gazeti lilipitisha riwaya yake jana.* | *Gazeti* (nomino) | *lilipitisha riwaya yake jana*<br>(kitenzi, nomino, kivumishi, kielezi) |
| 5. *Utaondoka lini?* | Ø U (kiambishi awali cha nafsi ya pili, umoja) | *Utaondoka lini?*<br>(kitenzi, kielezi) |

# Somo la 2: Utanzu wa hadithi fupi

## Vipindi 11-13: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kuchunguza kwa usahihi utanzu wa hadithi fupi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za hadithi fupi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 11-13;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ufafanuzi wa utanzu wa hadithi fupi. Hadithi fupi ni utanzu mojawapo wa fasihi andishi ambao huhusisha mgogoro mmoja mkuu na wahusika wachache ikilinganishwa na utanzu wa riwaya. Katika utanzu wa hadithi fupi, mandhari huwa machache ikilinganishwa na ilivyo kwenye riwaya na vilevile maudhui huwa machache. Vilevile, ni vyema mwalimu awe tayari kushughulikia sarufi katika somo hili. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kufahamu maana ya kirai pamoja na aina za virai. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kufahamu tofauti iliyopo kati ya sentensi na kirai katika Kiswahili. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi yafaayo kulingana na maelezo yaliyotolewa kwa kila zoezi husika.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wake maswali

mepesi kuhusiana na somo lililopita kuhusiana na fasihi andishi. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika somo lililotangulia. Baada ya haya, mwalimu atangulize somo hili kuhusu utanzu wa hadithi fupi. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha kuhusiana na michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 11. Maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye michoro hii? Wahusika wanaoonekana ni kina nani?* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona…."*. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na wanayoyaona katika michoro waliyopewa. Kwa mfano: "*Mimi ninaona msitu ulio na miti iliyokatwa. Mimi ninawaona wahusika ambao ni wanyama wakiwa katika mkutano."*

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea au wanachokiona katika michoro hiyo. Kutokana na michoro hiyo, wanafunzi wataweza kukisia hadithi fupi watakayosoma inahusu nini. Bila shaka hadithi hiyo inahusu wanyama na mazingira yao.

## 2.1 Kusoma na kufahamu

### *Hadithi fupi kuhusu uhifadhi wa mazingira*

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wasome kwa kimya kifungu cha habari walichopewa kuhusu kuyatunza mazingira. Wanafunzi wasome kifungu hicho kwa kimya huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho walichosoma ili kuhakikisha kuwa wamekielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Wanyama walifaidika vipi kutokana na mazingira? Uharibifu wa mazingira ulitekelezwa na kina nani?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu cha habari husika. Kwa mfano: *Wanyama walipata makao katika mazingira husika. Watu mbalimbali kama vile wawindaji, wavuvi, wachomaji makaa, wauza mbao na wauza kuni ndio waliotekeleza uharibifu katika mazingira husika.*

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti kifungu hicho ili kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe

wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hicho.

## Tathmini ya vipindi 11-13

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea ufafanuzi na uchambuzi wa hadithi fupi. Matukio, wahusika na dhamira ya mwandishi irejelewe katika kuhakiki iwapo wanafunzi wameuelewa utanzu huu wa hadithi fupi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kubaini sifa za utanzu wa hadithi fupi kwa kutumia kifungu cha habari walichopewa.

## Vipindi 14 -15: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na utanzu wa hadithi fupi;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na utanzu wa hadithi fupi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za hadithi fupi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 13-14;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ujifunzaji wa msamiati unaohusiana na kifungu cha habari kilicho kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 11-13 pamoja na utanzu wa hadithi fupi. Mwalimu aandae mifano ya hadithi fupi ambazo anaweza kuwapa wanafunzi wakazisoma darasani na kuchambua msamiati wake katika makundi. Pia, mwalimu anaweza kuandaa masimulizi kadhaa kuhusiana na hadithi fupi na kuwasimulia wanafunzi darasani. Hadithi fupi kadhaa zinaweza kurekodiwa na wanafunzi wakazisikiliza darasani au hata kuzitazama zikiigizwa kwenye runinga na baadaye kuchambua msamiati wake. Mwalimu anaweza kufanya maandalizi haya mapema kabla ya vipindi hivi.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilichotangulia.

## 2.2 Kujifunza msamiati wa hadithi kuhusu uhifadhi wa mazingira

Baada ya haya, mwalimu atangulize somo hili kuhusu msamiati unaohusiana na utanzu wa hadithi fupi.

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya waliopatana nao katika usomaji wao na jinsi msamiati huo ulivyotumiwa katika kifungu cha habari walichokisoma ambacho ni mfano wa hadithi fupi. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale inapohitajika. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua msamiati husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze msamiati waliopewa katika zoezi la 1 sehemu A pamoja na maelezo sahihi ya msamiati huo katika sehemu B kisha wauhusishe kwa usahihi msamiati huo na maelezo hayo.

Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika mfano wa hadithi fupi waliyosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba matumizi ya msamiati husika katika maongezi au maandishi ndiyo yatakayomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha sahihi.

## Tathmini ya vipindi 14-15

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mpya kuhusu utanzu wa hadithi fupi.

# Vipindi 16-18: Matumizi ya lugha

## a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu faida za kuyahifadhi mazingira;
- Kuandika ufupisho kwa kuzingatia taratibu zinazokubalika;
- Kuelewa jinsi ya kufupisha makala yoyote kwa usahihi.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za hadithi fupi za waandishi mbalimbali hasa kuhusu uhifadhi wa mazingira;
- Mtandao wa intaneti;
- Chati yenye kuonyesha taratibu za kuandika ufupisho;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 14-15;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha kuhusiana na uhifadhi wa mazingira. Mwalimu aandae michoro au picha zinazoonyesha shughuli mbalimbali za kuyahifadhi mazingira, kwa mfano: shughuli ya kupanda miti, shughuli ya kusafisha mazingira (*Umuganda*), shughuli ya kuwalinda wanyamapori katika mazingira yao n.k. Kwa upande mwingine, mwalimu anaweza kuandaa michoro ya kuonyesha shughuli za kuyaharibu mazingira kama vile kukata miti, kutupa takataka ovyo na kuchafua vyanzo vya maji ambayo hutumiwa na viumbe wote.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilichotangulia.

### 2.3 Majadiliano kuhusu uhifadhi wa mazingira

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wajadili kuhusu:

1. *Faida mbalimbali za kuhifadhi mazingira yetu.*
2. *Madhara ya kuharibu mazingira yetu.*
3. *Njia za kuhifadhi mazingira yetu.*
4. *Shughuli zinazoharibu mazingira yetu.*
5. *Umuhimu wa mazingira kwa wanyamapori.*

Mbali na hayo, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusimulia kuhusu shughuli mbalimbali ambazo wao wenyewe wameshawahi kutekeleza kuhusiana na uhifadhi au uharibifu wa mazingira. Kupitia majadiliano haya, mwalimu ataweza kuwaelekeza wanafunzi katika kutambua namna ya kuyahifadhi mazingira na shughuli za kuepuka zilizo na madhara kwa mazingira yetu.

## Tathmini ya vipindi 16-18

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kikundi kuhusiana na faida mbalimbali za kuhifadhi mazingira, madhara ya kuharibu mazingira, njia za kuhifadhi mazingira, shughuli zinazoharibu mazingira pamoja na umuhimu wa mazingira kwa wanyamapori.

Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kueleza umuhimu wa mazingira kwa viumbe wote.

## Vipindi vya 19-21: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kufahamu sifa bainifu za utanzu wa hadithi fupi;
- Kuchambua hadithi fupi kwa kuzingatia sifa zake bainifu;
- Kujadili kuhusu umuhimu wa utanzu wa hadithi fupi kwa jamii.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za hadithi fupi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;

- Rekodi za kazi za utanzu wa hadithi fupi;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 16;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia vipindi hivi kuhusu sifa bainifu za utanzu wa hadithi fupi pamoja na umuhimu wa hadithi fupi kwa jamii. Mwalimu anaweza kuandaa rekodi za hadithi fupi kadhaa ambazo wanafunzi wanaweza kuzisikiliza darasani kisha wakabaini sifa bainifu kutoka kwazo. Pia, mwalimu anaweza kuandaa masimulizi ya hadithi fupi ambayo anaweza kuwasimulia wanafunzi darasani. Wanafunzi wanaweza kupewa vitabu vya hadithi fupi wanazoweza kuzisoma kabla ya vipindi hivi.

### d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilichopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi ambalo wanafunzi walipewa katika kipindi kilichopita limesahihishwa na wanafunzi waliokuwa na matatizo wameelekezwa.

## 2.4 Majadiliano kuhusu sifa bainifu za hadithi fupi

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaongoze wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili waweze kujadiliana kuhusu sifa bainifu za utanzu wa hadithi fupi kama mojawapo wa utanzu wa fasihi andishi. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujadiliana kuhusu mambo ya kipekee ambayo yanautofautisha utanzu wa hadithi fupi na tanzu nyingine za fasihi andishi. Sehemu hii ipanue ujuzi wa wanafunzi kuhusu vipengele vyote vinavyoangaziwa katika utanzu wa hadithi fupi.

Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa hadithi fupi ni kama vile:

1. *Huwa ni fupi inayoweza kusomeka katika kikao kimoja.*
2. *Huwa na wahusika wachache.*
3. *Huwa na mhusika mmoja mkuu ambaye humwongoza msomaji.*
4. *Hushughulikia tukio moja muhimu katika maisha ya mhusika mkuu.*

5. *Huwa haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo kwa kulinganisha na tanzu nyingine za fasihi andishi.*

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wajitokeze mbele ya darasa ili wawaeleze wenzao kuhusu yale waliyoyajadili katika makundi yao. Wanafunzi wengine nao wasikilize matokeo ya majadiliano ya kila kikundi na wapewe muda wa kuchangia kwa yale yaliyozungumziwa huku wakiongozwa na mwalimu.

Baada ya majadiliano haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili wajadiliane kuhusu mambo muhimu yaliyopatikana katika hadithi fupi waliyosoma darasani kuhusu uhifadhi wa mazingira na kuyalinganisha na maisha yao ya kila siku. Wanafunzi waelezane kwa uwazi jinsi uhifadhi na uharibifu wa mazingira huyaathiri maisha yao ya kila siku.

Aidha, hatua hii ya kusikiliza na kuzungumza imehusisha pia majadiliano kuhusu umuhimu wa utanzu wa hadithi fupi kwa jamii. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kueleza faida za kuwepo kwa utanzu wa hadithi fupi kwa jamii mbalimbali. Wanafunzi wanaweza kujadiliana katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Umuhimu wa utanzu wa hadithi fupi ni sawa na umuhimu wa fasihi kwa ujumla. Kwa mfano, utanzu huu hutumika kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii mbalimbali, huelimisha, huburudisha, huasa, huonya, hukashifu tabia zisizokubalika katika jamii pamoja na kuweka wazi mifano mizuri ya wahusika wa kuigwa katika jamii kwa kurejelea maadili yao.

## Tathmini ya vipindi 19-21

Mwalimu atathmini iwapo ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, awaulize wanafunzi maswali ya kupima uwezo wao wa kurejelea sifa bainifu za utanzu wa hadithi fupi pamoja na umuhimu wa utanzu huu kwa jamii.

Vilevile, maswali mengine yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kujadiliana katika makundi kuhusu namna kazi za utanzu wa hadithi fupi walizosoma zinachangia katika kuboresha maisha yao ya kila siku. Mbali na hayo, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wamezielewa stadi za maisha kupitia maswali mbalimbali yanayohusiana na sifa bainifu za hadithi fupi pamoja na umuhimu wake kwa jamii.

# Vipindi vya 22-25: Sarufi (Virai)

## a) Malengo ya somo

- Kufahamu maana ya kirai;
- Kutambua aina za virai;
- Kutofautisha kirai na sentensi;
- Kueleza maana na muundo wa sentensi kamili katika Kiswahili;
- Kutunga sentensi yenye virai.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 16-18;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ajiandae kufundisha vipindi hivi. Mwalimu atunge mifano kadhaa ya virai mbalimbali pamoja na sentensi kamili katika Kiswahili. Mifano hii kadhaa itamwezesha kuwafundisha wanafunzi sehemu hii ya sarufi kuhusu virai pamoja na sentensi kamili katika Kiswahili. Iwapo mwalimu ana wanafunzi walio na matatizo ya kuona, basi itambidi kutunga na kuandika virai mbalimbali na sentensi kadhaa kwenye breli kwa manufaa ya wanafunzi hao. Kwa wanafunzi walio na matatizo ya kusikia, lugha ishara inaweza kutumika pamoja na kuiandika mifano ya mwalimu ubaoni.

## d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali kuhusu kipindi kilichopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu kipindi hicho. Mwalimu achukue fursa hii ya utangulizi ili kuwaomba wanafunzi kusahihisha mazoezi waliyopewa kuhusiana na kipindi kilichopita. Mwalimu aendeleze somo kwa kuwaomba wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kwa kila zoezi.

## 2.5 Maana ya kirai

Ujifunzaji wa sarufi katika hatua hii uchukuliwe kama mwendelezo wa yale yaliyofundishwa katika sehemu ya sarufi kuhusu sentensi kamili katika masomo yaliyotangulia kwenye viwango vya hapo awali. Kwa hivyo, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa maana ya sentensi kamili katika Kiswahili pamoja na miundo yake. Ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika kipengele hiki, mwalimu awaombe wanafunzi watunge sentensi mbalimbali zilizo na miundo mbalimbali ili kubaini sentensi zilizo kamili na zile zisizo kamili.

***Kwa mfano:***

1. *Mama yangu anapika chakula cha wageni. (Sentensi kamili)*
2. *Mwalimu pamoja na wanafunzi wake. (Sentensi isiyo kamili)*
3. *Mimi na nyanya yangu mzee. (Sentensi isiyo kamili)*
4. *Wao wanatembea kuelekea sokoni. (Sentensi kamili)*

Kutokana na zoezi hili, wanafunzi wataweza kutambua kuwa muundo wa sentensi kamili katika Kiswahili sharti uhusishe neno kuu ambalo ni kitenzi. Wanafunzi watunge sentensi kadhaa katika makundi yao, sentensi ndefu na fupi ili kuelewa zaidi kuhusiana na miundo ya sentensi kamili.

Baadaye katika makundi yao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuzichunguza sentensi zilizo katika *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 16* kisha wajadiliane kuhusu sehemu zinazounda sentensi hizo. Kwa mfano: *Mtoto mmoja alizaliwa jana*. Katika sentensi hii, kuna kiima na kiarifu ambapo kiima ni '*mtoto mmoja*' na kiarifu ni '*alizaliwa jana*'. Hii ni sentensi kamili kwa sababu inahusisha kitendo cha kuzaliwa kwa mtoto. Sehemu inayounda kiima ndiyo ***kirai nomino*** kwa sababu sehemu hii inahusisha nomino (ya mtenda, mtendwa, mtendewa au kitendwa, kitendewa) pamoja na kivumishi chake.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kujadili kuhusiana na sehemu za sentensi mbalimbali walizotunga ambazo ni virai nomino. Baada ya haya, mwalimu anaweza kuwashirikisha wanafunzi katika kutambua aina nyingine za virai kama vile: virai vitenzi na virai vivumishi Wanafunzi watunge sentensi kadhaa zenye kuonyesha sehemu za virai mbalimbali.

***Kwa mfano:***

1. *Mtoto mnene alikuwa anakula.*

   '*Mtoto mnene'* ni kirai nomino na '*alikuwa anakula'* ni kirai kitenzi.

2. *Mama amevaa viatu vizuri sana.*

   *'Mama'* ni kirai nomino, '*amevaa viatu'* ni kirai kitenzi na '*vizuri sana'* ni kirai kivumishi.

3. *Wazee na vijana wamefika mkutanoni.*

   *'Wazee na vijana'* ni kirai nomino na '*wamefika mkutanoni'* ni kirai kitenzi.

Baadaye, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamepata ujuzi kamili katika kutambua aina mbalimbali za virai na kuweza kuzitungia sentensi sahihi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 6 katika makundi ya wanafunzi wawili ambapo wanafunzi wanatakiwa kutofautisha sentensi kamili na virai.

Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na maelezo ya mwalimu yatilie mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwishowe, mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la 7 katika asehemu hii ambapo wanahitajika kuainisha sentensi na virai katika mifano waliyopewa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi hili limesahihishwa kabla ya kipindi kijacho.

## Tathmini ya vipindi 22-25

Mwalimu ahitimishe vipindi hivi kwa kuuliza maswali yanayodhamiria kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa maana ya kirai na aina zake mbalimbali pamoja na kuainisha virai katika sentensi. Wanafunzi pia waulizwe maswali mepesi ya kubaini iwapo wamefahamu tofauti kati ya sentensi kamili na virai. Wanafunzi nao, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kwa kudhihirisha iwapo wameelewa mambo yote muhimu yaliyotakikana kuzingatiwa katika vipindi hivi.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Neno moja au fungu la meneno ambayo hayana muundo wa kiima na kiarifu huitwa kirai. Aghalabu kirai huwa na neno moja kuu ambalo ndilo huwa msingi wa kirai kinachohusika. Aina za virai ni kama vile:

1. **Kirai nomino:** Kirai hiki hutawaliwa na nomino, viwakilishi vyake, vivumishi na viunganishi. Kwa mfano:
    a) Juma anasoma.
    Juma ni kirai nomino kilichoundwa kwa nomino moja pekee.
    b) Walimu na wanafunzi wanaimba.
    Walimu na wanafunzi ni kirai nomino kilichoundwa kwa nomino mbili zilizounganishwa kwa kiunganishi na.
    ch) Wanawake shupavu wametuzwa.
    Wanawake shupavu ni kirai nomino kilichoundwa kwa nomino na kivumishi.
    d) Sisi hatutaki kula wali.
    Sisi ni kirai nomino kilichoundwa kwa kiwakilishi pekee.
    e) Vyake vyote vimepotea.
    Vyake vyote ni kirai nomino kilichoundwa kwa kiwakilishi na kivumishi.
2. **Kirai kivumishi:** Kirai hiki hutawaliwa na kivumishi. Kirai hiki huundwa na kivumishi na kielezi:
    a) Mzuri sana
    b) Mweusi kupindukia
3. **Kirai kitenzi:** Kirai hiki hutawaliwa na kitenzi. Kirai hiki huundwa na kitenzi, nomino, kivumishi na kielezi. Kwa mfano:
    a) *Mtoto <u>alikuwa akiandika.</u>*
    b) *Nyanya <u>anakula wali.</u>*
    ch) *Kaka yake <u>anaimba vizuri.</u>*

## 2.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kufanikisha ujifunzaji wa pamoja, zoezi la ziada litolewe kwa wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kujibu swali hili:

*Taja aina ya virai vinavyopatikana katika sentensi hizi:*

**Kwa mfano:** Vitabu vichafu vimeuzwa leo.

**Jibu:** '*Vitabu vichafu'* ni kirai nomino na '*vimeuzwa leo'* ni kirai kitenzi.

1. Warefu wawili wamekamatwa.
2. Wazee na vijana wamesimama.
3. Mama hajawahi kula samaki.
4. Yeye ni mwenye kupenda kula.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

***Kwa mfano:***

1. Warefu wawili wamekamatwa.

   '*Warefu wawili'* ni kirai nomino na '*wamekamatwa* ni kirai kitenzi.
2. Wazee na vijana wamesimama.

   '*Wazee na vijana'* ni kirai nomino na '*wamesimama'* ni kirai kitenzi.
3. Mama hajawahi kula samaki.

   'M*ama'* ni kirai nomino na '*hajawahi kula samaki'* ni kirai kitenzi.
4. Yeye ni mwenye kupenda kula

   '*Yeye* ni kirai nomino na '*mwenye kupenda kula'* ni kirai kivumishi.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi mbili mbili ambazo zina zirai nomino na virai vitenzi.

**Kwa mfano:** *Simba mkali huvutia watalii.*

*'Simba mkali*' ni kirai nomino na '*huvutia watalii'* ni kirai kitenzi.

## 2.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 13

1. Kware, korongo, tai, mwewe na heroe.
2. Kulikuwa na wawindaji, wavuvi, wauza kuni, wauza mbao na wachoma makaa ambao waliuvamia msitu wa Nyarume kwa shughuli zao za kujinufaisha.
3. Misitu ni makazi ya wanyamapori kwa kuwa wao huishi humo na wengine katika mapango yaliyo misituni. Miti iliyo misituni huleta mvua ambayo maji yake hunywewa na wanyamapori.
4. Wanyamapori huwavutia watalii kutoka kote duniani kuja kuzuru nchi yetu kwa ajili ya kuwaona na kuiletea nchi yetu pesa zinazosaidia katika maendeleo mbalimbali nchini.
5. Huwahifadhi wanyamapori ambao watalii huja nchini kuwaona na kulipa pesa ambazo hutumika kuendeleza nchi.
6. Wanyamapori hukosa makazi na kufa. Wanyama wengine huhamia kwenye maeneo ya mbali na pale ambapo makao yao yameharibiwa.
7. Hupunguza idadi ya wanyamapori kutokana na wao kuuawa. Hupunguza idadi ya watalii wanaozuru nchi na maendeleo ya nchi huathirika kwa sababu pesa za kigeni kutoka kwa watalii hupungua.
8. Watu hukosa maji ya kunywa, kuoga, kupika na kufua nguo. Viumbe wanaoishi majini watakosa makao kwa sababu ya ukame. Maji ni uhai kwa viumbe wote pamoja na mimea.
9. Miti ni makao ya ndege, huleta mvua, hutupatia kuni na makaa na pia hutupatia mbao. Maji ni makao ya wanyama wanaoishi majini, hutumika katika shughuli za nyumbani za kuosha, kunywa na kupika na pia maji hunyunyiziwa mimea.
10. a) Bwana Bakame ni mwenye bidii kwa kuwa amefanya kazi kwa miaka mingi. Ni mpole, mcheshi na mwenye hekima kwa sababu watu wengi walimpenda sana. Yeye ni kiongozi bora kwa kuwa anachaguliwa na wapiga kura wengi sana.

    b) Mlinzi mkuu wa msitu Nyungwe ni mwenye hekima na maarifa. Anakanya dhidi ya kuharibu mazingira na pia anatoa maelezo kuhusu umuhimu wa wanyamapori.

**Zoezi la msamiati, ukurasa wa 13-14**

Mwalimu atathmini maelezo ambayo yatatolewa na wanafunzi kuhusu msamiati mpya kutoka kwenye kifungu walichokisoma. Pia, mwalimu atathmini sentensi zitakazotungwa na wanafunzi. Ahakikishe kuwa ni sahihi na zimezingatia muktadha wa matumizi ya msamiati husika katika kifungu walichosoma hapo awali.

***Kwa mfano:***

1. ***Wanyamapori -*** viumbe aghalabu wenye uhai na ambao wana miguu minne na huishi porini
2. ***Madhara -*** jambo lenye kuleta majanga au uharibifu

**Matumizi katika sentensi:**

1. ***Wanyamapori*** ni vivutio muhimu katika uchumi wa nchi.
2. Ukataji wa miti una ***madhara*** mengi kwa binadamu.

**Zoezi la 1, ukurasa 14**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. - J | 2. - F | 3. - G | 4. - D |
| 5. - H | 6. - B | 7. - CH | 8. - E |
| 9. - A | 10. - I | | |

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 14**

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika majadiliano ya makundi yao. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. -

***Kwa mfano:***

1. Faida mbalimbali za kuhifadhi mazingira yetu ni kama vile: *Kuepuka magonjwa mbalimbali, kupata mazao ya shambani, kupata maji safi ya matumizi* n.k.
2. Madhara ya kuharibu mazingira yetu ni kama vile: *Kukosa maji safi ya kutumiwa na viumbe na mimea, kukosa chakula na hata kushikwa na magonjwa mbalimbali.*
3. Njia za kuhifadhi mazingira yetu ni kama vile: *Kupanda miti mingi, kufyeka nyasi ndefu zilizo karibu na makao ya binadamu, kuepuka kutupa takataka ovyo* n.k.

4. Shughuli zinazoharibu mazingira yetu ni kama vile: *Kutupa takataka ovyo ovyo, kukata miti ovyo ovyo, kumwaga kemikali na uchafu kwenye vianzo vya maji* n.k.
5. Umuhimu wa mazingira kwa wanyamapori ni kama vile: *Wanyamapori hupata makao, chakula na hata maji safi ya kunywa.*

## Zoezi la 2, ukurasa 15

### *Mfano wa ufupisho*

*Bwana Bakame aliishi katika msitu wa Nyarume uliokuwa na ndege na wanyamapori wengi. Kando ya msitu huo kulikuwa na vijiji vya watu wengi waliomfahamu Bwana Bakame ambaye alikuwa na uwezo wa kuwaelekeza wageni wote katika msitu huo kwa kuwa alikuwa ndiye kiongozi huko. Msitu ulikumbwa na shambulizi baada ya miaka miwili na wanyama wengi walifariki. Hili lilisababisha kuandaliwa kwa mkutano mkubwa wa wanyamapori wote msituni humo. Katika mkutano huo, mlinzi mkuu aliwapa pole wanyama kwa shambulizi lililowakumba. Baadaye, aliwapa ushauri kuwa ni muhimu kuyatunza mazingira. Aliwaonya dhidi ya kukata miti kwa sababu huku kuliwakosesha wanyamapori makazi. Baadaye, aliwaeleza umuhimu wa wanyamapori kwa kusema kuwa walikuwa kivutio cha watalii ambao walileta pesa nyingi ili kuwaona wanyamapori hao. Mwisho, alitoa ushauri kuhusu maji na umuhimu wake na akaomba kuwa maziwa na mito ilindwe. Bwana Bakame alikamilisha mkutano kwa kumshukuru mlinzi mkuu na kuwaomba wanayamapori kusahau shambulizi lililowakumba na kuwasisitizia uimarishaji na ushirikiano mwema na watu wote katika shughuli za kuhifadhi msitu.*

## Zoezi la 3, ukurasa 16

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu sifa bainifu za hadithi fupi. Wanafunzi watoe maelezo yatakayolenga hoja zifuatazo:

1. Hadithi fupi huwa na wahusika wachache. Huwa na mhusika mmoja mkuu ambaye humwongoza msomaji.
2. Hadithi fupi huwa fupi na inaweza kusomeka katika kikao kimoja.
3. Hadithi fupi hushughulikia tukio moja kuu katika maisha ya mhusika mkuu.
4. Hadithi fupi huwa haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo ikilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi andishi.
5. Hadithi fupi huhusisha usimulizi wa moja kwa moja.

6. Hadithi fupi hulenga sana kuibua hisia za msomaji kuliko kuchochea fikira zake.
7. Hadithi fupi huenda haraka kimatendo, kiwakati, kimasafa na kimatukio.

**Zoezi la 4, ukurasa 16**

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi. Wanaweza kutaja hoja kama vile:

1. Ukataji wa miti ili kupata kuni, makaa na mbao husababisha uharibifu wa mazingira. Katika maisha ya kila siku, kuna watu ambao hujiingiza katika shughuli hizi za ukataji miti ovyo na kuishia kuyaharibu mazingira yetu. Hili linahitaji kurekebishwa.
2. Katika maisha yetu ya kila siku, panapotokea janga au shida fulani katika jamii, wanajamii huitwa kwenye mkutano ili kujadiliana kuhusu suluhisho la tatizo lililowakumba. Wanyamapori wote wanaitwa kwenye mkutano wanapokumbwa na shambulizi la mazingira yao kuharibiwa.
3. Mazingira ya msitu wa Nyarume yalianza kuhifadhiwa vyema tena baada ya kukumbwa na shambulizi la uharibifu. Katika maisha ya kila siku, mtu anapofanya kosa ni muhimu kurekebisha na kuanza upya tena.
4. Maji ni muhimu katika shughuli za binadamu za kila siku kama vile: kupika, kuoga na kusafisha mazingira n.k. Pia, maji ni muhimu kwa mimea na viumbe wengine.

**Zoezi la 5, ukurasa 16**

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi kuhusu umuhimu wa hadithi fupi kwa jamii.

***Kwa mfano:***

1. Huburudisha.
2. Huelimisha.
3. Hupitisha ujumbe kuhusu jamii fulani.
4. Hututahadharisha kuhusu mazingira yetu.
5. Hushauri wanajamii dhidi ya mambo mbalimbali.
6. Huhifadhi utamaduni na historia ya jamii fulani.

### Zoezi la sarufi, ukurasa 16

Mwalimu atathmini ugunduzi wa wanafunzi kuwa sehemu zilizopigiwa mistari ni ***virai***.

### Zoezi la 6, ukurasa 17

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

***Sentensi*** ni fungu la maneno lenye muundo wa kiima na kiarifu na huwa na maana kamili ilhali kirai ni kipashio kinachoundwa kwa neno moja au zaidi na hakina mwingiliano wa kimuundo wa kiima na kiarifu. Kirai pia huwa hakihitaji kitenzi (isipokuwa kirai kitenzi) ilhali sentensi sharti iwe na kitenzi.

***Kwa mfano:***

***Sentensi:*** Mwalimu mrefu anaandika ubaoni.

***Virai:*** *Mwalimu mrefu* (kirai nomino), *anaandika ubaoni* (kirai kitenzi)

### Zoezi la 7, ukurasa 18

1. Sentensi
2. Kirai
3. Sentensi
4. Kirai
5. Kirai

### Zoezi la makundi, ukurasa 18

1. Mchungaji wa nyumba
2. Walimu wetu
3. Babaye mlinzi wa pori
4. Rais wa Rwanda
5. Msichana mrefu mwembamba

# Somo la 3: Utanzu wa riwaya

## Vipindi vya 26-28: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha sura moja ya riwaya husika kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kuelewa ujumbe wa kifungu cha sura moja ya riwaya husika;
- Kutaja aina ya wahusika waliotumika katika kifungu husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 19-22;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ufafanuzi wa utanzu wa riwaya ambao ni mojawapo wa tanzu za fasihi andishi. Kifungu kilicho katika *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 19-22 ni sura moja kutoka katika riwaya iitwayo ***'Utengano'*** iliyoandikwa na Said A. Mohamed ambaye ni mwandishi maarufu wa kazi mbalimbali za kifasihi. Kifungu hicho cha sura moja ya riwaya kimehusisha wahusika mbalimbali pamoja na kushughulikia maudhui mbalimbali. Kila mhusika ana sifa mbalimbali. Mandhari mbalimbali pia yamehusishwa kama vile: nyumbani, mjini n.k. Mwalimu aandae mpangilio wa usomaji wa kifungu walichopewa. Ikiwezekana, mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi wasome riwaya ya ***'Utengano'*** kabla ya kuanza kwa funzo hili.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Kisha, mwalimu atangulize somo hili kuhusu utanzu

wa riwaya kwa kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali kama vile: *Umewahi kusoma riwaya gani? Riwaya hiyo imeandikwa na nani? Riwaya hiyo ilihusu nini? Riwaya hiyo ilikuwa na wahusika wa aina gani?* n.k. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kwa kueleza aina za riwaya ambazo wamewahi kusoma, waandishi wa riwaya hizo, aina za wahusika katika riwaya hizo pamoja na jumbe za riwaya hizo.

Mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili watazame mchoro ulio kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 19. Mwalimu awaulize wanafunzi swali kuhusiana na mchoro huo. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye mchoro huu?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu swali waliloulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona..."* Wanafunzi kwa upande wao, wajibu swali la mwalimu. Kwa mfano, "*Mimi ninaona umati wa watu*." Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha mchoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea au kinachoonekana katika mchoro huo. Mwalimu anaweza kuwaonyesha wanafunzi michoro au picha za mikutano mbalimbali ya kisiasa hasa kuhusiana na wagombeaji kuomba kura kutoka kwa wananchi.

## 3.1 Kusoma na kufahamu

### *Sura moja ya riwaya kuhusu uchaguzi wa viongozi*

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wasome kwa kimya kifungu cha sura moja ya riwaya ya ***'Utengano'*** kilicho katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 19-22. Wanafunzi wasome kwa kimya huku wakitambua na kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichosoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwauliza: *Wagombeaji walikuwa kina nani? Mkutano huu ulifanyika wapi? Umati wa watu ulimshangilia nani zaidi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma kutoka kwenye kifungu walichopewa. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kujibu: *Wagombeaji walikuwa Bwana Maksuudi, Kijana Siwa na Bwana Zanga. Mkutano ulifanyika katika uwanja wa Uhuru. Umati ulimshangilia zaidi kijana Siwa*. Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilichopo na kukielewa, mwalimu

awaombe wanafunzi wasome kwa sauti kifungu hicho kwa kuhakikisha kuwa wanatamka maneno kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali ya ufahamu waliyopewa katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 22. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo walitatizika katika kujibu kwao. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hicho.

## Tathmini ya vipindi 26-28

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kueleza maana ya riwaya pamoja na kuchambua jumbe za riwaya mbalimbali walizowahi kusoma.

## Vipindi vya 29-30: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kufafanua msamiati mpya kutokana na sura ya riwaya husika;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali;
- *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 23;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu kujenga uelewa zaidi kuhusiana na msamiati wa muktadha wa sura moja ya riwaya waliyosoma hapo awali. Uelewa huu unahusisha utambuzi wa maana na matumizi ya msamiati husika katika kutunga sentensi sahihi kisarufi pamoja na kuutumia katika maongezi ya kila siku. Riwaya huwa ni hadithi ndefu iliyo na wahusika wengi pamoja na msuko uliosukwa kwa migogoro kadhaa yakiwemo maudhui. Riwaya mbalimbali hushughulikia maudhui mbalimbali kwa kurejelea maisha ya wanajamii katika jamii.

## d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awachangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kama vile: *Je, umewahi kusoma riwaya gani? Riwaya hiyo ilihusu nini?* Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya.

### 3.2 Kujifunza msamiati kutokana na sura moja ya riwaya husika

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuwaomba wafanye zoezi la 1 kwa kujadili maana za msamiati mpya ambao walipatana nao katika usomaji wa kifungu cha sura moja ya riwaya walichopewa kutoka kwenye riwaya ya '***Utengano***'. Wanafunzi waeleze maana ya msamiati husika kwa kuzingatia jinsi ulivyotumiwa katika kifungu walichokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale watakapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua maana ya msamiati husika. Baadaye, wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati waliojadili. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kubaini usarufi na usahihi wa sentensi ambazo watatunga.

Baada ya hapo, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 2 na wachague maana sahihi ya msamiati huo kutoka kwenye majibu waliyopewa kwenye mabano. Mwisho, mwalimu awaombe wanafunzi wajadili maana za msamiati huo uliopigiwa mistari.

Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wasahihishe kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe tena kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika kifungu walichosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha rasmi na sahihi.

## Tathmini ya vipindi 29-30

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa katika kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kufafanua msamiati wa kifungu cha riwaya walichopewa pamoja na msamiati wa jumla utumikao katika utanzu wa riwaya pamoja na kutumia msamiati huo waliojifunza katika kutunga sentensi sahihi kisarufi na katika maongezi yao ya kila siku.

## Vipindi vya 31-33: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili sifa bainifu za utanzu wa riwaya;
- Kueleza tofauti kati ya riwaya na hadithi fupi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali;
- Kazi za hadithi fupi za waandishi mbalimbali;
- Wanafunzi wenyewe;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 24;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### a) Maandalizi ya somo

Sehemu hii itahusisha majadiliano ya wanafunzi katika makundi mbalimbali. Wanafunzi watapewa nafasi ya kutoa masimulizi yao wenyewe kuhusu riwaya mbalimbali pamoja na hadithi fupi walizowahi kusoma ili kuweza kujadili uhusiano na tofauti kati ya tanzu hizi mbili za fasihi andishi. Mwalimu anaweza kuandaa kazi kadhaa za riwaya na hadithi fupi za waandishi mbalimbali ambazo anaweza kuziwasilisha darasani. Pia, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi kazi kadhaa za riwaya na hadithi fupi ili waweze kuzisoma kabla ya funzo hili ili iwe rahisi kwao kulinganisha tanzu hizi mbili kwa kutumia mifano mbalimbali.

### b) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze kipindi kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha kuhusu kazi za hadithi fupi pamoja na riwaya walizowahi kusoma. Mifano ya maswali hayo ni kama vile: *Msuko (mtiririko) wa riwaya uliyowahi kusoma ulikuwa wa aina gani? Msuko (mtiririko) wa hadithi fupi uliyowahi kusoma ulikuwa wa aina gani?* n.k.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

## 3.3 Majadiliano kuhusu sifa bainifu za riwaya

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha awaombe wajadili kuhusu:

1. *Sifa bainifu za riwaya.*
2. *Tofauti kati ya riwaya na hadithi fupi.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kubaini sifa bainifu za riwaya kama vile:

1. Riwaya ni utanzu wa fasihi andishi.
2. Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo huchukua muda mrefu kuandikwa na huwa na wahusika wengi na wa aina nyingi. (wakuu na wadogo)
3. Mhusika mkuu ndiye huwakilisha mawazo muhimu ya mwandishi.

4. Katika riwaya, matukio mara nyingi huwa ni tata. Migogoro mingi hujengwa ili kukuza maudhui na mtiririko.
5. Mtunzi wa riwaya huwa hayafahamu maoni ya wasomaji, yaani hujitenga na hadhira.
6. Riwaya huwa na maneno mengi sana, zaidi ya kurasa sitini.
7. Riwaya huwa na maelezo ya simulizi kulingana na vile hadithi inavyotokea kiwakati na kimasafa.
8. Riwaya huwa na maelezo ya wahusika kuhusu wasifu wao, mavazi yao, tabia zao, sifa na dosari, matendo yao yanavyoathiri nafsi zao na kuwaathiri wahusika wengine.
9. Riwaya huwa na urefu wa kutosha kuyashughulikia mahitaji ya mtunzi.
10. Riwaya huchunguza kwa kina jamii inavyosawiriwa.

Katika makundi yao, mwalimu awashirikishe wanafunzi kuchunguza namna sifa bainifu walizozijadili hapo awali zinavyojitokeza katika kazi za riwaya wanazozifahamu au walizozisoma.

Majadiliano haya yote yatawawezesha wanafunzi kuelewa ubainifu wa utanzu wa riwaya ukilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi andishi. Zoezi hili pia litawasaidia wanafunzi kuzifahamu tofauti zilizopo kati ya utanzu wa riwaya na utanzu wa hadithi fupi ambazo ndizo tanzu zinazokaribiana kwa baadhi ya sifa zao. Baadhi ya sifa zinazofanana kati ya tanzu hizi mbili bi kuwa: hizi ni tanzu za fasihi andishi ambazo huhusisha utunzi wa hadithi ambazo huandikwa kwa njia ya kinathari (mfululizo wa matukio).

## Tathmini ya vipindi 31-33

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti ya kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea sifa bainifu za utanzu wa riwaya ili kutathmini iwapo wanafunzi wameelewa funzo hili. Kupitia kwa majadiliano ya wanafunzi pamoja na mawasilisho yao, wanafunzi wakuze ujasiri wao wa kuzungumza mbele ya watu na pia matumizi yao ya lugha rasmi na sahihi yaimarike zaidi. Pia, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ili kubaini iwapo wameelewa tofauti na mfanano uliopo katika ya utanzu wa riwaya na utanzi wa hadithi fupi.

# Vipindi vya 34-36: Kusikiliza na kuzungumza

## a) Malengo ya somo

- Kujadili mambo muhimu yaliyojitokeza katika kifungu husika;
- Kujadili tabia za wahusika kutokana na kifungu husika;
- Kueleza aina mbalimbali za wahusika katika fasihi andishi.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 24;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya funzo hili, mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika funzo hili kama vile: chati zenye kuonyesha aina mbalimbali za wahusika, uchambuzi wa maudhui mbalimbali pamoja na maigizo yaliyorekodiwa ya riwaya atakayoteua mwalimu ambayo wanafunzi wanaweza kuitazama darasani au katika ukumbi wao kisha waijadili. Kupitia kwa vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua na kuelewa kwa undani vipengele vinavyohusiana na utanzu wa riwaya kama vile wahusika na maudhui.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na waliyojifundisha katika kipindi kilichopita. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

## 3.4 Majadiliano kuhusu maudhui

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wajadiliane kuhusu mawazo muhimu (maudhui) yaliyopatikana katika kifungu cha sura moja ya riwaya walichosoma hapo awali kuhusu mkutano wa kisiasa uliofanyika katika uwanja wa Uhuru (kutoka kwenye riwaya ya '***Utengano'****)*. Baadaye, wanafunzi wayalinganishe mawazo hayo makuu na shughuli za maisha yao ya kila siku. Mwalimu ahakikishe kuwa kila kundi linapewa nafasi na wakati wa kuyawasilisha majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao. Mwalimu atumie nafasi hii kusahihisha makosa ya kimatamshi ya wanafunzi wakati wa mawasilisho yao. Kupitia kwa mawasilisho haya, wanafunzi wanapata fursa ya kukuza uwezo wao wa kuzungumza mbele ya watu kwa ujasiri na kwa lugha sahihi kisarufi.

Baada ya hapa, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika makundi yao wajadili kuhusu tabia za wahusika kutoka kwenye kifungu cha sura moja ya riwaya waliyosoma hapo awali kisha wazilinganishe tabia hizo na tabia za watu mbalimbali wanaotangamana nao katika maisha yao ya kila siku. Kila kundi lipewe nafasi na muda wa kuyawasilisha majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao. Wanafunzi wanaweza kuelezana jinsi viongozi hutafuta kura msimu wa uchaguzi unapokaribia. Wananchi nao huwa na kibarua kigumu cha kumchagua kiongozi mmoja kati ya wagombeaji kura wengi ambao hujitokeza kuwaomba kura. Wanafunzi wajadili jinsi siasa huendelezwa katika maeneo mbalimbali wanayotoka.

Mwalimu afuatilie kwa karibu majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao pamoja na mawasilisho yao hapo baadaye. Mawasilisho ya makundi mbalimbali ya wanafunzi yafanywe kwa lugha sanifu ya Kiswahili, wanafunzi wawe na motisha na mwalimu awahimize kuipenda lugha ya Kiswahili na kuipenda fasihi. Kutokana na mawasilisho ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaombe wanafunzi wasome riwaya nzima ya '*Utengano'* (iliyoandikwa na Said Mohamed) kisha wajadiliane kuhusu maudhui mbalimbali pamoja na tabia za wahusika katika riwaya hiyo nzima.

Baadhi ya maudhui katika riwaya hii ni kama vile: ufisadi, malezi, elimu, ukahaba, utovu wa maadili katika jamii, uongozi, uzazi miongoni mwa mengine mengi. Kutokana na riwaya hii, wanajamii wanashauriwa kuepuka utovu wa maadili katika jamii kwani matokeo ya utovu huo huwa ni mbaya kupindukia. Matokeo haya yanaweza kuwa hata mauti au ulemavu.

Baadhi ya wahusika katika hadithi hii ni Maimuna ambaye ndiye mhusika mkuu, Bwana Maksuudi, Kazija, Musa, Bi Tamima, Siwa miongoni mwa wengine. Wahusika wenye sifa chanya wanaweza kuigwa. Wahusika walio na sifa hasi wanatumiwa kuwaonya wanajamii dhidi ya kuwa na tabia kama zao zinazoweza kuwaletea maafa.

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashirikishwa katika kusoma huku na kujadiliana katika makundi yao. Mwalimu akosoe makosa ya kimatamshi pamoja na makosa mengine yanayoweza kujitokeza wakati wa mawasilisho ya wanafunzi.

## Tathmni ya vipindi 34-36

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kwa lengo la kuchunguza iwapo wanaweza kutambua na kueleza maudhui pamoja na tabia za wahusika mbalimbali katika utanzu wa riwaya pamoja na kazi nyingine za kifasihi. Kazi mbalimbali za kifasihi za utanzu wa riwaya zinaweza kutumika katika funzo hili ili kumpa mwanafunzi uelewa mpana wa maudhui na wahusika.

## Vipindi vya 37- 40: Sarufi (Kirai kivumishi)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua maana ya kirai kivumishi;
- Kufahamu tofauti kati ya kirai nomino na kirai kivumishi;
- Kutambua miundo mbalimbali ya kirai kivumishi;
- Kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia virai vivumishi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Chati yenye miundo mbalimbali ya virai vivumishi;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 25-27;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini maana ya kirai kivumishi pamoja na miundo mbalimbali ya kirai kivumishi. Pia, mwalimu alenge kuwaelekeza wanafunzi kubaini tofauti kati ya kirai nomino na kirai kivumishi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: chati zinazoonyesha miundo mbalimbali ya kirai kivumishi pamoja na sentensi kadhaa zilizo sahihi kisarufi zilizotumia virai vivumishi katika miundo yake mbalimbali. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hivi hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu kipindi kilichopita cha sarufi kuhusu tofauti kati ya kirai na sentensi pamoja na maana na miundo mbalimbali ya kirai nomino. Mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia kirai nomino katika miundo yake mbalimbali. Kwa mfano:

1. ***<u>Mtoto mwerevu</u>*** *amepita mtihani*. Katika sentensi hii, '*mtoto mwerevu'* ni kirai nomino kilichoundwa kwa nomino (*mtoto*) na kivumishi (*mwerevu*).
2. ***<u>Mwalimu</u>*** *anafundisha vizuri*. Katika sentensi hii, '*mwalimu'* ni kirai nomino kilichoundwa kwa nomino moja (*mwalimu*).

Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilichopita.

## 3.5 Kirai kivumishi

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awaombe wachunguze sehemu zilizopigiwa mistari katika sentensi walizopewa na hapo baadaye waelezane sehemu hizo zimeundwa kwa kutumia maneno gani. Zoezi hili litawasaidia wanafunzi kuweza kubaini maana ya kirai kivumishi pamoja na miundo yake mbalimbali. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua kuwa sehemu zote zilizopigiwa mistari katika sentensi walizopewa ni miundo mbalimbali ya kirai kivumishi. Kwa mfano:

1. *Baba alitusimulia hadithi* ***nzuri kabisa****.*

(Fungu la maneno ***'nzuri sana'*** ni kirai kivumishi ambacho kimeundwa kwa ***'kivumishi + kielezi')****.* Neno kuu linalotangulia katika fungu hili la maneno ni kivumishi ***nzuri***.

2. *Msichana* ***mwenye sauti laini*** *ametuzwa.*

(Fungu la maneno ***'mwenye sauti laini'*** ni kirai kivumishi ambacho kimeundwa kwa ***'kivumishi + nomino + kivumishi')****.* Neno kuu linalotangulia katika fungu hili la maneno ni kivumishi ***mwenye***.

3. *Wananchi* ***wenye kutukana viongozi*** *watachukuliwa hatua kali.*

(Fungu la maneno ***'wenye kutukana viongozi'*** ni kirai kivumishi ambacho kimeundwa kwa ***'kivumishi + kitenzi + nomino')****.* Neno kuu linalotangulia katika fungu hili la maneno ni kivumishi ***wenye***.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kutambua miundo mbalimbali ya virai vivumishi kwa kurejelea sentensi walizopwa hapo awali wazichunguze. Wanafunzi wafahamishwe kuwa fungu la maneno katika sentensi linalotanguliwa na kivumishi huchukua muundo wa kirai kivumishi. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kufanya zoezi la 6 na zoezi la 7.

## Tathmini ya vipindi 37-40

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu maana ya kirai kivumishi pamoja na miundo yake mbalimbali. Mwalimu anaweza kuunganisha maswali yake na aina nyingine za virai ambazo tayari wanafunzi wameshafundishwa kama vile virai nomino. Wanafunzi washirikishwe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia virai nomino pamoja na virai vivumishi.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Fungu la maneno yenye muundo ambao umekitwa katika kivumishi huitwa ***kirai kivumishi***. Kirai kivumishi huwa na neno kuu ambalo ni kivumishi kinachotangulia.

### Muundo wa kirai kivumishi:

1. Kivumishi pamoja na kielezi chake:

**Mifano**:

a) Habari niliyopewa ni njema kwelikweli.

Kirai kivumishi '***njema kwelikweli***' kimeundwa kwa *kivumishi + kielezi.*

b) Nguo aliyonunuliwa ni nzuri kabisa.

Kirai kivumishi ***'nzuri kabisa'*** kimeundwa kwa *kivumishi + kielezi.*

2. Kivumishi pamoja na kirai nomino:

**Mifano:**

a) Mwimbaji mwenye sauti laini ameshinda tuzo.

Kirai kivumishi ***'mwenye sauti laini'*** kimeundwa kwa *kivumishi + kirai nomino.*

b) Mhudumu mwenye kazi nzuri ameongezewa mshahara.

Kirai kivumishi ***'mwenye kazi nzuri'*** kimeundwa kwa *kivumishi + kirai nomino.*

3. Kivumishi pamoja na kirai kitenzi:

**Mfano:**

a) Hii ndiyo bunduki yenye kupiga risasi.

Kirai kivumishi ***'yenye kupiga risasi'*** kimeundwa kwa *kivumishi + kirai kitenzi.*

b) Huyu ndiye ndovu mwenye kuangusha miti.

Kirai kivumishi ***'mwenye kuangusha miti'*** kimeundwa kwa *kivumishi + kirai kitenzi.*

4. Kivumishi pamoja na kirai kivumishi:

**Mfano:**

a) Niliuziwa ng'ombe mwingine mwenye jicho moja.

Kirai kivumishi '***mwingine mwenye jicho moja'*** kimeundwa kwa *kivumishi + kirai kivumishi.*

b) Nitamtuza mwanafunzi mwingine mwenye viatu vyeusi.

Kirai kivumishi '***mwingine mwenye viatu vyeusi'*** kimeundwa kwa *kivumishi + kirai kivumishi.*

## 3.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango cha chini cha wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

***Kwa mfano:***

Tambua virai vivumishi katika sentensi zifuatazo.

1. Kiranja mwenye maringo ameadhibiwa.
2. Watu watatu wengine wanatakikana.
3. Wafilipino ni watu warefu na wenye nguvu sana.
4. Kikapu chetu kimejazwa matunda.
5. Ahishakiye ameomba msamaha.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

1. Kiranja mwenye maringo ameadhibiwa. (‘***mwenye maringo’*** ni kirai kivumishi)
2. Watu watatu wengine wanatakikana. (‘***watatu wengine’*** ni kirai kivumishi)
3. Wafilipino ni watu wenye nguvu sana. (‘***wenye nguvu sana’*** ni kirai kivumishi)
4. Kikapu chetu kipya kimejazwa matunda. (‘***chetu kipya*** ni kirai kivumishi)
5. Ahishakiye amevaa kofia nzuri sana. (‘***nzuri sana’*** ni kirai kivumishi)

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi tano zenye kirai nomino na nyingine tano zenye kirai kivumishi.

***Kwa mfano:***

i) Dawa za kulevya zimepigwa marufuku. *(‘**dawa za kulevya’** ni kirai nomino)*

ii) Mama alipika chakula kitamu sana. *(‘**kitamu sana’** ni kirai kivumishi)*

## 3.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 22

1. Inspekta Fadhili, Kazija, Mzee Bakari na askari.
2. Inspekta Fadhili alikuwa na jukumu la kiusalama, yaani, kuhakikisha kuwa kulikuwa na utulivu wakati wa mkutano.
3. Kwa sababu walistahili kujibu mashtaka ya kesi ya jinai mbali na madai ya ufisadi waliyokuwa wamelimbikiziwa.
4. Mwanasururu
5. Kuwasikiliza watetezi wakijielezea.
6. Alikuwa na ujeuri, majivuno na kujiona.
7. Kwa sababu alikuwa ametoa ahadi alizotaja awali na hakuwahi kuzitimiza.
8. Bwana Maksuudi alipokuwa Mkuu wa Wilaya alikula pesa za mkewe Mzee Japu ili kumtilia sahihi alipotaka kununua kiwanja cha kujengea nyumba.
9. Alipokewa kwa shangwe, nderemo, makofi na vigelegele.
10. Bwana Maksuudi ni fisadi, dhalimu na asiye na utu. (*Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu sifa za Bwana Maksuudi*)

### Zoezi la 1, ukurasa 23

Mwalimu atathmini maelezo ambayo yatatolewa na wanafunzi. Sharti maelezo hayo yahusishe msamiati waliopatana nao katika kifungu walichosoma.

***Kwa mfano:***

1. ***Umma*** - watu wengi waliokusanyika pamoja
2. ***Wamesawijika -*** wamekuwa katika hali mbaya kutokana na dhiki

**Matumizi katika sentensi:**

1. Umma ulikusanyika kumsikiliza mgombea wa urais.
2. Wananchi walikuwa wamesawijika kwa hasira baada ya mwanasiasa mmoja kuwatusi.

## Zoezi la 2, ukurasa 23

1. aliyokusanya
2. Wanaopigania wengine
3. tamko
4. kiburi
5. fimbo
6. Jina la kiongozi maalum
7. nguo za wanawake
8. Uhusiano
9. kikamweka kando

### Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 24

Wanafunzi wajadili baadhi ya sifa zifuatazo za riwaya:

1. Riwaya huwa na maelezo ya usimulizi kulingana na hadithi inavyotokea kiwakati na kimasafa.
2. Riwaya huwa na urefu wa kutosha kushughulikia mahitaji ya mtunzi.
3. Riwaya huchunguza kwa kina jamii inayosawiriwa.
4. Riwaya huhusisha: ploti/msuko, hadithi, usimulizi, uhusika, mazingira, wakati, mitazamo na mazungumzo ya wahusika.
5. Riwaya huwa na maelezo kuwahusu wahusika, mavazi yao, tabia zao, namna matendo yao yanavyoathiri nafsi zao na kuwaathiri wahusika wengine.

## Zoezi la 3, ukurasa 24

Mwalimu atathmini namna wanafunzi watakavyowaainisha wahusika.

***Kwa mfano:***

### i) Wahusika wakuu

Hawa ni wahusika ambao wanahusishwa na takribani visa vyote katika riwaya. Wahusika hawa huhusishwa kutoka mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano: Bwana Maksuudi.

### ii) Wahusika wasaidizi

Hawa ni wahusika wanaosaidia kumjenga mhusika mkuu. Hujitokeza mara nyingi katika hadithi. Wahusika wasaidizi wanaweza kuwa na visa vyao. Kwa mfano: wanaweza wakawa ni marafiki na aila za wahusika wakuu. Kwa mfano: Kazija na Inspekta Fadhili.

### iii) Wahusika wadogo

Hawa ni wahusika ambao wanafanya kazi ndogo sana katika fasihi kama vile kujenga maudhui au mandhari. Wahusika hawa wakitolewa, riwaya inaweza kuendela bila kubadilika sana. Kwa mfano: Mzee Japu na Mzee Bakari.

## Zoezi la 4, ukurasa 24

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu maudhui katika sura moja ya riwaya waliyoisoma. Baadhi ya maudhui ni:

1. ***Ufisadi:*** Bwana Maksuudi anadaiwa kuitisha shilingi mia mbili ili kutia sahihi stakabadhi za mkewe Mzee Japu za kununua kiwanja cha kujengea nyumba.
2. ***Bidii:*** Umati unaokusanyika uwanjani unadhihirisha bidii na ari waliyonayo katika siasa. Wamekusanyika ili kuwasikiliza watetezi wao wakiomba kura.
3. ***Ujasiri:*** Kazija haogopi kumwambia Bwana Maksuudi ukweli kuhusu uongozi wake na tabia zake. Anasimama kidete na kusema yote ayajuayo kumhusu Bwana Maksuudi bila woga wowote. Biti Shomari pia haoni woga kusema kuwa yeye anamjua mtetezi wake. Anatamka haya kwa sauti ya juu zaidi.
4. ***Umoja:*** Umma unasawiriwa kuwa wenye umoja. Hii ni kwa sababu wanapoghadhabika, wanaungana kwa pamoja ili kupigana na viongozi hao wabaya. Kunao wanaobeba bakora na wengine wanafinyanga ngumi ili kulipiza kisasi.

## Zoezi la 5, ukurasa 24

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu tabia za wahusika.

***Kwa mfano:***

*i)* ***Bwana Maksuudi:*** Mhusika huyu anasawiriwa kama fisadi na asiye na utu. Kwenye riwaya, Bwana Maksuudi anadaiwa kuitisha shilingi mia mbili ili kutia sahihi katika stakabadhi za kununua kipande cha kujengea nyumba. Huu ni ufisadi kwa kuwa kiongozi hafai kuchukua hongo ili kuwahudumia wananchi. Bwana Maksuudi anakosa utu pale ambapo tunaelezwa kuhusu yeye na mwanawe wa kiume ambao hawajaonana kwa mwaka mmoja sasa. Halikadhalika, Bwana Maksuudi anadaiwa kumnyang'anya mkewe mali yake na kusababisha kifo chake.

*ii)* ***Kazija:*** Kazija ni mhusika jasiri. Ni kutokana na ujasiri wake ndipo anaamua kusimama na kuzungumza kumhusu Bwana Maksuudi na matendo yake mabovu. Kazija haogopi lolote wala chochote. Anayatamka mambo mengi kumhusu Bwana Maksuudi na uongozi wake. Kazija pia ni msema ukweli kwa kuwa hadanganyi katika yote anayozungumza kumhusu Bwana Maksuudi.

*iii)* ***Mzee Bakari:*** Huyu ni mhusika mwoga. Baada ya Bwana Zanga kuzungumza, anawauliza wananchi iwapo walikuwa na swali. Mzee Bakari hasemi yaliyokuwa moyoni mwake kwa sauti ila anajisemea kimoyomoyo.

*iv)* ***Inspekta Fadhili:*** Huyu ni mpenda amani kwa kuwa zogo linapozuka, anaamua kuwatuliza wananchi kwa kuwaambia waiachie sheria itekeleze wajibu wake kufuatia madai waliyo nayo kwa Bwana Maksuudi na Bwana Zanga. Anafaulu katika kuutuliza umati wa watu kupitia sifa yake ya kupenda amani na pia umaarufu wake.

Mwalimu ahakikishe wanafunzi wanawalinganisha wahusika hawa na watu katika maisha yao ya kila siku. Kupitia majadiliano haya, wanafunzi wafahamu sifa nzuri za kuiga na sifa hasi za kutupilia mbali.

## Zoezi la sarufi, ukurasa 25

**A.**

1. Maneno '*nzuri kabisa*' ni kivumishi + kielezi, hivyo yanaunda *kirai kivumishi.*
2. Maneno '*mwenye sauti laini*' ni kivumishi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda *kirai kivumishi.*
3. Maneno '*yenye kuta ndefu*' ni kivumishi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda *kirai kivumishi.*

4. Maneno '*ndefu sana*' ni kivumishi + kielezi, hivyo yanaunda *kirai kivumishi*.
5. Maneno '*wenye kutukana viongozi*' ni kivumishi + kitenzi + nomino, hivyo yanaunda *kirai kivumishi*.
6. Maneno '*mwenye kuhifadhi sheria*' ni kivumishi + kitenzi + nomino, hivyo yanaunda *kirai kivumishi*.
7. Maneno '*nyingine yenye huduma nzuri*' ni kivumishi + kivumishi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda *kirai kivumishi*.
8. Maneno '*mzuri wa kuuzwa*' ni kivumishi + kivumishi '-a' unganifu + kitenzi, hivyo yanaunda *kirai kivumishi*.
9. Maneno '*mpungufu wa akili*' ni kivumishi + kivumishi '-a' unganifu + nomino, hivyo yanaunda *kirai kivumishi*.

**B.** Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu tofauti kati ya kirai nomino na kirai kivumishi.

Msingi wa *kirai nomino* ni nomino ambayo hutangulia na msingi wa *kirai kivumishi* ni kivumishi ambacho hutangulia. Kwa mfano:

***1. Kirai kivumishi:*** Kitabu kipya kikubwa kimelowa maji. (*kivumishi* +*kivumishi*)

***Kirai nomino:*** Kitabu kipya kikubwa kimelowa maji. (*nomino*+*kivumishi*+*kivumishi*)

***2. Kirai kivumishi:*** Mtoto mpole sana amelala. (*kivumishi* +*kielezi*)

***Kirai nomino:*** Mtoto mpole sana amelala.(*nomino*+*kivumishi*+*kielezi*)

## Zoezi la 6, ukurasa 26

1. 'fisadi sana (*kivumishi*+*kielezi*)
2. 'mengine yenye utamu' (*kivumishi* + *kirai kivumishi*)
3. 'mwenye kuuza matunda' (*kivumishi* +*kirai kitenzi*)
4. 'zile nzuri kweli' (*kivumishi* +*kirai kivumishi*)
5. 'mwenye gari kubwa' (*kivumishi* +*kirai nomino*)
6. 'warefu sana' (*kivumishi* + *kielezi*)
7. 'wanyonge wote' (*kivumishi* + *kivumishi kingine*)
8. 'zile kabisa' (*kivumishi* + *kielezi*)
9. 'mwenyewe' (*kivumishi*)
10. 'matamu matano' (*kivumishi* + *kivumishi kingine*)

**Zoezi la 7, ukurasa 27**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi kisarufi na zihusishe miundo mbalimbali ya virai vivumishi.

***Kwa mfano:***

1. Mwigizaji *mwenye ucheshi mwingi* amewasili.
2. Tutamtuza mwanafunzi *bora zaidi.*

## Somo la 4: Utanzu wa tamthilia

### Vipindi 41-43: Kusoma ufahamu

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha mazungumzo kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kuchunguza kwa usahihi utanzu wa tamthilia.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Kazi za tamthilia za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 28-34;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu ufafanuzi wa utanzu wa tamthilia. Tamthilia ni utanzu mojawapo wa fasihi andishi ambao huhusisha mazungumzo ya moja kwa moja kati ya wahusika mbalimbali. Hii ndiyo sifa kuu inayotofautisha utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya au utanzu wa hadithi fupi. Katika tamthilia, majina ya wahusika wanaozungumza huandikwa upande wa kushoto na usemi wao huandikwa upande wa kulia. Maandishi ya tamthilia aghalabu huwa katika kauli asili na wakati uliopo. Katika utanzu wa tamthilia, mandhari hutumika kwa wingi kutokana na maonyesho yake mbalimbali ambayo aghalabu hutendeka katika mazingira tofauti.

Vilevile, ni vyema mwalimu awe tayari kushughulikia sarufi katika somo hili. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kufahamu maana ya kirai kitenzi pamoja na miundo yake mbalimbali. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kufahamu tofauti iliyopo kati ya kirai kitenzi, kirai kivumishi na kirai nomino. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelezo yaliyotolewa kwa kila zoezi husika.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita kuhusiana na utanzu wa riwaya. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika somo lililotangulia.

Baada ya haya, mwalimu atangulize somo hili kuhusu utanzu wa tamthilia. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha kuhusiana na michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 28. Maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye michoro hii? Wahusika wanaoonekana ni kina nani?* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona…."*. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na wanayoyaona katika michoro waliyopewa. Kwa mfano: "*Mimi ninamwona nyanya akitembea kwa kutumia mkongojo. Mimi ninamwona mwanamke wa Kiislamu aliyevalia buibui."*

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea au wanachokiona katika michoro hiyo. Kutokana na michoro hiyo, wanafunzi wataweza kukisia sura moja ya tamthilia watakayosoma itahusu nini. Bila shaka sehemu hiyo ya tamthilia inawahusu wahusika Rahma na Zainabu kutoka katika tamthilia ya '***Kijiba cha moyo'*** iliyoandikwa na Timothy Arege.

### 4.1 Kusoma na kufahamu

***Sura moja ya tamthilia***

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne wasome kwa kimya sura moja ya tamthilia waliyopewa kuhusu mazungumzo kati ya Bi Rahma na Zainabu. Wanafunzi wasome mazungumzo hayo kwa kimya huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho walichosoma ili kuhakikisha kuwa wamekielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Bi Rahma alikuwa na uhusiano upi na Zainabu? Mazungumzo haya yanafanyika katika mandhari gani?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika sura ya tamthilia husika. Kwa mfano: *Bi Rahma ni shangazi yake Zainabu. Mazungumzo haya yanafanyika nyumbani kwa wazazi wake Sele.*

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti mazungumzo hayo ili kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna inayofaa na kwa usahihi. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika sura ya tamthilia hiyo.

## Tathmini ya vipindi 41-43

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea ufafanuzi na uchambuzi wa tamthilia. Mwalimu ahakikishe wanafunzi wanafahamu tofauti na ulinganisho kati ya tamthilia na riwaya au hadithi fupi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kubaini sifa za utanzu wa tamthilia kwa kutumia sura moja ya tamthilia waliyopewa.

## Vipindi 44-45: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na utanzu wa tamthilia;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na utanzu wa tamthilia.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Kazi za tamthilia za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 34-35;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Somo hili linahusu ujifunzaji wa msamiati unaohusiana na sura moja ya tamthilia iliyo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 28-34 pamoja na vipengele vya utanzu wa tamthilia kwa ujumla. Mwalimu aandae mifano ya tamthilia au hata sura mbalimbali za tamthilia teule ambazo anaweza kuwapa wanafunzi wakazisoma darasani na kuchambua msamiati wake katika makundi. Pia, mwalimu anaweza kuandaa maigizo kadhaa kuhusiana na utanzu wa tamthilia na kuwashirikisha wanafunzi katika makundi yao mbalimbali kuyaigiza mbele ya wanafunzi wenzao. Mifano kadhaa ya tamthilia inaweza kurekodiwa na wanafunzi wakasikiliza darasani au hata kuzitazama zikiigizwa kwenye runinga na baadaye kuchambua msamiati wake maalum. Mwalimu anaweza kufanya maandalizi haya mapema kabla ya vipindi hivi. Pia, mwalimu anaweza kuwashirikisha wanafunzi wake mapema kabla ya funzo hili ambapo wanaweza kusoma tamthilia fulani teule kisha wajaribu kufanya majaribio ya kuigiza sehemu fulani fulani za tamthilia hiyo. Uigizaji huu utawapa wanafunzi ujasiri wa kusimama mbele ya wanafunzi na hata kuzungumza kwa lugha rasmi na sahihi kisarufi.

## d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita kilichohusu utanzu wa riwaya. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilichotangulia. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kushirikishwa katika kujadili tofauti zilizopo kati ya utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya. Ulinganisho wa tanzu hizi mbili unaweza kujadiliwa pia.

## 4.2 Kujifunza msamiati kutokana na sura ya tamthilia husika

Mwalimu atangulize somo hili kuhusu msamiati unaohusiana na utanzu wa tamthilia.

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya waliopatana nao katika usomaji wao wa sura moja ya tamthilia waliyopewa katika vitabu vyao. Wanafunzi waeleze jinsi msamiati huo ulivyotumiwa katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma ambacho ni sura moja ya tamthilia teule. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale inapohitajika au hata vitabu vingine vya marejeleo vya msamiati. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua msamiati husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze msamiati waliopewa katika zoezi la 2 sehemu A pamoja na maana sahihi ya msamiati huo katika sehemu B kisha wauhusishe kwa usahihi msamiati huo na maana hizo kwa kutumia mshale.

Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe tena kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika sura moja ya tamthilia teule waliyosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba matumizi ya msamiati husika katika maongezi au maandishi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha sahihi.

## Tathmini ya vipindi 44-45

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha katika vipindi hivi. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mpya waliopatana nao kutoka kwenye sura moja ya tamthilia teule waliyosoma. Pia, mwalimu abaini iwapo wanafunzi wamepata uwezo wa kutambua sifa bainifu za utanzu wa tamthilia ukilinganishwa na tanzu za riwaya na hadithi fupi.

# Vipindi 46-48: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu sifa bainifu za utanzu wa tamthilia;
- Kujadili tofauti zilizopo kati ya utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za tamthilia za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha sifa bainifu za utanzu wa tamthilia;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 35-36;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha kuhusiana na utanzu wa tamthilia. Mwalimu aandae chati zinazoonyesha sifa bainifu za utanzu wa tamthilia ukilinganishwa na tanzu za riwaya na hadithi fupi. Kwa upande mwingine, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi tamthilia teule wakaisoma kabla ya funzo hili.

## d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita kuhusiana na utanzu wa tamthilia. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wanaweza kurejelea kazi mbalimbali za utanzu wa tamthilia ambazo wamewahi kuzisoma.

## 4.3 Majadiliano kuhusu sifa bainifu za utanzu wa tamthilia

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha wajadili kuhusu:

1. *Sifa bainifu za tamthilia.*
2. *Tofauti kati ya utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili katika makundi yao. Wanafunzi wanaweza kujadiliana kwa kutumia mifano kutoka kwenye tamthilia mbalimbali ambazo wamewahi kuzisoma. Kupitia majadiliano haya, mwalimu ataweza kuwaelekeza wanafunzi katika kutambua sifa bainifu za utanzu wa tamthilia pamoja na tofauti zilizopo kati ya utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya.

Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa tamthilia ni kama vile:

1. *Tamthilia hutawaliwa na mazungumzo na majibizano.*
2. *Tamthilia huwa na maelezo ya kumwelekeza msomaji ambayo huwa kwenye mabano na ambayo aghalabu hupendekeza jukwaa litakavyoonekana wakati wa maigizo.*
3. *Tamthilia hugawika katika sehemu (matendo na maonyesho) mbalimbali kutegemea matendo na matukio husika.*
4. *Tamthilia hushirikisha hadhira.*
5. *Tamthilia huwa na mgogoro fulani unaotanda katika hadithi nzima.*

   Tofauti moja kuu kati ya utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya ni kuwa tamthilia hutawaliwa na mazungumzo na majibizano ilhali riwaya hutawaliwa na masimulizi ya kinathari (mfululizo). Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili kuhusu tofauti nyingine kati ya utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya.

   Baada ya haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 4 na zoezi la 5.

## Tathmini ya vipindi 46-48

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kikundi kuhusiana na sifa bainifu za utanzu wa tamthilia.

Maswali yake pia yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kueleza tofauti zilizopo kati ya utanzu wa tamthilia na utanzu wa riwaya.

# Vipindi vya 49-51: Kusikiliza na kuzungumza

## a) Malengo ya somo

- Kuigiza tamthilia teule;
- Kuchambua tamthilia ya ***'Urunana'*** kwa kuzingatia sifa za wahusika wake;
- Kujadili kuhusu umuhimu wa wahusika utanzu wa kifasihi kwa jamii.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za utanzu wa tamthilia za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Rekodi za kazi za utanzu wa tamthilia;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 36-37;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia vipindi hivi kuhusu umuhimu wa utanzu wa tamthilia kwa jamii. Mwalimu anaweza kuandaa rekodi za tamthilia kadhaa ambazo wanafunzi wanaweza kuzisikiliza darasani na kuzitazama jukwaani kisha wakabaini umuhimu wake kwa jamii kupitia kwa maisha yao ya kila siku. Pia, mwalimu anaweza kuandaa maigizo ya tamthilia teule ambayo anaweza kuwashirikisha wanafunzi darasani. Wanafunzi wanaweza kupewa vitabu vya tamthilia ambazo mwalimu atateua mapema ili wazisome kabla ya vipindi hivi.

## d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilichopita kuhusu sifa bainifu za utanzu wa tamthilia. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa mazoezi ambayo wanafunzi walipewa katika kipindi kilichopita yamesahihishwa na wanafunzi waliokuwa na matatizo wameelekezwa vilivyo.

## 4.4 Maigizo ya sura ya tamthilia

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaongoze wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili waweze kuigiza sura moja ya tamthilia waliyosoma hapo awali kuhusu wahusika Bi Rahma, Zainabu na Aisha. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujadiliana kuhusu wahusika hao waliowasoma katika sura hiyo moja ya tamthilia na kuzieleza tabia zao. Kutokana na haya, wanafunzi watapata uwezo na maarifa ya kuigiza sura hiyo ya tamthilia waliyosoma. Sehemu hii itapanua ujuzi wa wanafunzi kuhusu vipengele mbalimbali vya utanzu wa tamthilia. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wajitokeze mbele ya darasa ili waigize sura hiyo moja ya tamthilia. Wanafunzi wengine nao wasikilize na kutazama maigizo ya wanafunzi wenzao na kuyafuata kwa makini. Kila kikundi kipewe muda wa kuigiza huku wakiongozwa na mwalimu.

Baada ya majadiliano haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kujadiliana kuhusu mambo muhimu yaliyopatikana katika maigizo yao darasani kuhusiana na sura ya tamthilia waliyopewa kwenye vitabu vyao. Wanafunzi waelekezwe katika kuyalinganisha maigizo yao na maisha yao ya kila siku. Wanafunzi waelezane kwa uwazi jinsi tabia za wahusika kadhaa zinavyohusiana na kuyaathiri maisha yao ya kila siku.

Aidha, hatua hii ya kusikiliza na kuzungumza imehusisha pia majadiliano kuhusu tabia za wahusika katika tamthilia ya ‘***Urunana’*** umuhimu wake kwa jamii. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuchambua tamthilia hiyo. Wanafunzi wanaweza kujadiliana katika makundi ya wanafunzi watatu watatu.

## Tathmini ya vipindi 49-51

Mwalimu atathmini iwapo ujifunzaji umefanyika kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, awaulize wanafunzi maswali ya kupima uwezo wao wa kurejelea sifa bainifu za utanzu wa tamthilia pamoja na umuhimu wa utanzu huu kwa jamii.

Vilevile, maswali mengine yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kujadiliana katika makundi kuhusu tabia za wahusika katika tamthilia ya ‘***Urunana’*** pamoja na uchambuzi wa wahusika katika kazi nyingine za kifasihi za kitamthilia. Wanafunzi waeleze namna kazi za utanzu wa tamthilia walizosoma zinachangia katika kuboresha maisha yao ya kila siku.

# Vipindi 52-55: Sarufi (Kirai kitenzi)

## a) Malengo ya somo

- Kutambua maana ya kirai kitenzi;
- Kutambua miundo mbalimbali ya kirai kitenzi;
- Kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia virai vitenzi.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Chati yenye miundo mbalimbali ya virai vitenzi;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 37-39;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini maana ya kirai kitenzi pamoja na miundo mbalimbali ya kirai kitenzi. Pia, mwalimu alenge kuwaelekeza wanafunzi kubaini tofauti kati ya kirai kitenzi na aina nyingine za virai ambazo tayari wameshafundishwa katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: chati zinazoonyesha miundo mbalimbali ya kirai kitenzi pamoja na sentensi kadhaa zilizo sahihi kisarufi zilizotumia virai vitenzi katika miundo yake mbalimbali. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hivi hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu kipindi cha hapo awali cha sarufi kuhusu kirai kivumishi pamoja na miundo yake mbalimbali. Mwalimu pia anaweza kuwauliza wanafunzi maswali ya kuwachangamsha kuhusiana na miundo mbalimbali ya virai vivumishi kama

walivyofundishwa katika kipindi cha hapo awali cha sarufi. Mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia kirai kivumishi katika miundo yake mbalimbali.

***Kwa mfano:***

1. *Mwanafunzi **yule mrefu sana** aliigiza vizuri*. Katika sentensi hii, '*yule mrefu sana'* ni kirai kivumishi kilichoundwa kwa kivumishi (*yule*)+ kirai kivumishi (*mrefu sana*).
2. *Kazi **ile nzuri** itafanywa na mama*. Katika sentensi hii, '*ile nzuri'* ni kirai kivumishi kilichoundwa kwa vivumishi viwili.

Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha zoezi walilopewa katika kipindi kilichopita.

## 4.5 Kirai kitenzi

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha awaombe wachunguze sehemu zilizopigiwa mistari katika sentensi walizopewa na hapo baadaye waelezane sehemu hizo zimeundwa kwa kutumia maneno gani. Zoezi hili litawasaidia wanafunzi kuweza kubaini maana ya kirai kitenzi pamoja na miundo yake mbalimbali. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua kuwa sehemu zote zilizopigiwa mistari katika sentensi walizopewa ni miundo mbalimbali ya kirai kitenzi.

***Kwa mfano:***

1. *Baba **alikuwa akitusimulia hadithi***.

(Fungu la maneno *'**alikuwa akitusimulia hadithi'*** ni kirai kitenzi ambacho kimeundwa kwa *'**vitenzi viwili + nomino'**)*. Neno kuu linalotangulia katika fungu hili la maneno ni kitenzi '***alikuwa'***.

*2. Mwalimu **angali anafundisha darasani***.

(Fungu la maneno *'**angali anafundisha darasani*** ni kirai kitenzi ambacho kimeundwa kwa *'**kitenzi + kitenzi + kielezi'**)*. Neno kuu linalotangulia katika fungu hili la maneno ni kitenzi '***angali'***.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kutambua miundo mbalimbali ya virai vitenzi kwa kurejelea sentensi walizopewa hapo awali

wazichunguze. Wanafunzi wafahamishwe kuwa fungu la maneno katika sentensi linalotanguliwa na kitenzi huchukua muundo wa kirai kitenzi.

Baadhi ya miundo ya virai vitenzi ni:

1. Kitenzi kimoja, kwa mfano: *Mwajiri* ***atatuajiri***.
2. Kitenzi + nomino, kwa mfano: *Mwajiri* ***atatulipa mishahara***.
3. Kitenzi + kirai nomino, kwa mfano: *Mwajiri* ***atatulipa mishahara mizuri***.
4. Kitenzi + kielezi, kwa mfano: *Mwajiri* ***atatulipa kesho***.

Baada ya haya, mwalimu awashirikishe wanafunzi kufanya zoezi la 9 na zoezi la 10.

## Tathmini ya vipindi 52-55

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu maana ya kirai kitenzi pamoja na miundo yake mbalimbali. Mwalimu anaweza kuunganisha maswali yake na aina nyingine za virai ambazo tayari wanafunzi wameshafundishwa kama vile virai vivumishi. Wanafunzi washirikishwe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia virai vivumishi pamoja na virai vitenzi.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Fungu la maneno yenye muundo ambao umekitwa katika kitenzi huitwa ***kirai kitenzi***.

**Muundo wa virai vitenzi:**

1. Kitenzi pamoja na kitenzi kingine au vingine:

   **Mifano**:

   a) Nyanya alikuwa hajamaliza kula. (*kitenzi* + *vitenzi viwili*)

   b) Neza anataka kukimbia (*kitenzi* + *kitenzi kingine*)

2. Kitenzi pamoja na kielezi:

   **Mifano:**

   a) Mwimbaji huyu anaimba vizuri. (*kitenzi* + *kielezi*)

   b) Babu anatembea polepole. (*kitenzi* + *kielezi*)

3. Kitenzi pamoja na nomino au kirai nomino:

   **Mfano:**

   a) Baba analima shamba. (*kitenzi* + *nomino*)

   b) Baba analima shamba kubwa. (*kitenzi* + *kirai nomino*)

4. Kitenzi pamoja na Kirai kielezi:

   **Mfano:**

   a) Mchezaji alikimbia upesi sana. (*kitenzi* + *kirai kielezi)*

   b) Mtoto alilia vibaya sana. (*kitenzi* + *kirai kielezi)*

## 4.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango cha chini cha wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

***Kwa mfano:***

Tambua virai vitenzi katika sentensi zifuatazo.

1. Maji yalikuwa yakimwagika jana usiku.
2. Mwalimu aliwafundisha wanafunzi kuandika insha.
3. Wafugaji waliwanywesha ng'ombe maji.
4. Baba ndiye aliyestahili kuwa meneja wa kampuni ile.
5. Wavulana na wasichana wanacheza vizuri.

## Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

1. *Maji yalikuwa yakimwagika jana usiku*. Fungu la maneno *'yalikuwa yakimwagika jana usiku'* ni kirai kitenzi kilichoundwa kwa vitenzi viwili na kielezi.
2. *Mwalimu aliwafundisha wanafunzi kuandika insha*. Fungu la maneno *'aliwafundisha wanafunzi kuandika insha'* ni kirai kitenzi kilichoundwa kwa kitenzi na kirai nomino.
3. *Wafugaji waliwanywesha ng'ombe maji*. Fungu la maneno *'waliwanywesha ng'ombe maji'* ni kirai kitenzi kilichoundwa kwa kitenzi na kirai nomino.
4. *Baba ndiye aliyestahili kuwa meneja wa kampuni ile*. Fungu la maneno *'ndiye aliyestahili kuwa meneja wa kampuni ile'* ni kirai kitenzi kilichoundwa kwa vitenzi vitatu na kirai nomino.
5. Wavulana na wasichana wanacheza vizuri. Fungu la maneno *'wanacheza vizuri'* ni kirai kitenzi kilichoundwa kwa kitenzi na kielezi.

## ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi tano sahihi kisarufi kwa kutumia virai vitenzi.

***Kwa mfano:***

1. *Mama anapika wali mtamu.*

Fungu la maneno '***anapika wali mtamu'*** ni kirai kitenzi ambacho kimeundwa kwa kitenzi (*anapika*) na kirai nomino (*wali mtamu*).

## 4.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 34

1. Wahusika watatu
2. Rahma ni shangazi yake Zainabu.
3. Aisha ni mjukuu wake Bi. Rahma. Kwa hivyo, Bi. Rahma ni nyanyake Aisha.
4. Sele anajitenga na watu, hamu ya chakula imemwisha, hasemi na akisema, anayosema hayaeleweki.
5. Wanashughulika na kazi zao nyingi tu ambazo sio za kinyumbani.
6. Zainabu ni mtu makini sana. Anachunguza mienendo ya Sele na kujua tabia yake. Pia, anaelewa namna Aisha alivyo mpishi hodari. Zainabu pia ni mdadisi. Anamuuliza Bi. Rahma maswali mengi kuhusiana na suala la kumpeleka Sele kwa waganga ili afanyiwe kafara. Yeye pia ni karimu kwa kuwa anamwambia Aisha atayarishe chai itakayonywewa na bibiye pamoja na Sele.
7. Katika onyesho hili, wanajadili: afya, elimu, mabadiliko na ushirikina. Onyesho hili linahusu hali ya kiafya ya Sele ambaye anaonekana mnyonge kwa sababu hali chochote. Kila anachoandaliwa akila anakula kidogo tu na mara nyingi hali kabisa. Kielimu, Aisha anaonekana kama aliyeegemea sana katika masomo ya kisasa na kusahau masuala ya kijamii hivi kwamba anawapuuza Bi. Rahma na Zainabu anapoingia chumbani na kuanza kupekuapekua penye vitabu. Mabadiliko yanadhihirika katika hali ya kimaisha ya Aisha na Sele. Sele anabadilika kiafya na kiakili kwa kuwa anaonekana msahaulifu sana na anayeongea maneno yasiyoeleweka. Aisha kwa upande wake, anabadilishwa na kisomo anachopata na pia mapito ya wakati. Anasema kwamba anaishi maisha ya kisasa wala sio ya kale. Suala la ushirikina linajitokeza waziwazi pale ambapo Bi. Rahma anasisitiza kuhusu kumpeleka Sele kwa waganga ili afanyiwe kafara.
8. Aisha na Sele ni mke na mume.
9. Aisha ni mwenye mapuuza kwa kuwa anapoingia chumbani, hatilii maanani kuwa wazee wake wapo chumbani na wanastahili kuamkiwa. Yeye anatamka tu salamu za jumla na kuendelea na shughuli zake. Aisha pia anadhihirisha kuwa amepuuza hali ya mumewe Sele kwa kuwa anasema hamwelewi mara nyingi anapoongea ila hasemi iwapo

kunacho anachofanya ili kuhakikisha kuwa amemwelewa. Aidha, Aisha amekengeuka hivi kwamba anasema kuwa mwanamke wa sasa hana tofauti na mwanamume kwani yeye anakwenda na majira ya usasa.

10. Bi. Rahma anashikilia kuwa Sele apelekwe kwa mganga ili afanyiwe kafara. Ana itikadi ya ushirikina.

## Zoezi la 1, ukurasa 34

Mwalimu atathmini maelezo ambayo wanafunzi watatoa kuhusu msamiati waliopatana nao katika usomaji wao wa sura ya tamthilia waliyopewa. Pia, atathmini sentensi watakazotunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***papa -*** samaki mkubwa kuliko samaki wote baharini, mwenye ngozi ngumu ya kijivu na meno makali
2. ***kitoweo -*** mboga, mchuzi, nyama au samaki ambayo huliwa pamoja na chakula kingine

**Matumizi katika sentensi:**

1. Wavuvi walimvua ***papa*** mmoja jana jioni.
2. Mama anapasha ***kitoweo*** moto.

## Zoezi la 2, ukurasa 35

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | G | 2. | I |
| 3. | H | 4. | E |
| 5. | CH | 6. | J |
| 7. | A | 8. | D |
| 9. | B | 10. | F |

## Zoezi la 3, ukurasa 35

a) Baadhi ya sifa bainifu za tamthilia ni:

1. Tamthilia huwa na maelezo ya jukwaa yanayoeleza namna jukwaa/ eneo la onyesho lilivyo.
2. Tamthilia hutawaliwa na mazungumzo na majibizano.

3. Tamthilia hutoa maelezo kuhusu wahusika – hisia zao, mavazi na matendo yao.
4. Tamthilia hugawika katika maonyesho/sehemu mbalimbali kutegemea matendo na matukio.
5. Tamthilia hushirikisha hadhira.
6. Tamthilia huhusisha mgogoro fulani hasa katika upeo wake.
7. Tamthilia huweza kutumia mtindo wa kishairi.
8. Utendaji wa tamthilia huambatana na miondoko - yaani, ni vipi viungo vya mwili vya mtendaji, kama vile: kichwa, mikono na miguu vinavyosongezwa.

b) ***Tofauti kati ya utanzu wa riwaya na utanzu wa tamthilia***

1. Riwaya huwa ndefu kimaandishi kuliko tamthilia.
2. Riwaya huandikwa kwa kinathari ilhali tamthilia huandikwa kwa muundo wa mazungumzo na majibizano.
3. Riwaya ina wahusika wengi kuliko tamthilia.

## Zoezi la 4, ukurasa 36

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu iwapo mwandishi alizingatia sifa bainifu za tamthilia.

***Kwa mfano:***

1. Kuna maelezo kuhusu jukwaa lilivyopangwa.
2. Maelezo kuhusu hisia za wahusika yametolewa hasa katika mabano.

## Zoezi la 5, ukurasa 36

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi kuhusiana na mchango wa tamthilia ya Kinyarwanda ya '*Urunana*' katika kuimarisha hatua za kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi.

## Zoezi la 6, ukurasa 36

Mwalimu atathmini maigizo ya wanafunzi katika makundi yao. Ahakikishe kuwa wanafunzi wamezingatia matamshi bora na ujasiri wa kuigiza mbele ya wanafunzi wenzao.

## Zoezi la 7, ukurasa 36

Mwalimu atathmini majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao kuhusu tabia za wahusika *Stefano, James* na *Nadine* katika tamthilia ya Kinyarwanda pamoja na mchango wa tamthilia katika kuwasaidia vijana kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi.

## Zoezi la 8, ukurasa 37

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi kuhusu tabia za wahusika waliotajwa. Wanafunzi wanaweza kutaja sifa kama vile:

1. ***Aisha*** ni mhusika mwenye mapuuza kwa kuwa anapoingia chumbani, hatilii maanani kuwa wazee wake wapo chumbani na wanastahili kusalimiwa. Yeye anatamka tu salamu za jumla na kuendelea na shughuli zake. Aisha pia anadhihirisha kuwa amepuuza hali ya mumewe Sele kwa kuwa anasema hamwelewi mara nyingi anapoongea ila hasemi iwapo kunacho anachofanya ili kuhakikisha kuwa amemwelewa. Aidha, Aisha amekengeuka hivi kwamba anasema kuwa mwanamke wa sasa hana tofauti na mwanamume kwani yeye anakwenda na majira ya usasa.
2. ***Zainabu*** ni mtu makini sana. Anachunguza mienendo ya Sele na kujua tabia yake. Pia, anaelewa namna Aisha alivyo mpishi hodari. Zainabu pia ni mdadisi. Anamuuliza Bi. Rahma maswali mengi kuhusiana na suala la kumpeleka Sele kwa waganga ili afanyiwe kafara. Yeye pia ni karimu kwa kuwa anamwambia Aisha atayarishe chai itakayonywewa na bibiye pamoja na Sele.
3. ***Bi. Rahma*** ni mdadisi. Yeye anauliza maswali mengi kuhusu hali ya Sele pamoja na jamaa wengine. Halikadhalika, anamuuliza Aisha maswali mengi sana kuhusu namna anavyoishi. Yeye pia ni mcheshi. Anapoambiwa kuwa Sele hali vidagaa kwa kuvionea huruma kwa kuliwa na papa, yeye anamshauri Zainabu kumpikia papa ili alipize kisasi kwa niaba ya vidagaa. Ni mshirikina kwa kuwa anashikilia kauli kuwa Sele alistahili kupelekwa kwa mganga ili afanyiwe kafara. Kwake, anaamini kuwa kumpeleka Sele kwa mganga ndiko kutamponya.

## Zoezi la sarufi, ukurasa 37-38

**A.**

1. Maneno '*alikuwa akitusimulia hadithi*' ni kitenzi + kitenzi + nomino, hivyo yanaunda *kirai kitenzi*.
2. Maneno '*angali anafundisha darasani*' ni kitenzi + kitenzi + kielezi, hivyo yanaunda *kirai kitenzi*.
3. Maneno '*anacheza vizuri*' ni kitenzi + kielezi, hivyo yanaunda *kirai kitenzi*.
4. Maneno '*wanalima shamba kubwa*' ni kitenzi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda *kirai kitenzi*.
5. Maneno '*anafua nguo zake*' ni kitenzi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda *kirai kitenzi*.
6. Maneno '*unampiga mbwa huyo*' ni kitenzi + nomino + kivumishi, hivyo yanaunda *kirai kitenzi*.
7. Maneno '*siwezi kula nyama*' ni kitenzi + kitenzi + nomino, hivyo yanaunda *kirai kitenzi*.

**B.** Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi kuhusu tofauti kati ya kirai kitenzi na kirai nomino.

Msingi wa *kirai kitenzi* ni kitenzi ambacho hutangulia na msingi wa *kirai nomino* ni nomino ambayo hutangulia. Kwa mfano:

***Kirai kitenzi:*** Nguo ya mama <u>imelowa maji</u>. (*kitenzi +nomino)*

***Kirai nomino:*** <u>Nguo ya mama</u> imelowa maji. (*nomino+kivumishi 'a' unganifu*)

## Zoezi la 9, ukurasa 39

1. *'iliendelea kunyesha usiku kucha'* (vitenzi viwili + kielezi)
2. '*aliwafundisha wanafunzi kukariri mashairi'* (kitenzi + kirai nomino)
3. *'walipalilia mimea yao'* (kitenzi + kirai nomino)
4. *'alikuwa akipika wali'* ( vitenzi viwili + nomino)
5. *'waliabiri basi jipya'* ( kitenzi + kirai nomino)

**Zoezi la 10, ukurasa 39**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe miundo mbalimbali ya virai vitenzi.

***Kwa mfano:***

1. Mwandishi <u>*ameandika tamthilia nzuri sana*</u>.

   Kirai kitenzi kimeundwa kwa '*kitenzi* + *kirai nomino chenye nomino na kirai kivumishi*'

2. Wanafunzi <u>*watakariri shairi fupi*</u>.

   Kirai kitenzi kimeundwa kwa '*kitenzi* + *kirai nomino chenye nomino na kivumishi*'

3. Gloria <u>*ameamka alfajiri na mapema*</u>.

   Kirai kitenzi kimeundwa kwa '*kitenzi* + *kirai kielezi*'

4. Neli <u>*atafika sasa*</u>.

   Kirai kitenzi kimeundwa kwa '*kitenzi* + *kielezi*'

5. Mwalimu Julia <u>*amewasili darasani humo*</u>.

   Kirai kitenzi kimeundwa kwa *'kitenzi + kirai nomino chenye nomino na kivumishi'*

# Somo la 5: Utanzu wa ushairi

## Vipindi 56-57: Kusoma shairi

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi shairi husika kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kuchunguza kwa usahihi utanzu wa ushairi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mashairi ya waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Mashairi yaliyorekodiwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 40-41;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ufafanuzi wa utanzu wa ushairi. Ushairi ni utanzu mojawapo wa fasihi andishi ambao hutumia maneno machache teule ambayo hupangwa katika beti na kuwasilishwa kisanaa. Utanzu huu ni tofauti na tanzu nyingine za fasihi kwa sababu huzingatia sheria (arudhi) fulani katika utunzi wake. Ujumbe wa shairi huandikwa kwenye mistari (mishororo) ya beti kadhaa. Katika utanzu wa ushairi, mandhari huwa finyu sana ikilinganishwa na ilivyo kwenye tanzu nyingine za fasihi andishi. Vilevile, ni vyema mwalimu awe tayari kushughulikia sarufi katika somo hili. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kufahamu maana ya kishazi pamoja na aina za vishazi. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kufahamu tofauti iliyopo kati ya kishazi huru na kishazi tegemezi katika Kiswahili. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelezo yaliyotolewa kwa kila zoezi husika.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wake maswali mepesi kuhusiana na funzo lililopita kuhusiana na fasihi andishi hasa kuhusu utanzu wa tamthilia. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilichotangulia. Baada ya haya, mwalimu atangulize funzo hili kuhusu utanzu wa ushairi. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha kuhusiana na michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 40. Maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye michoro hii? Watu wanaoonekana wanafanya nini?* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona..."*. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na wanayoyaona katika michoro waliyopewa. Kwa mfano: "*Mimi ninawaona ng'ombe wakiwa zizini wakila majani... Mimi ninawaona watu wanaopanda miti n.k."*

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea au wanachokiona katika michoro hiyo. Kutokana na michoro hiyo, wanafunzi wataweza kukisia shairi watakalosoma linahusu nini. Bila shaka shairi hilo linahusu kuyalinda mazingira.

## 5.1 Kusoma na kufahamu

### *Shairi kuhusu kuyalinda mazingira*

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wasome kwa kimya shairi walilopewa kuhusu kuyalinda mazingira. Wanafunzi wasome shairi hilo kwa kimya huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu shairi hilo walilosoma ili kuhakikisha kuwa wamelielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Waharibifu wa misitu wafanyiwe nini? Njaa na ukame vitaangamizwa vipi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika shairi husika. Kwa mfano: *Waharibifu wa misitu wachukuliwe hatua kali kisheria. Tunahimizwa kupanda mahindi mengi na mazao mengine ili kuangamiza njaa na ukame.*

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti shairi hili ili kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi wote pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya shairi huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika shairi hilo.

## Tathmini ya vipindi 55-57

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea ufafanuzi na uchambuzi wa shairi. Sehemu za shairi, maudhui pamoja na dhamira ya mwandishi irejelewe katika kuhakiki iwapo wanafunzi wameuelewa utanzu huu wa ushairi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kubaini sifa za utanzu wa ushairi kwa kutumia shairi walilopewa.

## Vipindi 58-59: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na utanzu wa ushairi;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na utanzu wa ushairi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za ushairi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Mashairi yaliyorekodiwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 42;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ujifunzaji wa msamiati unaohusiana na shairi lililopo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 40-41 pamoja na utanzu wa ushairi kwa jumla.

Mwalimu aandae mifano ya mashairi kadhaa ambayo anaweza kuwapa wanafunzi wayasome darasani na kuchambua msamiati wake katika makundi mbalimbali. Pia, mwalimu anaweza kuandaa mashairi kadhaa yaliyorekodiwa ili wanafunzi wayasikilize darasani na baadaye kuchambua msamiati wake. Mashairi haya yanaweza kukaririwa kwa mahadhi mbalimbali. Mwalimu anaweza kufanya maandalizi haya mapema kabla ya vipindi hivi.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita kuhusu utanzu wa tamthilia. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilichotangulia.

## 5.2 Kujifunza msamiati wa shairi kuhusu kuyalinda mazingira

Mwalimu atangulize somo hili kuhusu msamiati unaohusiana na utanzu wa ushairi. Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wafanye zoezi la 1 kwa kujadili maana za msamiati mpya waliopatana nao katika usomaji wao na jinsi msamiati huo ulivyotumiwa katika shairi walilosoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale inapohitajika. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua msamiati husika. Baadaye wanafunzi washirikishwe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati walioufafanua kama ulivyotumiwa kwenye shairi walilosoma.

Baada ya haya, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze msamiati waliopewa katika zoezi la 2 sehemu A pamoja na maelezo sahihi ya msamiati huo katika sehemu B kisha wauambatanishe kwa usahihi msamiati huo na maelezo hayo.

Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika shairi

walilosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba matumizi ya msamiati husika katika maongezi au maandishi ndiyo yatakayomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha sahihi.

## Tathmini ya vipindi 58-59

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali hayo yaegemee hasa katika kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mpya wa utanzu wa shairi katika maandishi na maongezi yao.

## Vipindi 60-61: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu sifa bainifu za utanzu wa ushairi;
- Kujadili tofauti zilizopo kati ya utanzu wa ushairi na utanzu wa riwaya.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za ushairi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Mashairi yaliyorekodiwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 42-43;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha ambapo majadiliano kuhusiana na sifa bainifu za utanzu wa ushairi yatahusishwa. Mwalimu anaweza kuandaa mashairi yaliyoandikwa ambayo wanafunzi wanaweza kuyasoma darasani au hata kuyakariri kwa mahadhi mbalimbali. Pia, mwalimu anaweza kuandaa mashairi yaliyorekodiwa ambayo wanafunzi wanaweza kuyasikiliza darasani. Kwa upande mwingine, mwalimu anaweza kuandaa chati zenye kuonyesha sifa bainifu za utanzu wa ushairi.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita kuhusu shairi la kuyalinda mashairi. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wanaweza kufafanua ujumbe wa shairi hilo na muundo wa shairi hilo kama kuwepo kwa beti, mistari au mishororo n.k.

## 5.3 Majadiliano kuhusu sifa bainifu za utanzu wa ushairi

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wajadili kuhusu:

1. *Sifa bainifu za utanzu wa ushairi.*
2. *Tofauli zilizopo kati ya utanzu wa ushairi na utanzu wa riwaya.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kuzieleza sifa bainifu za utanzu wa ushairi. Baadhi ya sifa hizo ni kama vile:

1. *Utanzu wa ushairi huwa na muundo maalum.*
2. *Shairi hufumbata ujumbe mpana kwa kutumia maneno machache teule.*
3. *Ushairi hutumia tamathali za semi kwa wingi zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi andishi.*
4. *Utanzu wa ushairi huzingatia sheria (arudhi) maalum katika utunzi wake.*
5. *Ushairi ni kazi ya kubuni kwa kutumia lugha teule.*

Mbali na hayo, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili kuhusu tofauti na ulinganisho uliopo kati ya utanzu wa ushairi na utanzu wa riwaya.

Mojawapo ya tofauti kuu kati ya shairi na riwaya ni kuwa shairi huwasilisha ujumbe wake kwa kutumia beti kadhaa ilhali ujumbe wa riwaya huandikwa katika aya ambazo hufululiza kutoka mwanzo hadi mwisho. Ulinganisho uliopo kati ya riwaya na shairi ni kuwa ujumbe za tanzu hizi mbili huandikwa kwa kinathari yaani kwa mfululizo kinyume na ilivyo katika utanzu wa tamthilia. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kujadili tofauti na ulinganisho zaidi wa utanzu wa ushairi na utanzu wa riwaya.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kufanya zoezi la 3 lililo katika vitabu vyao kuhusu kujadili vina, kibwagizo, beti, mizani, mishororo na maudhui kwa kurejelea shairi walilosoma hapo awali kuhusu kuyalinda mazingira.

## Tathmini ya vipindi 60-61

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kikundi kuhusiana na sifa bainifu za utanzu wa ushairi pamoja na tofauti zilizopo kati ya utanzu huu na utanzu wa riwaya pamoja na tanzu nyingine pia.

## Vipindi vya 62-63: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kukariri shairi kwa mahadhi mbalimbali;
- Kuchambua shairi kwa kuzingatia sifa zake bainifu.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mashairi ya waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Rekodi za mashairi mbalimbali;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 43;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia vipindi hivi utanzu wa ushairi pamoja na umuhimu wa utanzu huu kwa jamii. Mwalimu anaweza kuandaa rekodi za mashairi kadhaa ambazo wanafunzi wanaweza kusikiliza darasani na kisha wakabaini sifa zaidi za utanzu huu. Pia, mwalimu anaweza kuandaa mashairi kadhaa ambayo wanafunzi wanaweza kuyasoma darasani. Wanafunzi wanaweza kupewa vitabu vya mashairi wanayoweza kuyasoma kabla ya vipindi hivi.

### d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilichopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi ambalo wanafunzi walipewa katika kipindi kilichopita limesahihishwa na wanafunzi waliokuwa na matatizo wameelekezwa. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamepata uelewa wa vipashio mbalimbali vya shairi kama vile: vina (vya kati na nje), beti, mishororo, mizani, kibwagizo n.k.

## 5.4 Kukariri shairi

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaongoze wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili waweze kusoma shairi walilopewa katika vitabu vyao kuhusu kuyalinda mazingira kisha walikariri. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua mahadhi tofauti tofauti ya kukariri shairi. Mwalimu anaweza kutumia mashairi mbalimbali aliyoyarekodi kwa mahadhi tofauti tofauti. Wanafunzi wanaweza kusikiliza rekodi hizo kisha wakajaribu kukariri shairi walilopewa kuhusu kuyalinda mazingira kwa mahadhi tofauti tofauti. Sehemu hii ipanue ujuzi wa wanafunzi kuhusu vipashio vyote vinavyoangaziwa katika utanzu wa ushairi. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wajitokeze mbele ya darasa ili wawakaririe wenzao shairi kuhusu kuyalinda mazingira kwa kutumia mahadhi mbalimbali. Wanafunzi wengine nao wasikilize namna wanafunzi wenzao wanavyolikariri shairi hilo. Kila kikundi kipewe muda wa kuchangia katika mawasilisho ya wenzao huku wakiongozwa na mwalimu.

Baada ya majadiliano haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao wajadiliane kuhusu mambo muhimu yaliyopatikana katika shairi walilosoma darasani kuhusu kuyalinda mazingira na kuyalinganisha na maisha yao ya kila siku. Wanafunzi waelezane katika makundi yao jinsi kuyalinda mazingira kumeyaathiri maisha yao ya kila siku.

Aidha, mwalimu awaongoze wanafunzi katika kueleza umuhimu wa kuwepo kwa utanzu wa ushairi kwa jamii mbalimbali. Wanafunzi wanaweza kujadiliana katika makundi yao. Umuhimu wa utanzu wa ushairi ni sawa na umuhimu wa fasihi kwa ujumla. Kwa mfano, utanzu huu hutumika kuhifadhi historia na utamaduni wa jamii mbalimbali, kuelimisha, kuburudisha, kuasa, kuonya, kukashifu tabia zisizokubalika katika jamii.

## Tathmini ya vipindi 62-63

Mwalimu atathmini iwapo ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha baada ya vipindi hivi. Kwa hivyo, awaulize wanafunzi maswali mepesi ya kupima uwezo wao wa kurejelea sifa bainifu za utanzu wa ushairi pamoja na umuhimu wa utanzu huu kwa jamii.

Vilevile, maswali mengine yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kujadiliana katika makundi kuhusu namna mashairi mbalimbali waliyosoma yanachangia katika kuboresha maisha yao ya kila siku. Mbali na hayo, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wamezielewa stadi za maisha kupitia maswali mbalimbali yanayohusiana na vipashio vya ushairi pamoja na umuhimu wake kwa jamii.

## Vipindi vya 64-65: Sarufi (Vishazi)

### a) Malengo ya somo

- Kufahamu maana ya kishazi;
- Kutambua aina za vishazi;
- Kutofautisha aina za vishazi;
- Kutunga sentensi sahihi kisarufi yenye vishazi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha aina za vishazi na miundo yao;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 43-46;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ajiandae kufundisha vipindi hivi. Mwalimu atunge mifano kadhaa ya vishazi mbalimbali katika Kiswahili. Mifano hii kadhaa itamwezesha kuwafundisha wanafunzi sehemu hii ya sarufi kuhusu vishazi pamoja na aina zake katika Kiswahili. Iwapo mwalimu ana wanafunzi walio na matatizo ya kuona, basi itambidi kutunga na kuandika vishazi mbalimbali kwenye breli kwa

manufaa ya wanafunzi hao. Kwa wanafunzi walio na matatizo ya kusikia, lugha ishara inaweza kutumika pamoja na kuiandika mifano ya mwalimu ubaoni.

### d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali kuhusu kipindi kilichopita cha sarufi hasa kuhusiana na virai na aina zake mbalimbali. Kupitia kwa maswali haya, wanafunzi wataweza kuelewa kwa uwazi tofauti iliyopo kati ya kirai na kishazi. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu kipindi hicho cha hapo awali. Mwalimu achukue fursa hii ya utangulizi ili kuwaomba wanafunzi kusahihisha mazoezi waliyopewa kutokana na kipindi kilichopita. Mwalimu aendeleze funzo hili  kwa kuwaomba wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kwa kila zoezi.

## 5.5 Maana ya kishazi

Ujifunzaji wa sarufi katika hatua hii uchukuliwe kama mwendelezo wa yale yaliyofundishwa katika sehemu ya sarufi kuhusu sentensi kamili na sentensi isiyo kamili katika masomo yaliyotangulia kwenye viwango vya hapo awali. Kwa hivyo, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa kwanza maana ya sentensi kamili katika Kiswahili. Uelewa wa dhana hii ya sentensi kamili na sentensi isiyo kamili utamwezesha mwalimu kufundisha kuhusu vishazi. Ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika kipengele hiki, mwalimu awaombe wanafunzi watunge sentensi mbalimbali zilizo na miundo mbalimbali ili kubaini sentensi zilizo kamili na zile zisizo kamili.

***Kwa mfano:***

1. *Mpira ulionunuliwa utatumiwa kuchezea kandanda. (sentensi kamili)*

Kutokana na mfano huu, sehemu ya '*ulionunuliwa* ' ikiondolewa sentensi itakayosalia (*Mpira utatumiwa kuchezea kandanda*) itakuwa na maana kamili ila sehemu hiyo iliyoondolewa haiwezi kujisimamia na kuwa na maana kamili ikiwa pekee yake.

2. *Wasichana wanaotembea wanaelekea sokoni. (sentensi kamili)*

Kutokana na mfano huu, sehemu ya '*wanaotembea'*  ikiondolewa sentensi itakayosalia ( *Wasichana wanaelekea sokoni*) itakuwa na maana kamili ila sehemu hiyo iliyoondolewa haiwezi kujisimamia na kuwa na maana kamili ikiwa pekee yake.

3. *Kitabu ambacho ni kipya kimepotea. (sentensi kamili)*

Kutokana na mfano huu, sehemu ya '*ambacho ni'* ikiondolewa sentensi itakayosalia (*Kitabu kipya kimepotea*) itakuwa na maana kamili ila sehemu hiyo iliyoondolewa haiwezi kujisimamia na kuwa na maana kamili ikiwa pekee yake.

Kutokana na zoezi hili, wanafunzi wataweza kutambua kuwa sentensi inaweza kutegemezwa kitenzi pamoja na kirejeshi ikawa kamili na wakati huo huo inaweza kujisimamia bila kuwepo kwa vitegemezi vyovyote.

Wanafunzi waelekezwe kufahamu kuwa kuna aina mbili za vishazi ambazo ni vishazi huru na vishazi tegemezi. Vishazi huru vinaweza kujisimamia kimaana ilhali vishazi tegemezi haviwezi kujisimamia kimaana hadi viongezewe maneno fulani fulani ya kuvipa maana kamili.

Baadaye katika makundi yao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuzichunguza sentensi zilizo katika *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 44* kisha wajadiliane kuhusu sehemu zinazounda sentensi hizo. Kwa mfano: *Embe lililooza litatupwa kwenye jaa la takataka'.* Katika sentensi hii, sehemu ya '*lililooza*' haiwezi kujitegemea kivyake hadi iongezewe maneno mengine. Sehemu hii ni kishazi kitegemezi. Sehemu ya '*Embe litatupwa kwenye jaa la takataka'* inajitosheleza kimaana. Sehemu hii ni kishazi huru.

Baadaye, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamepata ujuzi kamili katika kutambua na kuzielewa aina mbili za vishazi na kuweza kuzitungia sentensi sahihi kisarufi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 5 katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ambapo wanafunzi wanatakiwa kubainisha vishazi vilivyotumika katika sentensi walizopewa.

Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na maelezo ya mwalimu yatilie mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwishowe, mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la 6, 7 na 8 katika sehemu hii. Mwalimu ahakikishe kuwa mazoezi haya yamesahihishwa kabla ya kipindi kijacho.

## Tathmini ya vipindi 64-65

Mwalimu ahitimishe vipindi hivi kwa kuuliza maswali yanayodhamiria kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa maana ya kishazi na aina zake mbili pamoja na kuainisha vishazi katika sentensi. Wanafunzi pia waulizwe maswali mepesi ya kubaini iwapo wamefahamu tofauti kati ya kishazi tegemezi na kishazi kamili. Wanafunzi nao, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kwa kudhihirisha iwapo wameelewa mambo yote muhimu yaliyotakikana kuzingatiwa katika vipindi hivi.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

**A.** Sanaa ya lugha teule na lugha ya kisanaa inayotumia mpangilio na uteuzi maalum wa maneno na sauti ili kupitisha ujumbe fulani huitwa **shairi**.

Shairi huwa na vipashio vifuatavyo:

- ***Vina*** - silabi za mwisho wa kila kipande katika mshororo
- ***Mizani*** - idadi ya silabi katika maneno ya kila mshororo
- ***Mshororo*** - mstari mmoja wa maneno katika ubeti wa shairi
- ***Ubeti*** - kifungu cha mishororo kadhaa
- ***Mloto*** - mshororo wa pili katika ubeti
- ***Kimalizio/ Kiishio*** - mshororo wa mwisho katika ubeti usiorudiwarudiwa katika kila ubeti
- ***Kibwagizo*** - mshororo wa mwisho katika ubeti unaorudiwarudiwa kila ubeti
- Mshairi hufupisha au kurefusha maneno ili kutosheleza idadi ya mizani

**B.** Kundi la maneno ambalo lina ujumbe uliokamilika au usiokamilika likiwa ndani ya sentensi kuu huitwa ***kishazi***.

Kuna kishazi chenye sentensi moja huru au sentensi mbili huru zinazounganishwa kwa kiunganishi au kishazi chenye sentensi mbili zinazosaidiana kutoa maana kamili.

Kuna aina mbili kuu za vishazi:

a) Vishazi huru

b) Vishazi tegemezi

- Vishazi huru ni sentensi zinazojitegemea, zenye maana kamili.

  **Mifano:** *Wakulima wanalima shamba* **na** *wafugaji wanalisha mifugo.*

- Vishazi tegemezi ni vipande katika sentensi kuu ambavyo vikiondolewa katika muktadha wa sentensi kuu, haviwezi kusimama peke yake kama sentensi kamili.

  **Mfano:** *Akifagia nyumba* wageni watakaribishwa.

Sehemu ya '*akifagia nyumba'* haiwezi kuwa sentensi kamili pekee yake hadi iambatanishwe na maneno mengine.

## 5.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango cha chini cha wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

***Kwa mfano:***

Tenganisha na uonyeshe aina za vishazi katika sentensi hizi.

1. Ukimtekenya mtoto mdogo sana atalia.
2. Dawa za kulevya zinapotumiwa husababisha wendawazimu.
3. Mpira ambao ni mpya umepotea.
4. Watoto wanaorandaranda mjini watatengewa makao yao.
5. Wazee wanakunywa pombe lakini vijana wanakunywa sharubati.

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu**

1. Ukimtekenya mtoto mdogo sana atalia.

   '*Ukimtekenya*' ni kishazi tegemezi ilhali '*mtoto mdogo sana atalia'* ni kishazi huru.
2. Dawa za kulevya zinapotumiwa husababisha wendawazimu.

   '*zinapotumiwa*' ni kishazi tegemezi ilhali '*Dawa za kulevya husababisha wendawazimu'* ni kishazi huru.
3. Mpira ambao ni mpya umepotea.

   '*ambao ni*' ni kishazi tegemezi ilhali '*mpira mpya umepotea'* ni kishazi huru.
4. Watoto wanaorandaranda mjini watatengewa makao yao.

   '*wanaorandaranda mjini*' ni kishazi tegemezi ilhali '*watoto watatengewa makao yao'* ni kishazi huru.
5. Wazee wanakunywa pombe lakini vijana wanakunywa sharubati.

   '*Wazee wanakunywa pombe*' ni kishazi huru na '*vijana wanakunywa sharubati'* pia ni kishazi huru.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao,

mwalimu awaombe watunge sentensi tano sahihi kisarufi kwa kutumia vishazi mbalimbali.

***Kwa mfano:***

*Wanafunzi waliotia bidii mwaka jana wamepita mtihani.*

'*waliotia bidii mwaka jana*' ni kishazi tegemezi ilhali '*wamepita mtihani'* ni kishazi huru.

## 5.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 41

1. Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.
2. Kilimo hutusaidia kujikimu kibiashara na hutupatia chakula.
3. Mazao ya mifugo ni muhimu kwa binadamu. Mifugo hutupatia maziwa na nyama kama chakula. Ngozi ya wanyama hutumika katika viwanda vya kuundia viatu na mikoba.
4. Beti sita
5. Nguru, dagaa na sangara
6. Hazina limetumika kama pesa.
7. Vina vya kati ni '***we***' na '***ma***' na vina vya mwisho ni '***mu***' na '***ra***'.
8. Mishororo thelathini (30).
9. Katika shairi, mwandishi anasema kuwa mashamba ni sharti yalimwe na mifugo kufugwa ili kujikimu kimaisha. Anasema pia biashara ifanywe kwa kuwa ni jukumu letu. Mwandishi anasisitiza umuhimu wa kuyalinda mazingira kwa kutokata miti. Maziwa sharti yalindwe ili tupate samaki wa kila aina na wanaoharibu maziwa wakemewe na kuadhibiwa. Mwandishi pia anasisitiza kuhusu usafi wa kila mahali kwa kuyalinda mabonde yanayotupa hewa safi.
10. Mizani ya ubeti wa kwanza:

    Mshororo wa 1: 8, 8

    Mshororo wa 1: 8, 8

    Mshororo wa 1: 8, 8

Mshororo wa 1: 8, 8

Mshororo wa 1: 8, 8

**Zoezi la 1, ukurasa 42**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati kutoka kwenye shairi walilosoma. Pia, atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga.

***Kwa mfano:***

1. ***Tujikimu -*** tujipatie mahitaji muhimu ya kimaisha kwa kufanya kazi
2. ***Waharibu -*** wanaoharibu

**Matumizi katika sentensi:**

1. Tumeajiriwa kama wafagizi ili ***tujikimu*** kimaisha.
2. Serikali itawafungulia mashtaka ***waharibu*** wa mazingira.

**Zoezi la 2, ukurasa 42**

| | |
|---|---|
| 1. - CH | 2. - A |
| 3. - G | 4. - I |
| 5. - H | 6. - D |
| 7. - J | 8. - E |
| 9. - F | 10. - B |

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 42**

**i) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa ushairi**

1. Huwa na muundo maalum. Yaani, hupangwa katika beti zinazoundwa kwa mishororo.
2. Ni kazi ya kubuni kwa kutumia lugha.
3. Hufumbata ujumbe mpana wa maneno machache teule.
4. Hutumia tamathali za usemi kwa wingi zaidi kuliko tanzu nyingine.
5. Huzingatia sheria/ arudhi fulani katika utunzi wake.
6. Hushikana zaidi na hisi- hisi za mapenzi, chuki, faraja au hata werevu hujidhihirisha katika shairi.

7. Hubeba mawazo, fikira, falsafa na hisia za mwandishi katika mtazamo wake kibinafsi na kuziwasilisha kwa hadhira.

**ii) Tofauti kati ya utanzu wa ushairi na utanzu wa riwaya**

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi. Wanaweza kutaja hoja kama vile:

1. Shairi huandikwa kwa lugha mkato na hupangwa katika beti ilhali riwaya huandikwa kwa lugha ya kinathari na hupangwa katika aya kadhaa.
2. Maneno katika shairi huwa teule na huweza kuandikwa kwa mbinu za kisanaa kama vile kufupisha (inkisari) na kubadilisha namna ya mwendelezo wa maneno fulani (tabdila) ilhali maneno katika riwaya hayabadilishwi kimaendelezo kwani riwaya huandikwa kwa lugha sanifu aghalabu bila ya kuiboronga.
3. Shairi halitoi maelezo kuhusu wahusika wake ilhali riwaya huwa na maelezo ya wahusika kuhusu wasifu wao, mavazi, tabia na dosari zao.

## Zoezi la 3, ukurasa 43

1. Vina ni silabi za namna moja zinazopatikana katikati na/au mwishoni mwa mishororo. Katika shairi hili, vina vya kati ni '***we***' na '***ma***' ilhali vina vya mwisho ni '***mu***' na '***ra***'.
2. Kibwagizo ni mshororo wa mwisho unaorudiwarudiwa katika kila ubeti. Kibwagizo hubeba kiini cha shairi. Kibwagizo hurudiwarudiwa katika kila ubeti. Kibwagizo cha shairi hili ni: ***Sote tusimame wima, tuyalinde mazingira.***
3. Ubeti (wingi ni beti) ni kifungu katika shairi kinachojitosheleza kimaana. Shairi hili lina beti sita.
4. Mizani ni silabi zinazotamkika katika maneno ya mshororo. Shairi hili lina mizani ya kumi na sita (16) katika kila mshororo, themanini (80) katika kila ubeti na mia nne na themanini (480) katika shairi zima.
5. Mshororo ni mstari katika ubeti. Shairi lina mishororo mitano katika kila ubeti na kwa jumla, shairi lina mishororo thelathini (30). Mshororo wa kwanza huitwa ***mwanzo***, wa pili ni ***mloto***, wa tatu ni ***mleo*** na wanne ni ***mwandamizi***.
6. Mawazo makuu katika shairi ni jumla ya mambo yanayozungumziwa kwenye shairi husika. Katika shairi hili, mwandishi anasema kuwa

mashamba ni sharti yalimwe na wanyama kufugwa ili kujikimu kimaisha. Anasema pia biashara ifanywe kwa kuwa ni jukumu letu. Mwandishi anasisitiza umuhimu wa kuyalinda mazingira kwa kutokata miti. Maziwa sharti yalindwe ili tupate samaki wa kila aina na wanaoharibu maziwa wakemewe na kuadhibiwa. Mwandishi pia anasisitiza kuhusu usafi wa kila mahali kwa kuyalinda mabonde yanayozaa hewa safi.

**Zoezi la 4, ukurasa 43**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kulikariri shairi husika. Anaweza kuanza kwa kukariri shairi kwa mahadhi fulani ili wanafunzi nao waige atakavyokariri.

**Zoezi la sarufi, ukurasa 43-44**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi, kwa mfano:

1. Sehemu ya '*lililotiwa hamira*' sio sentensi kamili (ni kishazi tegemezi). Sehemu ya '*andazi linafura na kujaa vizuri*' ni sentensi kamili (ni kishazi huru).
2. Sehemu ya '*waliotia bidii mwaka jana*' sio sentensi kamili (ni kishazi tegemezi). Sehemu ya '*wanafunzi walipita mtihani*' ni sentensi kamili (ni kishazi huru).
3. Sehemu ya '*alilonunua*' sio sentensi kamili (ni kishazi tegemezi). Sehemu ya '*shati limefuliwa na dadake*' ni sentensi kamili (ni kishazi huru).
4. Sehemu ya '*Kalisa anasoma Hisabati*' ni sentensi kamili (ni kishazi huru). Sehemu ya '*Gatete anachora michoro*' ni sentensi kamili (ni kishazi huru).
5. Sehemu ya '*nitawajibika*' ni sentensi kamili (ni kishazi huru). Sehemu ya '*utafaidika*' ni sentensi kamili (ni kishazi huru).

**Zoezi la 5, ukurasa 44**

1. a. aliyeishi hapa naye *(kishazi tegemezi*)
   b. Mwanamke alipoteza mtoto wake. (*kishazi huru*)
2. a. aliyepoteza maisha jana (*kishazi tegemezi*)
   b. Mtoto amepokelewa mbinguni. (*kishazi huru*)
3. a. alipomaliza masomo ya chuo mwaka jana naye *(kishazi tegemezi*)
   b. Gisa alipata shahada ya kwanza. (*kishazi huru*)
4. a. Watoto wanacheza. (*kishazi huru*)
   b. Wazazi wamekaa sebuleni. (*kishazi huru*)

5. a. Wavulana walishinda mabao mengi. (*kishazi huru*)
   b. Refa amewaonea sana. (*kishazi huru*)
6. Mama Kamana alifua nguo zake. (*kishazi huru*)
7. Mutoni ataondoka kesho. (*kishazi huru*)
8. Ninawapenda wote. (*kishazi huru*)
9. ` Waziri alizindua mkutano. (*kishazi huru*)
10. Mwenyekiti alisoma hotuba nzuri sana. (*kishazi huru*)

## Zoezi la 6, ukurasa 45

1. angewahi
2. alipigwa kalamu
3. tutafurahia
4. nitamweleza
5. atapelekwa
6. kukabidhiwa
7. alimwandalia
8. aliwadharau
9. kutupatupa
10. aliyefyatua

## Zoezi la 7, ukurasa 45

1. ***Kishazi huru*** ni kundi la maneno ambalo likitengwa kutoka kwa sentensi kuu litakuwa na: ujumbe uliokamilika, muundo wa kiima na kiarifu na pia sifa zote za sentensi. Kwa hivyo, kundi hili litakuwa sentensi zinazojitegemea. **Kwa mfano:**
   a. ***Kaka anasoma tamthilia*** ilhali ***dada anakariri shairi***.

      Sehemu za sentensi zilizokolezwa rangi zikitengwa na sentensi hiyo kuu bado zitajisimamia kimaana kama ifuatavyo:
   a. Kaka anasoma tamthilia.
   b. Dada anakariri shairi.
2. ***Kishazi tegemezi*** ni kundi la maneno ambalo likiondolewa katika muktadha wa sentensi kuu: haliwezi kuwa na ujumbe kamili, haliwezi kuwa na muundo wa kiima na kiarifu, haliwezi kuwa na sifa muhimu za sentensi, huondoa maelezo ya ziada katika sentensi na haliathiri sentensi pakubwa iwapo litatolewa kwa sababu maana kuu husalia.

***Kwa mfano:***

a. Mwalimu **aliyenifundisha kughani mashairi** amefariki leo asubuhi.

Sehemu ya sentensi iliyokolezwa rangi ikiondolewa, sentensi hiyo bado itaeleweka. Yaani, sentensi itakuwa: *Mwalimu amefariki leo asubuhi*. Hicho kitakuwa kishazi huru. Kishazi tegemezi ni sehemu ya sentensi iliyokolezwa rangi: *aliyenifundisha kughani mashairi*.

## Zoezi la 8, ukurasa 46

1. a. Kalisa aliandika vitabu (kishazi huru)
   b. Mkewe aliona asimulie hadithi (kishazi huru)
2. a. Wanawake walianzisha biashara (kishazi huru)
   b. Watoto wao hawasomi (kishazi huru)
3. a. Watumishi waliondoka (kishazi huru)
   b. Wake zao walibaki hapa (kishazi huru)
4. a. Tamthilia iliigizwa (kishazi huru)
   b. Mwalimu alikuwa nje (kishazi huru)
5. a. Umenitukana (kishazi huru)
   b. Unanipiga (kishazi huru)
6. a. Sichezi (kishazi huru)
   b. Sifanyi kazi (kishazi huru)
7. Walipoingia walishangaa sana (kishazi huru)
8. a. mtihani huo (kishazi tegemezi)
   b. Angeshinda angepewa ajira. (kishazi huru)
9. Aliyefundisha si mwalimu wetu. (kishazi huru)
10. a. kwenye miradi mingi (kishazi tegemezi)
    b. Angaliwekeza angalipata pesa nyingi (kishazi huru)

## Majibu ya tathmini ya mada ya 1

### Zoezi la 1, ukurasa 46

**a) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa riwaya:**

1. Riwaya ni utanzu wa fasihi andishi.
2. Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo huchukua muda mrefu kuandikwa na huwa na wahusika wengi na wa aina nyingi. (wakuu na wadogo)
3. Mhusika mkuu ndiye huwakilisha mawazo muhimu ya mwandishi.
4. Katika riwaya, matukio mara nyingi huwa ni tata. Migogoro mingi hujengwa ili kukuza maudhui na mtiririko.
5. Mtunzi wa riwaya huwa hayafahamu maoni ya wasomaji, yaani hujitenga na hadhira.
6. Riwaya huwa na maneno mengi sana, zaidi ya kurasa sitini.
7. Riwaya huwa na maelezo ya simulizi kulingana na vile hadithi inavyotokea kiwakati na kimasafa.
8. Riwaya huwa na maelezo ya wahusika kuhusu wasifu wao, mavazi yao, tabia zao, sifa na dosari, matendo yao yanavyoathiri nafsi zao na kuwaathiri wahusika wengine.
9. Riwaya huwa na urefu wa kutosha kuyashughulikia mahitaji ya mtunzi.
10. Riwaya huchunguza kwa kina jamii inavyosawiriwa.

**b) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa ushairi:**

1. Utanzu wa ushairi huwa na muundo maalum.
2. Shairi hufumbata ujumbe mpana kwa kutumia maneno machache teule.
3. Ushairi hutumia tamathali za semi kwa wingi zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi andishi.
4. Utanzu wa ushairi huzingatia sheria (arudhi) maalum katika utunzi wake.
5. Ushairi ni kazi ya kubuni kwa kutumia lugha teule.

**ch) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa tamthilia:**

1. Tamthilia hutawaliwa na mazungumzo na majibizano.
2. Tamthilia huwa na maelezo ya kumwelekeza msomaji ambayo huwa kwenye mabano na ambayo aghalabu hupendekeza jukwaa litakavyoonekana wakati wa maigizo.
3. Tamthilia hugawika katika sehemu (matendo na maonyesho) mbalimbali kutegemea matendo na matukio husika.
4. Tamthilia hushirikisha hadhira.
5. Tamthilia huwa na mgogoro fulani unaotanda katika hadithi nzima.

**d) Baadhi ya sifa bainifu za utanzu wa hadithi fupi:**

1. Huwa ni fupi inayoweza kusomeka katika kikao kimoja.
2. Huwa na wahusika wachache.
3. Huwa na mhusika mmoja mkuu ambaye humwongoza msomaji.
4. Hushughulikia tukio moja muhimu katika maisha ya mhusika mkuu.
5. Huwa haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo kwa kulinganisha na tanzu nyingine za fasihi andishi.
6. Hadithi fupi huhusisha usimulizi wa moja kwa moja.
7. Hadithi fupi hulenga sana kuibua hisia za msomaji kuliko kuchochea fikira zake.
8. Hadithi fupi huenda haraka kimatendo, kiwakati, kimasafa na kimatukio.

## Zoezi la 2, ukurasa 46

1.a) ***Riwaya*** ni hadithi ndefu ya kubuni ambayo huchukua muda mrefu kuandikwa na huwa na wahusika wengi na wa aina nyingi (wakuu na wadogo) ilhali ***hadithi fupi*** huwa haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo kwa kulinganisha na huwa na wahusika wachache. Hadithi fupi huweza kusomeka katika kikao kimoja kinyume na riwaya.

b) ***Tamthilia*** hutawaliwa na mazungumzo na majibizano ilhali shairi hufumbata ujumbe mpana kwa kutumia maneno machache teule yaliyopangwa kwenye beti kadhaa.

2. ***Maudhui*** ni ujumbe au mawazo makuu ya mtunzi kwa wasomaji wake ilhali ***dhamira*** ni sababu, lengo au nia ya mtunzi kubuni kazi yake ya kifasihi.

**Zoezi la 3, ukurasa 47**

a) Mtoto mrefu ameshinda mbio.

‘*ameshinda mbio’* ni kirai kitenzi

b) Nataka unipe kisu kikali.

‘*kisu kikali’* ni kirai nomino

ch) Sima na wali ni chakula kitamu.

‘*sima na wali’* ni kirai nomino

‘*chakula kitamu’* ni kirai nomino

d) Kalamu yenye rangi ya kijani iko wapi?

‘*yenye rangi ya kijani’* ni kirai kivumishi

e) Wazee wenye kondoo hawa wamekuja.

‘*wenye kondoo hawa’* ni kirai kivumishi

f) Wanafunzi waliondoka alfajiri na mapema.

‘*alfajiri na mapema’* ni kirai kielezi

g) Mama alikuwa amelala.

‘*alikuwa amelala’* ni kirai kitenzi

**Zoezi la 4, ukurasa 47**

a) Mama alifika leo alasiri.

‘*Mama alifika leo alasiri’* ni kishazi huru.

b) Mjomba alifika asubuhi lakini hakutuletea mkate.

‘*Mjomba alifika asubuhi’* ni kishazi huru.

‘hakutuletea mkate’ ni kishazi huru.

ch) Wachezaji ambao ni shupavu walishinda.

‘*Wachezaji walishinda’* ni kishazi huru.

‘*ambao ni shupavu’* ni kishazi tegemezi.

d) Waziri alifika baada ya watu kuondoka.

‘*Waziri alifika’* ni kishazi huru.

‘*baada ya watu kuondoka’* ni kishazi tegemezi.

e) Tunda lililo tamu litaliwa.

‘*Tunda litaliwa’* ni kishazi huru.

‘*lililo tamu’* ni kishazi tegemezi.

**Zoezi la 5, ukurasa 47**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi, kwa mfano:

*Fasihi huelimisha, huonya, huburudisha, huhifadhi historia ya jamii, hupongeza, hufunza maadili na kadhalika.*

**Zoezi la 6, ukurasa 48**

a) Sio sentensi kamili kwa sababu haina kitenzi.

b) Sio sentensi kamili kwa sababu haina kitenzi.

ch) Ni sentensi kamili kwa sababu ina kitenzi ‘ni’.

d) Sio sentensi kamili kwa sababu haina kitenzi.

e) Ni sentensi kamili kwa sababu ina kitenzi ‘huli’.

**Zoezi la 7, ukurasa 48**

a) ‘*Mwanafunzi mwerevu na mpole*’ ni kiima na ‘*ametuzwa na mwalimu mkuu*’ ni kiarifu.

b) ‘*Shule yetu ya sekondari*’ ni kiima na ‘*ina wanafunzi wengi sana*’ ni kiarifu.

ch) ‘*Choo chao*’ ni kiima na ‘*kimesafishwa na topasi yule*’ ni kiarifu.

d) ‘*Mama na baba*’ ni kiima na ‘*wanatazama runinga waliyonunuliwa jana*’ ni kiarifu.

e) ‘*Mimi na yeye*’ ni kiima na ‘*tuna bidii katika masomo yetu*’ ni kiarifu.

Sura ya **Pili**

# Mada Kuu 2: Fasihi katika Kiswahili

## Mada Ndogo: Uhakiki wa tanzu za fasihi andishi

## Uwezo upatikanao katika mada hii:

Mwanafunzi aweze kuelewa na kufuata mtindo wa kuchambua kazi za fasihi (vitabu, mashairi, nyimbo…) kwa minajili ya kukuza uelewa wa undani wa lugha na kutambua ujumbe unaojidhihirisha katika maendeleo ya fikira na utamaduni wa wananchi; kujua jinsi ya kunyambua kitenzi cha Kiswahili.

## Malengo ya kujifunza

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwendo mwema |
|---|---|---|
| • Kukumbuka utaratibu na hatua za kufuatwa wakati wa kuhakiki tanzu za fasihi andishi. | • Kuchambua au kuhakiki tanzu mbalimbali za fasihi andishi ya Kiswahili kutokana na ujuzi wa kuchambua alioupata. | • Mwanafunzi ataridhika na mtindo wa tanzu aliyochambua na kuwa na hamu ya kuiiga katika kazi za sanaa atakazoshughulikia kama msanii. |
| • Kuelezea athari za tanzu zilizoshughulikiwa kwa maisha ya jamii iliyolengwa. | • Kutoa tathmini ya tanzu ya fasihi andishi fulani aliyochambua kulingana na vipengele vya fani na maudhui. | • Mwanafunzi pia ataendeleza akili zake katika mambo ya kujadili, kutoa tafakari tunduizi, kutathmini n.k. |
| • Kutambua tofauti iliyopo kati ya tanzu za fasihi simulizi na tanzu za fasihi andishi wakati wa kuhakiki. | • Kutoa pendekezo kuhusu tabia za wahusika na athari zao katika ujenzi wa jamii. | • Kukuza na kuendeleza utamaduni wa jamii za Kiafrika. |

| | | |
|---|---|---|
| • Kunukuu sehemu fulani fulani za kazi ya sanaa inayohusika kwa kukamilisha tathmini yake. | • Kuhusianisha kichwa cha tanzu au jina la kitabu alichosoma na yaliyomo kisha kuhalalisha uteuzi wa jina hilo. | • Kujenga shauku na hatimaye kuingia katika dunia ya ubunaji wa fasihi andishi. |
| • Kutambua viambishi vya kitenzi kwa njia ya mnyambuliko. | • Kutoa hitimisho kwa kulinganisha matukio yaliyojitokeza katika utanzu ulioshughulikiwa na ukweli unaojidhihirisha leo. | |

## Maelezo kwa mwalimu

Mada hii inahusiana na masomo yanayohusu utafiti wa kielimu, kihistoria, uandishi wa shahada kwa wanafunzi wanaojitahidi kumaliza masomo yao katika vyuo vikuu.

Fasihi andishi katika Kiswahili itashughulikiwa katika sura hii. Fasihi andishi ni mojawapo ya matawi mawili makuu ya fasihi katika Kiswahili. Tawi jingine kando na fasihi andishi ni fasihi simulizi. Fasihi huhusisha matukio mbalimbali kuhusiana na jamii zetu na maisha yetu ya kila siku. Katika mada hii, tutajikita katika uhakiki wa tanzu za fasihi andishi. Tanzu hizi za fasihi andishi ni: *riwaya, hadithi fupi, ushairi* na *tamthilia*. Maana za tanzu hizi za fasihi andishi zitafafanuliwa pamoja na mifano kutolewa. Uhakiki wa tanzu hizi utaegemea kwenye dhamira, maudhui, mandhari pamoja na fani (matumizi ya lugha) katika kazi mbalimbali za kifasihi. Fasihi hutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya kiutamaduni na kiuchumi. Pia, watu huweza kujitegemea kupitia kwa sanaa ya fasihi andishi kwa kuwa waandishi, waigizaji na wakariri.

Mada hii pia inahusisha kutambua viambishi vya kitenzi kwa njia ya mnyambuliko.

## Masuala mtambuka

Masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni: *mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake, elimu ya pamoja, usawa wa kijinsia, amani na maadili.*

Wanafunzi watafundishwa umuhimu wa mazingira yao na namna ya kuyahifadhi. Fundisho hili litatekelezwa kupitia kwa tamthilia watakayoisoma pamoja na shairi watakalokariri. Katika kazi hizi za kifasihi, wanafunzi watazielewa njia mbalimbali za kuyahifadhi mazingira yao pamoja na mambo wanayofaa kujiepusha nayo ambayo huyaharibu mazingira yetu.

***Amani na maadili*** yatashughulikiwa kupitia kwa kazi za fasihi za waandishi mbalimbali ambazo wanafunzi watazisoma zinazogusia umuhimu wa umoja na ushirikiano wa wanajamii. Wanafunzi wataelekezwa kutangamana kwa amani na upendo hata katika shughuli zao za shuleni na hata nyumbani.

***Usawa wa kijinsia*** utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasichana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao licha ya jinsia zao tofauti. ***Elimu ya pamoja*** itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma kwa pamoja kwa kuwashirikisha hata wanafunzi wenye ulemavu na matatizo mbalimbali. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi wote kukubali na kushirikiana kwa pamoja na wenzao kutoka katika matabaka mbalimbali ya kijamii.

## Uwezo wa jumla

Mwalimu ahakikishe kuwa katika ufundishaji wa somo hili, wanafunzi wanapata uwezo wa kuwa na tafakuri tanduizi, stadi za utafiti, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu.

Ujifundishaji wa muda mrefu uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na fasihi andishi katika Kiswahili watakayotumia nje ya darasa katika maisha yao ya kila siku.

Mwalimu awaelekeze na awashirikishe wanafunzi wote katika kupata tafakuri tanduizi kwa kufikiri kwa undani zaidi kuhusiana na uhakiki wa tanzu mbalimbali za fasihi andishi watakazofundishwa. Ujuzi huu utawawezesha kuyajibu maswali katika somo hili kuhusiana na fasihi andishi katika Kiswahili.

Mazoezi ya kuigiza tamthilia na kukariri mashairi mbalimbali ambayo wanafunzi watakakumbana nayo yatawawezesha wanafunzi kupata uzoefu wa kuwasiliana kwa lugha rasmi pamoja na kuwa na utawala binafsi pamoja na kuzifahamu stadi mbalimbali za maisha. Stadi za utafiti zitakuzwa kupitia kwa wanafunzi kufanya utafiti kuhusiana na uhakiki wa tanzu mbalimbali za fasihi andishi katika Kiswahili.

## Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kuhusu uhakiki wa tanzu za fasihi andishi katika Kiswahili kama vile:

| | Msamiati | Maana |
|---|---|---|
| 1. | ***Uhakiki*** | uchunguzi wa ndani wa jambo au maandishi |
| 2. | ***maudhui*** | mawazo makuu yanayoelezwa katika masimulizi yoyote |
| 3. | ***fani*** | matumizi ya lugha ili kuonyesha umbo la nje la kazi ya kifasihi |
| 4. | ***mandhari*** | sura ya nchi ambapo matukio katika kazi za kifasihi hutendekea |
| 5. | ***vina*** | mapigo kamili ya sauti ambayo hupatikana kati na mwisho wa mishororo ya shairi |
| 6. | ***wahusika*** | viumbe ambao hutumiwa kutenda matukio mbalimbali katika kazi za kifasihi ili kujenga hadithi husika |
| 7. | ***mizani*** | silabi za maneno katika mishororo ya shairi |
| 8. | ***inkisari*** | mbinu ya kupunguza silabi katika maneno ya shairi ili kupata urari wa mizani |
| 9. | ***mishororo*** | mistari katika beti za shairi |
| 10. | ***dhamira*** | lengo, nia au sababu ya mtunzi wa kazi za kifasihi kutunga kazi yake |

## Usuluhishaji wa tatizo

Ili kushughulikia usuluhishaji wa tatizo katika mada hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kulingana na zoezi husika kisha awaombe wachunguze kwa makini michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 50 kuhusiana na mchoro wa kuonyesha fasihi andishi kupitia kwa wanafunzi wanaosoma vitabu vya hadithi pamoja na mchoro unaoonyesha fasihi simulizi kupitia kwa masimulizi ya babu kwa wajukuu wake. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika shughuli hii. Wanafunzi wachunguze michoro hiyo na mwalimu awaulize maswali kama vile: *Taja sifa za fasihi andishi. Taja sifa za fasihi simulizi*. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu maswali hayo na kuzielewa sifa za fasihi andishi pamoja na fasihi simulizi katika Kiswahili pamoja na tanzu zao mbalimbali. Kwa hivyo, mwalimu achochee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tanduizi kwa kuchunguza na kujibu maswali kuhusu uhakiki wa tanzu mbalimbali za fasihi andishi.

## Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Ili kuweza kuwashirikisha wanafunzi walio na ulemavu na matatizo mbalimbali, mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi hawa katika ujifundishaji wao. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, mwalimu ahusishe matumizi ya breli pamoja na vifaa vya kunasia sauti.

Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kusikia, mwalimu anaweza kuhusisha matumizi ya lugha ya ishara. Pia, mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri wa lugha ya ishara. Haya yatawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wanafunzi wenzao bila vikwazo vyovyote.

Nafasi ya wanawake na walemavu katika uhakiki wa tanzu mbalimbali za fasihi andishi itiliwe maanani kupitia kwa kazi mbalimbali za fasihi ambazo wanafunzi watasoma zikiwemo zilizo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*. Shughuli hii itasaidia katika kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja. Hili litadumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi.

## Orodha ya masomo na vipindi

| Mada ya somo | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| **Somo la 6:** | Uhakiki wa fasihi | 10 |
| **Somo la 7:** | Wahusika katika fasihi andishi | 15 |
| **Somo la 8:** | Maudhui na dhamira katika fasihi andishi | 10 |
| **Somo la 9:** | Mandhari katika fasihi andishi | 15 |
| **Somo la 10:** | Mbinu za lugha katika fasihi andishi | 15 |
| | | **JUMLA: 65** |

# Somo la 6: Uhakiki wa fasihi

## Vipindi 1-2: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha habari kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kubaini msamiati unaotumika katika fasihi ya Kiswahili;
- Kutambua tofauti kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi;

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Chati yenye kuonyesha matawi ya fasihi andishi na fasihi simulizi;
- Kazi za waandishi mbalimbali za kifasihi,
- *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 50;*
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Fasihi ni somo linalohusu maisha ya watu ya kila siku na inaibuka kila uchao. Mwalimu anastahili kutilia maanani dhana hii wakati wa uandalizi wa somo hili. Mwalimu akusanye vifaa vyake mapema na kuvihifadhi kabla ya vipindi hivi. Vifaa hivi ni kama vile: kazi za kifasihi za waandishi mbalimbali, chati yenye kuonyesha matawi ya fasihi andishi na fasihi simulizi miongoni mwa vifaa vingine. Kupitia michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 50, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua maana ya fasihi, maana ya fasihi simulizi, maana ya fasihi andishi, tanzu za fasihi andishi pamoja na tanzu za fasihi simulizi.

Wakati wa kuendesha somo hili, mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta darasani kwa kukumbuka kuwa matumizi ya michoro, picha, chati na vitabu halisi ni mbinu nzuri ambayo hutumika kuwafundisha wanafunzi; hasa wale ambao wana matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango cha chini katika ujifunzaji wao. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu ajitahidi kuandaa chati zake kwenye breli ili kuwawezesha wanafunzi wa aina hii kujifundisha kama wanafunzi wengine. Mwalimu atawaomba wanafunzi wa aina hii kuvigusa vifaa vilivyopo wakivitolea maelezo. Iwapo kuna wanafunzi walio na matatizo ya kusikia wavionyeshe vifaa vilivyopo kwa kuvigusa huku wakiandika maelezo yake ubaoni. Ili kutimiza malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu cha Mwanafunzi*.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu fasihi kutokana na vipindi vilivyotangulia. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu kisha waendelee kujibu maswali waliyoulizwa kuhusu fasihi katika Kiswahili. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kuchunguza michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa* 50. Mwalimu awachangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali mepesi kuhusiana na michoro hiyo. Baadhi ya maswali ambayo mwalimu anaweza kuuliza ni kama vile: *Michoro hii inasawiri aina gani ya fasihi*? *Watoto wanaoonekana wanafanya nini?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi ili waweze kujibu maswali hayo na kuelewa kinachoendelea katika michoro iliyopo. Kwa hivyo, mwalimu achochee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi, tafakuri tanduizi kwa kuchunguza na kujibu maswali kuhusu michoro hiyo. Vilevile, usawa wa kijinsia nao ugusiwe kwa kuonyesha nafasi kubwa ya mwanamke miongoni mwa wahusika waliopo na jinsi wanavyosoma na kusikiliza kwa pamoja. Mkazo utiliwe kuhusiana na ushirikiano unaojitokeza kati ya wasichana na wavulana ili waweze kufanikisha ujifundishaji wao.

## 6.1 Kusoma na kufahamu: Kifungu kuhusu fasihi katika Kiswahili

Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa kimya kifungu cha habari kinachohusika na kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Baadaye, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wamesoma na kuelewa kama alivyowaomba kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho walichosoma. Kwa mfano, anaweza kuwauliza: *Fasihi inagawanyika katika makundi mangapi? Tanzu za fasihi andishi ni zipi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kulingana na yale waliyoyasoma katika kifungu hicho. Kwa mfano: *Fasihi inagawanyika katika makundi mawili ambayo ni fasihi andishi na fasihi simulizi. Tanzu za fasihi andishi ni: riwaya, tamthilia, ushairi na hadithi fupi.* Mwalimu awaombe wanafunzi kusoma kwa sauti na kwa usahihi baada ya kutambua kwamba wanafunzi wamepata uelewa wa kile kinachozungumziwa katika kifungu kilichopo. Ni vyema mwalimu akumbuke kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapokosea.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu waliyopewa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanatatizika.

## Tathmini ya vipindi 1-2

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kufafanua makundi mawili ya fasihi yaliyopo katika Kiswahili, tanzu za fasihi andishi pamoja na tanzu za fasihi simulizi. Vilevile, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wanaweza kueleza tofauti zilizopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi.

## Vipindi 3-4: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati unaotumika katika fasihi andishi na fasihi simulizi;
- Kutaja tanzu za fasihi andishi na fasihi simulizi;
- Kutumia msamiati wa fasihi kwa usahihi katika sentensi na maongezi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za fasihi andishi na fasihi simulizi za waandishi mbalimbali;
- *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*;
- *Wanafunzi wenyewe*;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 52;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi unaofaa kuhusu msamiati unaotumika katika ufafanuzi wa fasihi andishi

na fasihi simulizi katika Kiswahili kupitia kwa kifungu watakachokisoma katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 50-52. Kwa kuwa kifungu walichopewa kinahusu makundi mawili makuu ambayo ni fasihi simulizi na fasihi andishi, ni vyema mwalimu alete vitabu mbalimbali vya fasihi andishi na fasihi simulizi ambavyo vinaweza kurahisisha uelewa wa msamiati katika mada hii.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza kuelewa somo hili aidha kwa kutumia lugha ya ishara au breli huku maelezo mengine yakiandikwa ubaoni. Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa shughuli hii ya wanafunzi ya kutambua na kuufafanua msamiati unaohusu fasihi andishi na fasihi simulizi.

## 6.2 Kujifunza msamiati kuhusu fasihi katika Kiswahili

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wajadiliane kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao wakati wao wa kusoma kifungu kinachohusika kuhusu fasihi katika Kiswahili. Ili kuimarisha stadi za utafiti na kudumisha uwezo wao wa kupata suluhisho kwa matatizo wanayokutana nayo, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze matumizi ya msamiati huo katika kifungu walichokisoma huku wakitumia kamusi pale wanapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Wanafunzi wajadiliane kwa kuzingatia maelekezo ya mwalimu wao. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati waliojadili. Katika kutunga sentensi zao, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wanapata ujuzi wa mawasiliano katika lugha rasmi, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano na hata utawala binafsi na stadi za maisha.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 2 ambapo wanahitajika kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa majibu sahihi kutoka kwa yale waliyopewa. Wanafunzi nao, katika makundi yao, wajadiliane kuhusu zoezi hilo. Mwalimu azunguke darasani ili kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika katika kufanya zoezi hili na baadaye awashirikishe wote katika kusahihisha zoezi hilo.

## Tathmini ya vipindi 3-4

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea msamiati mahususi uliopatikana katika kifungu cha habari walichokisoma kama vile: *fasihi, fasihi andishi, fasihi simulizi, tanzu, wahusika, maudhui, ushairi, riwaya, tamthilia* na kadhalika. Kwa hivyo, vifaa vilivyotumiwa kujifunzia somo hili vinaweza kutumiwa kuchunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kurejelea fasihi katika Kiswahili pamoja na makundi na tanzu zake mbalimbali.

## Vipindi 5-6: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kukuza stadi za utafiti za wanafunzi;
- Kujadili maudhui katika utanzu wa riwaya;
- Kujadili fani katika utanzu wa riwaya;

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali;
- Wanafunzi wenyewe;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 53;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali ambazo mwalimu alileta darasani au walizoleta wanafunzi zitumiwe kuwaongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kujadili maudhui katika fasihi andishi katika jamii. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu uhakiki wa maudhui katika fasihi andishi.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi katika makundi yao.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia kuhusu matumizi ya lugha. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

## 6.3 Matumizi ya lugha: Maudhui na fani katika fasihi

Katika hatua hii, mwalimu alenge kuwaelekeza wanafunzi kupata ujuzi kuhusu stadi za utafiti kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne watafiti, wasome na kujadiliana kuhusu:

1. Maudhui katika riwaya yoyote ambayo wamewahi kuisoma.
2. Fani katika riwaya yoyote ambayo wamewahi kuisoma.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili maswali yaliyo hapo juu. Wanafunzi warejelee kazi yoyote ya riwaya ambayo wamewahi kusoma ambayo wanafahamu.

Wanafunzi wanaweza kutoa majibu kama vile:

*a) Baadhi ya **maudhui** ambayo yameshughulikiwa katika riwaya nyingi ni: elimu, uongozi, ufisadi, umaskini, utajiri, ndoa na mapenzi, nafasi ya mwanamke miongoni mwa maudhui mengine.*

Wanafunzi wanaweza kueleza fani kama vile:

*b) **Fani** ni matumizi ya lugha kwa njia tofauti tofauti ili kupitisha ujumbe katika fasihi kwa njia ya kumsisimua msomaji au mtazamaji. Fani inaweza kuhusisha matumizi ya methali, majazi, uhaishaji, chuku, jazanda miongoni mwa nyingine.*

Wanafunzi wanaweza kuchagua mfano wa riwaya ambayo wameisoma au wanaifahamu kisha wajadili kuhusu maudhui na fani katika kazi hiyo ya kifasihi.

Pia, wanafunzi wanaweza kurejelea kazi mbalimbali za kifasihi ambazo wamewahi kuzisoma au wanazofahamu kasha wajadiliane kuhusu maswali waliyopewa katika sehemu hii. Baadaye, mwalimu aombe kila kundi la wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa na kuwaeleza wenzao matokeo ya majadiliano yao. Katika hatua hii, mwalimu arekebishe makosa ya kimatamshi pindi yanapotokea.

Ni vyema mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanaweza kujibu maswali haya kwa kiwango cha kuridhisha na kuonyesha kwamba wamefahamu uhakiki wa maudhui na fani kwa kurejelea kazi za kifasihi. Mwalimu azunguke darasani na kutoa maelezo pale yanapotakiwa ili kuelekeza makundi ya wanafunzi wanaotatizika.

## Tathmini ya vipindi 5-6

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea uhakiki wa maudhui na fani katika kazi za fasihi andishi huku wakirejelea kazi mbalimbali za kifasihi ambazo wamewahi kuzisoma au wanazofahamu. Kwa hivyo, vifaa vilivyotumiwa kujifunzia somo hili vinaweza kutumiwa kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa somo hili. Mwalimu pia awaulize wanafunzi maswali ya kuthibitisha iwapo wanaweza kueleza maana ya maudhui na fani katika fasihi.

## Vipindi vya 7-8: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kujadili tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi;
- Kujadili tofauti kati ya tanzu za fasihi andishi na tanzu za fasihi simulizi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za fasihi andishi za waandishi mbalimbali;
- Kazi za fasihi simulizi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 54;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Kazi mbalimbali za fasihi andishi na fasihi simulizi za waandishi mbalimbali zilizoandaliwa na mwalimu aidha kwa kurekodiwa au kuleta vitabu halisi zitumiwe kuwaongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kujadili tofauti

kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi. Mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kama alivyoagizwa kwenye zoezi husika.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi.

## d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia kuhusu uhakiki wa maudhui na fani katika fasihi andishi.

### 6.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi.

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha waelekezwe kujadiliana kuhusu:

1. *Tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi.*
2. *Tofauti kati ya tanzu za fasihi andishi na tanzu za fasihi simulizi.*

Mwalimu anaweza kuwashirikisha wanafunzi katika majadiliano haya kwa kuwaelekeza kurejelea kazi za fasihi andishi na fasihi simulizi za waandishi mbalimbali. Kupitia kazi hizi, wanafunzi wataweza kubaini tofauti zilizopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi.

Baadhi ya tofauti zilizopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi ni kama vile:

1. *Fasihi andishi huwasilishwa kwa maandishi yaliyo kitabuni ilhali fasihi simulizi huwasilishwa kwa njia ya mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine.*
2. *Katika fasihi andishi, maandishi yaliyoandikwa hayawezi kubadilishwa isipokuwa pale mwandishi anapoandika upya ilhali fasihi simulizi huweza kubadilishwa papo kwa hapo wakati msimulizi anapowasilisha jukwaani au mahali popote pale.*

3. *Uzuri wa fasihi andishi unategemea usanii wa mwandishi anayehusika ilhali uzuri wa fasihi simulizi unategemea ubingwa wa anayewasilisha jukwaani.*

Mwalimu azunguke darasani kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajadiliana vizuri kuhusiana na maswali waliyopewa. Mwalimu awasaidie wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baadaye, kila kundi lipewe muda wa kuwasilisha majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii. Mwalimu akosoe makosa ya kimatamshi kila mara yanapojitokeza ili kuwazoesha wanafunzi kutamka maneno kwa usahihi na kudumisha uwezo wao wa kuwasiliana kwa lugha rasmi.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua tanzu za fasihi andishi ambazo ni: riwaya, tamthilia, ushairi na riwaya pamoja na tanzu za fasihi simulizi kama vile: Hadithi, nyimbo, methali, vitendawili miongoni mwa nyingine.

## Tathmini ya vipindi 7-8

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha katika sehemu hii ya kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kueleza tofauti zilizopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi pamoja na tanzu zao. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutofautisha tanzu za fasihi andishi na tanzu za fasihi simulizi.

## Vipindi 9-10: Sarufi (Maana ya kitenzi)

### a) Malengo ya somo

- Kufafanua maana ya kitenzi katika Kiswahili;
- Kujadili mnyambuliko wa vitenzi;
- Kuainisha vitenzi katika kauli ya kutendea/kufanyia.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Vifaa vya darasani kama vile: madaftari, kalamu, rula n.k.;
- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyia;
- *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 54;*

- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile madaftari, kalamu, chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyia, michoro inayoonyesha vitendo vya kauli ya kutendea/kufanyia pamoja na chombo cha kunasia sauti au breli na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua maana ya kitenzi, kauli ya kufanyia/ kutendea ya mnyambuliko wa vitenzi pamoja na matumizi yao katika maongezi na sentensi sahihi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango cha chini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo pamoja na maandishi katika breli huku wakitoa maelezo kuvihusu na wale ambao hawawezi kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa vifaa hivyo huku wakiandika maelezo yake ubaoni. Ili kuyafikia malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu cha Mwanafunzi*.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika masomo ya viwango vya hapo awali kuhusiana na aina za maneno ya Kiswahili. Kutokana na swali hili la jumla, mwalimu aweze kuwashirikisha wanafunzi katika kutambua kuwa miongoni mwa maneno ya Kiswahili kuna kitenzi ambalo ni neno muhimu sana katika sentensi za Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu maana ya kitenzi.

## 6.5 Maana ya kitenzi

### Kauli ya kufanyia

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe wachunguze sentensi walizopewa katika vitabu vyao huku wakichunguza maneno yaliyopigiwa mistari. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua na kuelewa matumizi ya maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Wanafunzi wasome sentensi walizopewa kwa makini na kujadiliana kuhusu maneno yaliyopigiwa mistari. Wanafunzi waelekezwe kutambua kuwa maneno yaliyopigiwa mistari ni maneno yanayoonyesha vitendo mbalimbali hivyo maneno haya ni vitenzi.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kufafanua maana ya kitenzi kwa kuwaeleza kuwa ***kitenzi*** *katika Kiswahili ni neno ambalo hueleza kuhusu jambo lililofanywa, linalofanywa au litakalofanywa*. Wanafunzi wataje baadhi ya vitendo ambavyo wao hujihusisha navyo kila siku, kwa mfano: *kuamka, kuoga, kupiga mswaki, kuandika, kusoma, kuchora, kula, kucheza, kulala, kuzungumza* miongoni mwa vingine. Vitendo hivi walivyotaja huelezwa kwa maneno yanayoitwa vitenzi.

Baada ya majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaelekeze kufanya zoezi la 4 ambapo wanahitajika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi walivyopewa. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatunga sentensi sahihi kisarufi. Hatimaye, wanafunzi wote washirikishwe katika kusahihisha zoezi hili.

Kupitia kwa zoezi la makundi lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 55, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua mnyambuliko wa vitenzi huhusu nini. Hili si somo geni kwa wanafunzi katika kiwango hiki kwa sababu wamewahi kupatana na mada hii katika viwango vya hapo awali. Wanafunzi watambue kuwa kuna kauli kadhaa za mnyambuliko wa vitenzi mojawapo ikiwa kauli ya kutendea/kufanyia. Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa katika kauli ya kutendea/kufanyia, vitenzi huongezewa viambishi tamati na kupata maana ya *kutenda au kufanya kitendo kwa niaba ya*.

***Kwa mfano:***

| **Kauli ya kufanya/kutenda** | **Kauli ya kufanyia/kutendea** |
|---|---|
| ruka | rukia |
| nunua | nunulia |
| enda | endea |
| soma | somea |

***Mifano katika sentensi:***

1. *Mama anam**<u>pikia</u>** baba chai.* (Kutokana na kitenzi '*pika*')
2. *Mwalimu anamw**<u>andikia</u>** mwanafunzi insha.* (Kutokana na kitenzi '*andika*')
3. *Birasa amem**<u>bebea</u>** Kalisa vitabu vyake.* (Kutokana na kitenzi '*beba*')
4. *Mutoni amem***chorea** *mamake picha nzuri.* (Kutokana na kitenzi '*chora*')

Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha kuhusu vitenzi katika kauli hii ya kufanyia/kutendea, mwalimu awaombe wafanye zoezi la 5 na zoezi la 6. Mazoezi haya yasahihishwe darasani kwa maelekezo ya mwalimu. Mwalimu awasaidie wanafunzi walio na matatizo katika makundi yao.

## Tathmini

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kufafanua maana ya kitenzi pamoja na jinsi ya kunyambua kitenzi katika kauli ya kufanyia/kutendea. Utunzi wa sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli hii ndiko kutamhakikishia mwalimu kuwa wanafunzi wamepata uelewa wa funzo hili. Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao hata na nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la 7, zoezi la 8 na zoezi la 9 katika sehemu ya sarufi. Mazoezi haya yatasahihishwa kabla ya somo lijalo.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu kuwa:

- Neno ambalo hueleza kuhusu jambo linalofanywa, lililofanywa na litakalofanywa huitwa ***kitenzi***. Wingi wake ni ***vitenzi***.

**Mifano ya vitenzi:** *imba, chora, shona, rarua, lia, suka, ona, pika, keti, tazama, fuma* n.k.

### *Mifano katika sentensi:*

a) Mfumaji ali*fuma* sweta ya mtoto wangu vizuri.

b) Mwalimu ame*keti* ofisini.

Hali ya kuongeza herufi maalum au viambishi tamati mwishoni mwa mizizi ya vitenzi ili kupata maana ya ziada iliyo tofauti na ile ya asilia huitwa ***mnyambuliko wa vitenzi***. Kuna hali tofauti za kunyambua vitenzi kama vile:

### a) Hali ya kufanyia au kutendea:

Katika hali hii, vitenzi huongezwa viambishi tamati na kupata maana ya '*kutenda kwa niaba ya'*.

### *Kwa mfano:*

| Kauli ya kufanya/kutenda | Kauli ya kufanyia/kutendea |
|---|---|
| bomoa | bomolea |
| shona | shonea |
| imba | imbia |
| andika | andikia |

### *Mifano katika sentensi:*

1. Mama alimw***imbia*** mtoto wimbo mzuri.
2. Nyanya alim***shonea*** mjukuu wake nguo nzuri.

## 6.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wajaze nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali lifuatalo.

| Kauli ya kufanya/kutenda | Kauli ya kufanyia/kutendea |
|---|---|
| ____________________ | chomea |
| lia | ____________________ |
| ____________________ | inulia |
| pumua | ____________________ |
| ____________________ | samehea |

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

| Kauli ya kufanya/kutenda | Kauli ya kufanyia/kutendea |
|---|---|
| **choma** | chomea |
| lia | **lilia** |
| **inua** | inulia |
| pumua | **pumulia** |
| **samehe** | samehea |

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendea/kufanyia.

**Kwa mfano:** andika

**Matumizi katika sentensi**: Bakame alitu*andikia* barua ndefu.

1. soma
2. ruka
3. lala
4. chota
5. kimbia

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitenzi walivyopewa katika kauli ya kufanyia/kutendea.

## 6.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 52

1. Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kama malighafi yake makuu kwa lengo la kueleza maisha ya binadamu kwa njia ya usanii na ufundi unaoathiri na kusisimua msomaji na mtazamaji.
2. Fasihi simulizi na fasihi andishi
3. Hadithi za kubuni na hadithi za kihistoria.
4. Nyimbo, maghani, sifo na ngonjera.
5. Tanzu za fasihi andishi ni:
   a) ***Riwaya***: hii ni hadithi ndefu iliyoandikwa kwa maandishi ya nathari, aghalabu inayoeleza ukweli fulani wa maisha.
   b) ***Tamthilia***: ni utungo uliotungwa kwa lengo la kuigizwa jukwaani.
   ch) ***Ushairi***: ni utungo unaotumia maneno machache teule yaliyopangwa na kuwasilishwa kisanaa.
   d) ***Hadithi fupi***: ni hadithi inayoshughulikia suala fulani kwa muhtasari.
6. Huandikwa kwa njia ya nathari, huwa ndefu, ina wahusika wengi na walioelezewa kwa kina, mandhari mapana na matumizi mengi ya lugha kutokana na maudhui yake mengi.
7. Fasihi huwazindua wanajamii kupigania haki zao, huhimiza uzalendo na uananchi kwa wanajamii, huhifadhi historia na utamaduni wa jamii,

hukosoa na kuwakanya wanajamii dhidi ya tabia zisizokubalika katika jamii, huburudisha na hukuza umoja na ushirikiano baina ya watu katika jamii.

8. Ni jumla ya mambo yote yanayozungumziwa katika kazi ya fasihi.
9. Ni viumbe katika kazi ya fasihi wanaosema na kutenda matendo kwa niaba ya jamii husika.
10. Wao huzungumza kwa niaba ya mwandishi au jamii. Usimulizi huwahusu wao pamoja na tabia zao ili kudhihirisha mafunzo yanayolengwa na mtunzi wa fasihi husika.

**Zoezi la 1, ukurasa 52**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati pamoja na sentensi watakazotunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe msamiati waliokutana nao katika kifungu.

***Kwa mfano:***

1. ***Kusisimua -*** kusababisha mwili kupata hisi fulani kutokana na jambo la kutia furaha, huzuni au woga
2. ***Mbolezi*** - aina ya nyimbo ambazo huimbwa wakati wa msiba wa kifo ili kuwafariji waombolezaji

***Matumizi katika sentensi:***

1. Hadithi niliyosoma ilikuwa ya *kusisimua.*
2. Wasanii waliohudhuria maziko ya chifu waliimba *mbolezi* mbili.

**Zoezi la 2, ukurasa 53**

1. fasihi
2. fasihi andishi
3. kuhakiki
4. vina, mizani
5. Wahusika

## Zoezi la 3, ukurasa 54

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi kuhusu umuhimu wa fasihi simulizi.

***Kwa mfano:***

1. Hukosoa na kuonya dhidi ya tabia na matendo yasiyokubalika katika jamii. Fasihi simulizi huweza kutumia vitendawili ili kuwaonya wanajamii kuhusu tabia na mienendo fulani.
2. Hutahadharisha na kukuza maadili ya jamii. Ngano katika fasihi andishi huweza kutekeleza jukumu hili.
3. Huelimisha kuhusu historia, mila na tamaduni za jamii. Kupitia utambaji wa hadithi kama za visasili na visakale, historia, mila na tamaduni za jamii hutambulika.
4. Huburudisha: Malumbano ni baadhi ya vipera ambavyo huburudisha watu katika jamii. Pia kuna matani na vitanza ndimi.
5. Hututazamisha mambo yanayohusu jamii. Kwa mfano: siasa na elimu.
6. Hukuza umoja na ushirikiano wa wanajamii. Nyimbo mbalimbali huwaleta pamoja wanajamii husika. Wakati wa kazi, kuna nyimbo za kazi ambazo huimbwa. Nyimbo hizi hutumika kama njia ya kuwahimiza na kuwatia wanajamii moyo wa kuendelea kufanya kazi bila kuchoka.

## Zoezi la sarufi, ukurasa 54

Maneno yaliyopigiwa mistari ni vitenzi.

## Zoezi la 4, ukurasa 55

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe vitenzi walivyopewa.

***Kwa mfano:***

1. Mtambaji hodari *atakuja* Jumamosi.
2. Mvua *ilinyesha* katika kijiji cha Gitarama.
3. Kitabu cha mashairi *ndicho* hiki.
4. Mukamulina *anawaogopa* waigizaji wa tamthilia hii.

5. Mwalimu *anatembea* darasani akisahihisha kazi zao.
6. Mama *ataongea* na shangazi kwa simu.
7. Wanafunzi *wameuvuka* mto Ruzizi.
8. Nimemsamehe *aliyenichokoza* asubuhi.
9. Mimi *huonja* supu ya nyama wakati wa mapishi.
10. Habimana *ni* mwanafunzi wa shule ya upili ya Sebeya.

**Zoezi la makundi, ukurasa 55**

A. Vitenzi '*pika, shona, chora, andika* na *soma* vipo katika kauli ya kufanya/ kutenda.

B. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

**Kwa mfano:**

i) Mama *anampikia* mtoto chakula.

ii) Mimi *ninamshonea* dadangu nguo.

iii) Mwanafunzi *anamchorea* babake picha.

iv) Kaka *anamwandikia* mjomba wake barua.

v) Ngabo *anamsomea* mwalimu kitabu.

**Zoezi la 5, ukurasa 56**

1. letea
2. soma
3. chezea

**Zoezi la 6, ukurasa 56**

1. fumia
2. vutia
3. kimbilia
4. futia
5. pangusia

**Zoezi la 7, ukurasa 57**

1. Msichana anamchorea mtoto picha.
2. Gasimba anakimbilia shuleni.
3. Mama anamfumia Mutoni fulana.
4. Mimi ninamwandikia babangu barua.
5. Nitalifutia darasa letu ubao kesho.

**Zoezi la 8, ukurasa 57**

a) Mama anachota maji kwa niaba ya baba.
b) Nitaupiga mpira badala yako.
ch) Nyanya anaandaa chakula ili tukile.
d) Sitaandika barua kwa niaba yenu.
e) Ubao wa mwalimu unafutwa na kiranja wa darasa.

**Zoezi la 9, ukurasa 57**

a) samehe
b) ondoka
ch) zungumza
d) lima
e) chuma

# Somo la 7: Wahusika katika fasihi andishi

## Vipindi 11-13: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi hadithi fupi kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kuchunguza wahusika katika hadithi fupi husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za kifasihi za waandishi mbalimbali;
- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha aina mbalimbali za wahusika katika fasihi;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 58;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu uhakiki wa wahusika katika fasihi andishi. Wahusika ni viumbe ambao hutumiwa kupitisha ujumbe wa mwandishi kwa hadhira lengwa. Wahusika wanaweza kuwa binadamu, wanyama miongoni wa wengine. Wahusika hushirikishwa katika hadithi na msanii au mwandishi ili kuendeleza maudhui na dhamira yake. Katika fasihi, wahusika ni 'magari' ambayo huweza kumsafirisha msomaji kutoka mandhari mamoja hadi mengine hadi kufikia mwisho wa hadithi bunifu. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelezo yaliyotolewa kwa kila zoezi husika. Mwalimu pia anaweza kutayarisha chati zinazoonyesha aina mbalimbali za wahusika. Kazi za kifasihi za waandishi mbalimbali zinaweza kutumika ili kuwasaidia wanafunzi kulielewa funzo hili vizuri.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wake maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita kuhusiana na fasihi andishi. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika somo lililotangulia. Baada ya haya, mwalimu atangulize somo hili kuhusu uhakiki wa wahusika katika fasihi andishi. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali ya kuwachangamsha kuhusiana na mchoro ulio katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 58. Maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye mchoro huu? Wahusika wanaoonekana ni kina nani?* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona…."*. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na wanayoyaona katika mchoro waliopewa. Kwa mfano: "*Mimi ninaona wanaume wawili wakizungumza. Mimi ninawaona wahusika ambao ni Sululu na babake (kulingana na kifungu watakachosoma)."*

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha mchoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea au wanachokiona katika mchoro huo. Kutokana na mchoro huo, wanafunzi wataweza kukisia hadithi fupi watakayosoma inahusu nini. Bila shaka hadithi hiyo inahusu mvutano kati ya baba na mwanawe (Sululu) kuhusu urithi.

## 7.1 Kusoma na kufahamu

### Hadithi fupi kuhusu suala la urithi

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wasome kwa kimya hadithi fupi waliyopewa kuhusu suala la urithi. Wanafunzi wasome hadithi hiyo kwa kimya huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu hadithi hiyo waliyosoma ili kuhakikisha kuwa wameielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: '*Sululu alikuwa na tatizo lipi lililomsumbua akili?'* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu swali la mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika hadithi husika. Kwa mfano: '*Sululu alikuwa anamtaka babake amkatie kipande chake cha shamba kama urithi wake.'*

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti hadithi hiyo ili kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya ufahamu waliyopewa huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hicho.

Wanafunzi pia washirikishwe katika kubaini mawazo makuu yanayozungumziwa katika hadithi hiyo pamoja na wahusika wanaotumika kuupitisha ujumbe wa hadithi hiyo kwa wasomaji.

## Tathmini ya vipindi 11-13

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea uchambuzi wa hadithi waliyosoma kwa kurejelea mawazo yake makuu pamoja na wahusika waliotumika. Uhakiki wa aina ya wahusika waliotumika katika hadithi husika yarejelewe katika kuhakiki iwapo wanafunzi wameelewa umuhimu wa wahusika katika fasihi andishi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kubaini kuwa katika hadithi waliyosoma, Sululu ndiye mhusika mkuu ilhali wahusika wadogo ni kama vile: babake Sululu, mamake Sululu, mkewe Sululu pamoja ndugu zake Sululu. Wahusika hawa wadogo wanatumiwa kuzijenga sifa za mhusika mkuu, Sululu.

## Vipindi 14 -15: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na wahusika katika fasihi;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na wahusika katika fasihi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za fasihi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kamusi ya Kiswahili*;

- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 63;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ujifunzaji wa msamiati unaohusiana na hadithi fupi iliyo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 58 pamoja na wahusika katika fasihi andishi. Mwalimu aandae mifano ya hadithi fupi pamoja na kazi nyingine za fasihi andishi ambazo anaweza kuwapa wanafunzi wakazisoma darasani katika makundi yao na kuchambua msamiati wake wakirejelea wahusika waliotumika. Pia, mwalimu anaweza kuandaa masimulizi kadhaa kuhusiana na hadithi fupi na kuwasimulia wanafunzi darasani. Hadithi fupi kadhaa zinaweza kurekodiwa na wanafunzi wakazisikiliza darasani au hata kuzitazama zikiigizwa kwenye runinga na baadaye kuchambua msamiati wake wakirejelea wahusika waliotumika. Mwalimu anaweza kufanya maandalizi haya mapema kabla ya vipindi hivi.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofunzwa katika kipindi kilichotangulia.

## 7.2 Kujifunza msamiati wa hadithi kuhusu suala la urithi

Baada ya haya, mwalimu atangulize somo hili kuhusu msamiati unaohusiana na hadithi fupi waliyopewa huku wakirejelea wahusika waliotumika.

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya waliopatana nao katika usomaji wao na jinsi msamiati huo ulivyotumiwa katika hadithi fupi waliyokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale inapohitajika. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua msamiati husika katika makundi yao.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze sentensi walizopewa katika zoezi la 1 pamoja na misamiati iliyopigiwa mistari katika sentensi hizo. Wanafunzi washirikishwe katika kufafanua maana ya misamiati hiyo. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Wanafunzi washirikishwe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia misamiati waliyofafanua.

Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati husika, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika hadithi waliyosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba matumizi ya msamiati husika katika maongezi au maandishi ndio utakaomdhibitishia iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha sahihi.

## Tathmini ya vipindi 14-15

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mpya kuhusu hadithi husika huku wakirejelea wahusika waliotumika. Mwalimu abaini iwapo wanafunzi wanaweza kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia misamiati mbalimbali inayohusiana na fasihi andishi.

## Vipindi 16-18: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu aina mbalimbali za wahusika katika fasihi andishi;
- Kujadili tabia na sifa za wahusika katika hadithi husika;

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za fasihi andishi za waandishi mbalimbali;
- Wanafunzi wenyewe;

- Mtandao wa intaneti;
- Chati yenye kuonyesha aina za wahusika mbalimbali;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 64;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha kuhusiana na aina mbalimbali za wahusika katika fasihi andishi. Mwalimu aandae kazi kadhaa za fasihi andishi za waandishi mbalimbali ambazo zinaweza kutumika katika uainishaji wa wahusika mbalimbali. Kwa upande mwingine, mwalimu anaweza kuandaa chati zenye kuonyesha aina mbalimbali za wahusika katika fasihi andishi.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwasalimu wanafunzi. Wanafunzi wajibu salamu za mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika somo lililotangulia.

## 7.3 Majadiliano kuhusu aina mbalimbali za wahusika

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha wajadili kuhusu:

1. *Aina mbalimbali za wahusika katika fasihi andishi.*
2. *Tabia na sifa za wahusika katika hadithi fupi waliyosoma hapo awali kama vile: Sululu, mamake Sululu, mke wa Sululu, babake Sululu n.k.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika makundi yao kujadiliana kuhusu aina mbalimbali za wahusika katika fasihi andishi. Baadhi ya aina hizi za wahusika ni kama vile:

1. ***Wahusika wakuu:*** Hawa ndio nguzo ya hadithi ambao husheheni katika hadithi nzima. Hawa ndio wanaoisukuma hadithi mbele kwa sababu matendo na migogoro yote muhimu huwahusu wao. Kwa mfano, katika

hadithi iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 58-62 mhusika mkuu ni Sululu.

2. ***Wahusika wasaidizi:*** Hawa ni wahusika ambao hutumiwa ili kumsaidia msomaji kumwelewa vyema mhusika mkuu. Kupitia maingiliano ya wahusika hawa na mhusika mkuu, msomaji hupata mwanga zaidi kuhusu tabia ya mhusika mkuu. Kwa mfano, katika hadithi waliyopewa wanafunzi, wahusika wajenzi ni kama vile wazazi wa Sululu.
3. ***Wahusika wadogo:*** Hawa ni wahusika ambao hujitokeza katika maisha ya mhusika mkuu katika matukio machache sana au hata kwa kutajwa tu. Wao pia humsaidia msomaji kuzielewa tabia za mhusika mkuu. Kwa mfano, katika hadithi waliyosoma wanafunzi, wahusika wadogo ni kama vile ndugu zake Sululu.
4. ***Wahusika bapa:*** Hawa ni wahusika ambao hushikilia msimamo mmoja au huwa na tabia moja iliyo sawa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Hawa huwa hawabadiliki kitabia au kimsimamo.
5. ***Wahusika duara:*** Hawa ni wahusika ambao wana desturi ya kubadilika kitabia, kimawazo au hata kisaikolojia. Matendo na maisha yao yanaongozwa na hali halisi za maisha.

Mbali na hayo, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kuzijadili sifa za wahusika waliotumika katika hadithi waliyopewa kwenye vitabu vyao. Kwa mfano :

a) Sululu ni ***mwenye hasira***. Anaondoka kwake na kwenda kwa wazazi wake akiwa amebeba upanga. Anapofika huko, anazua fujo kwa kufoka akiitisha kipande cha ardhi na kutishia kumwua babake. Sululu pia ni ***mjinga*** kwa kuwa alikataa kusoma hata baada ya kupelekwa katika shule nzuri na kulipiwa karo. Baada ya kukataa kusoma, anarudi kwa wazazi wake na kuitisha urithi.

b) Mamake Sululu ni ***mvumilivu***. Licha ya kuwa Sululu anamjia na upanga na matusi, yeye anatulia na kujaribu kuzungumza naye kwa upole bila kumkaripia. Yeye pia ni ***mwenye hekima***. Mamake Sululu anajaribu kusema na mwanawe kwa kumkumbusha kuwa hata kipande cha ardhi ambacho amejenga nyumba yake ni urithi kutoka kwa babake.

ch) Mkewe Sululu ni ***mnyenyekevu*** kwa mumewe. Yeye pia ni ***mvumilivu*** kwani wamepitia mambo mengi (mazuri kwa mabaya) katika ndoa yake na Sululu.

Kupitia majadiliano haya, mwalimu ataweza kuwaelekeza wanafunzi katika kutambua namna ya kuhakiki wahusika katika kazi ya fasihi andishi.

Baada ya haya, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili na kuzieleza tabia na sifa za rafiki zao hapo darasani au hata nyumbani.

## Tathmini ya vipindi 16-18

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kikundi kuhusiana na uhakiki wa wahusika katika fasihi na pia kwa kurejelea mfano wa hadithi waliyopewa katika vitabu vyao.

Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kueleza aina mbalimbali za wahusika katika fasihi na uwezo wa kuwatambua wahusika mbalimbali katika hadithi.

## Vipindi vya 19-21: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kufahamu wahusika mbalimbali katika riwaya ya '***Siku Njema***';
- Kujadili tabia na sifa za wahusika mbalimbali katika riwaya ya '***Siku Njema***';

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Riwaya ya ***'Siku Njema'*** au riwaya nyingine teule;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 64;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia vipindi hivi kuhusu kujadili tabia na sifa za wahusika katika riwaya ya '***Siku Njema'*** au riwaya nyingine teule. Wahusika ni viumbe muhimu sana katika kupitisha ujumbe wa mwandishi kwa msomaji. Mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi nakala za riwaya teule ili waweze kuisoma mapema kabla ya vipindi hivi. Pia, mwalimu anaweza kuandaa rekodi za hadithi kadhaa ambazo wanafunzi wanaweza kuzisikiliza darasani au hata kuzitazama kisha wakabaini sifa na tabia za wahusika waliotumika. Pia, mwalimu anaweza kuandaa masimulizi ya hadithi ambayo anaweza kuwasimulia wanafunzi darasani na wanafunzi wakajadiliana kuhusiana na wahusika waliotumika katika hadithi hiyo.

### d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi ambalo wanafunzi walipewa katika kipindi kilichopita limesahihishwa na wanafunzi waliokuwa na matatizo wameelekezwa vilivyo.

## 7.4 Majadiliano kuhusu tabia na sifa za wahusika

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaongoze wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi watano watano ili waweze kujadiliana kuhusu tabia na sifa za wahusika mbalimbali kutoka katika riwaya moja teule kama vile '***Siku Njema***'. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujadiliana kuhusu aina za wahusika katika riwaya hiyo pamoja na sifa zao. Shughuli hii itawezekana kwa urahisi iwapo mwalimu atakuwa amewapa wanafunzi riwaya hii teule ili waweze kuisoma mapema kabla ya vipindi hivi. Sehemu hii ipanue ujuzi wa wanafunzi kuhusu uainishaji wa wahusika katika kazi za fasihi andishi.

Baadhi ya tabia na sifa za wahusika katika katika riwaya ya '***Siku Njema'*** ni kama vile: Mhusika mkuu ni Kongowea Mswahili.

1. Mhusika mkuu ni ***Kongowea Mswahili***. Matukio katika riwaya nzima yanamhusu yeye. Kongowea Mswahili ni *mnyenyekevu*, *mwenye heshima*, *karimu, mvumilivu, mwenye bidii, mwenye hekima* na *mtiifu*.
2. ***Zainabu Makame*** ni mhusika mjenzi kwa sababu anatumika kuzijenga tabia za mwanawe Kongowea Mswahili. Mama huyu ni *mwerevu,*

*mvumilivu, mwenye bidii* na alikuwa *msiri mkubwa* sana (aliificha siri ya aliyekuwa babake Kongowea Mswahili).

3. ***Juma Mukosi*** (Mzee Kazikwisha) ni mhusika mjenzi kwa vile anavyotumiwa kutusimulia sifa za mwanawe Kongowea Mswahili. Yeye ni *mvumilivu, msiri, mwenye hekima* na *mwenye bidii.*
4. ***Amina*** ni mhusika mdogo ambaye anatumiwa kumjenga mhusika mkuu na kumsawiri kuwa mtu aliyeshikilia maadili aliyokuwa amefundishwa na mama yake.

Miongoni mwa wahusika wengine katika riwaya hii ya 'Siku Njema' ni: *Rashidi, Zawadi, Mwana Saumu, Kitwana Makame, Selemani, Bakari, Vumilia, Amina* miongini mwa wengine.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wajitokeze mbele ya darasa ili wawaeleze wenzao kuhusu yale waliyoyajadili katika makundi yao. Wanafunzi wengine nao wasikilize matokeo ya majadiliano ya kila kikundi na wapewe muda wa kuchangia kwa yale yaliyozungumziwa huku wakiongozwa na mwalimu.

Baada ya majadiliano haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao wajadiliane kuhusu uhusiano wa mada ya riwaya teule waliyopewa na maudhui yaliyozungumziwa katika riwaya hiyo. Kwa mfano: *Mada 'Siku Njema' inaambatana kabisa na maudhui katika riwaya yenyewe kutokana na dhana kuwa kuna wahusika wengi akiwemo mhusika mkuu ambaye ni Kongowea Mswahili ambao walipitia changamoto nyingi maishani lakini hatimaye mambo yaliwanyookea hivyo siku zao njema ziliwadia.*

Mwalimu ahakikishe anawashirikisha wanafunzi wote katika majadiliano haya. Azunguke darasani akiwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

## Tathmini ya vipindi 19-21

Mwalimu atathmini iwapo ujifunzaji umetekelezwa kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, awaulize wanafunzi maswali ya kupima uwezo wao wa kurejelea tabia na sifa za wahusika mbalimbali katika riwaya teule waliyosoma au hata katika kazi nyingine ya kifasihi ambayo wameisoma au wanaifahamu

Vilevile, maswali mengine yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kujadiliana

katika makundi yao kuhusu namna mada ya kazi ya kifasihi inavyoambatana na maudhui yanayoshughulikiwa katika kazi yenyewe.

## Vipindi vya 22-25: Sarufi (Kauli ya kufanyiwa na kufanyika)

### a) Malengo ya somo

- Kufahamu mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyiwa;
- Kutaja mifano ya vitenzi katika kauli ya kufanyiwa;
- Kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kufanyiwa.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 65;
- Chati yenye kuonyesha mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyiwa;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ajiandae kufundisha vipindi hivi. Mwalimu atunge mifano kadhaa ya vitenzi katika kauli ya kufanya/kutenda na aonyeshe namna vinavyobadilika hadi kauli ya kufanyiwa/kutendewa katika Kiswahili. Mifano hii kadhaa itamwezesha kuwafundisha wanafunzi sehemu hii ya sarufi kuhusu mnyambuliko wa vitenzi, kauli ya kufanyiwa. Iwapo mwalimu ana wanafunzi walio na matatizo ya kuona, basi itambidi kutunga na kuandika mifano ya vitenzi hivyo pamoja na sentensi kadhaa kwenye breli kwa manufaa ya wanafunzi hao. Kwa wanafunzi walio na matatizo ya kusikia, lugha ishara inaweza kutumika pamoja na kuiandika mifano atakayotunga mwalimu ubaoni.

### d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali somo la sarufi lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu

somo hilo. Mwalimu achukue fursa hii ya utangulizi ili kuwaomba wanafunzi kusahihisha mazoezi waliyopewa kuhusiana na kipindi kilichopita. Mwalimu aendeleze somo kwa kuwaomba wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kwa kila zoezi.

## 7.5 Kauli ya kufanyiwa/kutendewa

Ujifunzaji wa sarufi katika hatua hii uchukuliwe kama mwendelezo wa yale yaliyofundishwa katika sehemu ya sarufi kuhusu maana ya kitenzi pamoja na kauli ya kufanyia/kutendewa katika vipindi vilivyotangulia. Kwa hivyo, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa kauli ya kufanyiwa/kutendewa pamoja na mabadiliko ya vitenzi katika kauli hii. Ili kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika kipengele hiki, mwalimu awaombe wanafunzi wataje vitenzi katika kauli ya kufanya/kutenda kisha wavibadilishe hadi kwenye kauli ya kufanyiwa/kutendewa.

***Kwa mfano:***

| Kauli ya kufanya/kutenda | Kauli ya kufanyiwa/kutendewa |
|---|---|
| beba | beb***ewa*** |
| shika | shik***iwa*** |
| ingia | ingi***liwa*** |
| anika | anik***iwa*** |
| lala | la***liwa*** |
| ondoka | ondok***ewa*** |

Kutokana na zoezi hili, wanafunzi wataweza kutambua kuwa vitenzi hubadilika kutoka katika kauli ya kufanya/kutenda hadi kwenye kauli ya kufanyiwa/kutendewa kwa kuongezewa viambishi tamati mbalimbali kama vile: ***–iwa, -ewa, -liwa*** na ***–lewa***. **Kwa mfano:**

i) pika – pik***iwa***

ii) chora – chor***ewa***

iii) kimbia – kimbi***liwa***

iv) tembea –tembe***lewa***

Baada ya wanafunzi kuelewa namna ya kubadilisha vitenzi mbalimbali kuwa katika kauli ya kufanyiwa/kutendewa, mwalimu awashirikishe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi wakitumia vitenzi vilivyonyambuliwa katika kauli ya kufanyiwa. Kwa mfano:

1. *Mama ali**pikiwa** chakula na shangazi.*
2. *Mwalimu ali**bebewa** vitabu na viranja.*
3. *Babu ata**tembelewa** na waumini wa kanisa lao.*
4. *Chakula kita**liwa** na wanafunzi hawa.*

Wanafunzi watunge sentensi kadhaa katika makundi yao kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kufanyiwa. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi kisarufi.

Baadaye katika makundi yao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kubadilisha vitenzi na kuwa katika kauli ya kufanyika/kutendeka.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la makundi lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 65* kisha wajadiliane kuhusu mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyika. Wanafunzi waelezwe kuwa vitenzi katika kauli ya kufanyika huongezewa viambishi tamati ***–ika, -lika, -eka*** na ***–leka.***

### *Kwa mfano:*

| **Kauli ya kufanya/kutenda** | **Kauli ya kufanyika/kutendeka** |
|---|---|
| beba | beb***eka*** |
| shika | shik***ika*** |
| ingia | ingi***lika*** |
| anika | anik***ika*** |
| lala | la***lika*** |
| ondoka | ondok***eka*** |

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kutunga sentensi sahihi wakitumia vitenzi katika kauli ya kufanyika. Sharti sentensi hizi ziwe sahihi kisarufi.

### Kwa mfano:

1. *Mlango wa darasa letu uli**fungika**.*
2. *Vitabu hivi vina**someka**.*
3. *Maziwa haya yana**nyweka**.*

Mwalimu ahakikishe anawashirikisha wanafunzi wote katika shughuli hii na wanafunzi wamepata ujuzi kamili katika kutambua vitenzi katika kauli ya kufanyiwa/kutendewa na kufanyika/kutendeka.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 6 katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ambapo wanafunzi wanatakiwa kukamilisha jedwali walilopewa kwa mnyambuliko sahihi.

Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na maelezo ya mwalimu yatilie mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwishowe, mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la 7 katika sehemu hii ambapo wanahitajika kutunga sentensi sahihi kisarufi katika kauli ya kufanyiwa na kufanyika kwa kutumia vitenzi walivyopewa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi hili limesahihishwa kabla ya kipindi kijacho.

## Tathmini ya vipindi 22-25

Mwalimu ahitimishe vipindi hivi kwa kuuliza maswali yanayodhamiria kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa mnyambuliko wa vitenzi katika kauli ya kufanyiwa na kufanyika. Wanafunzi pia waulizwe maswali mepesi ya kubaini iwapo wamefahamu tofauti kati ya kauli hizi mbili. Wanafunzi nao, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kwa kudhihirisha iwapo wameelewa mambo yote muhimu yaliyotakikana kuzingatiwa katika vipindi hivi.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

- Viumbe wa kisanaa ambao hutumiwa katika kazi ya fasihi kuupitisha ujumbe wa mwandishi huitwa ***wahusika***. Wahusika ndio msingi wa hadithi yoyote ile kwa sababu hadithi huwahusu wao. Wahusika wanaweza kuwa: binadamu, wanyama, mazimwi, vitu, sauti n.k.

Kuna aina mbalimbali za wahusika kama vile: *wahusika wakuu, wahusika wadogo, wahusika nguli, wahusika bapa, wahusika kielelezo, wahusika bapa sugu* miongoni mwa wengine.

- Kauli inayoleta maana ya kitendo kufanywa kwa niaba ya nomino au kwa ajili ya nomino fulani huitwa ***kauli ya kutendewa/ kufanyiwa***. Silabi za mwisho katika vitenzi vilivyo katika kauli ya kutendewa ni: ***-iwa, -ewa, -liwa*** na ***-lewa.***

### *Mifano:*

| **Kauli ya kufanya/kutenda** | **Kauli ya kufanyiwa/kutendewa** |
|---|---|
| fagia | fagi***liwa*** |
| soma | som***ewa*** |
| imba | imb***iwa*** |
| tembea | tembe***lewa*** |

- Kauli inayoleta maana ya kitendo kufanyika lakini mtendaji haonyeshwi au hajulikani huitwa kauli ya ***kutendeka/kufanyika.*** Kauli ya kutendeka/ kufanyika pia huleta maana ya kuwepo kwa uwezekano wa kufanyika kwa kitendo fulani. Silabi za mwisho kwenye vitenzi katika kauli ya kufanyika/ kutendeka huwa: ***-ika, -lika, -eka, -leka.***

### *Kwa mfano:*

| **Kauli ya kufanya/kutenda** | **Kauli ya kufanyika/kutendeka** |
|---|---|
| vunja | vunj***ika*** |
| kaa | ka***lika*** |
| lea | lel***eka*** |
| sema | sem***eka*** |

## 7.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kufanikisha ujifunzaji wa pamoja, zoezi la ziada litolewe kwa wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kujibu swali hili:

*Kamilisha jedwali lifuatalo kwa usahihi.*

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanyiwa | Kauli ya kufanyika |
|---|---|---|
| ______________ | onjewa | ______________ |
| samehe | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | tembeleka |
| ______________ | shonewa | ______________ |
| toboa | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | bebeka |

## Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanyiwa | Kauli ya kufanyika |
|---|---|---|
| **onja** | onjewa | onjeka |
| samehe | **samehewa** | **sameheka** |
| **tembea** | **tembelewa** | tembeleka |
| **shona** | shonewa | **shoneka** |
| toboa | **tobolewa** | **toboleka** |
| **beba** | **bebewa** | bebeka |

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi tano kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kufanyiwa na sentensi nyingine tano kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kufanyika.

***Kwa mfano:***

***Kauli ya kufanyiwa:*** Nyumba ya nyanya ili***fagiliwa*** na mjukuu wake.

***Kauli ya kufanyika:*** Nyumba ya nyanya ili***fagilika*** vizuri.

## 7.7 MAJIBU

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 62-63**

1. Sululu alitaka kupewa kasma yake ambayo ni kipande cha ardhi. Hakuwa na ucheshi kwa kuwa alienda kwa babake ili kudai kasma yake kwa hasira nyingi.
2. Ndoa ya Sululu ilikuwa ya kuvumiliana. Sululu na mkewe waliishi kwa uchochole mwingi na hali hii haikumpa raha. Mkewe alikuwa mnyenyekevu kwake na walikuwa wamepitia mambo mengi (mazuri kwa mabaya) pamoja.
3. Nyumba hiyo ilikuwa imeezekwa kwa mabati ambayo yalikuwa yamepiga kutu. Kuta za nyumba hiyo zilikuwa zimejengwa kwa matofali yaliyoshikamanishwa na udongo.
4. Sululu ni mwenye hasira. Anaondoka kwake na kwenda kwa wazazi wake akiwa amebeba upanga. Anapofika huko, anazua fujo kwa kufoka akiitisha kipande cha ardhi na kutishia kumwua babake. Sululu pia ni mjinga kwa kuwa alikataa kusoma hata baada ya kupelekwa katika shule nzuri na kulipiwa karo. Baada ya kukataa kusoma, anarudi kwa wazazi wake na kuitisha urithi.
5. Kwa sababu aliacha masomo na akawa hana jambo muhimu la kufanya kutokana na umaskini uliomkumba.
6. Mwalimu atathmini ulinganisho wa wanafunzi kuhusu namna urithi wa ardhi umeshughulikwa na unavyofanywa katika jamii zao.
7. Toili Kauka, Ayubu Kauka na Matayo Kauka.
8. Mamake Sululu ni mvumilivu. Licha ya kuwa Sululu anamjia na upanga na matusi, yeye anatulia na kujaribu kuzungumza naye Sululu kwa upole bila kumkaripia. Yeye pia ni mwenye hekima. Mamake Sululu anajaribu kusema na mwanawe kwa kumkumbusha kuwa hata kipande cha ardhi ambacho amejenga nyumba yake ni urithi kutoka kwa babake. Anaendelea

kwa kumfahamisha kuwa hawezi akapewa ekari kumi za ardhi ilhali kaka zake hawana urithi wao na hivyo ni bora wagawane wote. (Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi)

9. ***a) Utamaduni:*** maudhui haya yanadhihirishwa kutokana na dhana kuwa ni sharti mtoto wa kiume apewe urithi kutoka kwa wazazi wake. Sululu anadai urithi ambao anautaja kama kasma yake yaani haki yake.

   ***b) Elimu:*** elimu ni ngao ya maisha ya binadamu yeyote. Katika hadithi hii, babake Sululu anasoma na kuwa mwalimu. Ni kupitia kwa elimu aliyopata ndipo anaweza kuhifadhi pesa ambazo anazitumia kununua mashamba yake. Kaka zake Sululu pia wanatilia maanani elimu na wanafaulu katika maisha yao hadi hawaoni haja ya kupewa urithi. Sululu, kinyume na wenzake, anaamua kuachia masomo njiani na kujiingiza katika ulevi. Yeye haoni ubora wa elimu.

10. Mwandishi amekusudia kuwasihi wasomaji wa hadithi hiyo kuwa kuna ubora katika elimu. Mbali na hayo, mwandishi amekusudia kuwaonya watu wenye pupa kama ya Sululu kuzingatia upole na ustaarabu katika kila jambo wanalofanya.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 63**

Mwalimu atathmini maelezo ambayo yatatolewa na wanafunzi. Sharti maelezo hayo yahusishe msamiati waliokutana nao katika kifungu cha habari.

***Kwa mfano:***

1. ***Vilivyorishai -*** vilivyoloa
2. ***Kaptura -*** vazi kama suruali lakini fupi na linaloishia magotini; bombo

**Zoezi la 1, ukurasa 63**

Mwalimu atathmini maelezo ambayo yatatolewa na wanafunzi. Sharti maelezo hayo yahusishe msamiati waliopatana nao katika kifungu cha habari. Pia, atathmini sentensi ambazo wanafunzi  watatunga.

***Kwa mfano:***

1. ***ulitweta -*** ulihema kwa nguvu

2. ***alimpapasa -*** alimgusagusa kwa njia ya kumbembeleza
3. ***kaptura -*** vazi kama suruali lakini fupi na linaloishia magotini; bombo
4. ***ucheshi -*** tabia ya kuwa mchangamfu na kuwafurahisha watu
5. ***kero -*** jambo linaloudhi
6. zinazipiku - zinazizidi
7. ***hamaki -*** hasira
8. ***kutu -*** kitu cha rangi nyekundu kinachoota juu ya chuma na kukiharibu kipatapo maji
9. ***msonge -*** nyumba yenye umbo la duara na paa la umbo la pia
10. ***aliachama -*** aliweka kinywa wazi kwa mshangao

**Matumizi katika sentensi:**

1. Moyo wangu ***ulitweta*** baada ya kukimbia kwa muda mrefu.
2. Mtoto ***alimpapasa*** paka aliyekuwa amelala kochini.
3. **Kaptura** ya Kayitesi imeraruka.
4. Mwigizaji huyu ana ***ucheshi*** mwingi.
5. Unywaji wa pombe kupita kiasi ni ***kero*** kubwa kwa wanajamii.
6. Bidhaa nzuri ***zinazipiku*** zile ghushi kwa ubora.
7. Mhubiri alishikwa na ***hamaki*** muumini alipoingia kanisani na pombe.
8. Chuma cha gari langu kimeshikwa na ***kutu***.
9. Kaka zangu wanaishi katika nyumba ya ***msonge***.
10. Maria alipomwona duma akikimbia, ***aliachama***.

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 64**

1. Mwalimu atathmini namna wanafunzi watakavyowaainisha wahusika.

***Kwa mfano:***

**i) *Wahusika wakuu***

Hawa ni wahusika ambao wanahusishwa na takribani visa vyote katika kazi ya kifasihi. Wahusika hawa huhusishwa kutoka mwanzo hadi mwisho.

### *ii) Wahusika wasaidizi*

Hawa ni wahusika wanaosaidia kumjenga mhusika mkuu. Hujitokeza mara nyingi katika hadithi. Wahusika wasaidizi wanaweza kuwa na visa vyao. Kwa mfano: wanaweza wakawa ni marafiki na aila za wahusika wakuu.

### *iii) Wahusika wadogo*

Ni wahusika ambao wanafanya kazi ndogo sana katika fasihi kama vile kujenga maudhui au mandhari. Wahusika hawa wakitolewa, hadithi inaweza kuendela bila kubadilika sana.

### iv) Wahusika bapa

Hawa ni wahusika wasiobadilika kutoka mwanzo hadi mwisho. Kwa mfano, mhusika mbaya anabakia kuwa mbaya kutoka mwanzo hadi mwisho. Sifa za wahusika bapa huweza kutambulika mwanzoni mwa hadithi. Wahusika bapa hawawakilishi sifa halisia za binadamu. Nia yao ni kujenga tabia moja tu. Kuna aina mbili za wahusika bapa:

- **Wahusika bapa-sugu** - huonyesha msimamo wao kulingana na masimulizi ya msanii.
- **Wahusika bapa-vielelezo** - msimamo wao hutambulika kulingana na majina yao. Msanii hutumia mbinu ya majazi au lakabu kuwapatia wahusika majina yanayolingana na sifa zao.

### v) Wahusika duara

Wahusika duara hubadilika kitabia katika fasihi. Hawana msimamo thabiti. Hubadilika kulingana na maudhui na mazingira. Kwa mfano, msichana aliyeanza kama mpole na mwadilifu anapobadilika na kuwa mtovu wa nidhamu, kahaba na asiyeshirikiana na mtu yeyote.

### vi) Wahusika wafoili

Hawa huwa katikati ya wahusika bapa na wahusika duara. Wanaweza kuchukua msimamo fulani katika masuala fulani lakini pia wanaweza kubadilisha msimamo huo wakati mwingine kulingana na hali. Wahusika hawa hutegemea wahusika duara na wahusika bapa ili kutoa sifa zao. Kwa mfano, wakiishi na mhusika bapa, wanaweza kuchukua msimamo wa mhusika huyo lakini wakikaa sana

na mhusika mwengine, wanabadilika. Wahusika hawa aghalabu huwakilisha uhalisi wa binadamu.

1.

**a)** ***Sululu*** ni *mwenye hasira*. Anaondoka kwake na kwenda kwa wazazi wake akiwa amebeba upanga. Anapofika huko, anazua fujo kwa kufoka akiitisha kipande cha ardhi na kutishia kumwua babake. Sululu pia ni *mjinga* kwa kuwa alikataa kusoma hata baada ya kupelekwa katika shule nzuri na kulipiwa karo. Baada ya kukataa kusoma, anarudi kwa wazazi wake na kuitisha urithi.

**b)** ***Mamake Sululu*** ni *mvumilivu*. Licha ya kuwa Sululu anamjia na upanga na matusi, yeye anatulia na kujaribu kuzungumza naye Sululu kwa upole bila kumkaripia. Yeye pia ni *mwenye hekima*. Mamake Sululu anajaribu kusema na mwanawe kwa kumkumbusha kuwa hata kipande cha ardhi ambacho amejenga nyumba yake ni urithi kutoka kwa babake. Anaendelea kwa kumfahamisha kuwa hawezi akapewa ekari kumi za ardhi ilhali kaka zake hawana urithi wao na hivyo ni bora wagawane wote.

**ch)*****Mkewe Sululu*** ni *mnyenyekevu* kwa mumewe. Yeye pia ni *mvumilivu* kwani wamepitia mambo mengi (mazuri kwa mabaya) katika ndoa yake na Sululu.

### Zoezi la 2, ukurasa 64

Mwalimu atathmini maelezo ya kila mwanafunzi kuhusu sifa na tabia za rafiki yake.

## Zoezi la 3, ukurasa 64

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Sharti yalenge kazi ya kifasihi waliyopewa. Kwa mfano:

*Mada '**Siku Njema'** inaambatana kabisa na maudhui katika riwaya yenyewe kutokana na dhana kuwa kuna wahusika wengi akiwemo mhusika mkuu ambaye ni Kongowea Mswahili ambao walipitia changamoto nyingi maishani lakini hatimaye mambo yaliwanyookea hivyo siku zao njema ziliwadia. Maudhui kama vile ya umaskini, upweke na dhuluma kwa baadhi ya wahusika kama vile Kongowea Mswahili yanamalizika simu njema inapofika.*

**Zoezi la makundi, ukurasa 65**

1. Mama ***anaandikiwa*** barua na baba.
2. Babu na nyanya ***watafuliwa*** nguo nami.
3. Vikombe vya wageni ***vimenunuliwa*** na Gasimba.
4. Shangazi yetu ***atatembelewa*** na mama.
5. Gari la mwajiri ***linasafishwa*** na dereva.

**Zoezi la 4, ukurasa 65**

1. chungiwa
2. eleza
3. haribiwa
4. kamata

**Zoezi la makundi, ukurasa 66**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga katika kauli ya kufanyika/kutendeka.

**Kwa mfano:**

*1. Wimbo huo umeimbika.*

*2, Barua aliyokuwa akiandika imeandikika.*

*3. Mchezo wanaocheza unachezeka.*

**Zoezi la 5, ukurasa 66**

1. Picha ya ndovu mkubwa ***ilichoreka***.
2. Barua ndefu ***iliandikika***.
3. Maandishi yaliyo ubaoni ***yatasomeka***.
4. Mchezo mwingine ***utachezeka***.
5. Ubao ***ulifutika***.

**Zoezi la 6, ukurasa 67**

1. choma
2. chungika

3. tema
4. orodhesheka
5. piga
6. ombeka

**Zoezi la 7, ukurasa 67**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitenzi katika kauli ya kufanyiwa na kufanyika.

***Kwa mfano:***

1. a) Mama alisafishiwa vyombo na Neza.
   b) Vyombo vilisafishika.
2. a) Maji yote yalinywewa na wageni wachache.
   b) Maji yalinyweka.
3. a) Wagonjwa wote watatibiwa na daktari wa akiba.
   b) Wagonjwa wote watatibika.
4. a) Mfalme ataendeshewa gari na dereva wake.
   b) Gari litaendesheka.
5. a) Mpishi alionjewa mchuzi na dadake.
   b) Mchuzi ulionjeka.

# Somo la 8: Maudhui na dhamira katika fasihi andishi

## Vipindi 26-27: Kusoma shairi

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi shairi husika kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kuchunguza maudhui na dhamira katika fasihi andishi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mashairi ya waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Mashairi yaliyorekodiwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 68;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu uhakiki wa maudhui na dhamira katika fasihi andishi. Utanzu utakaotumika katika uhakiki huu ni utanzu wa ushairi. Ushairi ni utanzu mojawapo wa fasihi andishi ambao hutumia maneno machache teule ambayo hupangwa katika beti na kuwasilishwa kisanaa. Ujumbe wa shairi ambao huandikwa kwenye mistari (mishororo) ya beti kadhaa ndio huwa maudhui ya shairi husika. Vilevile, ni vyema mwalimu awe tayari kushughulikia dhamira ya mwandishi katika sehemu hii. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelezo yaliyotolewa kwa kila zoezi husika.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na funzo lililopita kuhusiana na fasihi andishi hasa kuhusu uainishaji wa wahusika. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika funzo lililotangulia. Baada ya haya, mwalimu atangulize funzo hili kuhusu uhakiki wa maudhui na dhamira katika fasihi andishi. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha kuhusiana na michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 68. Maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye michoro hii? Watu wanaoonekana wanafanya nini?* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona….".* Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na wanayoyaona katika michoro waliyopewa. Kwa mfano: "*Mimi ninaona jembe. Mimi ninawaona watu wakilima shambani n.k."*

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea au wanachokiona katika michoro hiyo. Kutokana na michoro hiyo, wanafunzi wataweza kukisia shairi watakalosoma linahusu nini. Bila shaka shairi hilo linahusu ukulima.

## 8.1 Kusoma na kufahamu

### Shairi kuhusu ukulima

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wasome kwa kimya shairi walilopewa kuhusu ukulima. Wanafunzi wasome shairi hilo kwa kimya huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu shairi hilo walilosoma ili kuhakikisha kuwa wamelielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Kwa nini jembe huenziwa? Masika yanapokuja, tunashauriwa kufanya nini?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika shairi husika. Kwa mfano: *Jembe huenziwa kwa sababu*

*huwasaidia watu kupanda mimea na kupata chakula pamoja na riziki. Masika yanapokuja, tunashauriwa kupanda mimea ili kupata chakula.*

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti shairi hili ili kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya shairi waliyopewa huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa ujumbe katika shairi hilo.

## Tathmini ya vipindi 26-27

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea ufafanuzi na uchambuzi wa ujumbe katika fasihi andishi kupitia kwa shairi walilopewa. Sehemu za shairi, maudhui pamoja na dhamira ya mwandishi irejelewe katika kuhakiki iwapo wanafunzi wamelielewa shairi walilopewa.

## Vipindi vya 28-29: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na shairi walilopewa;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na shairi husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Shairi husika;
- Mtandao wa intaneti;
- *Kamusi ya Kiswahili;*
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 70;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ujifunzaji wa msamiati unaohusiana na shairi lililopo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 68-69. Mwalimu anaweza kuandaa mifano ya mashairi kadhaa ambayo anaweza kuwapa wanafunzi wakayasoma darasani na kuchambua msamiati wake katika makundi mbalimbali. Pia, mwalimu anaweza kuandaa mashairi kadhaa yaliyorekodiwa ili wanafunzi wayasikilize darasani na baadaye kuchambua msamiati wake. Mashairi haya yanaweza kukaririwa kwa mahadhi mbalimbali. Mwalimu anaweza kufanya maandalizi haya mapema kabla ya vipindi hivi.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita kuhusu shairi kuhusu ukulima. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika kipindi kilichotangulia.

## 8.2 Kujifunza msamiati wa shairi kuhusu ukulima

Mwalimu atangulize somo hili kuhusu msamiati unaohusiana na shairi kuhusu ukulima lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 68-69. Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuwaomba waeleze maana ya msamiati waliopatana nao katika usomaji wao wa shairi kuhusu ukulima. Baada ya ufafanuzi wao, wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati huo walioufafanua kama ulivyotumiwa katika shairi walilosoma. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kufanya zoezi la 1 ambapo wanahitajika kuchunguza sentensi walizopewa na kufafanua maana ya misamiati iliyopigiwa mistari katika sentensi hizo. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale inapohitajika. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua msamiati husika. Baada ya ufafanuzi wa msamati huo, wanafunzi

washirikishwe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika shairi walilosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba matumizi ya msamiati husika katika maongezi au maandishi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha sahihi.

## Tathmini ya vipindi 28-29

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mpya wa utanzu wa shairi katika maandishi na maongezi yao.

## Vipindi 30-31: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu maudhui katika fasihi andishi (shairi);
- Kujadili dhamira ya mwandishi wa fasihi andishi (shairi);
- Kuelewa tofauti kati ya maudhui na dhamira katika fasihi andishi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za ushairi za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Shairi husika;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 71;

- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha ambapo majadiliano kuhusiana na maudhui na dhamira katika fasihi andishi kupitia kwa shairi kuhusu ukulima. Mwalimu anaweza kuandaa mashairi mengine yaliyoandikwa ambayo wanafunzi wanaweza kuyasoma darasani au hata kuyakariri kwa mahadhi mbalimbali na baadaye kuyachambua kwa kurejelea maudhui na dhamira. Pia, mwalimu anaweza kuandaa mashairi yaliyorekodiwa ambayo wanafunzi wanaweza kuyasikiliza darasani na kisha wachambue maudhui yake pamoja na dhamira ya malenga husika. *Malenga ni mtunzi wa mashairi.*

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita kuhusu msamiati wa shairi la ukulima. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika kipindi kilichotangulia.

## 8.3 Majadiliano kuhusu maudhui na dhamira ya shairi

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha wajadili kuhusu:

1. *Maudhui yaliyoangaziwa katika shairi walilosoma.*
2. *Dhamira ya mtunzi wa shairi walilosoma.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kufafanua maana ya maudhui na dhamira katika fasihi andishi ili kuleta mwanga kwa wanafunzi kuhusiana na vipengele hivi vya fasihi andishi.

i) ***Maudhui*** ni ujumbe au mawazo makuu ambayo hushughulikiwa katika kazi za kifasihi. Matukio mbalimbali katika kazi ya kifasihi huwa na nia ya kupitisha ujumbe fulani kwa msomaji au mtazamaji. Ujumbe huo

unaopitishwa ndio unaoitwa maudhui. Kwa mfano, kutokana na shairi kuhusu ukulima, mawazo makuu au ujumbe unaopitishwa kwa wasomaji ni kuhusu: *Bidii, ukulima, utamaduni, ukame* miongoni we mengine.

ii) ***Dhamira*** ni nia, sababu, kusudi au lengo la mwandishi kubuni kazi ya kifasihi ambayo anatarajia imwathiri msomaji kwa namna fulani. Msukumo ambao humfanya mtunzi kuitunga kazi ya kifasihi ndio unaoitwa dhamira. Kwa kurejelea shairi kuhusu ukulima, dhamira ya mtunzi wa shairi hilo ni kuwahamasisha watu kuwa wasiwe wavivu ila watie bidii katika kila jambo. Mtunzi wa shairi hili anatumia jembe kama ishara ya kuonyesha namna watu wanahitaji kuwa na bidii bila kuchoka hadi wakamilishe waliyokusudia kufanya. Mtunzi wa shairi hili pia anawazindua watu kuwa ukulima una faida nyingi katika maisha ya binadamu, kwa hivyo wasiupuuze.

Mbali na hayo, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili na kuelewa tofauti iliyopo kati ya maudhui na dhamira katika fasihi andishi. Tofauti ni kuwa maudhui ni ujumbe unaopitishwa kwa msomaji ilhali dhamira ni sababu ya mtunzi kutunga hadithi yake.

Mwalimu ahakikishe anawashurikisha wanafunzi wote katika shughuli hii. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

## Tathmini ya vipindi 30-31

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kikundi kuhusiana na maudhui na dhamira katika fasihi andishi kwa kurejelea shairi walilopewa kuhusu ukulima.

## Vipindi vya 32-33: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kukariri mashairi kwa mahadhi mbalimbali;
- Kuchambua mashairi kwa kuzingatia maudhui na dhamira.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mashairi ya waandishi mbalimbali;
- Wanafunzi wenyewe;

- Rekodi za mashairi mbalimbali;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 71;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufundishia vipindi hivi kuhusiana na uchambuzi wa mashairi mbalimbali kwa kuzingatia vipengele vya maudhui na dhamira. Mwalimu anaweza kuandaa rekodi za mashairi kadhaa ambazo wanafunzi wanaweza kusikiliza darasani kisha wakayachambua. Pia, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi shairi tofauti katika kila kundi ambapo watalichambua. Pia, mwalimu anaweza kuandaa mashairi kadhaa ambayo wanafunzi wanaweza kuyakariri darasani. Wanafunzi wanaweza kupewa mashairi haya ili waweze kuyasoma kabla ya vipindi hivi.

### d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilichopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi ambalo wanafunzi walipewa katika kipindi kilichopita limesahihishwa na wanafunzi waliokuwa na matatizo wameelekezwa.

## 8.4 Majadiliano

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaongoze wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili waweze kusoma shairi walilopewa katika kundi lao na mwalimu wao. Mwalimu ahakikishe kuwa kila kundi lina shairi ambalo watalisoma, walikariri na kisha walichambue kwa kurejelea vigezo vya maudhui na dhamira. Kwa hivyo, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua mahadhi tofauti tofauti ya kukariri mashairi. Mwalimu anaweza kutumia mashairi mbalimbali aliyoyarekodi kwa mahadhi tofauti tofauti. Wanafunzi wanaweza kusikiliza rekodi hizo kisha wakajaribu kukariri mashairi waliyopewa katika makundi yao. Sehemu hii ipanue ujuzi wa wanafunzi kuhusu vipashio vyote vinavyoangaziwa katika mashairi husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wayachambue mashairi waliyopewa kwa kuzingatia maudhui yao pamoja na dhamira ya waandishi wa mashairi hayo. Kila kundi lijitokeze mbele ya wanafunzi wenzao darasani ili wawakaririe wenzao shairi walilopewa na mwalimu wao kwa kutumia mahadhi mbalimbali. Baadaye, kila kundi liwasilishe matokeo ya majadiliano yao kuhusiana na maudhui na dhamira katika mashairi waliyopewa na mwalimu wao. Wanafunzi wengine nao wasikilize namna wanafunzi wenzao wanavyokariri na kuchambua mashairi yao. Kila kikundi kipewe muda wa kuchangia katika mawasilisho ya wenzao huku wakiongozwa na mwalimu.

## Tathmini ya vipindi 32-33

Mwalimu atathmini iwapo ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha baada ya vipindi hivi. Kwa hivyo, awaulize wanafunzi maswali mepesi ya kupima uwezo wao wa kurejelea maudhui na dhamira katika mashairi mbalimbali.

Vilevile, maswali mengine yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kujadiliana katika makundi kuhusu maudhui na dhamira katika mashairi mbalimbali waliyopewa na mwalimu wao. Mbali na hayo, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wamezielewa stadi za maisha kupitia maswali mbalimbali yanayohusiana na maudhui na dhamira katika fasihi andishi kwa jumla.

## Vipindi vya 34-35: Sarufi (Kauli ya kufanyisha/kutendesha)

### a) Malengo ya somo

- Kuainisha vitenzi katika kauli ya kutendesha/kufanyisha;
- Kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kufanyisha.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyisha/kutendesha;
- *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 72;*
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza

kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyisha, michoro inayoonyesha vitendo vya kauli ya kutendesha/kufanyisha pamoja na chombo cha kunasia sauti au breli na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyisha/kutendesha ya mnyambuliko wa vitenzi pamoja na matumizi yao katika maongezi na sentensi sahihi kisarufi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu kwa haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango cha chini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo pamoja na maandishi yaliyo katika breli huku wakitoa maelezo kuvihusu na wale ambao hawawezi kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa vifaa hivyo huku wakiandika maelezo yake ubaoni. Ili kuyafikia malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika Kitabu cha Mwanafunzi.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika vipindi vya sarufi vilivyotangulia kuhusu kauli ya kufanyiwa/kutendewa na kufanyika/kutendeka. Kutokana na maswali haya, mwalimu aweze kuwashirikisha wanafunzi katika kujikumbusha mabadiliko ya vitenzi katika kauli za kufanyiwa/kutendewa na kufanyika/kutendeka katika sentensi za Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

## 8.5 Sarufi

### Kauli ya kufanyisha/kutendesha

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na awaombe kila mmoja ajaribu kumtendea mwenzake kitendo chochote aidha kwa kumsaidia au kwa kumlazimisha. Kwa mfano: *kumbebesha mwenzake vitabu, kumketisha mwenzake kwenye kiti, kumpigisha makofi, kumwimbisha* n.k. Kisha wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kurejelea vitendo walivyowasaidia au kuwalazimisha wenzao kuvitenda.

***Kwa mfano:***

1. Kamana alini***pangisha*** viti darasani.
2. Birasa alitu***imbisha*** nyimbo mbili.
3. Ngabo alitu***pigisha*** makofi.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kuchunguza sentensi ambazo wanafunzi watazitunga katika makundi yao.

Wanafunzi waelekezwe kufanya zoezi la makundi lililo katika *Kitabu cha Mwanafunz*i, ukurasa 72 ambapo wanahitajika kuchunguza mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyisha/kutendesha. Wanafunzi katika makundi yao, wajaze nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali walilopewa.

Baada ya majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaelekeze kufanya zoezi la 3 ambapo wanahitajika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendesha/kufanyisha. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatunga sentensi sahihi kisarufi. Hatimaye, wanafunzi wote washirikishwe katika kusahihisha zoezi hili.

Kupitia kwa zoezi la makundi lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 73, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyiana/kutendeana. Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa katika kauli ya kutendeana/kufanyiana, vitenzi huongezewa viambishi tamati na kupata maana kuwa *wahusika wawili au zaidi wanatendeana kitendo kimoja. Huenda ni kitendo cha wakati huo tu au ni mazoea.* Viambishi tamati ambavyo hutumika katika kauli hii ni: ***-iana*** na ***–eana.***

***Kwa mfano:***

| **Kauli ya kufanya/kutenda** | **Kauli ya kufanyiana/kutendeana** |
|---|---|
| ruka | ruk***iana*** |
| nunua | nunul***iana*** |
| enda | end***eana*** |
| soma | som***eana*** |
| panga | pang***iana*** |
| cheza | chez***eana*** |

***Mifano katika sntensi:***

1. *Wanafunzi wali**tandikiana** vitanda.* (Kutokana na kitenzi '*tandika*')
2. *Watoto wali**andikiana** barua.* (Kutokana na kitenzi '*andika*')
3. *Wageni wali**bebeana** mizigo.* (Kutokana na kitenzi '*beba*')
4. *Wazazi wali**pigiana** makofi.* (Kutokana na kitenzi '*piga*')

Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha kuhusu vitenzi katika kauli hii ya kufanyiana/kutendeana, mwalimu awaombe wafanye zoezi la 6. Zoezi hili lisahihishwe darasani kwa maelekezo ya mwalimu. Mwalimu awasaidie wanafunzi walio na matatizo katika makundi yao.

## Tathmini ya vipindi 34-35

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kunyambua kitenzi katika kauli ya kufanyisha/kutendesha pamoja na kauli ya kufanyiana/kutendeana. Utunzi wa sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli hizi ndiko kutamhakikishia mwalimu kuwa wanafunzi wamepata uelewa wa funzo hili.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufahamu kuwa:

- Kurefusha maneno katika shairi kwa kuyaongezea silabi ili kutosheleza idadi ya mizani inayotakikana huitwa ***mbinu ya mazida***.
- **Kwa mfano:** '*naifuatile'* (silabi sita) badala ya '*naifuata'* (silabi tano)
- Kupunguza idadi ya silabi katika maneno ya shairi ili kupata idadi ya mizani inayotakikana huitwa ***mbinu ya inkisari***.
- **Kwa mfano:** *'usende'* (silabi tatu) badala ya *'usiende'* (silabi nne)
- Mawazo makuu au ujumbe unaojitokeza katika kazi ya fasihi huitwa ***maudhui***. **Kwa mfano:** maudhui ya maadili katika jamii, umaskini, ufisadi, uongozi, elimu, siasa, udhalimu, mapenzi, ndoa, utamaduni, usasa, teknolojia, uhifadhi wa mazingira, kilimo na ufugaji miongoni mwa mengine.
- Sababu, lengo au nia ya mwandishi kubuni kazi ya fasihi huitwa ***dhamira*** ya mwandishi. Dhamira ni kusudi na msukumo unaomfanya mwandishi kuandika kazi ya kifasihi.
- **Kwa mfano:** mwandishi anaweza kuwa na lengo la kuwahimiza wanajamii kuhusiana na maadili katika jamii, wahifadhi mazingira, waelimike, wathamini utamaduni wao n.k.
- Hali ya kumsaidia mtu au kumlazimisha mtu kutenda kitendo fulani ndiyo kauli ya ***kutendesha/kufanyisha***. Katika kauli hii, silabi za mwisho humalizika kwa: -***sha***, -***za***, -***sa***, -***fya*** na -***nya***.

***Kwa mfano:***

1. Mutoni ***alimlisha*** mtoto wao.
2. Mama ***alimtembeza*** mtoto barabarani.
3. Mbwa ***alinusa*** chakula alichopewa.
    - Kauli inayoleta maana kuwa wahusika wawili au zaidi wanatendeana kitendo kile kimoja huitwa ***kauli ya kutendeana/kufanyiana***. Silabi za mwisho kwenye vitenzi katika kauli hii huwa: ***-iana, -eana***.

***Kwa mfano:***

1. Walimu ***wanafundishana*** hisabati.
2. Wafanyakazi ***walisaidiana*** kupanga vitabu.

## 8.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wajaze nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali lifuatalo.

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanyisha | Kauli ya kufanyiana |
|---|---|---|
| ______________ | vunjisha | ______________ |
| lia | ______________ | ______________ |
| ______________ | ______________ | angukiana |
| vaa | ______________ | ______________ |
| ______________ | kaliwa | ______________ |
| ______________ | | ombeana |

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanyisha | Kauli ya kufanyiana |
|---|---|---|
| **vunja** | vunjisha | **vunjiana** |
| lia | **liza** | **liliana** |
| **anguka** | angusha | angukiana |
| vaa | **valisha** | **valiana** |
| **kaa** | **kalisha** | **kaliana** |
| **omba** | **ombesha** | ombeana |

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendesha/kufanyisha na sentensi nyingine tano katika kauli ya kutendeana/kufanyiana. **Kwa mfano:** Tumia kitenzi '*ruka*'

***Kauli ya kufanyisha:*** *Mchezaji aliu**rusha** mpira uwanjani.*

***Kauli ya kufanyiana:*** *Wachezaji wali**rukiana** walipofunga bao.*

1. Imba 2. Vaa 3. Kimbia 4. Cheza 5. Soma

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe kauli ya kufanyisha/kutendesha na kauli ya kufanyiana/kutendeana.

## 8.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 69

1. Mishororo ishirini
2. Vina vya kati ni '***ka***' na '***la***'. Vina vya mwisho ni '***ma***' na '***nga***'.
3. 
    a) Jembe ndilo chanzo cha kipato kwa baba na mama.
    b) Jembe linashauriwa kuwa tayari kulima baada ya shamba kufyekwa.
4. Kifaa muhimu kwa wakulima kinachotumiwa katika kutayarisha mashamba kwa upanzi.
5. Jembe ndiwe mtawala, tangu enzi za wahenga. Kibwagizo kinamaanisha kuwa jembe limetumika tangu zamani.
6. 
    a) Mbinu ya mazida - *tunausema*
    b) Mbinu ya inkisari - *usende*
7. Mizani 320
8. 
    a) ***mtima*** – moyo
    b) ***kukongoka*** – kuzembea
    ch) ***mrama*** – visivyo
    d) ***pasi*** – bila
9. Shairi linalisifu jembe pamoja na kulitia moyo wa kuzidi kufanya kazi. Mtunzi wa shairi analisihi jembe kutochoka katika utendakazi wake kwa wakati wowote ule. Pia, analiombea jembe maisha marefu na yasiyo na vikwazo. (Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi).
10. Ubeti wa kwanza ulisihi jembe limfariji mtunzi wa shairi hili ili naye aliweke liishi zaidi. Hii ni kwa sababu jembe ni kifaa muhimu ambacho kinaenziwa na watu wengi. Jembe ni chanzo cha kipato kwa watu wote na limekuwepo tangu zamani.

### Zoezi la 1, ukurasa 70

Mwalimu atathmini maelezo ambayo yatatolewa na wanafunzi. Sharti maelezo hayo yahusishe msamiati uliopigiwa mistari.

Pia atathmini sentensi za wanafunzi.

***Kwa mfano:***

1. ***uzima -*** hali ya kuwa na afya njema; uhai
2. ***taji -*** ubingwa anaopewa mtu au kitu baada ya ushindi
3. ***dhima -*** wajibu
4. ***mpaji -*** mwenye kutoa kitu kwa wengine; mwenye kuwapa wengine
5. ***mtawala -*** mwenye madaraka ya juu kati ya watu
6. ***tutafyeka -*** tutasafisha kwa kukata chaka na miti
7. ***mtama -*** punje ndogondogo zitokazo mmea wa nafaka wenye bua refu kama mhindi lenye kutoa masuke nchani.
8. ***masika -*** msimu wa mvua nyingi ambayo hunyesha mfululizo.
9. ***homa -*** joto kali la mwili linalosababishwa na maradhi mbalimbali
10. ***mrama -*** kombokombo; visivyo

**Matumizi katika sentensi:**

1. Wagonjwa wote wanatamani ***uzima***.
2. Baba alipewa ***taji*** la kuwa mkulima bora wa viazi vitamu.
3. Mashairi yana ***dhima*** ya kuburudisha.
4. Tunamwabudu Mungu kwa kuwa yeye ni ***mpaji*** wa vyote.
5. ***Mtawala*** mkoa wa Kati atatutembelea.
6. ***Tutafyeka*** uwanja wetu ili tulime na kupanda nyasi.
7. Mama anavuna ***mtama*** leo.
8. Mafuriko yamesababishwa na mvua ya ***masika***.
9. Nimeugua ***homa*** kwa muda mrefu sana.
10. Mambo yalianza kwenda ***mrama*** alipoanza kunywa pombe.

**Zoezi la 2, ukurasa 71**

Mwalimu akariri shairi kwa mahadhi fulani kisha awape wanafunzi fursa ya kukariri shairi lililo katika vitabu vyao. Ahakikishe kuwa wamezingatia matamshi sahihi ya maneno katika shairi husika na wahusishe mahadhi mbalimbali.

**Zoezi la makundi, ukurasa 72**

1. lima
2. pitisha
3. imba
4. chezesha
5. cheka
6. ita
7. andikisha
8. soma
9. keti

**Zoezi la 3, ukurasa 72**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na ziwe na vitenzi katika kauli ya kutendesha.

***Kwa mfano:***

1. Mama anam***lisha*** mtoto wali.
2. Mbwa alim***kimbiza*** mgeni.
3. Nyanya atam***karibisha*** mjomba.
4. Njia hii itatu***fikisha*** mbali.
5. Yeye amem***chezesha*** mgeni wa heshima.

**Zoezi la 4, ukurasa 73**

1. ruka
2. pita
3. andikiana
4. imbiana
5. samehea
6. tembeleana
7. itana
8. beba
9. pikiana
10. tembeza
11. laliana

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi zenye vitenzi katika kauli ya kutendeana. **Kwa mfano:**

1. Wanafunzi wali***someana*** hadithi zao.
2. Mukamulina na Maria hu***tembeleana*** kila mwezi.
3. Wawili hao wali***salimiana*** hewani.
4. Kondoo wali***karibiana*** walipomwona mbwamwitu.
5. Daktari na mgonjwa wali***angaliana***.

**Zoezi la 5, ukurasa 74**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga katika kauli ya kutendeana.

**Kwa mfano:**

*1. Maharusi wanaimbiana nyimbo.*

*2. Dada na kaka wanafuliana nguo.*

*3. Wanafunzi wansomeana hadithi.*

*4. Wachezaji wa mpira wanapigiana mpira.*

*5. Madereva wanaendesheana magari.*

**Zoezi la 6, ukurasa 74**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi zenye vitenzi katika kauli ya kutendeana na kutendesha.

***Kwa mfano:***

***A. Kauli ya kutendesha:***

1. Kaka ali***pandisha*** mizigo garini.
2. Mimi nitam***nywesha*** mtoto uji.
3. Mwalimu alim***pigisha*** mwanafunzi magoti.
4. Mbwa wakali huni***ogofya***.
5. Sara hatani***onjesha*** peremende yake.

***B. Kauli ya kutendeana:***

1. Rita na Anita wali***pandiana*** mlima Virunga.
2. Watoto na akina mama wali***nyweana*** uji.
3. Mutesi na Mutoni wali***pigiana*** simu.
4. Simba na chui wana***ogopeana***.
5. Mimi na mama tuli***onjeana*** mchuzi.

## Somo la 9: Mandhari katika fasihi andishi

## Vipindi 36-38: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha maonyesho mawili ya tamthilia kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kueleza maana ya mandhari katika fasihi;
- Kuchunguza kwa usahihi mandhari katika fasihi andishi kwa kurejelea utanzu wa tamthilia.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za tamthilia za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Maigizo ya tamthilia teule;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 75;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ufafanuzi wa mandhari katika fasihi andishi kwa kurejelea utanzu wa tamthilia. Kama tulivyofundishwa hapo awali, tamthilia ni utanzu mojawapo wa fasihi andishi ambao huhusisha mazungumzo ya moja kwa moja kati ya wahusika mbalimbali. Katika utanzu wa tamthilia, mandhari hutumika

kwa wingi kutokana na maonyesho yake mbalimbali ambayo aghalabu hutendeka katika mazingira tofauti. Sifa hii ya kutumia mandhari mengi ndiyo huifanya tamthilia kuweza kuigizika kwa urahisi kwenye jukwaa.

Ikiwezekana, mwalimu anaweza kupanga kuwapeleka wanafunzi kutazama maigizo ya tamthilia yoyote teule ili waweze kuelewa mandhari mbalimbali na umuhimu wao katika kuyasukuma matukio ya tamthilia mbele.

Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelezo yaliyotolewa kwa kila zoezi husika.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita kuhusiana na maudhui na dhamira katika fasihi andishi kwa kurejelea utanzu wa ushairi. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika somo lililotangulia.

Baada ya haya, mwalimu atangulize somo hili kuhusu mandhari katika fasihi andishi kwa kurejelea utanzu wa tamthilia. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha kuhusiana na michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 75. Maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye michoro hii? Wahusika wanaoonekana ni kina nani? Mandhari yaliyotumika ni gani?* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona ..."* Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kulingana na wanayoyaona katika michoro waliyopewa. Kwa mfano: "*Mimi ninawaona wahusika wawili, mmoja ni wa kike na mwingine ni wa kiume. Hawa huenda wakawa ni Bi Rahma na Sele. Mandhari ya nyumbani yanaonekana hasa ya chumba cha maakuli. Pia, kuna wahusika wengine katika mandhari ya hospitalini"*

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea au wanachokiona katika michoro hiyo. Kutokana na michoro hiyo, wanafunzi

wataweza kukisia sura moja ya tamthilia watakayosoma itahusu nini. Bila shaka sehemu hiyo ya tamthilia inawahusu wahusika Bi Rahma na Sele wakiwa nyumbani pamoja na wahusika Sele na jamila wakiwa hospitalini kutoka katika tamthilia ya '***Kijiba cha moyo'*** iliyoandikwa na Timothy Arege.

## 9.1 Kusoma na kufahamu

### Sura moja ya tamthilia yenye mandhari mbalimbali

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watano watano wasome kwa kimya sura moja ya tamthilia waliyopewa kuhusu mazungumzo kati ya Bi Rahma na Sele wakiwa nyumbani pamoja na Sele na Jamila wakiwa hospitalini. Wanafunzi wasome mazungumzo hayo kwa kimya huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho walichosoma ili kuhakikisha kuwa wamekielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Bi Rahma alikuwa na sababu gani ya kumtembelea Sele? Mazungumzo kati ya Jamila na Sele yanafanyika katika mandhari gani?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika sura ya tamthilia husika. Kwa mfano: *Bi Rahma alienda kumtembelea Sele alipofahamu kuwa Sele alikuwa mgonjwa. Mazungumzo kati ya Sele na jamila yanafanyika katika mandhari ya hospitalini.*

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti mazungumzo hayo ili kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna inayofaa na kwa usahihi. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

## Tathmini ya vipindi 36-38

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea ufafanuzi na uchambuzi wa mandhari kwa kurejelea tamthilia. Mwalimu ahakikishe wanafunzi wanafahamu maana ya mandhari na jinsi ya kuyatambua katika kazi ya kifasihi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kubaini umuhimu wa mandhari katika kazi yoyote ya kifasihi kwa sababu mandhari humsaidia mwandishi kufanikisha dhamira yake ya kubuni kazi yake.

# Vipindi vya 39-40: Kujifunza msamiati

## a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na mandhari katika tamthilia husika;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na mandhari katika utanzu wa tamthilia.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za tamthilia za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- Maigizo ya tamthilia;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 79;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ujifunzaji wa msamiati unaohusiana na msamiati uliotumika katika sura moja ya tamthilia iliyo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 75-78. Mwalimu aandae mifano ya tamthilia au hata sura mbalimbali za tamthilia teule ambazo anaweza kuwapa wanafunzi wakazisoma darasani na kuchambua msamiati wake katika makundi yao. Pia, mwalimu anaweza kuandaa maigizo kadhaa kuhusiana na utanzu wa tamthilia na kuwashirikisha wanafunzi katika makundi yao mbalimbali kuyaigiza mbele ya wanafunzi wenzao. Wanafunzi wanaweza kujaribu kuhusisha mandhari kadhaa katika maigizo yao. Mifano kadhaa ya tamthilia inaweza kurekodiwa na wanafunzi wakasikiliza darasani au hata kuzitazama zikiigizwa kwenye runinga na baadaye kuchambua msamiati wake maalum. Mwalimu anaweza kufanya maandalizi haya mapema kabla ya vipindi hivi. Pia, mwalimu anaweza kuwashirikisha wanafunzi wake mapema kabla ya funzo hili ambapo wanaweza kusoma tamthilia fulani teule kisha wajaribu kufanya majaribio ya kuigiza sehemu fulani fulani za tamthilia hiyo. Uigizaji huu utawapa wanafunzi ujasiri wa kusimama mbele ya wanafunzi na

hata kuzungumza kwa lugha rasmi na sahihi kisarufi pamoja na kuelewa dhana ya mandhari katika kazi ya kifasihi.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika kipindi kilichotangulia. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kushirikishwa katika kujadili mandhari tofauti waliyokumbana nayo katika usomaji wao wa sura moja ya tamthilia waliyopewa katika vitabu vyao.

## 9.2 Kujifunza msamiati kutokana na maonyesho ya tamthilia husika

Mwalimu atangulize somo hili kuhusu msamiati unaohusiana na utanzu wa tamthilia na mandhari mbalimbali.

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya waliopatana nao katika usomaji wao wa sura moja ya tamthilia waliyopewa katika vitabu vyao. Wanafunzi waeleze jinsi msamiati huo ulivyotumiwa katika kifungu cha mazungumzo walichokisoma ambacho ni sura moja ya tamthilia teule. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale inapohitajika au hata vitabu vingine vya marejeleo vya msamiati. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua msamiati husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati walioufafanua. Mwalimu ahakikishe wanafunzi wote wanashirikishwa katika shughuli hii.

Baada ya zoezi hili, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao wafanye zoezi la 1 ambapo wanahitajika kufafanua maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati huo.

Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe tena kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika sura moja ya tamthilia teule waliyosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba matumizi ya msamiati husika katika maongezi au maandishi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha sahihi.

## Tathmini ya vipindi 39-40

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha katika vipindi hivi. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia msamiati mpya waliopatana nao kutoka kwenye sura moja ya tamthilia teule waliyosoma. Pia, mwalimu abaini iwapo wanafunzi wamepata uwezo wa kutambua mandhari mbalimbali kwa kurejelea sura moja ya tamthilia waliyosoma.

# Vipindi 41-43: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu mandhari mbalimbali katika tamthilia husika;
- Kujadili umuhimu wa mandhari katika kazi za kifasihi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za tamthilia za waandishi mbalimbali;
- Wanafunzi wenyewe;
- Maigizo ya tamthilia;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 79;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha kuhusiana na mandhari mbalimbali katika fasihi andishi kwa kurejelea utanzu wa tamthilia. Mwalimu aandae kazi za tamthilia za waandishi mbalimbali pamoja na maigizo ya tamthilia teule. Kwa upande mwingine, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi tamthilia teule wakaisoma kabla ya funzo hili. Wanafunzi wanaweza kutazama tamthilia iliyoigizwa na kurekodiwa. Shughuli hii itawawezesha kupata uelewa mpana wa mandhari mbalimbali pamoja na umuhimu wake.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita kuhusiana na msamiati uliotumika katika sura moja ya tamthilia waliyopewa katika vitabu vyao. Shughuli hii ni ya kuendeleza ujifundishaji wa wanafunzi. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wanaweza kurejelea kazi mbalimbali za utanzu wa tamthilia ambazo wamewahi kuzisoma.

## 9.3 Majadiliano kuhusu mandhari

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha wajadili kuhusu:

1. *Mandhari mbalimbali kwa kurejelea utanzu wa tamthilia.*
2. *Umuhimu wa mandhari katika fasihi andishi.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili masuala hayo katika makundi yao. Wanafunzi wanaweza kujadiliana kwa kutumia mifano kutoka kwenye tamthilia mbalimbali ambazo wamewahi kuzisoma au kuzitazama au hata wanazofahamu. Kupitia majadiliano haya, mwalimu ataweza kuwaelekeza wanafunzi katika kutambua mandhari mbalimbali yanayoweza kutumika katika fasihi andishi hasa kwa kurejelea utanzu wa tamthilia.

Baadhi ya mandhari yanayoweza kujitokeza katika kazi ya kifasihi ni kama vile mandhari ya: *nyumbani (sebuleni, jikoni, chumba cha kulala, msalani), barabarani,*

*hospitalini, mkutanoni, sokoni, kanisani, vyumba vya densi, vilabu, kwenye mazishi, hotelini, msikitini, pangoni, msituni, ndani ya vyombo vya usafiri, shuleni, uwanjani, kwenye kituo cha polisi, kwenye harusi,* miongoni mwa mengine. Mwandishi wa kazi yoyote ya kifasihi huwa ana uhuru wa kuisuka kazi yake katika mandhari yoyote. Mandhari mbalimbali huipa hadithi ladha ya kusomeka na sifa ya kuaminika kwa kiwango fulani. Kama tujuavyo, maisha ya binadamu huhusisha matendo mbalimbali katika mandhari ya kila aina. Mara mtu ameenda sokoni, mara ameenda kanisani, ameenda hospitalini, yuko nyumbani kwake n.k.

Mwalimu ahakikishe amewashirikisha wanafunzi wote katika ujifundishaji huu.

## Tathmini ya vipindi 41-43

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kikundi kuhusiana na matumizi ya mandhari mbalimbali katika kazi ya kifasihi kwa kurejelea utanzu wa tamthilia.

Maswali yake pia yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kueleza umuhimu wa mandhari katika uandishi wa kazi za kifasihi.

## Vipindi vya 44-46: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kuchambua mandhari katika tamthilia ya ***'Urunana'***;
- Kujadili kuhusu umuhimu wa mandhari katika tamthilia ya ***'Urunana'***.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Tamthilia ya ***'Urunana'*** au tamthilia nyingine teule;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 80;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia vipindi hivi kuhusu uchambuzi wa mandhari yaliyotumika katika tamthilia ya ***'Urunana'.*** Mwalimu anaweza kuandaa rekodi ya tamthilia hii iwapo hili linawezekana kisha wanafunzi wanaweza kuisikiliza darasani na kuitazama jukwaani. Shughuli hii itawawezesha wanafunzi kubaini kwa uwazi kabisa mandhari mbalimbali ambayo yametumika katika tamthilia hii teule. Pia, mwalimu anaweza kuandaa mapema maigizo ya tamthilia hii au tamthilia nyingine atakayoteua (inayopatikana kwa urahisi) kwa kuwashirikisha wanafunzi wa pale darasani. Wanafunzi wanaweza kupewa vitabu vya tamthilia hii au tamthilia nyingine ambayo mwalimu atateua ili waweze kuisoma mapema kabla ya somo hili. Hili likifanyika, itakuwa rahisi sana kufundisha somo hili.

**d) Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilichopita kuhusu mandhari mbalimbali ambayo hutumika katika kazi za kifasihi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa mazoezi ambayo wanafunzi walipewa katika kipindi kilichopita yamesahihishwa na wanafunzi waliokuwa na matatizo wameelekezwa vilivyo.

## 9.4 Majadiliano

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaongoze wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili waweze kujadiliana kuhusiana na mandhari mbalimbali yaliyotumika katika tamthilia ya '***Urunana***' au tamthilia nyingine ambayo mwalimu aliteua. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujadiliana kuhusu matukio mbalimbali katika tamthilia teule waliyopewa kwa kuzingatia mahali matukio hayo yanapotendekea. Mahali pa kutendekea kwa matukio mbalimbali katika kazi ya kifasihi ndio huitwa ***mandhari***. Kutokana na haya, wanafunzi watapata uwezo wa kuyatambua mandhari katika kazi zozote za kifasihi. Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wajitokeze mbele ya darasa ili wawasilishe matokeo ya majadiliano yao kuhusiana na zoezi walilopewa la kujadili suala la mandhari katika tamthilia waliyopewa. Wanafunzi wengine nao wasikilize mawasilisho ya wanafunzi wenzao na kuyafuata kwa makini. Kila kikundi kipewe muda wa kuwasilisha majadiliano yao wakiongozwa na mwalimu.

Baada ya majadiliano haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kujadiliana kuhusu umuhimu wa mandhari mbalimbali katika kazi za kifasihi. Wanafunzi waelekezwe katika kuyalinganisha maisha yao ya kila siku na matukio mbalimbali katika kazi za kifasihi kwa kurejelea mandhari husika.

## Tathmini ya vipindi 44-46

Mwalimu atathmini iwapo ujifunzaji umefanyika kwa namna ya kuridhisha. Kwa hivyo, awaulize wanafunzi maswali ya kupima uwezo wao wa kurejelea suala la mandhari mbalimbali katika kazi za kifasihi.

Vilevile, maswali mengine yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kujadiliana katika makundi yao kuhusu umuhimu wa mandhari mbalimbali katika kazi za kifasihi na kwa maisha ya msomaji lengwa.

# Vipindi 47-50: Sarufi (Kauli ya kufanywa/kutendwa)

### a) Malengo ya somo

- Kufahamu mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanywa;
- Kutaja mifano ya vitenzi katika kauli ya kufanywa;
- Kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kufanywa.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 80;
- Chati yenye kuonyesha mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanywa;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ajiandae kufundisha vipindi hivi. Mwalimu atunge mifano kadhaa ya vitenzi katika kauli ya kufanya/kutenda na aonyeshe namna vinavyobadilika hadi

kauli ya kufanywa/kutendwa katika Kiswahili. Mifano hii kadhaa itamwezesha kuwafundisha wanafunzi sehemu hii ya sarufi kuhusu mnyambuliko wa vitenzi, kauli ya kufanywa. Iwapo mwalimu ana wanafunzi walio na matatizo ya kuona, basi itambidi kutunga na kuandika mifano ya vitenzi hivyo pamoja na sentensi kadhaa kwenye breli kwa manufaa ya wanafunzi hao. Kwa wanafunzi walio na matatizo ya kusikia, lugha ishara inaweza kutumika pamoja na kuiandika mifano atakayotunga mwalimu ubaoni.

### d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali somo la sarufi lililopita kuhusu mnyambuliko wa vitenzi. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu somo hilo. Mwalimu achukue fursa hii ya utangulizi ili kuwaomba wanafunzi kusahihisha mazoezi waliyopewa kuhusiana na kipindi kilichopita. Mwalimu aendeleze somo kwa kuwaomba wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kwa kila zoezi.

## 9.5 Kauli ya kufanywa/kutendwa

Ujifunzaji wa sarufi katika hatua hii uchukuliwe kama mwendelezo wa yale yaliyofundishwa katika sehemu ya sarufi kuhusu mnyambuliko wa vitenzi katika kauli ya kufanyia/kutendea, kufanyiwa/kutendewa, kufanyika/kutendeka na kufanyisha/kutendesha katika vipindi vilivyotangulia. Kwa hivyo, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa kauli ya kufanywa/kutendwa pamoja na mabadiliko ya vitenzi katika kauli hii kwa kuwashirikisha kufanya zoezi la makundi lililo katika vitabu vyao. Katika zoezi hili, wanafunzi wanahitajika kujaza jedwali walilopewa kwa kutumia vitenzi sahihi katika kauli ya kufanya na kufanywa.

Ili kurahisisha zaidi uelewa wa wanafunzi katika kipengele hiki, mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wataje vitenzi katika kauli ya kufanya/kutenda kisha wavibadilishe hadi kwenye kauli ya kufanywa/kutendwa. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutambua viambishi tamati ambavyo huongezwa kwenye mizizi ya vitenzi vilivyo katika kauli ya kufanya ili kuvibadilisha na kuwa katika kauli ya kufanywa/kutendwa.

***Kwa mfano:***

| Kauli ya kufanya/kutenda | Kauli ya kufanywa/kutendwa |
|---|---|
| panda | pand***wa*** |
| soma | som***wa*** |
| vunja | vunj***wa*** |
| beba | beb***wa*** |
| cheza | chez***wa*** |

Kutokana na zoezi hili, wanafunzi wataweza kutambua kuwa vitenzi hubadilika kutoka katika kauli ya kufanya/kutenda hadi kwenye kauli ya kufanywa/ kutendwa kwa kuongezewa kiambishi ‘***-wa’.***

***Kwa mfano:***

a) piga – pig***wa***

b) chonga – chong***wa***

ch) dunga - dung***wa***

Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutambua kuwa vitenzi katika kauli ya kufanywa *hutujulisha mtendwa au mtendaji wa kitendo fulani.*

Baada ya wanafunzi kuelewa namna ya kubadilisha vitenzi mbalimbali kuwa katika kauli ya kufanywa/kutendwa, mwalimu awashirikishe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi wakitumia vitenzi vilivyonyambuliwa katika kauli ya kufanywa.

***Kwa mfano:***

1. *Mbwa wao ali**pigwa** kwa mawe na jirani.*
2. *Shamba la nyanya yetu lime**pandwa** mahindi mengi na wafanyakazi wake.*
3. *Biblia hii ime**somwa** na baba yake.*

Wanafunzi watunge sentensi kadhaa katika makundi yao kwa kutumia vitezi katika kauli ya kufanywa. Sharti sentensi hizo ziwe sahihi kisarufi.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 2 katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ambapo wanafunzi wanatakiwa kutunga sentensi sahihi katika kauli ya kufanywa.

Zoezi hili lisahihishwe kwa kuwashirikisha wanafunzi wote na maelezo ya mwalimu yatilie mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika. Mwishowe, mwalimu awaombe wanafunzi wafanye zoezi la 3 na zoezi la 4 katika sehemu hii. Mwalimu ahakikishe kuwa mazoezi haya yamesahihishwa kabla ya kipindi kijacho.

## Tathmini ya vipindi 47-50

Mwalimu ahitimishe vipindi hivi kwa kuuliza maswali yanayodhamiria kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa mnyambuliko wa vitenzi katika kauli ya kufanywa. Wanafunzi pia waulizwe maswali mepesi ya kubaini iwapo wamefahamu namna ya kuvibadilisha vitenzi kutoka kwenye kauli nyingine hadi kwenye kauli ya kufanywa/kutendwa. Wanafunzi nao, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kwa kudhihirisha iwapo wameelewa mambo yote muhimu yaliyotakikana kuzingatiwa katika vipindi hivi.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

### Maelezo muhimu kwa mwalimu

- Wakati, hali au mahali ambapo tukio linaelezewa kutokea katika fasihi huitwa ***mandhari***.
- Mandhari yanaweza kuwa ya kihalisia (kweli) kama vile: *mtoni, hospitalini, nyumbani, shambani, barabarani, sokoni, msalani, kanisani, msikitini* n.k.
- Mandhari pia yanaweza kuwa ya kidhahania (ya kufikiria tu) kama vile: *hewani, angani, kuzimu, kwenye jua* n.k.
- Mandhari pia yanaweza kuhusisha wakati wa kutendeka kwa tukio fulani, kwa mfano: *asubuhi, jioni, usiku, mchana, mafungulia ng'ombe, alasiri* n.k.
    - Katika mnyambuliko wa vitenzi, hali ya kutufahamisha kuhusu mtendaji au mtendwa wa kitendo fulani huitwa kauli ya ***kufanywa/ kutendwa***. Mara nyingi katika kauli hii, silabi za mwisho humalizika kwa: -***wa***.

***Kwa mfano:***

a) Ubao ume***futwa*** na kiranja.

b) Nguo ya mama ime***shonwa*** tena na fundi huyu.

## 9.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kufanikisha ujifunzaji wa pamoja, zoezi la ziada litolewe kwa wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kujibu swali hili:

*Kamilisha jedwali lifuatalo kwa usahihi.*

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanywa |
|---|---|
| onja | ______________ |
| ______________ | fungwa |
| andika | ______________ |
| ______________ | onwa |
| ficha | ______________ |
| ______________ | kunjwa |

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanywa |
|---|---|
| onja | **onjwa** |
| **funga** | fungwa |
| andika | **andikwa** |
| **ona** | onwa |
| ficha | **fichwa** |
| **kunja** | kunjwa |

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi tano kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kufanywa.

***Kwa mfano:***

***Kauli ya kufanya:*** Mukandayisenga atai***<u>paka</u>*** rangi nyumba yetu mpya.

***Kauli ya kufanywa:*** Nyumba yetu mpya ita***<u>pakwa</u>*** rangi na Mukandayisenga.

## 9.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 78

1. Nyumbani kwake Sele.
2. Sele anaonekana mwenye mawazo ila ni mtulivu. Anajipepea kwa kuwa kuna joto jingi.
3. Bi. Rahma alitaka kumjulia Sele hali.
4. Bi. Rahma alipata tetesi kuwa Sele ni mgonjwa.
5. Kwa sababu ya mawazo mengi baada ya kusimamishwa kazi.
6. Hospitalini
7. Ili damu ifanyiwe uchunguzi wa kutambua mgonjwa anaugua wapi.
8. Jamila ni muuguzi wake Sele.
9. Kipimajoto
10. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Wanaweza kutoa hoja kama vile:
    a) ***Afya:*** hali ya kiafya ya Sele ndiyo imepelekea kuwepo kwa maonyesho haya mawili. Sele amedhoofika kiafya kutokana na kusimamishwa kazi. Anapelekwa hospitalini ili afanyiwe uchunguzi wa kiafya.
    b) ***Kazi:*** kama njia ya kujikimu kimaisha, ni sharti binadamu wafanye kazi. Sele pamoja na wenzake wanasimamishwa kazi kufuatia agizo lililotolewa. Hali hii ya kukosa kazi inampa Sele mawazo mengi ambayo yanaathiri hali yake ya afya na kumfanya apelekwe hospitalini.

### Zoezi la msamiati, ukurasa 79

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati kutoka kwenye tamthilia waliyosoma. Pia, atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***uvundo -*** harufu mbaya
2. ***kusimamishwa kazi*** - hali ya mtu kukoseshwa kazi kwa kipindi fulani ambacho huenda ni cha kumfanyia uchunguzi fulani kisha baadaye atarejea kazini au afutwe kazi kufuatia matokeo ya uchunguzi.

**Matumizi katika sentensi:**

1. Mzoga uliooza unatoa ***uvundo***.
2. Meneja wa kampuni ya mafuta anastahili ***kusimamishwa kazi*** ili uchunguzi wa madai ya utumizi mbaya wa mamlaka dhidi yake ukamilike.

**Zoezi la 1, ukurasa 79**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati kutoka kwenye maonyesho ya tamthilia waliyosoma.

***Kwa mfano:***

1. ***kochini -*** kwenye kiti chenye sehemu ya kuwekea mikono na kilichowekwa mito katika sehemu ya kukalia na kuegemea
2. ***mtulivu -*** mtu mpole asiyewasumbua na kuwakera wengine
3. ***tetesi -*** uvumi; habari ambayo haijathibitishwa
4. ***alikata tama -*** alitamauka
5. ***aliachishwa kazi -*** alikoseshwa kazi au ujira
6. ***kunguru -*** aina ya ndege anayetumiwa kama ishara ya woga; mtu mwoga
7. ***akitafakari -*** akiwaza
8. ***akijipepea -*** akijitikisia kipepeo ili kupata upepo
9. ***uvundo -*** harufu mbaya
10. ***nawathamini -*** nawaenzi

**Matumizi katika sentensi:**

1. Babu amelala ***kochini.***
2. Paka wa bibi ni ***mtulivu*** sana.
3. Kuna ***tetesi*** kuwa watu walioathirika na ukame ni wengi sana.
4. Mwalimu ***alikata tamaa*** wanafunzi wake walipofeli mtihani wa kitaifa.
5. Mkurugenzi mkuu wa benki ***ameachishwa kazi*** na serikali.
6. ***Kunguru*** hawapatikani katika mbuga ya Akagera.
7. Mwanafunzi alibaki ***akitafakari*** jawabu la swali la Hisabati.
8. Mwigizaji alikuwa ***akijipepea*** mchezo ulipokamilika.

9. Matunda yaliyoharibika yameleta ***uvundo*** katika nyumba ya shangazi.
10. Mimi ***nawathamini*** wauguzi wote.

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 79**

Mwalimua atathmini maelezo ya wanafunzi katika majadiliano yao. Wanafunzi wataje mandhari kama vile: *nyumbani, sokoni, mahakamani, shuleni au kwenye kituo cha mabasi*. Wanaweza pia kutaja muda kwa kuzingatia, saa na nyakati kama vile: *jioni, asubuhi, mchana* na *usiku*. Wanapoeleza mandhari, ni vyema maelezo hayo yaelekee kujenga taswira ya mandhari hayo akilini mwa msomaji. Wanaweza wakatoa maelezo ya vitu vilivyo katika maeneo hayo.

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 80**

Mwalimua atathmini majadiliano ya wanafunzi kuhusu matumizi ya mandhari mbalimbali katika tamthilia ya '***Urunana***' au katika tamthilia yoyote ambayo mwalimu ataiteua kulingana na kupatikana kwake. Wanafunzi wataje mahali pa kutendeka kwa matukio mbalimbali pamoja na wakati wa kutendeka kwa matukio hayo. Haya yote ndiyo yanayounda mandhari katika kazi ya kifasihi.

**Zoezi la makundi, ukurasa 80**

1. panda
2. (ku)la
3. rushwa
4. vunja
5. someshwa
6. cheka
7. ita
8. pigwa
9. beba
10. chorwa

**Zoezi la 2, ukurasa 81**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitenzi katika kauli ya kutendwa.

***Kwa mfano:***

1. Kazi ya ziada ita***fanywa*** na wanafunzi wote.
2. Gunia la viazi lita***bebwa*** na wavulana wanne.
3. Picha ya rais ita***chorwa*** na msanii huyu chipukizi.
4. Tamthilia ita***igizwa*** na wanafunzi wa shule ya Amagoro.
5. Mila potovu zime***pitwa*** na wakati.

**Zoezi la 3, ukurasa 81**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe vitenzi katika kauli ya kutendwa.

***Kwa mfano:***

1. Mbegu za mihogo ***zitapandwa*** na nyanya.
2. Gari la askari ***lilipitwa*** na pikipiki yetu.
3. Mwalimu wetu ***aliombwa*** kusafiri na afisa wa elimu.
4. Kambi ya wakimbizi ***ilichomwa*** jana na waandamanaji.
5. Mbuzi ***anavutwa*** kwa kamba na mfugaji.

**Zoezi la 4, ukurasa 82**

1. Gari ***liliendeshwa*** vibaya na dereva yule.
2. Nyama ***ilikatwa*** vipande vidogovidogo.
3. Kwa nini sebule yenu ***imepangwa*** hivi?
4. Barua ya kuomba msamaha ***iliandikwa*** na mwanafunzi.
5. Mungu ***huombwa*** na binadamu wote.

# Somo la 10: Uhakiki wa mbinu za lugha katika fasihi andishi

## Vipindi vya 51-53: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi sura moja ya riwaya husika kwa utambuzi wa herufi, silabi, maneno na sentensi;
- Kuelewa ujumbe wa sura moja ya riwaya husika;
- Kutambua mbinu za lugha zilizotumika katika sura moja ya riwaya husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali;
- Mtandao wa intaneti;
- Riwaya ya '***Utengano***';
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 83-86;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ufafanuzi wa mbinu za lugha katika fasihi andishi kwa kurejelea utanzu wa riwaya ambao ni mojawapo wa tanzu za fasihi andishi. Kifungu kilicho katika *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 83-86 ni sura moja kutoka katika riwaya iitwayo ***'Utengano'*** iliyoandikwa na Said A. Mohamed ambaye ni mwandishi maarufu wa kazi mbalimbali za kifasihi. Kifungu hicho cha sura moja ya riwaya kimehusisha matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha kwa namna ya kuufanya usomaji wake uvutie. Mwalimu aandae mpangilio wa usomaji wa sura moja ya riwaya waliyopewa. Ikiwezekana, mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi wasome riwaya nzima ya ***'Utengano'*** kabla ya kuanza kwa funzo hili ili waweze kuelewa kwa urahisi sura hii moja inahusu nini.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Baadaye, mwalimu atangulize somo hili kuhusu matumizi ya mbinu za lugha kwa kurejelea utanzu wa riwaya kwa kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha. Maswali kama vile: *Umewahi kusoma riwaya gani? Riwaya hiyo ilihusu nini? Riwaya hiyo imetumia lugha ya aina gani katika kuwasilisha maudhui yake?* n.k. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kwa kueleza aina za riwaya ambazo wamewahi kusoma, aina ya lugha iliyotumiwa katika riwaya hizo pamoja na jumbe za riwaya hizo.

Mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili watazame mchoro ulio kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 83. Mwalimu awaulize wanafunzi swali kuhusiana na mchoro huo. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye mchoro huu?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu swali waliloulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"Mimi ninaona..."* Wanafunzi kwa upande wao, wajibu swali la mwalimu. Kwa mfano, "*Mimi ninamwona binti aliyeketi peke yake chini ya mti. Binti huyu anaonekana ana mawazo mengi.*" Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha mchoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea au kinachoonekana katika mchoro huo.

## 10.1 Kusoma na kufahamu

### Sura ya riwaya yenye mbinu za lugha

Mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili wasome kwa kimya kifungu cha sura moja ya riwaya ya ***'Utengano'*** kilicho katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 83-86. Wanafunzi wasome kwa kimya huku wakitambua na kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu kifungu walichosoma ili kuhakikisha kuwa wamekisoma na kukielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwauliza: *Kwa nini mhusika Maimuna alitoroka kutoka kwao? Je, alipata kazi gani huko mjini Pumziko? Nani aliyemsafirisha Maimuna hadi mjini Pumziko?*

Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma kutoka kwenye sura moja ya riwaya waliyopewa. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kujibu: *Mhusika Maimuna alitoroka kutoka kwao kwa kuogopa hasira ya babake iwapo angegundua kuwa alikuwa mjamzito. Maimuna alipata kazi ya ukahaba huko mjini Pumziko. Maimuna alisafirishwa na Bi Farashuu hadi mjini Pumziko.* Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya kifungu kilichopo na kukielewa, mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti kifungu hicho kwa kuhakikisha kuwa wanatamka maneno kwa namna inayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa. Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali ya ufahamu waliyopewa katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 86. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo walitatizika katika kujibu kwao. Mwalimu awasaidie wanafunzi wenye matatizo ya kuelewa msamiati uliotumika katika kifungu hicho.

Baada ya haya, mwalimu awape wanafunzi zoezi la kutambua mbinu za lugha zilizotumika katika sura moja ya riwaya waliyoisoma hapo awali kutoka kwenye riwaya ya '***Utengano***'. Haya yatajadiliwa katika kipindi kitakachokuja baada ya kipindi cha ujifunzaji wa msamiati.

## Tathmini ya vipindi 51-53

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifunza. Maswali hayo yaegemee hasa katika kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutambua lugha iliyotumika katika sura moja ya riwaya waliyoisoma pamoja na kuchambua ujumbe wa sura hiyo.

## Vipindi vya 54-55: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kufafanua msamiati mpya kutokana na sura ya riwaya husika;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali;
- *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*;
- *Riwaya ya '**Utengano**'*;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 86;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu kujenga uelewa zaidi kuhusiana na msamiati wa muktadha wa sura moja ya riwaya ambayo wanafunzi waliisoma hapo awali. Uelewa huu unahusisha utambuzi wa maana na matumizi ya msamiati husika katika kutunga sentensi sahihi kisarufi pamoja na kuutumia katika maongezi ya kila siku. Mwalimu anaweza kuandaa kamusi mbalimbali za kusaidia katika kufafanua msamiati kutoka katika kifungu kilichopo. Kamusi ya istilahi za fasihi itafaa hapa iwapo itapatikana.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awachangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika shughuli hii.

## 10.2 Kujifunza msamiati kutokana na sura ya riwaya husika

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kuwaomba wachunguze msamiati mpya ambao walipatana nao katika usomaji wa kifungu cha sura moja ya riwaya walichopewa kutoka kwenye riwaya ya '***Utengano***' kisha waufafanue kwa kuueleza. Wanafunzi waeleze maana ya msamiati husika kwa kuzingatia jinsi ulivyotumiwa katika kifungu walichokisoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale watakapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi

wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua maana ya msamiati husika. Baadaye, wanafunzi watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati waliojadili. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kubaini usahihi wa sentensi ambazo watatunga.

Baada ya hapo, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 2 na waufafanue kwa maelezo sahihi. Baada ya ufafanuzi wa msamiati huo, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika makundi yao watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati walioufafanua.

Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wasahihishe kwa pamoja zoezi hilo la msamiati. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe tena kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika sura ya riwaya waliyosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha rasmi na sahihi.

## Tathmini ya vipindi 54-55

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali hayo yaegemee hasa katika kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kufafanua msamiati wa kifungu cha sura ya riwaya walichopewa pamoja na kuutumia msamiati huo waliojifunza katika kutunga sentensi sahihi kisarufi na katika maongezi yao ya kila siku.

## Vipindi vya 56-58: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili mbinu za lugha mbalimbali katika fasihi andishi;
- Kueleza matumizi ya mbinu za lugha katika riwaya ya '***Utengano***'.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Wanafunzi wenyewe;
- Riwaya ya '***Utengano***';
- Kamusi ya fasihi;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 87;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Sehemu hii itahusisha majadiliano ya wanafunzi katika makundi mbalimbali. Wanafunzi watapewa nafasi ya kutoa masimulizi yao wenyewe kuhusu hadithi zozote za kifasihi ili kubainisha matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha. Mwalimu anaweza kuandaa kazi kadhaa za kifasihi za waandishi mbalimbali ambazo anaweza kuziwasilisha darasani. Pia, mwalimu anaweza kuwapa wanafunzi riwaya ya '***Utengano***' au riwaya nyingine atakayoteua kwa minajili ya kuisoma kabla ya funzo hili ili iwe rahisi kwao kutambua na kuelewa matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha kwa kutumia mifano kadhaa.

**d) Utaratibu wa somo**

***Utangulizi***

Mwalimu aanze kipindi kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi ya kuwachangamsha kuhusu kazi za kifasihi ambazo wametangamana nazo. Mifano ya maswali hayo ni kama vile: *Mbinu za lugha zilizotumika katika kazi ulizosoma ni zipi?*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

## 10.3 Majadiliano kuhusu mbinu za lugha

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awaombe wajadili kuhusu mbinu mbalimbali za lugha ambazo zimetumika katika sehemu ya riwaya ya '***Utengano***' waliyoisoma hapo awali. Wanafunzi waelekezwe kujadili kuhusu:

1. Matumizi ya tanakali za sauti
2. Matumizi ya semi
3. Matumizi ya majazi
4. Matumizi ya mbinu ya kuchanganya ndimi
5. Matumizi ya mbinu ya uhaishaji

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili kuhusu maswali yaliyo hapo juu. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii huku wakirejelea sura ya riwaya waliyopewa katika vitabu vyao.

Baadhi ya majibu ambayo wanafunzi wanaweza kuyapendekeza ni kama vile:

1. ***Tanakali ya sauti*** ni mbinu ya kuiga milio ya vitendo na hali mbalimbali katika uandishi na usimulizi. Mifano ni kama vile: *kulala fofofo, kulia kwikwikwi, kunyamaza ji* n.k.

Kwa kurejelea sura ya riwaya waliyosoma wanafunzi, tanakali ya sauti imetumika kueleza huzuni aliokuwa nao Maimuna na jinsi alivyokuwa amelia sana. Tunaambiwa: '*Maimuna hakujibu neno. Alivuta* ***kwikwi za kilio'***.

2. ***Semi*** ni matumizi ya fungu la maneno ili kuashiria hali fulani kwa maana iliyofichika. Kwa mfano: aga dunia (*fariki, kufa*), kata kauli (*amua*), pigwa kalamu (*futwa kazi*) n.k.

Kwa kurejelea sura ya riwaya waliyosoma wanafunzi, baadhi ya semi zilizotumika ni kama vile:

i) '*Farashuu na Mama Jeni walikw**enda chemba***.' Semi '*enda chemba'* imetumika kumaanisha kujitenga na watu na kuwa katika mahali mbali kidogo na pa siri ili kuzungumza kuhusu jambo ambalo halifai kusikika na watu wengine.

ii) '*Ulipita muda. Hatimaye ali**kata shauri'***. Semi hii inamaanisha kufanya uamuzi.

iii) '*Maimuna ali**salimu amri'***. Semi hii inamaanisha Maimuna alikubaliana na aliyokuwa akiambiwa.

1. Mbinu ya ***majazi*** imetumika kwenye neno '***Pumziko***' linaloashiria mji alikopelekwa Maimuna na Bi Farashuu. Huu ni mji wa kupumzika na kustarehe tu kama walivyoufahamu wenyeji wake na kama jina lenyewe linavyomaanisha. Majazi ni kumpa mtu au mahali jina kulingana na sifa zake.

2. Mbinu ya ***kuchanganya ndimi*** huhusisha matumizi ya maneno ya lugha nyingine isipokuwa Kiswahili, kwa mfano: *darlin, drive ins* n.k.
3. Mbinu ya ***uhaishaji*** hutumika kuvipa vitu visivyo na uhai sifa za binadamu. Kwa mfano: '*Aliuzamisha uso wake kwenye mto* ***akaunywesha machozi'***. Viumbe hai kama vile wanyama ndio wenye uwezo wa kunywa kitu kiowevu.

Katika makundi yao, mwalimu awashirikishe wanafunzi kuchunguza mifano mingine zaidi kutoka kwenye sura ya riwaya waliyopewa katika vitabu vyao. Wanafunzi waelekezwe katika kufanya utafiti zaidi kuhusiana na mbinu nyingine ambazo hutumika katika kazi za kifasihi kama vile: *chuku, jazanda, utohozi, taharuki, mbinu rejeshi, uzungumzi nafsia* miongoni mwa nyingine.

Majadiliano haya yote yatawawezesha wanafunzi kuelewa kwa mapana na marefu matumizi ya mbinu za lugha katika kazi za kifasihi na namna ya kuzibainisha wakati wa usomaji wao.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusoma riwaya nzima ya '***Utengano***' au riwaya nyingine ambayo ataichagua kisha wanafunzi wabainishe mbinu mbalimbali za lugha zilizotumiwa katika hadithi hiyo.

Shughuli hii itawasaidia wanafunzi kuzifahamu mbinu tofauti za lugha zinazotumika katika kazi za kifasihi.

## Tathmini ya vipindi 56-58

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti ya kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea mbinu mbalimbali za lugha kutokana na hadithi waliyoisoma katika utanzu wa riwaya ili kutathmini iwapo wanafunzi wameelewa funzo hili. Kupitia kwa majadiliano ya wanafunzi pamoja na mawasilisho yao, wanafunzi wakuze ujasiri wao wa kuzungumza mbele ya watu na pia matumizi yao ya lugha rasmi na sahihi yaimarike zaidi. Pia, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi ili kubaini iwapo wameelewa namna ya kuzitambua mbinu mbalimbali za lugha katika kazi ya kifasihi.

# Vipindi vya 59-61: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kujadili mbinu mbalimbali za lugha katika riwaya ya '***Siku Njema'*** au riwaya nyingine teule;
- Kutaja na kueleza mifano ya namna mbinu mbalimbali za lugha zilivyotumika katika riwaya husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Kazi za riwaya za waandishi mbalimbali;
- Riwaya ya '***Siku Njema'*** au riwaya nyingine teule;
- Wanafunzi wenyewe;
- Kamusi ya fasihi;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 88;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### c) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya funzo hili, mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika funzo hili kama vile: kamusi ya fasihi pamoja na vitabu vingine vya rejea vya kuonyesha ufafanuzi wa mbinu mbalimbali ambazo hutumika katika fasihi andishi. Kupitia kwa vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua na kuelewa kwa undani mbinu mbalimbali za lugha zitumiwazo na waandishi wa kazi za kifasihi.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na waliyojifundisha katika kipindi kilichopita.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

## 10.4 Majadiliano kuhusu mbinu za lugha

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha wajadiliane kuhusu mbinu mbalimbali za lugha ambazo zimetumika katika riwaya ya '***Siku Njema'***. Mwalimu anaweza kuchagua riwaya nyingine ambayo inaweza kupatikana kwa urahisi ili wanafunzi waijadili. Riwaya ni nyingi mno, itategemea na ile itakayopatikana kwa urahisi ili wanafunzi waweze kuichambua.

Mwalimu ahakikishe kila kundi linapewa nafasi na wakati wa kutosha wa kujadiliana kuhusu suala hili la mbinu za lugha kwa undani. Wanafunzi watolee mbinu hizo za lugha mifano ya kutosha kutoka kwenye riwaya watakayosoma.

Baadhi ya majadiliano ambayo yanaweza kuwasilishwa na wanafunzi katika makundi yao iwapo watakuwa wanarejelea riwaya ya '*Siku Njema'* kuhusiana na mbinu mbalimbali za lugha ni kama vile:

1. ***Matumizi ya methali***: Hii ni kauli fupi ambayo hutumiwa katika jamii kutoa ukweli fulani wenye lengo la kuonya, kufundisha, kuhukumu n.k. Katika riwaya ya '*Siku Njema'*, methali zimetumika kwingi kwenye riwaya nzima, kama vile, ukurasa 2 (*Dau la mnyonge haliendi joshi*), ukurasa 18 (*Ukweli una nguvu kuliko uongo*), ukurasa 79 (Mui huwa mwema) miongoni mwa methali nyingine nyingi.
2. ***Kinaya:*** Hali ya kuonyesha kinyume cha matarajio ya msomaji. Kwa mfano, kutokana na riwaya ya '*Siku Njema'*, mamake Kongowea Mswahili alikuwa na sifa tele ila alikuwa maskini. Msomaji anatarajia Zainabu Makame awe tajiri kadri ya sifa alizokuwa nazo.
3. ***Chuku:*** Hii ni mbinu ya kutia maelezo chumvi zaidi ya yanavyofaa kuwa. Kwa mfano, katika ukurasa 15 tunapoambiwa kuwa '*mazishi ya Zainabu Makame yalikuwa yamejaa watu hata hapakuwa na nafasi ya kutema mate wala nzi kupita*'.

Mbinu nyingine ambazo wanafunzi wanaweza kujadili kuhusu ni: *uhaishaji, matumizi ya maswali ya balagha, jazanda, taharuki, utohozi, kuchanganya ndimi, majazi, uzungumzi nafsia, matumizi ya tashbihi* miongoni mwa nyingine.

Mwalimu awape wanafunzi muda wa kutosha kujadiliana kuhusiana na mbinu mbalimbali za lugha katika kazi teule ya kifasihi.

Baadaye kila kundi lipewe muda wa kuwasilisha matokeo ya majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao. Mwalimu atumie nafasi hii kusahihisha makosa ya kimatamshi ya wanafunzi wakati wa mawasilisho yao. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wanashirikishwa katika shughuli hii.

Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadiliana kuhusu uhakiki wa waandishi mashuhuri wa fasihi ya Kiswahili. Wanafunzi wataje waandishi wa fasihi ya Kiswahili wanaowafahamu nchini Rwanda na katika nchi nyingine zinazoenzi lugha ya Kiswahili.

## Tathmni ya vipindi 59-61

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kwa lengo la kuchunguza iwapo wanaweza kutambua na kueleza mbinu mbalimbali za lugha kwa kuzitolea mifano kutoka kwenye utanzu wa riwaya pamoja na kazi nyingine za kifasihi. Kazi mbalimbali za kifasihi zinaweza kutumika katika funzo hili ili kumpa mwanafunzi uelewa mpana wa matumizi ya mbinu mbalimbali za lugha.

## Vipindi vya 62-65: Sarufi (Kauli ya kufanyua/kutendua)

### a) Malengo ya somo

- Kuainisha vitenzi katika kauli ya kutendua/kufanyua;
- Kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kufanyua.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyua/kutendua;
- *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 89;*
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile: chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyua, michoro inayoonyesha vitendo katika kauli ya kutendua/kufanyua pamoja na chombo cha kunasia sauti au breli na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua mabadiliko ya vitenzi katika kauli ya kufanyua/kutendua ya mnyambuliko wa vitenzi pamoja na matumizi yao katika maongezi na sentensi sahihi kisarufi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu kwa haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango cha chini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ili kuyafikia malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu cha Mwanafunzi*.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika vipindi vya sarufi vilivyotangulia kuhusu kauli ya kufanywa/kutendwa. Kutokana na maswali haya, mwalimu aweze kuwashirikisha wanafunzi katika kujikumbusha mabadiliko ya vitenzi katika kauli za kufanywa/kutendwa katika sentensi za Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

## 10.5 Kauli ya kufanyua/kutendua

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili. Mwanafunzi mmoja atende kitendo fulani kwa mfano: *kupanga vitabu, kuinama, kutia vitabu mkobani* miongoni mwa vitendo vingine. Mwanafunzi wa pili ajaribu kufanya kinyume cha vitendo alivyotenda mwenzake, kwa mfano: *kupangua vitabu, kuinuka na kuvitoa vitabu mkobani*.

Huu utakuwa msingi mwema wa kujifundisha kauli ya kufanyua/kutendua. Wanafunzi waelekezwe kutambua kuwa kauli ya mnyambuliko wa vitenzi ya kufanyua/kutendua huonyesha maana ya kinyume. Wanafunzi washirikishwe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kurejelea vitendo walivyofanya na kufanya kinyume yavyo.

***Kwa mfano:***

1. Kalisa ali***panga*** vitabu naye Mutoni akavi***pangu***a.
2. Neza ali***inama*** na baadaye aka***inuka***.
3. Mwalimu alivi***tia*** vitabu mkobani naye Ngabo akavi***toa***.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kuchunguza sentensi ambazo watazitunga katika makundi yao. Sentensi hizo sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitendo katika kauli ya kufanyua.

Wanafunzi waelekezwe kufanya zoezi la makundi lililo katika *Kitabu cha Mwanafunz*i, ukurasa 89 ambapo wanahitajika kuchunguza mabadiliko ya vitenzi kutoka katika kauli ya kufanya/kutenda hadi kwenye kauli ya kufanyua/kutendua. Wanafunzi katika makundi yao, wajaze nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali walilopewa.

Baada ya majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaelekeze kufanya zoezi la 2 ambapo wanahitajika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendua/kufanyua. Mwalimu azunguke darasani akiwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatunga sentensi sahihi kisarufi. Hatimaye, wanafunzi wote washirikishwe katika kusahihisha zoezi hili.

Viambishi tamati ambavyo huongezwa kwenye mizizi ya vitenzi katika kauli ya kufanyua/kutendua ni: ***-oa*** na ***-ua***. Sharti ikumbukwe kuwa vitenzi ambavyo huwa katika kauli ya kufanyua ni vile vinavyoweza kuwa na kinyume chake pekee, kwa mfano *tia – toa*.

***Kwa mfano:***

| **Kauli ya kufanya/kutenda** | **Kauli ya kufanyua/kutendua** |
|---|---|
| fuma | fum***ua*** |
| tega | teg***ua*** |
| shona | shon***oa*** |
| choma | chom***oa*** |

**Mifano katika sentensi:**

1. *Mama ali**bandika** picha ukutani naye baba akai**bandu**a.*
2. *Shangazi ali**anika** nguo asubuhi nami nikazi**anua** jioni.*

Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha kuhusu vitenzi katika kauli hii ya kufanyua/kutendua, mwalimu awaombe wafanye zoezi la 3 na zoezi la 4. Mazoezi haya yasahihishwe darasani kwa maelekezo ya mwalimu. Mwalimu awasaidie wanafunzi walio na matatizo katika makundi yao.

## Tathmini ya vipindi 62-65

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kunyambua vitenzi katika kauli ya kufanyua/kutendua. Utunzi wa sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli hii ndio utamhakikishia mwalimu kuwa wanafunzi wamepata uelewa wa funzo hili.

### Maelezo muhimu kwa mwalimu

- Matumizi ya lugha kwa njia ya kipekee katika fasihi huitwa ***mbinu za lugha*** au ***fani.***

Mifano ya mbinu za lugha ni kama vile: *matumizi ya methali, tashbihi, majazi, mbinu rejeshi, semi, istiara, tanakali za sauti, jazanda, uhaishaji, utohozi, kuchanganya ndimi, taharuki, uzungumzi nafsia, chuku* miongoni mwa nyingine.

- Hali ya kuonyesha kinyume cha kitendo huwa katika kauli ya ***kutendua/ kufanyua***. Katika kauli hii, viambishi tamati ambavyo huongezwa kwenye mizizi ya vitenzi ni: ***-ua*** na ***-oa***.

***Kwa mfano:***

**1.** Baba ali***angua*** koti lake alilo*angika* ukutani.

**2.** Tuli*funika* sufuria zetu ambazo watoto walikuwa wamezi***funua***.

## 10.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wajaze nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali lifuatalo.

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanyua |
|---|---|
| ______________ | fumua |
| choma | ______________ |
| ______________ | toa |
| tega | ______________ |
| ______________ | pakua |

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanyua |
|---|---|
| **fuma** | fumua |
| choma | **chomoa** |
| **tia** | toa |
| tega | **tegua** |
| **pakia** | pakua |

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutenda/kufanya kisha wazibadilishe sentensi hizo ziwe katika kauli ya kutendua/kufanyua.

**Kwa mfano:** Tumia kitenzi '*tega*'

***Kauli ya kufanya:*** *Mkulima ali**tega** mtego wa kuwakamata panya.*

***Kauli ya kufanyua:*** *Mkulima ali**tegua** mtego wa kuwakamata panya*

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe kauli ya kufanya/kutenda na kauli ya kufanyua/kutendua.

## 10.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 86

1. Maimuna, Mama Jeni, Bi Farashuu na Dora.
2. Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi.

***Kwa mfano:***

***a) Uhuru:*** Maimuna anatoroshwa kwao kwa sababu anataka uhuru. Anatamani kufanya atakavyo na ndio sababu yake ya kutoka kwao.

***b) Uchumi:*** Katika eneo la Pumziko, tunaelezwa kuhusu majengo ya kibiashara yalivyojengwa na namna shughuli za biashara zinavyoendeshwa na Wahindi. Kuna biashara nyingi ambazo zinaendeshwa katika eneo hilo. Biashara hizi zinahusisha zile halali na zile zisizo halali.

3. Kutufahamisha na kutuelimisha kuhusu namna watu wanavyoishi katika jamii. Pia, amekusudia kutuonya na kututahadharisha dhidi ya matendo yasiyokubalika katika jamii.
4. ***Pandikizi la nyama*** - kumaanisha mtu mkubwa zaidi.
5. Majumba makubwa ya kisasa, vilabu, nyumba za siri, hoteli kubwa na mandhari yaliyojaa ghasia na zogo kila wakati.
6. Maisha ya Pumziko yalikuwa yenye ghasia, mbio, zogo na pupa wakati wote. Watu walikuwa mbioni mchana na usiku ili kujipatia kipato.
7. Majazi ni mbinu ya kuwapa wahusika na vitu katika kazi ya fasihi majina kwa kutegemea tabia, maumbile na hali zao. ***Pumziko*** ni jina la mahali katika riwaya hii. Mahali hapo pamepewa jina hilo kimakusudi kwa sababu ya watu kukimbilia sehemu hiyo ili kujipumzisha kutoka kwa pilkapilka za kila siku kama alivyofanya Maimuna. ***Toweni striti*** ni jina la kimajazi. Limetumika kuashiria kuwa kunatolewa shughuli za kibiashara katika eneo hilo kwa namna ambavyo maduka yamepangwa na barabara katikati ambapo watu wanapishana wakitoa huduma zao.
8. Kwikwi za kilio
9. Alitaka kupata uhuru wa kufanya atakavyo/apendavyo.
10. ***Utohozi*** ni mbinu ya kifani ambayo mwandishi huswahilisha maneno ya lugha nyingine. Baadhi ya maneno yaliyotoholewa katika riwaya hii ni: ***striti*** kutokana na **street**, ***rafu*** kutokana na ***rough*** na ***teksi*** kutokana na ***taxi***. Hayo ni maneno ya Kiingereza ambayo yametoholewa na kufanywa kuwa ya Kiswahili.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 86**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati kutoka kwenye riwaya husika. Pia, atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***zogo* -** hali ya ukosefu wa utulivu
2. ***mkufu* -** pambo la wanawake ambalo huvaliwa kwa kuning'inizwa shingoni

**Matumizi katika sentensi:**

1. Vijana waliozua ***zogo*** mjini walikamatwa na polisi.
2. Shangazi alininunulia ***mkufu*** wa dhahabu.

**Zoezi la 1, ukurasa 87**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati kutoka kwenye riwaya husika. Pia, atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***alipohisi* -** alipofahamu/alipotambua kupitia milango ya fahamu kama vile: macho, ulimi n.k.
2. ***alimnyatia* -** alimwendea polepole bila kutoa kelele
3. ***alimkaripia* -** alimsemesha kwa ukali; alimgombeza
4. ***kubiruliwa* -** kugeuzwa ndani nje
5. ***tunasakwa* -** tunatafutwa
6. ***zogo* -** hali ya ukosefu wa utulivu
7. ***uliotutumka* -** uliovimba kwa unene
8. ***wananong'ona* -** wanasemezana kwa sauti za chini
9. ***ndewe* -**sehemu ya chini ya sikio iliyo duara
10. ***teksi* -** gari linalotoa huduma za uchukuzi kwa kutoza kiasi fulani cha pesa

**Matumizi katika sentensi:**

1. Mama ***alipohisi*** kuwa ninamdanganya, aliondoka kwa hasira.
2. Paka **alimnyatia** panya na kumla.
3. Mwalimu ***alimkaripia*** mwanafunzi aliyevunja chaki yake.
4. Watu wengi huchukia ***kubiruliwa*** midomo.
5. Tulipoambiwa ***tunasakwa*** na makachero, tulishtuka.
6. Washambuliaji walizua ***zogo*** katika kambi ya wakimbizi.
7. Mtoto mwenye mwili ***uliotutumka*** amewasili.
8. Wanafunzi watundu ***wananong'ona*** bwenini mwao.
9. Nimeweka kipuli kwenye ***ndewe*** ya sikio la mtoto wangu.
10. Leo nitaabiri ***teksi*** kwenda nyumbani.

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 87**

***Tanakali za sauti*** ni tamathali ya usemi ambayo hutumiwa kurejelea sauti inayoigiza jinsi kitu fulani kinavyotendeka. Katika riwaya ya '***Utengano'***, mwandishi ametumia tanakali za sauti kama vile: *alivuta kwikwi za kilio* kuashiria sauti aliyoitoa Maimuna.

***Semi*** ni mafungu ya maneno yanayotumiwa kuleta maana nyingine badala ya maana halisi ya maneno yaliyotumika. Kuna fani mbili za semi: ***nahau*** - ni semi zenye kitenzi na ***misemo*** - ni semi zisizokuwa na vitenzi. Katika riwaya ya '***Utengano'*** kuna semi kama vile: ***pandikizi la nyama***. Huu ni msemo wa kuashiria ukubwa wa Mama Jeni.

***Majazi*** ni mbinu ya kuwapa wahusika au viumbe katika kazi ya fasihi majina kulingana na tabia, hulka au maumbile yao. ***Pumziko*** ni jina la mahali katika riwaya hii. Mahali hapo pamepewa jina hilo kimakusudi kwa sababu ya watu kukimbilia sehemu hiyo ili kujipumzisha kutoka kwa pilkapilka za kila siku kama alivyofanya Maimuna. ***Toweni striti*** ni jina la kimajazi. Limetumika kuashiria kuwa kunatolewa shughuli za kibiashara katika eneo hilo kwa namna ambavyo maduka yamepangwa na barabara katikati ambapo watu wanapishana wakitoa huduma zao.

***Kuchanganya ndimi*** ni mbinu itumikayo katika kazi za kifasihi ili kuwasilisha ujumbe kwa zaidi ya lugha moja. Katika riwaya ya '***Utengano'***, mwandishi

ametumia maneno ya Kiingereza katika kazi yake. Kwa mfano: *darlin* na *drive ins.*

**Uhaishaji** ni mbinu ya kuvipa viumbe visivyo na uhai sifa za viumbe hai. Kupitia mbinu hii, viumbe hivyo huweza kutenda, kusema na hata kuwaza kama wafanyavyo viumbe walio hai. Kwa mfano: mwandishi amesema kuwa '*Maimuna alizamisha uso wake kwenye mto akaunywesha machozi'*. Hapa, mto umepewa sifa za kibinadamu za kuwa na uwezo wa kunywa.

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 88**

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi kuhusu matumizi ya lugha katika riwaya ya riwaya ya '***Siku Njema'.***

Baadhi ya majadiliano ambayo yanaweza kuwasilishwa na wanafunzi katika makundi yao iwapo watakuwa wanarejelea riwaya ya '*Siku Njema'* kuhusiana na mbinu mbalimbali za lugha ni kama vile:

1. ***Matumizi ya methali***: Hii ni kauli fupi ambayo hutumiwa katika jamii kutoa ukweli fulani wenye lengo la kuonya, kufundisha, kuhukumu n.k. Katika riwaya ya '*Siku Njema',* methali zimetumika kwingi kwenye riwaya nzima, kama vile, ukurasa 2 (*Dau la mnyonge haliendi joshi*), ukurasa 18 (*Ukweli una nguvu kuliko uongo*), ukurasa 79 (Mui huwa mwema) miongoni mwa methali nyingine nyingi.
2. ***Kinaya:*** Hali ya kuonyesha kinyume cha matarajio ya msomaji. Kwa mfano, kutokana na riwaya ya '*Siku Njema'*, mamake Kongowea Mswahili alikuwa na sifa tele ila alikuwa maskini. Msomaji anatarajia Zainabu Makame awe tajiri kadri ya sifa alizokuwa nazo.
3. ***Chuku:*** Hii ni mbinu ya kutia maelezo chumvi zaidi ya yanavyofaa kuwa. Kwa mfano, katika ukurasa 15 tunapoambiwa kuwa '*mazishi ya Zainabu Makame yalikuwa yamejaa watu hata hapakuwa na nafasi ya kutema mate wala nzi kupita*'.

Mbinu nyingine ambazo wanafunzi wanaweza kujadili ni: *uhaishaji, matumizi ya maswali ya balagha, jazanda, taharuki, utohozi, kuchanganya ndimi, majazi, uzungumzi nafsia, matumizi ya tashbihi* miongoni mwa nyingine.

**Zoezi la makundi, ukurasa 89**

1. chomoa
2. funga
3. shonoa
4. tega
5. bandua
6. tia
7. wazua
8. pakia
9. anua
10. chimbua
11. fumba

**Zoezi la 2, ukurasa 89**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na ziwe na vitenzi katika kauli ya kutendua/kufanyua.

***Kwa mfano:***

1. Mtoto ali***funua*** chakula.
2. Mwalimu ali***bandua*** chati ukutani.
3. Nita***pangua*** vikapu vya nyanya leo jioni.

**Zoezi la 3, ukurasa 90**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitenzi walivyopewa katika kauli ya kutendua/kufanyua.

***Kwa mfano:***

1. Wanaume wata***pakua*** mizigo bandarini.
2. Sitaki ku***kunjua*** kitambaa chako.
3. Kijakazi ame***anua*** nguo zote.
4. Nita***funua*** hema ile mchana.
5. Ninataka ku***fungua*** mlango.

**Zoezi la 4, ukurasa 90**

a) Fundi anaachanisha nyuzi zilizotumika kufuma fulana ya mteja wake.

b) Neza anaharibu/ anavuruga kwa maksudi mpangilio wa viti sebuleni.

ch) Nyanya aliyaweka wazi mafumbo yote.

d) Siwezi kuiondoa mizigo kwenye gari kwa kuwa ni mizito.

## Majibu ya Tathmini ya mada ya 2

**Zoezi la 1, ukurasa 91**

1. ***Shairi*** ni mtungo wenye muundo na lugha ya kisanii unaofuata utaratibu wa vina na mizani, hisi au tukio juu ya maisha au jambo na hufuata utaratibu maalumu wa urari na muwala unaozingatia kanuni za utunzi wa mashairi yanayohusika.
2. Muundo wa shairi huhusisha: *aina ya shairi, bahari ya shairi, idadi ya mishororo, jumla ya beti, kibwagizo (iwapo kipo), mpangilio wa vina, mpangilio na idadi ya mizani* na *vipande vya shairi.*
3. 
   a) Mishororo ni mistari katika ubeti wa shairi.

   b) Mizani ni silabi zinazotamkika katika mshororo wa shairi.

   ch) Vina ni silabi za namna moja zinazopatikana katikati na/au mwishoni mwa mishororo.

   d) Kibwagizo ni mshororo wa mwisho unaorudiwarudiwa katika kila ubeti. Kibwagizo hubeba kiini cha shairi.

**Zoezi la 2, ukurasa 91**

| Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendeka |
|---|---|
| kimbilia | **kimbilika** |
| chomea | **chomeleka** |
| lia (chakula) | **lika** |
| pandia | **pandika** |
| kalia | **kalika** |

## Zoezi la 3, ukurasa 91

| Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendeka | Kauli ya kutendewa | Kauli ya kutendua |
|---|---|---|---|
| pakia | **pakika** | pakiwa | **pakua** |
| **chomea** | chomeka | **chomewa** | chomoa |
| tendea | **tendeka** | **tendewa** | **tendua** |
| fyatia | **fyatika** | **fyatiwa** | **fyatua** |
| chimba | **chimbika** | **chimbiwa** | **chimbua** |

## Zoezi la 4, ukurasa 92

1. ***Tamthilia*** ni utungo uliotungwa kwa lengo la kuigizwa jukwaani na huwa kwa muundo wa mazungumzo baina ya wahusika. Pia, huitwa *mchezo wa kuigiza*.
2. Sifa za tamthilia:
   a) Huwa na mazungumzo na majibizano.
   b) Huwa na maelezo ya jukwaani yanayopendekeza jukwaa litakavyokuwa.
   ch) Huwa na maelezo kuhusu wahusika: *mavazi yao, hisia* na *matendo*.
   d) Hugawika katika maonyesho/matendo mbalimbali kutegemea matukio.
   e) Huhusisha mgogoro fulani hasa katika upeo wake.
   f) Utendaji wa tamthilia huambatana na miondoko – viungo vya mwili kusogezwa.
   a) Hushirikisha hadhira.
3. Tofauti kati ya riwaya na tamthilia
   a) Riwaya huwa ndefu kuliko tamthilia.
   b) Riwaya huandikwa kinathari ilhali tamthilia huwa katika muundo wa mazungumzo na majibizano.
   ch) Riwaya ina wahusika wengi kuliko tamthilia.

## Zoezi la 5, ukurasa 92

1. Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni iliyoandikwa kinathari, aghalabu inayoeleza ukweli fulani wa maisha.

2. Sifa za riwaya:
   a) Huwa na vipengele vifuatavyo: *ploti/msuko, hadithi, usimulizi, uhusika, mazingira, wakati, mitazamo na mazungumzo ya wahusika.*
   b) Huwa na maelezo ya simulizi kulingana na vile hadithi inavyotokea kiwakati na kimasafa.
   ch) Huwa na maelezo ya wahusika kuhusu: *wasifu wao, mavazi yao, tabia zao, sifa na dosari, matendo yao yanavyoathiri nafsi zao na kuwaathiri wahusika wengine.*
   d) Huwa na urefu wa kutosha kushughulikia mahitaji ya mtunzi.
   e) Huchunguza kwa kina jamii inayosawiriwa.
3. Wahusika hutumiwa kama vyombo vya kuuwasilisha ujumbe wa mwandishi wa riwaya kwa wasomaji.

**Zoezi la 6, ukurasa 92**

1. Ni hadithi inayoshughulikia suala fulani kwa muhtasari.
2. Sifa za hadithi fupi:
   a) Huwa fupi na inayoweza kusomeka kwa mkao mmoja.
   b) Huwa na wahusika wachache.
   ch) Huwa na mhusika mkuu mmoja ambaye humwongoza msomaji.
   d) Hushughulikia tukio moja kuu katika maisha ya mhusika mkuu.
   e) Haina upana wa kimaudhui wala uchangamano mkubwa wa kimuundo.
3.
   a) Hadithi fupi huwa na wahusika wachache sana ilhali riwaya huwa na wahusika wengi.
   b) Hadithi fupi huhusisha visa vifupi vifupi ilhali riwaya huwa usimulizi wa matukio marefu.

## Zoezi la 7, ukurasa 92

Tofauti kati ya fasihi andishi na fashi simulizi

| **Fasihi simulizi** | **Fasihi andishi** |
|---|---|
| i) **Umri:** Ina umri mkubwa kuliko fasihi andishi. Huitwa fasihi kongwe. | Ina umri mfupi kuliko fasihi simulizi. Hii inatokana na ukweli kuwa maandishi yamegunduliwa hivi karibuni. |
| ii) **Uhifadhi:** Inahifadhiwa kwenye kichwa cha msimulizi na kusambazwa kwa njia ya masimulizi/kimapokeo. | Inahifadhiwa kwa maandishi na kusambazwa kwa njia ya kusoma maandishi. |
| iii) **Tanzu:** Ina tanzu mbalimbali lakini ni tanzu nyingi kuliko zile za fasihi andishi. Kwa mfano: mazungumzo, ushairi, hadithi, semi, ngomezi, miviga n.k. | Ina tanzu nne tu: ushairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya. |
| iv) **Uwasilishaji:** Huwasilishwa kwa njia ya simulizi ya mdomo. Hutegemea sauti. | Huwasilishwa kwa njia ya maandishi. |
| v) **Mabadiliko:** Hubadilika kulingana na mfumo wa kihistoria. Aidha, fanani/msimulizi anaposimulia hadithi anaweza kuongeza au kupunguza jambo kila anapowasilisha sanaa yake. Pia, fanani akifa, kazi yake nayo italazimika kubadilika kutokana na yule atakayechukua nafasi yake. | Haibadiliki baada ya kuandikwa ila mwandishi anapoandika upya. |
| vi) **Umiliki:** Jamii nzima ndiyo inayohusika katika kuimiliki fasihi hii. | Mtunzi wa kazi hiyo ndiye mmiliki wa kazi yake. |
| vii) **Muda wa utunzi:** Baadhi ya tanzu za fasihi simulizi huibuka papo hapo. Kwa mfano: semi. | Huhitaji muda kutunga. |

Sura ya Tatu

# Mada Kuu 3: Ubunaji
## Mada Ndogo: Hotuba na Ufupisho

### Uwezo upatikanao katika mada hii:

Mwanafunzi ataweza kuelewa mtindo wa hotuba na kuuzingatia katika mazoezi ya utungaji pamoja na ufupisho; kujua kuchambua kitenzi kwa njia ya uambishaji.

### Malengo ya kujifunza

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema |
|---|---|---|
| • Kuelezea tofauti iliyopo kati ya insha na hotuba.<br>• Kutaja sehemu kuu za hotuba.<br>• Kukumbuka mwongozo wa kutunga hotuba na ufupisho.<br>• Kutoa mfano wa sifa za hotuba na ufupisho.<br>• Kuonyesha jinsi kitenzi kinavyoweza kuongezewa viambishi zaidi kwa njia ya uambishaji. | • Kutathmini hotuba kulingana na sifa zake.<br>• Kulinganisha hotuba na insha au hotuba fulani kwa hotuba nyingine.<br>• Kuendeleza hotuba kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa.<br>• Kufupisha hotuba inayohusika.<br>• Kulinganisha ufupisho uliotolewa kutoka makundi tofauti.<br>• Kuongezea mzizi wa kitenzi viambishi zaidi vyenye kuusababishia maana mpya. | • Kutokana na mada ya hotuba, mwanafunzi ataathiriwa katika nyanja tofauti. Kwa mfano: atafuata maadili mema ya kuwa na adabu, usafi, kupigana na wivu, uvivu, ukatili, uzinifu, ulevi, ujinga, umaskini n.k. |

## Maelezo kwa mwalimu

Mada hii inahusiana na masomo yanayohusiana na kujenga mahusiano mema, kujenga tabia njema, umoja na ushirikiano, umoja na maridhiano, mapendo, adabu, siasa, dini, afya n.k.

Mada hii inashughulikia ubunaji. Huu ni uandishi wa hotuba na ufupisho. Kwa hivyo, mifano ya aina mbalimbali za hotuba, sehemu kuu za insha hotuba, sifa za hotuba, mambo za kuzingatiwa katika uandishi wa hotuba, uandishi wa ufupisho na utaratibu wa kuandika ufupisho, hayo yote yamezungumziwa katika mada hii. Mbali na hayo, mada hii imegusia uambishaji wa vitenzi.

Dhana muhimu zinazojitokeza katika mada hii ni pamoja na: *sehemu kuu za hotuba, mambo ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba, sifa za hotuba, uandishi wa ufupisho na taratibu za kufuatwa katika uandishi huu* pamoja na *uambishaji wa vitenzi*.

## Masuala mtambuka

Masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni: *usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, amani na maadili, mazingira pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake*.

Suala la ***amani na maadili*** litafundishwa kupitia kwa ushirikiano wa wanafunzi katika kazi mbalimbali za makundi pale darasani hasa utunzi na utoaji wa hotuba mbalimbali. Hotuba watakazotunga wanafunzi zitahusisha mada mbalimbali zikiwemo mada kuhusiana na umuhimu wa maadili, umoja na uzalendo kwa wananchi wote.

***Elimu ya pamoja*** itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma pamoja kwa kuwashirikisha hata na wanafunzi wenye ulemavu na matatizo mbalimbali. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi kutoka katika matabaka mbalimbali kukubali na kushirikiana kwa pamoja katika shughuli za pale darasani na hata nje ya darasa. Utunzi wa hotuba mbalimbali na kuandika ufupisho ni shughuli ambazo zitawawezesha wanafunzi kujifundisha kwa pamoja.

***Usawa wa kijinsia*** utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasichana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao licha ya jinsia zao tofauti. Wanafunzi wafahamishwe kuwa jinsia hizi mbili hazina kasoro yoyote ila wote wana uwezo sawa iwapo watatia bidii katika

yote wayafanyayo. Mwalimu awahusishe wanafunzi wa kike pamoja na wale wa kiume katika utunzi wa hotuba na kuandika ufupisho katika makundi mbalimbali. Wanafunzi pia watafundishwa ***umuhimu wa mazingira*** yao na namna ya kuyahifadhi.

## Uwezo wa jumla

Mwalimu ahakikishe kuwa katika ufundishaji wake, wanafunzi wanapata uwezo wa kuwa na *tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha pamoja na ujifunzaji wa muda mrefu*.

Wanafunzi wataweza kuwa na ***tafakuri tanduizi*** kwa kufikiri kwa undani (kutafakari zaidi) ili kuweza kushiriki katika utunzi wa hotuba kwa kurejelea mada mbalimbali pamoja na kuyajibu maswali waliyopewa. Kupitia kwa mazoezi ya kuigiza namna ya kuwahutubia watu, wanafunzi watahimizwa kuwasiliana kwa lugha rasmi na sahihi pamoja na kuwa na ***utawala binafsi*** pamoja na kuzifahamu ***stadi mbalimbali za maisha***. ***Stadi za utafiti*** zitahitajika hapa ambapo wanafunzi watafanya utafiti mbalimbali kuhusiana na mada za kuangaziwa kuhusiana na maisha ya kila siku ya binadamu. ***Ujifunzaji wa muda mrefu*** uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na shughuli zinazoweza kuboresha uchumi wa nchi yao. Wanafunzi watayatumia maarifa  watakayopata kwenye mada hii katika ***usuluhishaji wa matatizo*** nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku.

## Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kuhusu hotuba na ufupisho, kama vile:

| | **Msamiati** | **Maana** |
|---|---|---|
| 1. | ***hadhira*** | jumla ya wasikilizaji au wasomaji wa kazi maalumu |
| 2. | ***hotuba*** | maelezo au mazungumzo yanayohusu jambo maalumu ambayo hutolewa hadharani na mtu mmoja |
| 3. | ***mada*** | kichwa cha hotuba kinachoeleza hotuba inahusu nini |
| 4. | ***hitimisho*** | maelezo yanayoandikwa mwishoni mwa hotuba |
| 5. | ***hutubia*** | toa maelezo kuhusu jambo fulani |
| 6. | ***ufupisho*** | tendo au  hali ya kupunguza idadi ya maneno katika makala bila kupoteza maana asilia |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | ***mzizi wa kitenzi*** | sehemu ya kitenzi isiyobadilika baada ya mnyambuliko wa kitenzi hicho |
| 8. | ***kitenzi*** | neno ambalo hueleza kuhusu kitendo kinachotendwa, kilichotendwa au kitakachotendwa |
| 9. | ***kiambishi tamati*** | herufi ambazo huwekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi |
| 10. | ***uambishaji*** | hali ya kuongeza viambishi kwenye mzizi wa neno |

## Usuluhishaji wa tatizo

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kulingana na kila zoezi husika kisha awaombe wachunguze kwa makini mfano wa hotuba iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 94-96 kuhusiana na umuhimu wa usafi katika jamii. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika shughuli hii. Wanafunzi wachunguze hotuba hiyo na mwalimu awaulize swali kama vile: *Mmejifundisha nini kutokana na hotuba hiyo?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu swali hilo. Kwa hivyo, mwalimu achochee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tanduizi kwa kuchunguza na kujibu maswali kuhusu hotuba husika.

## Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali katika ujifundishaji wao. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, mwalimu anaweza kuhusisha matumizi ya breli pamoja na vifaa vya kunasia sauti.

Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kusikia, mwalimu anaweza kuhusisha matumizi ya lugha ya ishara. Mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri ambao wana ujuzi wa kutumia lugha ya ishara. Vifaa hivi vitawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wanafunzi wenzao bila vikwazo vyovyote.

Nafasi ya wanawake katika shughuli za kudumisha usafi zitiliwe maanani kupitia kwa michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa wa 94 ili kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja. Hili litadumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi na kuwafanya kuwa wazalendo kamili katika umri wao.

## Orodha ya masomo na vipindi:

| Mada ya somo | Idadi ya vipindi |
|---|---|
| **Somo la 11:** Sehemu kuu za hotuba | 12 |
| **Somo la 12:** Sifa za hotuba | 13 |
| **Somo la 13:** Hotuba na insha | 12 |
| **Somo la 14:** Ufupisho | 13 |
| **Somo la 15:** Mwongozo wa kuandika ufupisho | 12 |
| | **JUMLA: 62** |

# Somo la 11: Sehemu kuu za hotuba

## Vipindi 1-3: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi hotuba kuhusu usafi kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutambua sehemu kuu za hotuba.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Chati yenye mchoro wa umbo la hotuba kwa ujumla kuonyesha sehemu zake;
- Hotuba zilizorekodiwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi,* ukurasa 94-96;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu anaweza kuanza somo hili kwa kuwaomba wanafunzi wasimuliane hadithi fupi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu. Hili litawawezesha

wanafunzi kufahamu utangulizi wa hadithi, mwili wa hadithi na vilevile mwisho wa hadithi watakazosimuliana. Mwanafunzi mmoja anaweza kusimama mbele ya darasa na kuwasimulia wanafunzi wengine hadithi moja fupi. Baada ya hapa, wanafunzi wajadiliane kuhusiana na utangulizi, mwili na mwisho wa hadithi hiyo. Hapa mwalimu ataweza kupata nafasi ya kuwatangulizia wanafunzi somo hili la sehemu za hotuba.

Mwalimu ahakikishe pia kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi hasa wale wa kiwango cha chini katika ujifunzaji. Vifaa kama vile: chati yenye umbo la hotuba linaloonyesha sehemu za hotuba pamoja na hotuba mbalimbali zilizoandikwa zitamsaidia mwalimu katika somo hili. Vilevile, ni vyema mwalimu azingatie wakati unaofaa wa kuonyesha vifaa hivyo hadharani ili wanafunzi wapate ufahamu unaotarajiwa katika muda unaotakikana. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu atumie vifaa hivyo kwa kuwaomba wao wenyewe kuvigusa huku wakieleza wanachoweza kusoma. Katika somo hili, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli inayohusika darasani.

## d) Utaratibu wa somo

### *Hatua ya 1: Utangulizi*

Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi wake. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Baada ya mwalimu kuwajulia hali wanafunzi anaweza kuwaomba watazame michoro iliyo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 94*. Mwalimu ahakikishe wanafunzi wote wanashirikishwa katika shughuli hii. Mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali kuhusu michoro ambayo wanafunzi watakuwa wameitazama.

Kwa mfano:

- Je, mnaona nini katika michoro hii? Watu mnaowaona wanafanya nini?

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama: "*Mimi ninaona*…." . Kwa mfano: *Mimi ninaona watu walio katika harakati ya kudumisha usafi. Mtu mmoja anaoga, mwingine anafagia mazingira, mwingine anakata kucha zake na mwingine anafua nguo.* Ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu ubunifu na ugunduzi, tafakuri tanduizi kwa kusisitiza uchunguzi wa michoro husika ili kuelewa mtiririko wa hotuba nzima. Mwalimu awahusishe wanafunzi katika

kueleza shughuli ambazo zinaendelea katika michoro husika. Vilevile, masuala ya elimu ya pamoja nayo yasisitizwe pale ambapo miongoni mwa wanafunzi pale darasani huenda kukawa na wanafunzi wenye ulemavu na ambao wanajifunza pamoja na wengine. Wanafunzi wenye ulemavu wahusishwe pia. Kwa hivyo, wanafunzi watazame au waguse picha (iwapi ziko kwenye breli) walizoonyeshwa na mwalimu wao na kujibu maswali waliyoulizwa.

## 11.1 Kusoma na kufahamu: Hotuba kuhusu usafi

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wasome kwa kimya hotuba kuhusu usafi iliyotolewa na Bwana John Gatete. Katika usomaji wao, wanafunzi wanaweza kuandika msamiati mpya wanaopatana nao. Baadaye, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamesoma na kuielewa hotuba husika kama alivyowaomba kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu kifungu hicho. Kwa mfano, anaweza kuwauliza: *Umuhimu wa usafi ni upi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao kulingana na yale waliyoyasoma katika hotuba hiyo. Kwa mfano: *Usafi humwepusha binadamu na magonjwa mengi.* Ni vyema mwalimu akumbuke kusahihisha matamshi ya wanafunzi pale wanapokosea.

Wanafunzi washirikishwe katika makundi yao kujadiliana kuhusiana na usafi wa aina mbalimbali pamoja umuhimu wao kwa binadamu. Wanafunzi pia waelezane shughuli mbalimbali za kudumisha usafi wanazoweza kujihusisha nazo.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali ya ufahamu waliyopewa. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo kwa kutilia mkazo pale ambapo wanatatizika.

## Tathmini ya vipindi 1-3

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha ili kutambua ikiwa wanaweza kueleza umuhimu wa usafi na jinsi ya kudumisha usafi miongoni mwao. Mwalimu anaweza kuuliza maswali mengine ambayo yanalenga kutathmini malengo ya ujifunzaji wa mada hii.

## Vipindi cha 4-5: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na sehemu kuu za hotuba;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na sehemu kuu za hotuba.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Chati yenye mchoro wa umbo la hotuba kwa ujumla kuonyesha sehemu zake kuu;
- Hotuba zilizorekodiwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 97;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu msamiati unaohusiana na sehemu kuu za hotuba. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika utungaji wa hotuba, somo hili litasaidia pia kuelewa maana ya msamiati unaohusiana na utungaji huo. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kumwezesha kutunga hotuba nzuri kwa kutumia lugha rasmi na sahihi. Katika maandalizi ya somo lake, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta chati yenye mchoro wa umbo la hotuba kwa ujumla ili kuonyesha sehemu kuu za hotuba ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi hasa wanafunzi wenye ulemavu au matatizo fulani.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali mepesi kuhusu utungaji wa hotuba ambao walijifundisha katika viwango vya hapo awali. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika

kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi katika kupata ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

## 11.2 Ujifunzaji wa msamiati wa hotuba kuhusu usafi

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kwanza kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao katika hotuba waliyosoma. Wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za msamiati huo kwa kuzingatia matumizi yake katika hotuba inayohusika. Wanafunzi wanaweza kutumia kamusi pale panapohitajika. Kwa hivyo, mwalimu azunguke darasani akitoa maelekezo pale yanapohitajika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 1 la msamiati lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 97. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wameelewa maana ya msamiati wote uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Wanafunzi, katika makundi yao, waelekezwe kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa ambao tayari wameshaufafanua.

Mwalimu ahakikishe anazunguka darasani kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya kufanya zoezi hili jibu, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha zoezi hilo.

Kuhusu zoezi la 2, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujipanga katika makundi ya wanafunzi wawili wawili ili waweze kuchunguza michoro waliyopewa katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 98. Wanafunzi waelezane madhara ya shughuli wanazoziona kwenye michoro hiyo. Ni vyema mwalimu awaambie wanafunzi warejelee hotuba waliyosoma hapo awali. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote kujadiliana kuhusu madhara ya ukosefu wa usafi kwa binadamu, wanyama, mimea na mazingira kwa jumla. Wakati wa majadiliano haya, mwalimu arejelee pia mifano mingine inayoweza kuwasaidia wanafunzi kupata stadi za utafiti, utawala binafsi na stadi za maisha.

## Tathmini ya vipindi 4-5

Katika hatua hii ya tathmini, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kuhusu sehemu kuu za hotuba wakirejelea mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa hotuba.

# Vipindi 6-8: Matumizi ya lugha

## a) Malengo ya somo

- Kutaja sehemu kuu za hotuba;
- Kutoa maelezo kuhusu sehemu kuu za hotuba.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye mchoro wa umbo la hotuba kwa ujumla kuonyesha sehemu zake kuu;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 98;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi zaidi kuhusu sehemu kuu za hotuba. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kumwezesha mwanafunzi kujadili na wenzake katika makundi kuhusiana na sehemu kuu za hotuba ambazo wamefundishwa huku wakirejelea hotuba waliyosoma hapo awali kuhusu usafi.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na msamiati wa sehemu kuu za hotuba. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi wapate ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

## 11.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajipange katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili kujadiliana kuhusu sehemu kuu za hotuba ambazo wamefundishwa huku wakirejelea hotuba waliyosoma hapo awali. Wanafunzi katika makundi yao waelezane ***mada ya hotuba*** huhusu nini, ***utangulizi wa hotuba*** huandikwa kwa namna gani, ***mwili wa hotuba*** huhusu nini, ***hitimisho la hotuba*** huandikwa kwa namna gani na lugha inayotumika kuandika hotuba hustahili kuwa ya aina gani? Baadaye, kila kundi lieleze waliyoyazungumzia mbele ya wanafunzi wenzo. Mwalimu arekebishe makosa ya kimatamshi katika mawasilisho ya wanafunzi.

Baadaye, mwalimu achukue fursa hii kuwaeleza wanafunzi kuhusu muundo sahihi wa hotuba. Awaeleze kuwa hotuba huwa na: *mada inayofaa, utangulizi wa kuvutia, mwili wenye ujumbe unaofaa, hitimisho la kuvutia* pamoja na *lugha sahihi na iliyopambwa*. Wanafunzi washirikishwe katika kuzitaja sehemu kuu za kuzingatia katika kuandika hotuba.

Mambo ya kuzingatiwa ni kama vile:

***Sehemu za hotuba ni:***

### *1. Mada au kichwa cha hotuba*

Mada ya hotuba hutambulisha jambo linalozungumziwa. Mada ya hotuba haifai kuzidi maneno manane. Mara nyingi mada ya hotuba huandikwa kwa herufi kubwa na kupigiwa mstari.

### *2. Utangulizi au mwanzo wa hotuba*

Utangulizi wa hotuba mara nyingi huwa ni aya moja tu. Huhusisha kuwatambua wanaokusikiliza pamoja na kutoa salamu. Mzungumzaji hujitambulisha hapa.

### *3. Mwili wa insha*

Hii ndiyo sehemu muhimu sana kwa sababu inabeba ujumbe kamili wa hotuba nzima. Aya nyingi huandikwa hapa na ni bora aya hizi ziandikwe kwa namna ya kutiririsha maudhui yanayozungumziwa kutoka mwanzo hadi mwisho wa hotuba.

### *4. Hitimisho au mwisho wa hotuba*

Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyozungumziwa katika mwili wa hotuba. Mzungumzaji huwashukuru wasikilizaji na kuwaaga.

Mwalimu ahakikishe amewasaidia wanafunzi walio na matatizo katika makundi yao. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii.

## Tathmini ya vipindi 6-8

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea mambo waliyofundishwa kuhusiana na sehemu kuu za hotuba. Vifaa vilivyotumiwa kujifunzia somo hili vinaweza kutumiwa kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa funzo hili. Mwalimu pia awaulize wanafunzi maswali ya kuthibitisha iwapo wanaweza kutambua sehemu kuu za hotuba kwa kurejelea hotuba waliyosoma hapo awali kuhusu usafi.

## Vipindi vya 9-10: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kujadili sehemu kuu za hotuba;
- Kutunga hotuba kwa kuzingatia sehemu kuu za hotuba.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Hotuba mbalimbali zilizoandikwa au kurekodiwa;
- Chati yenye kuonyesha umbo la hotuba;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 99;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Hotuba mbalimbali kuhusu mada tofauti tofauti zilizoandikwa au kurekodiwa zitumiwe kuwaongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kujadili

kuhusu sehemu kuu za hotuba. Mifano hii ya hotuba itawawezesha wanafunzi kupata ujuzi ufaao wa kutunga hotuba zao wenyewe. Mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kama alivyoagizwa kwenye zoezi husika. Iwapo itawezekana, mwalimu anaweza kupanga kuwapeleka wanafunzi kuhudhuria hafla yoyote ambapo hotuba zitasomwa. Hii itakuwa fursa nzuri kwa wanafunzi kusikiliza hotuba zikitolewa moja kwa moja. Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi.

## d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia kuhusu umbo la hotuba.

## 11.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga hotuba

Sehemu hii inalenga kuwawezesha wanafunzi kutunga hotuba kuhusu mada yoyote ambayo wao wenyewe wataichagua. Sharti wazingatie umbo la hotuba lenye sehemu kuu inazofaa kuhusishwa. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili kujadili kuhusiana na mada watakayoandikia hotuba yao pamoja na namna ya kuandika hotuba yenyewe.

Mwalimu anaweza kuwaongoza wanafunzi katika makundi yao wajaribu kuigiza wakihutubia hadhira fulani ili waweze kupata hoja za kutosha kuandika hotuba yao. Mwalimu aombe kila kundi la wanafunzi lijitokeze mbele ya darasa na kuigiza kuhusu majadiliano yao ya hotuba watakayoandika. Mwalimu naye achukue muda wake kwa kusahihisha makosa ya wanafunzi hasa ya kimatamshi pindi yanapotokea na awapongeze pale wanapofanikiwa huku akiomba makundi mengine kuwaiga wenzao na kusahihisha makosa waliyofanya ili waboreshe mawasilisho yao yawe mazuri zaidi kuliko ya makundi yaliyotangulia. Wanafunzi waelekezwe katika makundi yao kuandika kwa usahihi hotuba zao baada ya kuziwasilisha huku wakihusisha marekebisho ya mwalimu au wanafunzi wenzao.

Vilevile, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wanatunga sentensi kamili zisizo na makosa ya kisarufi ili wapate uwezo wa kuwasiliana kwa lugha

fasaha. Aidha, ni vyema pia mwalimu awasaidie wanafunzi kupata ujuzi katika tafakuri tanduizi, usuluhishaji wa matatizo, stadi za utafiti, ubunifu na ugunduzi, ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha na elimu kuhusu fedha kupitia kwa hotuba mbalimbali zitakazowasilishwa na makundi mbalimbali darasani.

## Tathmini ya vipindi 9-10

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kundi kuhusu hotuba mbalimbali walizotunga. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kueleza kuhusu sehemu kuu za hotuba ili kutathmini ikiwa wanafunzi wameelewa funzo hili. Vilevile, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kwa kuchunguza ikiwa wanafunzi wametambua jinsi ya kutoa maelezo kwa kila sehemu kuu ya hotuba.

## Vipindi 10-11: Sarufi (Uambishaji wa vitenzi)

### a) Malengo ya somo

- Kufafanua maana ya kitenzi katika Kiswahili;
- Kujadili uambishaji wa vitenzi;
- Kuainisha vitenzi katika kauli mbalimbali.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Vifaa vya darasani kama vile: madaftari, kalamu, rula n.k.;
- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya vitenzi katika kauli mbalimbali;
- Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 99-101;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya vitenzi

katika kauli mbalimbali, michoro inayoonyesha vitendo vya kauli mbalimbali pamoja na chombo cha kunasia sauti au breli. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua maana ya kitenzi, kauli mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi pamoja na matumizi yao katika maongezi na sentensi sahihi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango cha chini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona, ni lazima mwalimu awaombe wao wenyewe kuvigusa vifaa vilivyopo pamoja na maandishi katika breli huku wakitoa maelezo kuvihusu na wale ambao hawawezi kusikia wavionyeshe kwa kuvigusa vifaa hivyo huku wakiandika maelezo yake ubaoni. Ili kuyafikia malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika vitabu vyao.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika masomo ya sarufi ya viwango vya hapo awali kuhusiana na mnyambuliko wa vitenzi katika Kiswahili. Kutokana na swali hili la jumla, mwalimu aweze kuwashirikisha wanafunzi katika kutambua kuwa kuna kauli mbalimbali za kunyambua vitenzi katika Kiswahili kama vile: *kauli ya kufanyia, kufanyiwa, kufanywa, kufanyika, kufanyisha, kufanyua* n.k. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi waeleze kuhusu maana ya kitenzi na kauli mbalimbali za mnyambuliko wanazozifahamu.

## 11.5 Sarufi: Uambishaji wa vitenzi

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na awaombe wachunguze jedwali walilopewa katika vitabu vyao. Wanafunzi wachunguze mabadiliko ya vitenzi walivyopewa kwenye jedwali

husika kwa kurejelea kauli mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua na kuelewa mabadiliko ya vitenzi husika katika kauli mbalimbali. Wanafunzi washirikishwe katika kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika jedwali walilopewa.

Wanafunzi waelekezwe kutambua mizizi ya vitenzi mbalimbali kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali husika. Mwalimu awaeleze wanafunzi kuwa ***mzizi wa kitenzi*** ni sehemu ambayo huwa haibadiliki baada ya mnyambuliko wa kitenzi hicho.

***Kwa mfano:***

| **Kauli ya kufanya** | **Kauli ya kufanyia** | **Kauli ya kufanywa** | **Kauli ya kufanyika** | **Mzizi wa kitenzi** |
|---|---|---|---|---|
| cheza | chezea | chezwa | chezeka | chez’ |
| piga | pigia | pigwa | pigika | pig’ |
| andika | andikia | andikwa | andikika | andik’ |
| soma | somea | somwa | someka | som’ |

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika makundi yao ili kuelewa funzo hili kuhusu uambishaji wa vitenzi. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanapata uelewa wa mizizi ya vitenzi mbalimbali.

Kupitia kwa zoezi la 3 lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 100, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua sehemu mbalimbali zinazounda vitenzi vya Kiswahili. Sehemu hizi ni: *viambishi awali, mizizi ya vitenzi na viambishi tamati.*

***Kwa mfano:***

Kitenzi ***anapika*** kimeundwa kwa:

i) Viambishi awali: ***a+na***

ii) Mzizi wa kitenzi: ***‘pik’***

iii) Kiambishi tamati: ***‘a’***

Ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wamepata ufahamu wa kutosha kuhusu sehemu mbalimbali zinazounda vitenzi, mwalimu awaombe wafanye zoezi la 4. Zoezi hili lisahihishwe darasani kwa maelekezo ya mwalimu. Mwalimu awasaidie wanafunzi walio na matatizo katika makundi yao.

## Tathmini ya vipindi 10-11

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kufafanua maana ya kitenzi pamoja na jinsi ya kunyambua kitenzi katika kauli mbalimbali. Utunzi wa sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali ndiko kutamhakikishia mwalimu kuwa wanafunzi wamepata uelewa wa funzo hili. Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifunzaji wao nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la 5 na zoezi la 6 katika sehemu ya sarufi. Mazoezi haya yatasahihishwa kabla ya somo lijalo.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mwalimu afafanue zaidi kuhusiana na sehemu kuu za hotuba kwa kuwaeleza wanafunzi:

***Sehemu za hotuba ni:***

***a) Mada au kichwa cha hotuba***

Mada ya hotuba hutambulisha jambo linalozungumziwa na mara nyingi huwa haizidi maneno manane.

***b) Utangulizi au mwanzo wa hotuba***

Utangulizi wa hotuba mara nyingi huwa ni aya moja tu. Huhusisha kuwatambua wanaokusikiliza pamoja na kutoa salamu. Mzungumzaji hujitambulisha hapa.

***ch) Mwili wa hotuba***

Sehemu hii hubeba ujumbe kamili wa hotuba nzima. Aya kadhaa huandikwa hapa kwa namna ya kutiririsha maudhui yanayozungumziwa kutoka mwanzo hadi mwisho wa hotuba.

***d) Hitimisho au mwisho wa hotuba***

Sehemu hii huwa na sentensi chache tu katika aya moja. Hitimisho hufupisha yaliyozungumziwa katika mwili wa hotuba. Mzungumzaji huwashukuru wasikilizaji na kuwaaga.

1. Aya ya kwanza huhusu kutambulisha kitakachozungumziwa, salamu na kujitambulisha kwa msemaji.
2. Hotuba huandikwa katika nafsi ya kwanza na huwa katika usemi asili.
3. Hotuba huandikwa katika wakati uliopo.
4. Aya kadhaa zinazofuata utangulizi huhusu ujumbe wa hotuba nzima.
5. Aya ya mwisho huhitimisha hotuba kwa kutoa shukrani na kuwaaga wasikilizaji.

6. Lugha sahihi kisarufi na inayoeleweka hutumika.
    - Hali ya kuongeza herufi maalum au viambishi mwanzoni na mwishoni mwa mizizi ya vitenzi ili kupata maana ya ziada huitwa ***uambishaji wa vitenzi***.

**Mifano:** ***anapenda*** = a+na+pik+a

'a-' ni kiambishi cha nafsi ya tatu umoja (yeye)

'na-' ni kiambishi cha wakati uliopo

'pik' ni mzizi wa kitenzi 'pika'

'a-' ni kimalizio cha kitenzi 'pika'.

Herufi maalum zinazoongezwa mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa kitenzi huitwa ***viambishi***.

- Sehemu ya kitenzi ambayo haibadiliki baada ya kitenzi hicho kunyambuliwa huitwa ***mzizi wa kitenzi***.

## 11.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kuwasaidia wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaelekeze wanafunzi hao kukamilisha jedwali lifuatalo:

| Kauli ya kufanya | Kauli ya kufanyisha | Kauli ya kufanyiwa | Kauli ya kufanyua | Mzizi wa kitenzi |
|---|---|---|---|---|
| tega | _______ | tegewa | _______ | ________ |
| _______ | shonesha | _______ | _______ | shon' |
| _______ | ________ | _______ | fichua | ________ |

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu**

| **Kauli ya kufanya** | **Kauli ya kufanyisha** | **Kauli ya kufanyiwa** | **Kauli ya kufanyua** | **Mzizi wa kitenzi** |
|---|---|---|---|---|
| tega | tegesha | tegewa | tegua | teg' |
| **shona** | shonesha | shonewa | **shonoa** | shon' |
| ficha | fichisha | fichiwa | fichua | fich' |

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge watunge sentensi sahihi kisarufi katika kauli ya kufanyisha, kufanyiwa na kufanyua.

**Kwa mfano:** Tumia kitenzi '***tega'***

***Kauli ya kufanyisha:*** Mkulima alii***tegesha*** mitego yake shambani.

***Kauli ya kufanyiwa:*** Mkulima ali***tegewa*** mitego yake na mwanawe.

***Kauli ya kufanyua:*** Mkulima alii***tegua*** mitego iliyokuwa shambani mwake.

## 11.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 96

1. Mkuu wa Mkoa wa Kusini, wazazi, walimu, wanafunzi na wageni waalikwa.
2. Afisa wa Afya katika Mkoa wa Kusini.
3. Mazingira safi husababisha kuwepo kwa hewa safi ya kupumua, maji safi ya kutumiwa na mahali safi pa kuishi.
4. Kumwaga kemikali na uchafu kwenye vianzo vya maji.
5. Usafi wa mwili huzuia harufu mbaya kwa binadamu na huzuia magonjwa ya tumbo.
6. Mbu na chawa. Mbu husababisha malaria na chawa hufyonza damu.
7. Kuoga kila siku, kupiga mswaki kila siku, kunyoa nywele zinazofaa kunyolewa na kuchana zile za kichwani, kuvaa nguo safi kila siku, kukata kucha na kulala kwenye malazi safi.

8. Inatoa utambulisho wa waliohudhuria, mzungumzaji na pia mada ya hotuba.
9. Nafsi ya kwanza, umoja.
10. Kwa kuwashukuru wote waliohudhuria.

**Zoezi la 1, ukurasa 97**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati uliopigiwa mistari. Pia atathmini sentensi zitakazotungwa na wanafunzi. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

**Kwa mfano:**

1. ***waalikwa -*** watu walioalikwa kuhudhuria hafla fulani
2. ***natumai -*** natarajia
3. ***mkoa -*** eneo la kijiografia linalotawaliwa na mkuu wa mkoa
4. ***mkutano -*** shughuli fulani maalumu yenye watu wanaojadiliana jambo au kuisikiliza hotuba
5. ***madhara -*** jambo lenye kuleta maangamizi au uharibifu
6. ***kemikali -*** dawa yenye uwezo wa kubadilisha kitu kikemikali
7. ***mitaro -*** mifereji mirefu ya kupitisha bomba la maji
8. ***majaa -*** mahali maalumu palipotengwa kutupia taka
9. ***maadili -*** tabia njema
10. ***vianzo -*** maeneo ambayo ni asili ya kitu fulani

Mifano ya sentensi:

1. Wageni ***waalikwa*** watakaa kwenye hema.
2. ***Natumai*** umeoga ukaacha kunuka.
3. ***Mkoa*** wa Kati umeathirika na kiangazi.
4. Nitaomba kwenye ***mkutano*** ujao.
5. ***Madhara*** ya ukosefu wa maji safi ni mengi.
6. Kuna ***kemikali*** hatari kwenye lango la kiwanda hiki.
7. ***Mitaro*** iliyochimbwa juzi imezibwa.

8. Takataka katika jiji hutupwa kwenye ***majaa***.
9. ***Maadili*** mema ya mtoto ni furaha ya kila mzazi.
10. Kulikuwa na samaki kwenye ***vianzo*** vya maji yale.

**Zoezi la 2, ukurasa 97-98**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu michoro waliyopewa. Wanaweza kusema:

A. Wanyama wakinywa maji machafu watapatwa na ugonjwa. Pia, wanyama hawa wakikanyaga ndani ya maji na kuacha samadi yao humo basi huweza kuyachafua maji na kuyafanya kuwa hatari kwa binadamu.

B. Kemikali zinazomwagwa na viwanda ni hatari kwa afya ya binadamu, mimea na wanyama.

CH. Utupaji wa taka ovyo husababisha harufu mbaya ambayo huathiri afya ya binadamu. Baadhi ya wadudu ambao huvutiwa na takataka huweza kusababisha magonjwa mbalimbali kwa binadamu.

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 99**

Mwalimu atathmini namna wanafunzi watakavyotoa hotuba mbele ya wanafunzi wenzao. Awahimize wazingatie ujasiri wakati wa kuongea mbele ya watu pamoja na matumizi ya lugha rasmi na sahihi kisarufi.

**Zoezi la kuandika, ukurasa 99**

Mwalimu atathmini hotuba za wanafunzi. Sharti zizingatie muundo kamili wa kuandika hotuba.

**Kwa mfano:**

***HOTUBA KUHUSU UMUHIMU WA MAJI KWA BINADAMU NA WANYAMA***

*Mwenyekiti wa chama cha mazingira, walimu na wanafunzi, hamjambo? Leo nina furaha kuwa hapa ili niwape hotuba yangu kuhusu umuhimu wa maji kwa binadamu na wanyama. Kwanza kabisa, maji ni muhimu kwetu sisi binadamu kwa sababu maji ni uhai. Sisi hunywa maji ili kukata kiu.*

*Maji hutumika katika shughuli zetu za nyumbani. Ili kuosha nguo zetu, sisi hutumia maji. Pia, maji hutumika kusafisha vyombo na nyumba. Sharti binadamu waishi katika mazingira safi. Hii ndiyo maana sisi hutumia maji kudumisha usafi. Mbali na usafi wa mazingira yetu, kuna usafi wa mwili ambao huhitaji maji. Sisi hutumia maji kuoga ili tuonekane nadhifu.*

*Binadamu pia hutumia maji katika shughuli za kilimo. Mimea yetu haiwezi kunawiri bila kunyunyiziwa maji. Sisi huinyunyizia mimea yetu maji ili inawiri na kutupa mazao mengi. Maji pia hutumiwa na binadamu katika kufuga samaki. Kunao binadamu ambao hujenga vidimbwi vya kufuga samaki na wao huhitaji maji. Samaki hao hukua na kuuzwa kisha wakawaletea binadamu pesa za kujikimu kimaisha.*

*Wanyama pia huhitaji maji. Maji ni muhimu kwa wanyama kwa sababu wao hunywa maji ili kukata kiu. Mbali na hayo, wanyama wanaofugwa nyumbani hurashiwa dawa ya kuzuia magonjwa. Dawa hiyo huwa imechanganywa na maji.*

*Wanyama wa majini na samaki huhitaji maji ili kuishi. Wanyama hawa ni kama vile: mamba, viboko na kobe wa majini. Wao hutegemea maji kama makazi yao. Ni wajibu wetu sisi binadamu kuyatunza mazingira na vianzo vya maji ili tuishi maisha mema.*

*Asanteni nyote kwa kuhudhuria na kunisikiliza. Mungu awabariki.*

### *Zoezi la sarufi, ukurasa 99*

| **Kitenzi (kauli ya kutenda)** | **Kauli ya kutendea** | **Kauli ya kutendeka** | **Kauli ya kutendewa** | **Kauli ya kutendesha** | **Mzizi wa kitenzi** |
|---|---|---|---|---|---|
| *lim*a | *lim*ia | *lim*ika | *lim*iwa | *lim*isha | lim- |
| *chor*a | *chor*ea | *chor*eka | *chor*ewa | *chor*esha | chor- |
| *tembe*a | *tembe*lea | *tembe*leka | *tembe*lewa | *tembe*za | tembe- |
| andika | andikia | andikika | andikiwa | andikisha | andik- |
| **soma** | somea | someka | somewa | somesha | som- |
| samehe | samehea | sameheka | samehewa | samehesha | samehe |
| **vunja** | vunjia | vunjika | vunjiwa | vunjisha | vunj- |

## Zoezi la 3, ukurasa 100

1. (*atachora*) = a+ta+chor+a
2. (*anakimbia*) = a+na+kimb+ia
3. (*alipanda*) = a+li+pand+a
4. (*anawafundisha*) = a+na+wa+fund+ish+a

## Zoezi la 4, ukurasa 100

| Kitenzi | Kiambishi cha nafsi | Kiambishi cha wakati | Mzizi wa kitenzi | Kimalizio |
|---|---|---|---|---|
| alicheza | a | li | chez- | a |
| ataimba | a | ta | imba- | **a** |
| tutatembea | tu | ta | temb- | **e + a** |
| watapanda | wa | ta | pand- | **a** |

## Zoezi la 5, ukurasa 101

1. -shon-
2. -som-
3. -samehe, -kose-
4. -angali-
5. -andik-

## Zoezi la 6, ukurasa 101

1. a+na+chor+a (nafsi ya tatu umoja, wakati uliopo, mzizi, kimalizio)
2. a+na+kimb+i+a (nafsi ya tatu umoja, wakati uliopo, mzizi, kiambishi cha mnyambuliko, kimalizio)
3. ni+ta+m+samehe (nafsi ya kwanza umoja, wakati ujao, mtendewa, mzizi)
4. ni+na+andik+a (nafsi ya kwanza umoja, wakati uliopo, mzizi, kimalizio)
5. ni+ta+fut+a (nafsi ya kwanza umoja, wakati ujao, mzizi, kimalizio)

# Somo la 12: Sifa za hotuba

## Vipindi 13-15: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha hotuba kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutaja mambo muhimu yaliyozungumziwa katika hotuba husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Hotuba kadhaa zilizoandikwa au kurekodiwa;
- Wanafunzi wenyewe;
- Mtandao wa intaneti;
- Michoro au picha zenye kuonyesha ushirikiano wa kijinsia;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 102-104;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu hotuba kuhusu ushirikiano wa kijinsia. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika. Michoro au picha zenye kuonyesha ushirikiano wa kijinsia zinaweza kutumika katika somo hili.

## d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha mazoezi

waliyopewa katika kipindi cha hapo awali. Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili watazame michoro iliyo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 102. Mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali kuhusu michoro hiyo.

Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye michoro hiyo?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu swali waliloulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"mimi ninaona…."* . Wanafunzi wajibu swali la mwalimu, kwa mfano: *Mimi ninawaona watu wa jinsia mbalimbali wakishirikiana katika kuyasafisha mazingira pamoja na kupanda na wengine kuvuna shambani.* Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea katika michoro hiyo.

### 12.1 Kusoma na kufahamu: Hotuba kuhusu ushirikiano wa kijinsia

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya hotuba kuhusu ushirikiano wa kijinsia huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu hotuba waliyosoma ili kuhakikisha kuwa wameielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Kwa nini ushirikiano wa kijinsia ni muhimu kwa Wanyarwanda?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika hotuba husika. Kwa mfano: *Kila Mnyarwanda, awe wa kike au wa kiume ana uwezo wa kutekeleza majukumu yake.* Baada ya kuhakikisha kwamba wanafunzi wamesoma kwa kimya hotuba iliyopo, mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa sauti hotuba hiyo kwa kuhakikisha kuwa wanasoma kwa namna na matamshi yanayofaa. Mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa.

Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujibu maswali ya ufahamu yaliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 104.

## Tathmini ya vipindi 13-15

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutokana na hotuba waliyosoma. Mwalimu anaweza kuuliza maswali mengine ambayo yanalenga kutathmini malengo ya ujifunzaji wa mada hii. Wanafunzi wachunguzwe iwapo wameweza kubaini sifa za hotuba kutokana na hotuba waliyosoma hapo awali.

## Vipindi 16-17: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na hotuba husika;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na sifa za hotuba.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Chati yenye kuonyesha sifa za hotuba;
- Hotuba zilizorekodiwa;
- Wanafunzi wenyewe;
- Kamusi ya Kiswahili;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 105;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu msamiati unaohusiana na sifa za hotuba. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu kuhusu utungaji wa hotuba, somo hili litasaidia pia kuelewa maana ya msamiati unaohusiana na utungaji huo. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kuandika hotuba nzuri kwa kutumia lugha rasmi na sahihi. Katika maandalizi ya somo lake, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta chati yenye kuonyesha sifa za hotuba kwa ujumla ili kuonyesha sehemu kuu hotuba. Hili litawasaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi hasa wanafunzi wenye ulemavu au matatizo yoyote.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali mepesi kuhusu utungaji wa hotuba na msamiati unaohusiana na utungaji huu ambao walijifundisha katika

vipindi vya hapo awali. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi katika kupata ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

### 12.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na hotuba ya ushirikiano

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kujadiliana kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao katika hotuba waliyosoma. Wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za msamiati huo kwa kuzingatia matumizi yake katika hotuba husika. Wanafunzi wanaweza kutumia kamusi pale panapohitajika. Mwalimu azunguke darasani akitoa maelekezo pale yanapohitajika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 1 la msamiati lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 105. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wameelewa maana ya misamiati yote iliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Hivyo basi, wanafunzi, katika makundi yao, wajadiliane kuhusu zoezi hilo la msamiati huku mwalimu akizunguka darasani kuwaelekeza wale wanaotatizika. Wanafunzi watunge sentensi kwa kutumia msamiati walioufafanua. Baada ya kufanya zoezi hili, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha zoezi hilo.

### Tathmini ya vipindi 16-17

Katika hatua hii ya tathmini, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifundisha kutokana na hotuba waliyopewa kuhusu ushirikiano wa kijinsia pamoja na sifa za hotuba huku wakirejelea mambo muhimu ya kuzingatia katika utungaji wa hotuba. Vifaa na picha zilizotumiwa kujifunzia somo hili zitumiwe kuchunguza iwapo wanafunzi wamelielewa funzo hili.

## Vipindi 18-20: Matumizi ya lugha

#### a) Malengo ya somo

- Kutaja sifa za hotuba kwa ujumla;
- Kujadili kuhusu vipengele muhimu katika utungaji wa hotuba;

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Hotuba mbalimbali zilizoandikwa kwa kuzingatia sifa zake muhimu;
- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha umbo la hotuba;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 105-106;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya funzo hili, mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi kama vile hotuba mbalimbali zilizoandikwa kwa kuzingatia sifa zake muhimu pamoja na mambo muhimu ambayo hufaa kuzingatiwa katika utungaji wa hotuba nzuri. Kupitia kwa vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua mambo muhimu ya kuzingatia katika kutunga hotuba nzuri ya kuvutia inayoweza kutuzwa alama nyingi ikiwa ni insha.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi kuhusu waliyojifundisha katika kipindi kilichopita kuhusu sehemu kuu za hotuba. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

### 12.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu sifa za hotuba

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wajadiliane kuhusu sifa za hotuba pamoja na mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa katika utungaji wa hotuba. Wanafunzi wanaweza kurejelea hotuba waliyosoma hapo awali kuhusiana na ushirikiano wa kijinsia. Wanafunzi waelezane kuhusu: *hotuba hustahili kuwa na mada, utangulizi, mwili, hitimisho, lugha yenye matumizi ya wakati uliopo, matumizi ya nafsi ya kwanza* n.k. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Baada ya muda mfupi wa majadiliano, mwalimu aombe kila kundi liwasilishe matokeo ya majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa sifa za hotuba pamoja na mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba. Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa jambo hili.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutambua mambo mengine muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba kama vile: *lugha rasmi na sahihi kisarufi, maendelezo sahihi ya maneno, mapambo yanayofaa* n.k. Mwalimu awahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi kuhusu namna ya kuandika hotuba.

## Tathmini ya vipindi 18-20

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusiana na sifa za hotuba pamoja na mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba. Vifaa vilivyotumiwa kujifunzia somo hili vinaweza kutumiwa kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa somo hili. Mwalimu pia awaulize wanafunzi maswali ya kuthibitisha iwapo wanaweza kueleza sifa za hotuba kwa ujumla. Wanafunzi waendelee kufanya mazoezi ya kutunga hotuba na hata kujaribu kuzisoma mbele ya wanafunzi wenzao kwa kutumia lugha rasmi na sahihi kisarufi.

## Vipindi vya 21-22: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu athari za unyanyasaji wa kijinsia katika jamii;
- Kutunga hotuba kuhusu shughuli zinazohamasisha umoja wa Wanyarwanda.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Hotuba mbalimbali kuhusu umoja wa Wanyarwanda;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 106;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Hotuba mbalimbali kuhusu umoja wa Wanyarwanda zilizoandaliwa na mwalimu aidha kwa kurekodiwa au kuandikwa zitumiwe kuwaongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kujadili kuhusu shughuli mbalimbali ambazo huhamasisha umoja wa Wanyarwanda. Mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kama ilivyoagizwa kwenye zoezi husika.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi. Vifaa hivi vitarahisisha ujifundishaji wa wanafunzi.

## d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia kuhusu sifa za hotuba na mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba.

### 12.4 Kusikiliza na kuzungumza: Majadiliano

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi wa kutunga hotuba kuhusu shughuli mbalimbali ambazo Wanyarwanda hujihusisha nazo ili kuimarisha umoja kati yao.

Pia, katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha waelekezwe kujadiliana kuhusu: *Athari za unyanyasaji wa kijinsia kwa jamii na taifa zima*.

Mwalimu anaweza kuwashirikisha wanafunzi katika majadiliano haya kwa kuwaelekeza kurejelea mambo ambayo huchangia katika kunyanyasa jinsia mbalimbali. Kutokana na majadiliano haya, wanafunzi wataweza kutambua kuwa umoja na ushirikiano miongoni mwa watu katika jamii ni muhimu sana kwani hujenga utangamano mwema wa wanajamii katika taifa zima.

Baadhi ya athari za unyanyasaji wa jinsia ni kusababisha utengano na kukwamiza maendelea ya wanajamii.

Mwalimu azunguke darasani kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajadiliana vizuri kuhusiana na swali walilopewa. Mwalimu awasaidie wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baadaye, kila kundi lipewe muda wa kuwasilisha majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii. Mwalimu akosoe makosa ya kimatamshi kila mara yanapojitokeza ili kuwazoesha wanafunzi kutamka maneno kwa usahihi na kudumisha uwezo wao wa kuwasiliana kwa lugha rasmi na sahihi kisarufi.

### Tathmini ya vipindi 21-22

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha katika sehemu hii ya kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kuweza kujadiliana katika makundi. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutambua umuhimu wa kuzithamini jinsia zote za binadamu. Wanafunzi pia, waelekezwe kutunga hotuba kuhusu shughuli ambazo huchangia kuwepo kwa umoja na utangamano miongoni mwa Wanyarwanda.

## Vipindi 23-25: Sarufi (Uambishaji wa vitenzi)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua majukumu ya viambishi awali katika vitenzi;
- Kutambua majukumu ya viambishi tamati katika vitenzi;
- Kuainisha vitenzi kwa kuzingatia viambishi mbalimbali.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Chati yenye kuonyesha vitenzi vilivyoainishwa;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 106;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini sehemu ambazo huunda vitenzi katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kutosha kufundishia somo hili kama vile: chati yenye kuonyesha vitenzi vilivyoainishwa. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hadharani pamoja na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu kipindi kilichopita kuhusu sarufi ya uainishaji wa vitenzi kwa kurejelea mnyambuliko wa vitenzi katika katika kauli mbalimbali. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha mazoezi waliyopewa katika kipindi kilichopita.

## 12.5 Viambishi awali na viambishi tamati

Katika hatua hii, wanafunzi watapata fursa ya kufahamu sehemu zinazounda vitenzi katika Kiswahili kisha watafahamu majukumu ya sehemu hizo. Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kufanya zoezi la makundi lililo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 106-107 ambapo wanahitajika kuunganisha silabi walizopewa ili kuunda vitenzi sahihi. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii. Wanafunzi wahakikishe kuwa wanaunganisha silabi hizo kwa usahihi ili kuunda vitenzi sahihi.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kuwa baadhi ya silabi walizounganisha hapo juu kuunda vitenzi kamili ni viambishi awali na viambishi tamati. ***Viambishi awali*** huwa ni silabi au herufi zinazowekwa kabla ya mzizi wa kitenzi. ***Viambishi tamati*** ni silabi au herufi ambazo huwekwa baada ya mzizi wa vitenzi. Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuwa mzizi wa kitenzi ni sehemu ambayo huwa haibadiliki wakati wa kunyambua kitenzi katika kauli mbalimbali.

### *Kwa mfano:*

**Mfano 1:** *wa+si+tu+chor+e*

**Jibu:**

- Kiambishi *'wa-'* kinasimamia nafsi
- Kiambishi '-si-' kinasimamia kikanushi
- Kiambishi '-tu-' kinasimamia watendewa (wanaotendewa kitendo cha kuchorwa)
- Sehemu ya '-chor-' ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi '-e' ni kimalizio katika hali kanushi

**Mfano 2:** i+li+yo+jeng+w+a

**Jibu:**

- Kiambishi *'i-'* kinasimamia ngeli ya I-ZI au I-I
- Kiambishi *'-li-'* kinasimamia wakati uliopita
- Kiambishi *'-yo-'* kinasimamia kirejeshi (kinarejelea nomino husika)
- Sehemu ya *'-jeng-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-w'* ni kiambishi cha mnyambuliko (kauli ya kutendwa)
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

Katika hatua hii, mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wanashirikishwa kutambua namna ya kuviainisha vitenzi kwa kurejelea viambishi awali na viambishi tamati pamoja na majukumu ya viambishi hivi.

Baada ya wanafunzi kuelewa majukumu ya viambishi awali na tamati, mwalimu awaelekeze kufanya zoezi la 3 ambapo wanahitajika kuainisha vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa kisha waeleze majukumu ya viambishi awali na tamati vilivyotumika. Baada ya kukamilisha zoezi hili, wanafunzi washirikishwe kusahihisha zoezi hilo kwa kuwachochea kupata ujuzi ainasafu kama vile tafakuri tanduizi ambapo mwalimu anaweza kuwaomba wanafunzi wengine kuchunguza majibu yanayotolewa na wenzao.

## Tathmini ya vipindi 23-25

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kuchunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kuainisha vitenzi mbalimbali na kuonyesha viambishi awali na viambishi tamati vilivyotumika pamoja na majukumu yao.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Mwalimu awaeleze wanafunzi kuhusu:

Baadhi ya sifa za hotuba:

- Aya ya kwanza huwa utangulizi na hutambulisha kitakachozungumziwa, salamu na msemaji.
- Aya kadhaa zinazofuata utangulizi huhusu ujumbe wa hotuba nzima.
- Hotuba huandikwa katika nafsi ya kwanza na huwa katika usemi asili.
- Hotuba huandikwa katika wakati uliopo.
- Aya ya mwisho huhitimisha hotuba kwa kutoa shukrani na kuwaaga wasikilizaji.

Silabi ambazo huwekwa mwanzoni mwa mzizi wa kitenzi huitwa ***viambishi awali***. Viambishi awali huweza kubeba maana ya*: nafsi, nyakati, vikanushi, watendewa, watendwa, virejeshi* n.k.

**Kwa mfano:** *tusiowapenda* = (‘*tu-’* – nafsi, ‘*-si-’* - kikanushi, *‘-o-’*- kirejeshi, *‘-wa-’* - mtendewa)

- Sehemu ya kitenzi ambayo huwa haibadiliki baada ya kunyambua kitenzi hicho katika kauli mbalimbali huitwa ***mzizi wa kitenzi*** hicho.

**Kwa mfano:** mzizi wa kitenzi ‘*penda’* ni ‘*pend’*.

- Silabi ambazo huwekwa mwishoni mwa mzizi wa kitenzi huitwa ***viambishi tamati*** ambavyo huweza kuwa na maana ya kuonyesha minyambuliko mbalimbali au kuwa vimalizio au viishio.

**Kwa mfano:** Katika kitenzi ‘*alipigiwa*’, viambishi tamati ni ‘*-iw-*’ (mnyambuliko) na ‘*-a*’ (kimalizio).

## 12.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada lifuatalo ambalo linalenga kuinua kiwango cha chini kwa wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

*Ainisha vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo.*

1. Mama *amepika* wali.
2. Yule ndiye kiongozi *niliyemtaja*.
3. Viatu *visivyouzwa* hutupwa.
4. Bakame *alituimbia* wombo mzuri.
5. Kwa nini *unacheka*?

## Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini namna wanafunzi wataainisha vitenzi katika sentensi walizopewa.

**Sentensi 1:** a+me+ pik+ a

- Kiambishi *'a-'* kinasimamia nafsi
- Kiambishi *'-me-'* kinasimamia wakati uliotimilika
- Sehemu ya *'-pik-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

**Sentensi 2:** ni+li+ye+m+taj+ a

- Kiambishi *'ni-'* kinasimamia nafsi
- Kiambishi *'-li-'* kinasimamia wakati uliopita
- Kiambishi *'-ye-'* kinasimamia kirejeshi (kinarejelea nomino husika)
- Kiambishi *'-m-'* kinasimamia mtendewa/mtendwa (kinarejelea nomino husika)
- Sehemu ya *'-taj-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

**Sentensi 3:** vi+si+vyo+uz+w+ a

- Kiambishi *'vi-'* kinasimamia ngeli ya KI-VI (wingi)
- Kiambishi *'-si-'* kinasimamia kikanushi
- Kiambishi *'-vyo-'* kinasimamia kirejeshi (kinarejelea nomino husika)
- Sehemu ya *'uz-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-w-'* kinasimamia kiambishi cha kauli ya kufanywa
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

**Sentensi 4:** a+li+tu+imb+i+ a

- Kiambishi *'a-'* kinasimamia nafsi
- Kiambishi *'-li-'* kinasimamia wakati uliopita
- Kiambishi *'-tu-'* kinasimamia mtendewa/mtendwa (kinarejelea nomino husika)
- Sehemu ya *'imb-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-i-'* kinasimamia kiambishi cha kauli ya kufanyia
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

**Sentensi 5:** u+na+chek+ a

- Kiambishi *'u-'* kinasimamia nafsi
- Kiambishi *'-na-'* kinasimamia wakati uliopo
- Sehemu ya *'chek-'* ni mzizi wa kitenzi
- Kiambishi *'-a'* ni kimalizio

## ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi kumi sahihi kwa kutumia vitenzi vilivyo na viambishi awali na viambishi tamati.

***Kwa mfano:***

1. Mwalimu *anaandika* ubaoni.
2. Mama *aliyamwaga* maji yote.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitenzi vilivyo na viambishi awali na viambishi tamati.

## 12.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 104

1. Ili kujadili umuhimu wa kushirikiana kijinsia ili kuboresha maisha.
2. Mgeni wa heshima, wageni waalikwa, machifu, manaibu wa machifu, mwenyekiti wa baraza la wazee, wazee wa kijiji na wananchi.
3. Kuwatambua waliohudhuria na kutaja madhumuni ya mkutano.
4. Kwa ushirikiano.
5. Shughuli za ukulima na ufugaji.
6. Wanaume hudhani kuwa wanawake hawana uwezo wa kufanya kile ambacho wao hufanya. Wao huwaona wanawake kama viumbe dhaifu. (*Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi).*
7. Ndio. Mwanamke ana faida katika jamii kwa kuwa yeye hushiriki katika takribani shughuli zote za kuendeleza jamii. (*Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi*).
8. Usafishaji wa mazingira.
9. Himizo kwa wananchi wote kujitahidi kadri ya uwezo wao ili kuishi vyema na watu wa jinsia zote bila kuwabagua wala kuwadharau wengine.
10. Mungu alituumba kwa kutumia vifaa sawa.

### Zoezi la msamiati, ukurasa 105

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa.

**Kwa mfano:**

1. ***mwito -*** taarifa ya kumtaka mtu aende mahali fulani; mwaliko
2. ***ushirikiano -*** hali au tendo la watu kuungana na kusaidiana katika shughuli

### Zoezi la 1, ukurasa 105

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati kutoka kwenye kifungu. Pia, atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***mwenyekiti -*** mtu anayeteuliwa kuongoza mkutano
2. ***mwito -*** taarifa ya kumtaka mtu aende mahali fulani; mwaliko
3. ***dhahiri shahiri -*** wazi kabisa
4. ***unyanyapaa -*** tabia ya kumtenga mtu kwa hali aliyo nayo
5. ***jinsia -*** hali ya mtu kuwa mwanamume au mwanamke
6. ***alituhimiza -*** alitushawishi
7. ***malalamiko -*** matamko ya kuonyesha kutopendezwa na yale uliyofanyiwa
8. ***potovu -*** -enye kuenda kinyume na maadili
9. ***mkurugenzi -*** mkuu wa idara kuu ya wizara, shirika au taasisi
10. ***ubaguzi -*** hali ya upendeleo katika kuwahudumia watu

**Matumizi katika sentensi:**

1. ***Mwenyekiti*** wa mkutano ameondoka.
2. Tuliitikia ***mwito*** wa kuhudhuria kongamano la mwaka.
3. Ni ***dhahiri shahiri*** kuwa usawa wa kijinsia hauzingatiwi Afrika.
4. ***Unyanyapaa*** dhidi ya wanawake ni jambo baya.
5. Wanafunzi wa ***jinsia*** ya kike ni wengi kuliko wale wa kiume.
6. Mwalimu ***alituhimiza*** kuzingatia uakifishaji wakati wa kuandika hotuba.
7. ***Malalamiko*** ya wanawake yatasikilizwa na afisa mkuu.
8. Dhana kuwa wanawake ni dhaifu ni ***potovu***.
9. ***Mkurugenzi*** wa shirika la kahawa atatuongelesha.
10. ***Ubaguzi*** wa rangi hufanyika sana Ulaya.

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 106**

Mwalimu atathmini hoja za wanafunzi wakati wa majadiliano yao. Wanaweza kutaja hoja kama vile:

1. Unyanyasaji wa kijinsia husababisha vita miongoni mwa wanajamii.
2. Huleta kutoelewana baina ya watu wanaohusika.

3. Huwafanya wanaonyanyaswa kukosa ari ya kushirikiana kikazi na wenzao.
4. Huathiri uchumi wa jamii.

**Zoezi la 2, ukurasa 106**

Mwalimu atathmini hotuba za wanafunzi kuhusu shughuli mbalimbali za kuhamasisha umoja na utangamano wa Wanyarwanda.

**Zoezi la sarufi, ukurasa 106**

1. tutawafunika
    a) kiambishi *'tu-'* kinasimamia nafsi ya kwanza ,wingi
    b) kiambishi *'-ta-'* kinasimamia wakati ujao
    ch) kiambishi *'-wa-'* kinasimamia watendewa
    d) sehemu ya *'-funik'* ni mzizi wa kitenzi
    e) kiambishi *'-a'* ni kimalizio
2. mnatuchezea
    a) kiambishi *'m-'* kinasimamia nafsi ya pili, wingi
    b) kiambishi *'-na-'* kinasimamia wakati uliopo
    ch) kiambishi *'-tu-'* kinasimamia watendewa
    d) sehemu ya *'-chez'* ni mzizi wa kitenzi
    e) kiambishi *'-e-'* ni kimalizio cha kauli ya kutendea
    f) kiambishi *'-a'* ni kimalizio
3. msinipige
    a) kiambishi *'m-'* kinasimamia nafsi ya tatu, umoja
    b) kiambishi *'-si-'* kinasimamia kikanushi
    ch) kiambishi *'-ni-'* kinasimamia mtendewa
    d) sehemu ya *'-pig'* ni mzizi wa kitenzi
    e) kiambishi *'-e'* ni kimalizio cha hali kanushi
4. kilichochorwa
    a) kiambishi *'ki-'* kinasimamia ngeli ya KI-VI
    b) kiambishi *'-li-'* kinasimamia wakati uliopita

ch) kiambishi *'-cho-'* kinasimamia kitendwa

d) sehemu ya -*'chor'* ni mzizi wa kitenzi

e) kiambishi *'-w-'* ni kimalizio cha kauli ya kutendwa

f) kiambishi *'-a'* ni kimalizio

5. aliyelima

a) kiambishi *'a-'* kinasimamia nafsi ya pili, umoja

b) kiambishi *'-li-'* kinasimamia wakati uliopita

ch) kiambishi *'-ye-'* kinasimamia mtendewa

d) sehemu ya *'-lim'* ni mzizi wa kitenzi

e) kiambishi *'-a'* ni kimalizio

**Zoezi la 3, ukurasa 107-108**

1. Aliyonunuliwa

*a)* *'a-'* ni kiambishi awali cha nafsi ya pili umoja

*b)* *'-li-'* ni kiambishi cha wakati uliopita

*ch)* *'-yo-'* ni kiambishi kinachoashiria kitendwa

*d)* *'-nunu-'* ni mzizi wa kitenzi

*e)* *'-liw'* ni kiishio cha kauli ya kufanyiwa

*f)* *'-a'* ni kimalizio

2. Alichimbua

*a)* *'a-'* ni kiambishi awali cha nafsi ya pili, umoja

*b)* *'-li-'* ni kiambishi cha wakati uliopita

*ch)* *'-chimb'* ni mzizi wa kitenzi

*d)* *'-u-'* ni kiishio cha kauli ya kufanyua

*e)* *'-a'* ni kimalizio

3. Unaniangalia

*a)* *'u-'* ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu, umoja

*b)* *'-na-'* ni kiambishi cha wakati uliopo

*ch)* *'-ni-'* ni kiambishi cha mtendewa

a) '-angali' ni mzizi wa kitenzi

*b)* *'-a'* ni kimalizio

3. Anafundisha

   *a)* *'a-'* ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu, umoja

   *b)* *'-na-'* ni kiambishi cha wakati uliopo

   ch) '-*fundish*' ni mzizi wa kitenzi

   *d)* *'-a'* ni kimalizio

4. Aliwahutubia

   *a)* *'a-'* ni kiambishi awali cha nafsi ya tatu, umoja

   *b)* *'-li-'* ni kiambishi cha wakati uliopita

   *ch)* *'-wa-'* ni kiambishi cha watendewa

   d) '-*hutubi*' ni mzizi wa kitenzi

   *e)* *'-a'* ni kimalizio

5. Halijafunguliwa

   *a)* *'ha-'* ni kiambishi awali cha ngeli ya LI-YA

   *b)* *'-li-'* ni kiambishi cha wakati uliopita

   *ch)* *'-ja-'* ni kiambishi kikanushi

   d) *'-fungu'* ni mzizi wa kitenzi

   *e)* *'-liw-'* ni kimalizio cha kauli ya kufanyiwa

   *f)* *'-a'* ni kimalizio

6. Sitapiga

   *a)* *'si-'* ni kiambishi awali cha ukanusho wa nafsi ya kwanza, umoja

   *b)* *'-ta-'* ni kiambishi cha wakati ujao

   *ch)* *'-pig'* ni mzizi wa kitenzi

   *d)* *'-a'* ni kimalizio

7. Hakijasomwa

   *a)* *'ha-'* ni kiambishi awali cha ukanusho wa nafsi ya pili, umoja

   *b)* *'-ki-'* ni kiambishi cha ngeli ya KI-VI

   *ch)* *'-ja-'* ni kiambishi cha ukanusho wa wakati uliotimilika

a) '-som' ni mzizi wa kitenzi

*b) '-w-'* ni kimalizio cha kauli ya kufanywa

*ch) '-a'* ni kimalizio

4. Anamwandikia

*a) 'a-'* ni kiambishi awali cha nafsi ya pili, umoja

*b) '-na-'* ni kiambishi cha wakati uliopo

*ch) '-mw-'* ni kiambishi cha mtendewa

d) '-andik' ni mzizi wa kitenzi

*e) '-i-'* ni kimalizio cha kauli ya kufanyia

*f) '-a'* ni kimalizio

5. Tutasafiri

*a) 'tu-'* ni kiambishi awali cha nafsi ya kwanza wingi

*b) '-ta-'* ni kiambishi cha wakati ujao

ch) '-safiri' ni mzizi wa kitenzi

**Zoezi la 4, ukurasa 108-109**

1. Mwalimu ***ananifundisha*** Hisabati.
2. Kalamu ***iliyonunuliwa*** imepotea.
3. Mama ***ataniletea*** mkate.
4. Nyinyi ***msinisumbue***.
5. Chumbani humo ***mmefagiliwa***.

# Somo la 13: Hotuba na insha

## Vipindi 26-28: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha hotuba kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutambua namna ya kupigana na umaskini.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Michoro iliyo kwenye kitabu cha mwanafunzi;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 110-112;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusisha hotuba kuhusu njia za kupigana dhidi ya umaskini. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Mwalimu anaweza kuandaa hotuba kuhusu madhara ya umaskini ambayo atawasomea wanafunzi darasani au airekodi ili wanafunzi waisikilize darasani. Hotuba hii itamsaidia sana mwalimu katika kuwapa wanafunzi msingi wa kujadili kuhusu njia za kupigana dhidi ya umaskini. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu wao. Pia, wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa na mwalimu wao. Baadaye, mwalimu achukue fursa hii

kuomba wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa wakati wa somo lililopita kisha waendelee na somo hili. Baada ya haya, mwalimu awachangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 110. Kwa mfano mwalimu anaweza kuuliza: *Mnaona nini kwenye michoro hii?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu maswali waliyoulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"mimi ninaona..."* Kwa mfano: *Mimi ninaona mifugo. Mimi ninawaona wafanyabiashara sokoni. Mimi ninawaona wanafunzi wakifundishwa darasani na mwalimu*. Katika hatua hii, ni lazima mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kupata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi huku akiwasaidia kuwasiliana kwa lugha rasmi na sahihi kisarufi.

## 13.1 Kusoma na kufahamu:

## Hotuba kuhusu kupigana na umaskini

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya hotuba kuhusu njia za kupigana dhidi ya umaskini huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hivyo basi, wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya. Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wamesoma kama walivyoambiwa, mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu hotuba iliyopo. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: *Baadhi ya njia za kupigana dhidi ya umaskini ni zipi?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu swali la mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika hotuba hiyo. Kwa mfano: *Baadhi ya njia za kupigana dhidi ya umaskini ni kupata elimu, kufanya ukulima, ufugaji pamoja na biashara mbalimbali*.

Baada ya kupata picha ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu hotuba husika, mwalimu awaelekeze wanafunzi kujibu maswali ya hotuba waliyosoma. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika shughuli hii. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha maswali hayo huku akitoa maelezo yake kwa kutilia mkazo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

## Tathmini ya vipindi 26-28

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha ili kutambua ikiwa wanaweza kujadili kuhusu njia za kupigana dhidi ya umaskini. Wanafunzi wanaweza kurejelea hotuba waliyosoma hapo awali. Mwalimu anaweza kuuliza maswali mengine ambayo yanalenga kutathmini malengo ya ujifunzaji wa mada hii.

# Vipindi 29-30: Kujifunza msamiati

## a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na hotuba husika;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na hotuba husika.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 113;
- Kamusi ya Kiswahili;
- Wanafunzi wenyewe;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu msamiati unaohusiana na hotuba waliyosoma hapo awali kuhusu njia za kupigana dhidi ya umaskini Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu kuhusiana na suala hili, somo hili litasaidia pia kuelewa maana ya msamiati unaohusiana na hotuba kuhusu vita dhidi ya umaskini. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kujadiliana kwa lugha rasmi na sahihi kisarufi. Katika maandalizi ya somo lake, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa atakavyohitaji kufundishia somo ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi hasa wanafunzi wenye ulemavu au matatizo fulani.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali mepesi kuhusu msamiati waliopatana nao katika usomaji wao wa hotuba waliyopewa kuhusu vita dhidi ya umaskini waliyosoma hapo awali. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha zoezi

walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi katika kupata ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

### 13.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na hotuba husika

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na kujadiliana kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao katika hotuba waliyosoma kuhusu njia za kupigana dhidi ya umaskini. Wanafunzi wajadiliane kuhusu maana za msamiati huo kwa kuzingatia matumizi yake katika hotuba husika. Wanafunzi wanaweza kutumia kamusi pale panapohitajika. Mwalimu azunguke darasani akitoa maelekezo kwa wanafunzi pale yanapohitajika. Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 1 la msamiati lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 113. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wote wameelewa maana ya msamiati wote uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika vitabu vyao. Hivyo basi, wanafunzi, katika makundi yao, wajadiliane kuhusu zoezi hilo la msamiati huku mwalimu akizunguka darasani kuwaelekeza wale wanaotatizika. Wanafunzi washirikishwe katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati walioufafanua. Baada ya zoezi hili, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha zoezi hilo.

Wakati wa kusahihisha zoezi hili, mwalimu arejelee mifano mingine inayoweza kuwasaidia wanafunzi kupata stadi za utafiti, utawala binafsi na stadi za maisha.

### Tathmini ya vipindi 29-30

Katika hatua hii ya tathmini, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifundisha kutokana na hotuba waliyosoma hapo awali kuhusu njia za kupigana dhidi ya umaskini. Hivyo basi, vifaa na picha zilizotumiwa kujifunzia somo hili zitumiwe kuchunguza iwapo wanafunzi wamepata uelewa wa funzo hili.

## Vipindi 31-33: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu tofauti kati ya hotuba na insha;
- Kujadili kuhusu uhusiano uliopo kati ya hotuba na insha.

- Vifaa vya kujifunzia  Chati yenye kuonyesha uhusiano uliopo kati ya insha na hotuba;
- Insha na hotuba kadhaa zilizoandikwa;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 113-114;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

### b) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha kuhusiana na majadiliano kuhusiana na uhusiano uliopo kati ya insha na hotuba. Mwalimu aandae chati yenye kuonyesha uhusiano uliopo kati ya insha na hotuba. Mifano kadhaa ya insha na hotuba iandaliwe kwa ajili ya kufundishia somo hili. Mwalimu anaweza kurekodi hotuba kadhaa ili kuwasomea wanafunzi darasani au kuwawekea wakazisikiliza. Ili kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi katika makundi yanayotakikana kwa kila zoezi husika.

### ch) Utaratibu wa somo

#### Utangulizi

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita kuhusu msamiati wa hotuba kuhusu vita dhidi ya umaskini. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika kipindi kilichotangulia.

## 13.3 Matumizi ya lugha: Tofauti kati ya hotuba na insha

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha wajadiliane kuhusu:

1. *Tofauti zilizopo kati ya hotuba na insha.*
2. *Uhusiano uliopo kati ya hotuba na insha.*

Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano mwalimu anaweza kuwapa

wanafunzi kutoka kwenye makundi yote nafasi ya kuwasomea wanafunzi wenzao matokeo ya majadiliano yao. Wanafunzi washiriki katika kuelezana ugunduzi wao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kudondoa hoja mbalimbali kutoka kwa mawasilisho ya makundi mbalimbali kuhusiana na uhusiano uliopo kati ya insha na hotuba.

Baadhi ya mawasilisho ambayo wanafunzi katika makundi yao wanaweza kuwasilisha ni kuwa:

1. Mojawapo ya tofauti kati ya insha na hotuba ni kuwa hotuba huwa ni taarifa ambayo husemwa mbele ya hadhira ilhali insha huandikwa hasa kwa minajili ya kutahiniwa au kusomwa na wasomaji wengine.
2. Uhusiano uliopo kati ya insha na hotuba ni kuwa zote mbili zina umbo sawa la kuwepo kwa *mada, utangulizi, mwili* na *hitimisho*.

Majadiliano katika makundi yatawasaidia wanafunzi katika kuelewa uhusiano wa insha na hotuba kwa mapana na marefu.

Baada ya mawasilisho ya wanafunzi, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 2 lililo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 114. Katika zoezi hili, wanafunzi wanahitajika kubuni hotuba kuhusu umuhimu wa maji. Pia, wanafunzi wabuni insha kuhusu umuhimu wa maji. Wanafunzi wote washirikishwe katika zoezi hili ambapo hapo baadaye watalinganisha hotuba na insha walizotunga kuhusu mada sawa ya '*umuhimu wa maji'*. Wanafunzi waelezane ugunduzi wao.

## Tathmini ya vipindi 31-33

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali haya yatamsaidia mwalimu kudhibitisha iwapo wanafunzi wanaweza kutambua uhusiano na tofauti zilizopo kati ya insha na hotuba.

# Vipindi 34-35: Kusikiliza na kuzungumza

## a) Malengo ya somo

- Kutunga hotuba;
- Kutambua sehemu kuu za hotuba.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha umbo la hotuba;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 114;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.)

## ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mwalimu anaweza kutumia aina mbalimbali za hotuba alizoandika awali au alizorekodi kabla ya somo hili ili azitumie kuwafundishia wanafunzi na kuwaongoza kwa kuwapa mwelekeo kamili wa kuandika hotuba waliyopewa kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 106. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kuzingatia katika uandishi hotuba husika ili mwanafunzi apate picha kamili ya hotuba nzuri na jinsi inavyofaa kuandikwa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi katika uandishi wa hotuba katika makundi yao.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali

kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie aina za hotuba alizoandaa kutanguliza funzo hili.

## 13.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga hotuba

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha watunge hotuba kuhusu umuhimu wa *Umuganda* kwa Wanyarwanda. Wanafunzi wahakikishe kwanza kuwa wanajikumbusha kuhusu sehemu kuu za hotuba kama walivyofundishwa katika somo la hapo awali. Sehemu kuu za hotuba ni: *mada, utangulizi, mwili* na *hitimisho*.

Baada ya wanafunzi kujikumbusha kuhusiana na umbo la hotuba, wajadili hoja za kujenga hotuba ambayo watatunga. Baadaye, waunganishe hoja zao pamoja ili kuunda hotuba. Wanafunzi wahakikishe wanazingatia umbo kamili la hotuba pamoja na mada waliyopewa. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Mwalimu ateue mwanafunzi mmoja mmoja kutoka kwa kila kundi asimame mbele ya wanafunzi wenzake na awasomee hotuba waliyoandika katika kundi lao. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi ya wanafunzi wakati wa mawasilisho yao. Wanafunzi wapewe fursa ya kujadili hotuba watakazosomewa kwa kuchunguza iwapo zimedhibiti mada waliyopewa pamoja na kuzingatia umbo kamili la hotuba. Wanafunzi wahakikishe pia kuwa hotuba zao zimezingatia mambo mengine muhimu ya kuzingatia katika kuandika hotuba nzuri.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kufanya zoezi la 3 lililo katika *Kitabu cha mwanafunzi*, ukurasa 114 ambapo wanafunzi wanahitajika kubuni hotuba kuhusu madhara ya uchafuzi wa mazingira. Wanafunzi wazingatie umbo la hotuba bora na kamili katika utunzi wao.

## Tathmini ya vipindi 34-35

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi yenye kuchunguza na kudhihirisha uwezo wao wa kubuni hotuba kuhusu mada mbalimbali kwa kutilia mkazo mambo muhimu yanayozingatiwa kama vile: *sehemu kuu za hotuba, lugha rasmi na sahihi kisarufi, wakati uliopo* na kadhalika.

# Vipindi 36-37: Sarufi (Viambishi tamati)

## a) Malengo ya somo

- Kufafanua maana ya viambishi tamati katika Kiswahili;
- Kujadili majukumu ya viambishi tamati;
- Kutenga viambishi tamati katika vitenzi mbalimbali.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya viambishi tamati;
- Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa 114;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi katika somo hili kama vile chati yenye majedwali yaonyeshayo mabadiliko ya viambishi tamati katika kauli mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi pamoja na chombo cha kunasia sauti au breli na kadhalika. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua maana ya kiambishi tamati pamoja na majukumu mbalimbali ya viambishi tamati katika vitenzi hasa kwa kurejelea kauli mbalimbali za mnyambuliko wa vitenzi.

Mwalimu atambue wakati mwafaka wa kuweka hadharani vifaa alivyovileta. Wanafunzi walio na matatizo mbalimbali katika kuelewa na kufahamu haraka yale wanayofundishwa darasani au wale walio na kiwango cha chini katika ujifunzaji wao wataweza kufaidika kutokana na matumizi ya vifaa mbalimbali katika somo hili. Ili kuyafikia malengo yake katika somo hili, ni vyema mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika *Kitabu cha Mwanafunzi*.

### d) Utaratibu wa somo

*Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika masomo ya viwango vya hapo awali kuhusiana na mabadiliko ya viambishi tamati kwa kurejelea mnyambuliko wa vitenzi mbalimbali katika Kiswahili. Kutokana na swali hili la jumla, mwalimu aweze kuwashirikisha wanafunzi katika kutambua majukumu mbalimbali ya viambishi tamati katika vitenzi mbalimbali. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

## 13.5 Sarufi: Viambishi tamati

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na awaombe wachunguze vitenzi walivyopewa kwenye jedwali lililo katika vitabu vyao. Jedwali hili linahusisha vitenzi vilivyonyambuliwa katika kauli mbalimbali kwa lengo la kubaini mabadiliko ya viambishi tamati vyao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua na kuelewa mabadiliko haya pamoja na majukumu mbalimbali ya viambishi tamati katika vitenzi mbalimbali. Wanafunzi washirikishwe katika makundi yao kutambua kuwa baadhi ya majukumu ya viambishi tamati ni kuwakilisha kiambishi cha mnyambuliko wa kitenzi hicho husika au kuwa kimalizio (kiishio).

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 4 ambapo wanahitajika kuonyesha mizizi ya vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa kasha waeleze majukumu ya viambishi tamati vilivyo katika vitenzi hivyo.

Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatunga sentensi sahihi kisarufi. Hatimaye, wanafunzi wote washirikishwe katika kusahihisha zoezi hili.

## Tathmini ya vipindi 36-37

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kutambua mizizi ya vitenzi mbalimbali pamoja na kueleza majukumu ya viambishi tamati mbalimbali.

Ili kuwasaidia wanafunzi kuendeleza ujifundishaji wao nje ya darasa lao, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la 5 na 6 katika sehemu ya sarufi. Mazoezi haya yatasahihishwa kabla ya somo lijalo.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

- ***Hotuba*** ni taarifa kuhusu mada mbalimbali zinazoathiri jamii kwa namna fulani ambayo huandaliwa kwa minajili ya kusemwa mbele ya hadhira na mtu mmoja. Huzingatia umbo la kuwa na *mada, utangulizi, mwili* na *hitimisho*.
- ***Insha*** huandikwa hasa kwa minajili ya kutahiniwa au kusomwa na wasomaji wengine. Huhusu mada mbalimbali. Pia, huzingatia umbo la kuwa na *mada, utangulizi, mwili* na *hitimisho*.
- Herufi au silabi ambazo huwekwa mwishoni mwa mizizi ya vitenzi huitwa ***viambishi tamati***. Viambishi hivi huwa na majukumu mbalimbali yakiwemo:

a) Kuwakilisha mnyambuliko wa kitenzi husika katika kauli mbalimbali

**Kwa mfano:** a+li+ni+pik+i+a (viambishi tamati ni ***'-i-+-a-'***) kuwakilisha mnyambuliko wa kauli ya kufanyia na kimalizio mtawalia.

b) Huwa ni kimalizio au kiishio

**Kwa mfano:** pik+a (kiambishi tamati ni ***'-a'***) ambacho ni kimalizio/ kiishio

ch) Kuwakilisha kimalizio cha ukanushi

**Kwa mfano:** u+si+m+pig+e (viambishi tamati ni ***'-e'***) kuwakilisha kimalizio cha ukanushi.

d) Kuwakilisha wingi wa wahusika wanaotenda kitendo fulani.

**Kwa mfano:** lal+e+ni (viambishi tamati ni ***'-e- +-ni'***) kuwakilisha kimalizio cha masharti pamoja na kimalizio cha kuonyesha wingi.

## 13.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Ili kuwasadia wanafunzi wa kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe wanafunzi hawa kutambua mizizi ya vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo.

**Kwa mfano:** Mama *alishonewa* nguo nzuri.

**Jibu:** Mzizi ni ***shon-***

1. Mimi *ninapenda* kula wali.
2. Mkulima *alitegua* mitego yake yote.
3. Simba *alimnyemelea* swara.
4. Kwa nini *unalia*?
5. Kikombe chake *kimevunjika*.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

1. Mimi *ninapenda* kula wali.

   Mzizi wa kitenzi ni '–pend-'
2. Mkulima *alitegua* mitego yake yote.

   Mzizi wa kitenzi ni '-teg-'
3. Simba *alimnyemelea* swara.

   Mzizi wa kitenzi ni '-nyemele-'
4. Kwa nini *unalia*?

   Mzizi wa kitenzi ni '–li-'
5. Kikombe chake *kimevunjika*.

   Mzizi wa kitenzi ni '-vunj-'

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge hotuba kuhusu manufaa ya vyakula mbalimbali katika miili ya binadamu.

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Mwalimu atathmini hotuba ambazo wanafunzi watabuni. Baadhi ya hoja watakazohitajika kueleza ni:

1. Vyakula kama vile: *mahindi, wali, viazi vitamu, viazi mviringo, mihogo* n.k. hutupatia nguvu mwilini.
2. Vyakula kama vile: *nyama, maharagwe, mayai, maziwa* n.k. hutupatia protini ambayo husaidia katika ukuaji wa viungo na misuli mwilini.
3. Vyakula kama vile: *mboga na matunda* huisaidia miili yetu kupigana na maradhi mbalimbali.
4. Maji ni muhimu sana kwa mwili wa binadamu.

## 13.7 MAJIBU

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 112**

1. Kujitambulisha, kuwatambua waliohudhuria mkutano na pia aliyemtuma mtoaji wa hotuba na mwisho pamoja na kufafanua mada ya hotuba.
2. Mkoa ulikuwa umekumbwa na umaskini mwingi.
3. Watu wakielimika itakuwa rahisi kwao kupata ajira baadaye au kufanya biashara nzuri na kuinua kiwango cha uchumi wa jamii.
4. Ukulima na ufugaji utasababisha kuwepo kwa vyakula vya kutosha kukidhi mahitaji ya wanajamii. Mazao ya shambani na ya mifugo yakiuzwa huleta fedha. Pia, kutokana na kilimo, watu wanaweza kupata ajira mbalimbali.
5. Kwa sababu wakiwachagua viongozi fisadi na walafi, wataishia kuwa maskini kwa kuwa viongozi hao watajilimbikizia pesa za serikali.
6. Biashara zinapotanda kila mahali, watu hupata ajira na faida tele. Wanajamii wanaweza kuuza na kununua bidhaa zao kutoka mataifa mengine kwa bei nafuu.
7. Mahusiano mema huweza kupanua masoko na kusababisha biashara kuwanda.
8. Hotuba hii ina mwanzo ambao unawatambulisha waliohudhuria mkutano, anayetoa hotuba pamoja na mada ya hotuba. Mwili wa hotuba umetaja na kuelezea mbinu mbalimbali za kupigana na umaskini. Mwanzo kabisa ni kupitia kwa wanajamii kupata elimu ambayo baadaye itapelekea

wanajamii kupata ajira. Pili, ni kupitia kwa shughuli za kilimo na ufugaji. Mazao ya kilimo na ufugaji yakiuzwa yataleta pesa kwa wanajamii. Tatu, ni kupitia kuwateua viongozi bora kwa makini ili wasije wakawateua wale wafisadi na walafi watakaojilimbikizia pesa za serikali. Pia, mahusiano mema na mataifa mengine ni muhimu na pia kukuza shughuli za kibiashara kupitia serikali kubuni mikakati ya kutengeneza baadhi ya bidhaa za kutumia nchini badala ya kununua bidhaa hizo kutoka mbali. Mwisho wa hotuba unawahimiza wanajamii kujitahidi kutafuta shughuli ambazo zinaweza kuwapa pesa za matumizi ya kila siku.

9. Kwa kuwahimiza wanajamii kujitahidi kutafuta shughuli ambazo zinaweza kuwapa pesa za matumizi ya kila siku. Pia, amewashukuru kwa kumsikiliza na kuwapa changamoto kupitia kwa msemo.
10. Kulima katika mashamba, kuvuna, kuuza dawa za kuwanyunyizia mifugo na mimea, kazi ya usafirishaji n.k.

**Zoezi la 1, ukurasa 113**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati uliopigiwa mistari.

***Kwa mfano:***

1. ***waheshimiwa -*** watu wenye madaraka ambao wanaheshimiwa
2. ***adimu -*** nadra kupatikana
3. ***kutukirimia -*** kutupatia kwa wingi
4. ***kutenga -*** hali ya kuweka kando shughuli fulani au muda fulani
5. ***harakati -*** jitihada zinazofanywa na watu
6. ***utapiamlo -*** maradhi yanayosababishwa na ukosefu wa lishe bora
7. ***riziki -*** kipato
8. ***kujilimbikizia -*** kujiwekea kwa wingi bila kuwajali wengine
9. ***lindi -*** shimo kubwa la aina yoyote
10. ***fisadi -*** watu wapotovu wa maadili wanaofanya mambo bila kuwajali wengine

***Matumizi katika sentensi***

1. Chumba hiki ni cha wageni ***waheshimiwa***.
2. Pesa zimekuwa ***adimu*** kupatikana.
3. Mungu ***ametukirimia*** uhai wa bure.
4. Ni bora kutenga pesa kidogo za matumizi ya ***dharura***.
5. Niko katika ***harakati*** za kuanzisha chama cha kilimo.
6. Watoto wasiopata lishe bora huugua ***utapiamlo***.
7. Mimi huuza mazao ya shambani ili kupata ***riziki***.
8. Wanasiasa wenye tamaa ya ***kujilimbikizia*** mali ya umma wasipigiwe kura.
9. Ajira hii imenitoa kwenye ***lindi*** la umaskini.
10. Viongozi ***fisadi*** wametukosea.

***Zoezi la 2, ukurasa 114***

Mwalimu atathmini insha za wanafunzi. Sharti zihusishe umuhimu wa maji.

***Mfano wa insha:***

***UMUHIMU WA MAJI***

*Maji ni kiowevu kisichokuwa na rangi. Maji ni muhimu sana katika maisha ya binadamu. Maji hutokana na mvua, mito, visima, ziwa na hata bahari. Maji ni uhai. Mtu akikosa maji huweza kuona kiu na hata kukata kamba. Mimea ikikosa maji, hunyauka na kukauka. Mimea ikikosekana husababisha njaa ambayo huwaua watu wengi.*

*Maji hutokana na mvua. Mvua hutokana na mawingu. Mawingu hutokana na mvuke utokao kwenye majani ya miti. Kwa hivyo, sehemu ambazo zina miti mingi hupata mvua nyingi na huwa na maji mengi.*

*Mvua inaponyesha, huunda mikondo ambayo huitwa mito. Mito hii huwa mikubwa na hatimaye hupeleka maji yake kwenye ziwa au baharini. Maji haya katika mito husaidia kunyunyizia mimea. Maji haya pia hunywewa.*

*Maji hutumiwa na binadamu, wanyama na hata ndege wa angani. Binadamu hutumia maji kufanyia shughuli kama vile: kuogea mwili, kufulia nguo na kudumisha*

*usafi wa nyumbani kwa jumla. Maji pia hutumiwa kukata kiu wakati wa joto kali. Wakati wa kupika, maji hutumiwa sana ili kuivisha chakula. Vyakula haviwezi kupikika bila ya kuwa na maji. Mchuzi huandaliwa kutumia maji.*

*Ndege wa angani hutaka maji kwa kunywa. Baada ya kupaa kwa muda, wao huona kiu. Huwalazimu kutafuta maji ili kukata kiu. Wapo ndege wengine ambao hutaka maji ili kuoga. Ndege kama heroe hupata chakula chao majini. Wao hula wadudu wadogo wadogo ambao huishi majini.*

*Maji ni makao ya wanyama. Mamba na kiboko huishi majini. Maji yakikosekana, wanyama hawa pia watakosa makao. Wanaweza kuaga dunia. Samaki pia huishi majini. Ikiwa maji yatachafuliwa, basi samaki wengi wataangamia. Tukumbuke kuwa samaki ni chakula muhimu sana katika maisha ya binadamu.*

*Maji pia hutumiwa katika kusafiri. Meli, motaboti, ngalawa na vyombo vingine vya majini huhitaji maji ili kutumika. Wanajeshi wa majini pia huhitaji maji ili kufanya kazi yao ya kuilinda nchi.*

***Mfano wa hotuba:***

## ***HOTUBA KUHUSU UMUHIMU WA MAJI***

*Mwenyekiti wa chama cha mazingira, walimu na wanafunzi, hamjambo? Leo nina furaha kama mwanachama wa chama cha mazingira kuwa hapa ili niwape hotuba yangu kuhusu umuhimu wa maji kwa binadamu na wanyama. Kwanza kabisa, maji ni muhimu kwetu sisi binadamu kwa sababu maji ni uhai. Sisi hunywa maji ili kukata kiu.*

*Maji hutumika katika shughuli zetu za nyumbani. Ili kuosha nguo zetu, sisi hutumia maji. Pia, maji hutumika kusafisha vyombo na nyumba. Sharti binadamu waishi katika mazingira safi. Hii ndiyo maana sisi hutumia maji kudumisha usafi. Mbali na usafi wa mazingira yetu, kuna usafi wa mwili ambao huhitaji maji. Sisi hutumia maji kuoga ili tuonekane nadhifu.*

*Binadamu pia hutumia maji katika shughuli za kilimo. Mimea yetu haiwezi kunawiri bila kunyunyiziwa maji. Sisi huinyunyizia mimea yetu maji ili inawiri na kutupa mazao mengi. Maji pia hutumiwa na binadamu katika kufuga samaki. Kunao binadamu ambao hujenga vidimbwi vya kufuga samaki na wao huhitaji maji. Samaki hao hukua na kuuzwa kisha wakawaletea binadamu pesa za kujikimu kimaisha.*

*Wanyama pia huhitaji maji. Maji ni muhimu kwa wanyama kwa sababu wao hunywa maji ili kukata kiu. Mbali na hayo, wanyama wanaofugwa nyumbani hurashiwa dawa ya kuzuia magonjwa. Dawa hiyo huwa imechanganywa na maji.*

*Wanyama wa majini na samaki huhitaji maji ili kuishi. Wanyama hawa ni kama vile: mamba, viboko na kobe wa majini. Wao hutegemea maji kama makazi yao. Ni wajibu wetu sisi binadamu kuyatunza mazingira na vianzo vya maji ili tuishi maisha mema.*

*Asanteni nyote kwa kuhudhuria na kunisikiliza. Mungu awabariki.*

**Zoezi la 3, ukurasa 114**

Mwalimu atathmini hotuba za wanafunzi kuhusu madhara ya uchafuzi wa mazingira.

***Kwa mfano:***

***HOTUBA KUHUSU UCHAFUZI WA MAZINGIRA***

*Mkuu wa mkoa wa Kaskazini, mwenyekiti wa chama cha mazingira, chifu na wanajamii wote, hamjambo? Mimi ni Julia Mukamunana. Niko hapa kwa niaba ya wizara ya afya na mazingira ili kuwapa hotuba kuhusu madhara ya uchafuzi wa mazingira. Chochote kinachotuzunguka ndiyo mazingira yetu. Uchafuzi wa mazingira hutukosesha raha. Uchafuzi wa mazingira unahusu kutupa takataka ovyoovyo, viwanda kuelekeza kemikali zao kwenye mito ya maji na uchomaji wa vitu vinavyotoa moshi mwingi na kuuelekeza kwenye hewa tunayopumua. Harufu mbaya ya watu kukojoa mahali pasipofaa hufanya maeneo hayo kunuka fe!*

*Ukipita mitaani utashangaa. Mahali pa jalala panapotengwa, wakazi huwa waaminifu kwa siku chache tu. Uaminifu wa kuzoa takataka majumbani mwao, kutembea hadi kwenye shimo la takataka na kuzimwaga humo unapungua siku zinavyozidi kupita. Watu wanazitupa tu ovyoovyo. Takataka nyingi zinabaki nje. Hali hii huendelea hadi takataka hujirundika kuelekea kwenye majumba. Kila mmoja hujitia hamnazo eti mchango wa takataka zake huwezi kuongeza maradhi. Wazazi na watoto wao wanatumia muda mwingi kuenda hospitalini. Wamesahau kuwa heri kinga kuliko tiba.*

*Mito katika miji imekuwa ndiyo mifereji ya maji machafu yatokayo misalani. Inavunda. Ukidhani wenye viwanda ndio wenye tabasuri, umekosea! Viwanda vyao*

*vinaelekeza maji yenye kemikali za sumu humo mitoni. Uchafuzi wote huo umeua viumbe wote waliokuwa wakifurahia maji mawewa. Watu wenyewe na wanyama wanayakosa maji yayo hayo.*

*Wanaovuta sigara ndio wauaji nambari moja. Hawajali wala hawatishiki kuwa wanayakaribisha maradhi mengi mwilini mwao. Ni kweli pia jamaa na watu walio karibu nao wana hatari kubwa zaidi ya kiafya. Moshi wa sigara husababisha saratani. Vigae vinavyosalia baada ya kuvuta sigara ni hatari zaidi. Hivi vikirushwa ovyo huweza kusababisha moto. Moto ukiwaka mahali penye mali, husababisha hasara kwa kuteketeza mali na kusababisha vifo vya watu.*

*Ni jukumu letu sisi sote kuyatunza mazingira yetu ili kujiepusha na madhara yanayosababishwa na uchafuzi wa mazingira. Nawapa shukrani za dhati kwa kujitokeza kwa wingi ili kuhudhuria mkutano huu. Asanteni sana.*

## Zoezi la sarufi, ukurasa 114

| Kauli | Kitenzi 'pika' | Mzizi wa kitenzi | Kiambishi tamati cha mnyambuliko | Kimalizio |
|---|---|---|---|---|
| Kauli ya kutendea | pikia | pik' | i | a |
| Kauli ya kutendewa | pikiwa | pik' | iw | a |
| Kauli ya kutendeka | pikika | pik' | ik | a |
| Kauli ya kutendesha | pikisha | pik' | ish | a |
| Kauli ya kutendwa | pikwa | pik' | w | a |

## Zoezi la 4, ukurasa 115

1. a) Mzizi wa kitenzi ni '-chez-'
   b) Kiambishi tamati '-e' ni kimalizio
2. a) Mzizi wa kitenzi ni '-shangaz-'
   b) Kiambishi tamati '-w-' ni cha kauli ya mnyambuliko – kauli ya kutendwa
   ch) Kiambishi tamati '–a-' ni kimalizio
3. a) Mzizi wa kitenzi ni '-nunul-'
   b) Kiambishi tamati '-iw-' ni cha kauli ya mnyambuliko – kauli ya kutendewa
   ch) Kiambishi tamati '-a' ni kimalizio
4. a) Mzizi wa kitenzi ni '-hitaj-'

b) Kiambishi tamati '-ik-' ni cha kauli ya mnyambuliko – kauli ya kutendeka

ch) Kiambishi tamati '-a' ni kimalizio

5. a) Mzizi wa kitenzi ni '-va-'

b) Kiambishi tamati '-liw-' ni cha kauli ya mnyambuliko – kauli ya kutendwa

ch) Kiambishi tamati '-a' ni kimalizio

## Zoezi la 5, ukurasa 115

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vitenzi vyenye viambishi tamati.

**Kwa mfano:**

1. Mtoto ***ameingiwa*** na woga.
2. Mimi ***sijaondokewa*** na maumivu.
3. Chakula ***kililika*** chote.
4. Mbwa ***alimhangaisha*** mgeni.
5. Gari ***lilimkaribia*** abiria.

## Zoezi la 6, ukurasa 115

Mwalimu atathmini namna wanafunzi watakavyoainisha viambishi tamati vya vitenzi.

**Kwa mfano:**

1. kuitikia

a) Mzizi wa kitenzi ni '-itik-'

b) Kiambishi tamati '-i-' ni cha kauli ya kufanyia

ch) Kiambishi tamati '-a' ni kimalizio

2. wamedharauliwa

a) Mzizi wa kitenzi ni '-dharau-'

b) Kiambishi tamati '-iw-' ni cha kauli ya mnyambuliko - kutendewa

ch) Kiambishi tamati '-a' ni kimalizio

3. kushirikiana
   a) Mzizi wa kitenzi ni '-shirik-'
   b) Kiambishi tamati '-ian-' ni cha kauli ya mnyambuliko - kutendeana
   ch) Kiambishi tamati '-a' ni kimalizio
4. mliohudhuria
   a) Mzizi wa kitenzi ni '-hudhuri-'
   b) Kiambishi tamati '-i-' ni cha kauli ya mnyambuliko - kutenda
   ch) Kiambishi tamati '-a' ni kimalizio
5. kuyasafisha
   a) Mzizi wa kitenzi ni '-saf-'
   b) Kiambishi tamati '-ish-' ni cha kauli ya mnyambuliko - kutendesha
   ch) Kiambishi tamati '-a' ni kimalizio

# Somo la 14: Ufupisho

## Vipindi 38-40: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha hotuba kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi.
- Kutaja mambo ya kuzingatia katika kuandika ufupisho kwa ujumla.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mifano ya ufupisho mbalimbali;
- Chati zenye makala yaliyofupishwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 116;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu hotuba kuhusu umuhimu wa maadili. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

### d) taratibu wa somo

#### *Hatua ya 1: Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha mazoezi waliyopewa katika kipindi kilichotangulia. Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu watazame michoro iliyo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi 116*. Mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali kuhusu michoro hiyo.

Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye michoro hiyo?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu swali waliloulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"mimi ninaona ..."* Wanafunzi wajibu swali la mwalimu, kwa mfano: *Mimi ninaona watoto wanaomsalimu babu yao kwa heshima. Mimi ninamwona mwizi akifukuzwa. Mimi ninawaona vijana wakitumia dawa za kulevya.* Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea katika michoro hiyo.

### 14.1 Kusoma na kufahamu: Hotuba kuhusu umuhimu wa maadili

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watano watano kisha wasome kwa kimya hotuba kuhusu umuhimu wa maadili huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu hotuba waliyosoma ili kuhakikisha kuwa wameielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Kwa nini mkurugenzi aliteua mada ya hotuba husika?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika hotuba husika. Kwa mfano: *Mkurugenzi aliteua mada hiyo baada ya kukumbana na visa mbalimbali vya utovu wa maadili pale shuleni.* Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kuyajibu maswali ya ufahamu waliyopewa katika vitabu vyao. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika.

Baada ya zoezi hili, wanafunzi washirikishwe katika kusahihisha maswali hayo ya ufahamu huku akitoa maelekezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

## Tathmini ya vipindi 38-40

Katika hatua hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kuchunguza iwapo wanaweza kurejelea waliyosoma katika hotuba kuhusu umuhimu wa maadili. Wanafunzi wadhihirishe utambuzi wao wa umuhimu wa maadili katika maisha yao pamoja na madhara ya kutokuwa na maadili katika maisha yao.

## Vipindi 41-42: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kutambua msamiati unaohusiana na hotuba husika;
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia msamiati unaohusiana na hotuba husika.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Kamusi ya Kiswahili;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 119;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu ujifunzaji wa msamiati unaohusiana na hotuba kuhusu umuhimu wa maadili iliyo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi* ukurasa 116-118. Mwalimu aandae mifano ya hotuba kadhaa ambazo anaweza kuwapa wanafunzi wakazisoma darasani na kuchambua msamiati wake katika makundi mbalimbali. Pia, mwalimu anaweza kuandaa hotuba kadhaa zilizorekodiwa ili wanafunzi wazisikilize darasani na baadaye kuchambua msamiati wake. Mwalimu anaweza kufanya maandalizi haya mapema kabla ya vipindi hivi.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na kipindi kilichopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika kipindi kilichotangulia.

## 14.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na hotuba ya umuhimu wa maadili

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne na kuwaomba wajadili maana za msamiati mpya ambao walipatana nao katika usomaji wa hotuba waliyopewa kuhusu umuhimu wa maadili. Wanafunzi waeleze maana ya msamiati husika kwa kuzingatia jinsi ulivyotumiwa katika hotuba waliyosoma. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale wanapoihitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi au kufafanua maana ya msamiati husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kuchunguza msamiati uliopigiwa mstari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 1 na kuutolea maana kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati.

Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe tena kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika hotuba waliyosoma. Ni vyema mwalimu azingatie kwamba utunzi wa sentensi za wanafunzi ndio utakaomfahamisha iwapo wanafunzi wamepata ujuzi unaotakikana katika tafakuri tanduizi, suluhisho kwa matatizo na mawasiliano kwa lugha rasmi na sahihi.

## Tathmini ya vipindi 41-42

Mwalimu ahitimishe funzo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundishwa. Maswali hayo yaegemee hasa katika kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kutumia kwa usahihi msamiati waliojifundisha kutokana na hotuba waliyosoma kuhusu umuhimu wa maadili katika maongezi yao hata nje ya darasa.

# Vipindi 43-45: Matumizi ya lugha

## a) Malengo ya somo

- Kujadili kuhusu maana ya ufupisho;
- Kutaja mambo ya kuzingatia katika kuandika ufupisho;
- Kujadili kuhusu sifa za ufupisho.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Mifano ya ufupisho mbalimbali;
- Chati zenye makala yaliyofupishwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 120;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu matumizi ya lugha kwa kurejelea majadiliano kuhusu sifa za ufupisho pamoja na mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandika ufupisho. Mwalimu aandae chati zenye makala yaliyofupishwa pamoja na kuonyesha taratibu zilizofuatwa katika kuandika ufupisho husika. Ili kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa amewagawa wanafunzi katika makundi yanayotakikana kwa kila zoezi husika.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu aanze kipindi hiki kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali mepesi kuhusiana na somo lililopita. Wanafunzi kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na waliyofundishwa katika kipindi cha hapo awali.

## 14.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu sifa za ufupisho

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha wajadiliane kuhusu mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa katika kuandika ufupisho. Wanafunzi waelezane kuhusu:

a) *Maana ya ufupisho.*

b) *Sifa za ufupisho.*

ch) *Taratibu za kuzungatiwa katika kuandika ufupisho.*

Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano mwalimu awaombe wanafunzi katika kila kundi wawasilishe matokeo ya majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao darasani. Mwalimu ahakikishe kuwa anakosoa makosa ya kimatamshi wakati wa mawasilisho ya wanafunzi.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa maana ya ufupisho pamoja na mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa ufupisho. Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa jambo hili. ***Ufupisho*** *ni muhtasari wa mambo muhimu katika taarifa fulani. Ufupisho ni stadi ambayo humsaidia mwanafunzi kuweza kusoma taarifa aliyopewa, kudondoa hoja muhimu na kuziunganisha ili kuunda taarifa nyingine iliyo fupi bila kupoteza ujumbe wa taarifa asilia.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutambua mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa ufupisho kama vile:

a) *Kusoma taarifa waliyopewa kwa mfululizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.*

b) *Kusoma taarifa hiyo kwa mara ya pili huku wakidondoa hoja muhimu na kuziandika.*

ch) *Kuchunguza iwapo kuna hoja ambazo zimesahaulika katika taarifa asilia.*

d) *Kuunganisha hoja zao kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.*

e) *Kusoma hoja walizounganisha kuhakikisha zina mtiririko mzuri.*

f) *Kuhariri makala yao kuondoa makosa ya kisarufi.*

g) *Kuzingatia idadi ya maneno yanayostahili.*

Kutokana na majadiliano ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaelekeze kudondoa na kuzitaja baadhi ya sifa za ufupisho kama vile:

1. *Ufupisho huwa mfupi ukilinganishwa na taarifa asilia.*
2. *Ufupisho huhifadhi ujumbe wa taarifa asilia.*
3. *Ufupisho huandikwa kwa kuzingatia idadi ya maneno yanayotakikana.*
4. *Viunganishi hutumika ili kupunguza idadi ya maneno katika kuandika ufupisho.*

Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano, mwalimu anaweza kuwachagua wanafunzi kadhaa kutoka katika makundi mbalimbali wasome matokeo ya majadiliano yao mbele ya wanafunzi wengine na kuwaomba wanafunzi waelezane ugunduzi wao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa mambo ya kuzingatia katika uandishi wa ufupisho pamoja na sifa zake kuu.

Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa funzo hili vyema.

### Tathmini ya vipindi 43-45

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kikundi kuhusiana na sifa za ufupisho pamoja na taratibu za kuzingatiwa wakati wa kuandika ufupisho.

## Vipindi 46-47: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kubuni hotuba kuhusu umuhimu wa wanyamapori;
- Kufupisha hotuba kuhusu umuhimu wa wanyamapori;
- Kutambua taratibu za kuzingatiwa katika uandishi wa ufupisho.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Makala yaliyofupishwa;
- Mtandao wa intaneti;
- Wanafunzi wenyewe;

- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 120;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia vipindi hivi kubuni hotuba kuhusu umuhimu wa wanyamapori pamoja na kuifupisha hotuba hiyo. Mwalimu anaweza kuandaa makala kadhaa yaliyofupishwa ili kukuza uzoefu wa kuandika ufupisho miongoni mwa wanafunzi katika makundi yao na kibinafsi. Kwa wanafunzi walio na matatizo ya kusikia, lugha ishara inaweza kutumika pamoja na kuyaandika maelezo ya mwalimu ubaoni. Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi katika makundi yanayotakikana kulingana na zoezi husika.

### d) Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali kuhusu kipindi kilichopita. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu na maswali watakayoulizwa. Mwalimu ahakikishe kuwa zoezi ambalo wanafunzi walipewa katika kipindi kilichopita limesahihishwa na wanafunzi waliokuwa na matatizo wameelekezwa.

## 14.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kufupisha hotuba

Hatua hii inahusu kusikiliza na kuzungumza. Mwalimu awaongoze wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili waweze kubuni hotuba kuhusu umuhimu wa wanyamapori nchini Rwanda.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutambua umuhimu wa wanyamapori katika nchi yetu. Kila mwanafunzi katika kila kundi ahakikishe kuwa anatoa hoja kuhusiana na umuhimu wa wanyamapori katika nchi yetu. Baadhi ya hoja ambazo wanafunzi wabnaweza kuzieleza ni:

1. *Wanayamapori huvutia watalii kutoka nchi mbalimbali ambao huja kuwatazama. Katika harakati za watalii kuja nchini kuwatazama wanyamapori hawa, nchi yetu hufaidika kwa kupokea pesa nyingi za kigeni ambazo husaidia katika ukuaji na kuboresha wa uchumi wa nchi.*
2. *Wanyamapori hutupatia mbolea kutokana na samadi zao. Mbolea hii inaweza kutumika katika shughuli za kilimo.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadiliana kuhusu umuhimu zaidi wa wanyamapori kwa Wanyarwanda. Sehemu hii ipanue ujuzi wa wanafunzi kuhusu umuhimu wa wanyamapori ambao wanapatikana nchini Rwanda. Wanafunzi waelekezwe kutunga hotuba yao kwa kutumia hoja za wanakikundi husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wajitokeze mbele ya darasa ili wawasilishe matokeo ya majadiliano yao kwa wanafunzi wenzao. Wanafunzi wengine nao wasikilize namna wanafunzi wenzao wanavyowasilisha hotuba yao Kila kikundi kipewe muda wa kuchangia katika mawasilisho ya wenzao huku wakiongozwa na mwalimu.

Baada ya majadiliano haya, mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao kufupisha hotuba waliyotunga kwa kutumia idadi ya maneno mia moja pekee. Mwalimu awakumbushe wanafunzi kuhusiana na taratibu za kuzingatia katika uandishi wa ufupisho. Wanafunzi wazingatie taratibu hizo katika ufupishaji wao.

Wanafunzi wote washirikishwe katika kusahihisha mawasilisho ya makundi yote.

## Tathmini ya vipindi 46-47

Mwalimu atathmini iwapo ujifunzaji umefanywa kwa namna ya kuridhisha baada ya vipindi hivi. Kwa hivyo, awaulize wanafunzi maswali mepesi ya kupima uwezo wao wa kurejelea sifa za hotuba pamoja na taratibu za kuzingatiwa wakati wa kuandika ufupiho. Mwalimu ahakikishe amebaini uwezo wa wanafunzi wa kutunga makala na kisha kuyafupisha kw ataratibu zifaazo.

## Vipindi 48-50: Sarufi (Uundaji wa nomino kutokana na vitenzi)

### a) Malengo ya somo

- Kufahamu maana ya nomino na kitenzi;
- Kuunda nomino kutokana na vitenzi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye nomino zilizoundwa kutokana na vitenzi;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 121;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza

kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Mwalimu ajiandae kufundisha vipindi hivi. Mwalimu aorodheshe mifano kadhaa ya nomino na mingine ya vitenzi ili kumwezesha kuwakumbusha wanafunzi tofauti kati ya aina hizi mbili za maneno katika Kiswahiili. Mifano hii kadhaa itamwezesha kuwafundisha wanafunzi sehemu hii ya sarufi kuhusu uundaji wa nomino kutokana na vitenzi. Iwapo mwalimu ana wanafunzi walio na matatizo ya kuona, basi itambidi kutunga na kuandika mifano yake mbalimbali kwenye breli kwa manufaa ya wanafunzi hao. Kwa wanafunzi walio na matatizo ya kusikia, lugha ishara inaweza kutumika pamoja na kuiandika mifano ya mwalimu ubaoni.

**d) Utangulizi**

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali kuhusu kipindi kilichopita cha sarufi hasa kuhusiana na viambishi tamati na majukumu yake mbalimbali. Kupitia kwa maswali haya, wanafunzi wataweza kuelewa kwa uwazi kuwa neno linaweza kufanywa kuwa na maana nyingine kwa kuongeza viambishi awali au viambishi tamati kwenye mzizi wa neno husika.

Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu wao kuhusu kipindi cha hapo awali. Mwalimu achukue fursa hii ya utangulizi ili kuwaomba wanafunzi kusahihisha mazoezi waliyopewa kutokana na kipindi kilichopita. Mwalimu aendeleze funzo hili kwa kuwaomba wanafunzi kujigawa katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana kwa kila zoezi.

## 14.5 Uundaji wa nomino kutokana na vitenzi

Ujifunzaji wa sarufi katika hatua hii uchukuliwe kama mwendelezo wa yale yaliyofundishwa katika sehemu ya sarufi kuhusu viambishi awali, mizizi ya vitenzi pamoja na viambishi tamati kwenye vipindi vya hapo awali. Kwa hivyo, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kukumbuka kwanza maana ya kitenzi na maana ya nomino katika Kiswahili. Uelewa wa dhana hii ya viambishi mbalimbali pamoja na mzizi itamwezesha mwalimu kufundisha kuhusu namna ya kuunda nomino kutokana na vitenzi mbalimbali.

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne kisha awaombe wachunguze aina za maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 121. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua aina hizo za maneno. Katika makundi yao, wanafunzi wajadiliane kuhusu ugunduzi wao kuhusiana na maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi hizo. Wanafunzi waelekezwe kutambua kuwa maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi hizo ni vitenzi pamoja na nomino zilizoundwa kutokana na vitenzi hivyo.

***Kwa mfano:***

1. *Nomino* ***mchezaji*** *kutokana na kitenzi* ***cheza***
2. *Nomino* ***mlevi*** *kutokana na kitenzi* ***lewa***
3. *Nomino* ***mvuvi*** *kutokana na kitenzi* ***vua***
4. *Nomino* ***mkulima*** *kutokana na kitenzi* ***lima***
5. *Nomino* ***mrina*** *kutokana na kitenzi* ***rina***

Kutokana na mifano hii, ni wazi kuwa ili kuunda nomino kutokana na vitenzi, mizizi ya vitenzi husika huongezewa viambishi awali au viambishi tamati.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuunda nomino nyingine kutokana na vitenzi watakavyopendekeza wenyewe katika makundi yao. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya zoezi hili, kila kundi lipewe muda wa kuwasilisha matokeo ya majadiliano yao. Wanafunzi wengine wasikilize kwa makini pamoja na kuandika kwenye madaftari yao vitenzi na nomino zilizoundwa na wanafunzi wengine ambazo wao hawakuunda katika kundi lao.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kufanya zoezi la 3 na la 4. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii. Mazoezi haya yatasahihishwa kabla ya kipindi kijacho.

## Tathmini ya vipindi 48-50

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali ya kuchunguza iwapo wanafunzi wameelewa jinsi ya kuunda nomino kutokana na vitenzi mbalimbali. Wanafunzi wachunguzwe iwapo wameelewa kuwa katika uundaji wa nomino kutokana na vitenzi mbalimbali, viambishi awali na viambishi tamati huongezwa kwenye mizizi ya vitenzi husika.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

- *Taratibu za kuandika ufupisho:*

1. Soma taarifa uliyopewa kwa mfululizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.
2. Soma taarifa hiyo kwa mara ya pili huku ukidondoa hoja muhimu na kuziandika.
3. Chunguza iwapo kuna hoja ambazo zimesahaulika katika taarifa asilia.
4. Unganisha hoja zako kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.
5. Soma hoja ulizounganisha kuhakikisha zina mtiririko mzuri.
6. Hariri makala yako ili kuondoa makosa ya kisarufi.
7. Zingatia idadi ya maneno yanayostahili.
   - Kuunda maneno kunahusu uzalishaji wa maneno mapya kutokana na kuambisha mzizi wa neno linaloshughulikiwa kwa kutumia viambishi awali na viambishi tamati. Maneno yanayotumiwa kuunda maneno mengine yanaweza kuwa vitenzi, nomino au vivumishi. Shughuli hii ya kuunda maneno mapya kutokana na maneno mengine huitwa ***uambishaji***.

***Kwa mfano:***

| Kitenzi | Nomino |
|---|---|
| chora | mchoraji *(m+chor+a+ji)* |
| paka | mpakaji *(m+pak+a+ji)* |
| shona | mshonaji *(m+shon+a+ji),* mshono *(m+shon+o)* |

## 14.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada ambalo linalenga kuinua kiwango cha chini cha wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

*Unda nomino kutokana na vitenzi vilivyopigiwa mistari katika sentensi zifuatazo.*

**Kwa mfano:** Mtangazaji alitu***arifu*** kuhusu hafla ya kitaifa.

**Jibu:** taarifa, kuarifu

1. Mwalimu mkuu aliwa***shtaki*** wezi walioiba vitabu vyetu.
2. Baba ali***rithi*** mali yake kutoka kwa babu yetu.
3. Wanafunzi wana***jadili*** swali waliloulizwa.
4. Waumini wali***tubu*** dhambi zao.
5. Kwa nini unani***tisha*** hivi?

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

1. mashtaka, shtaka, mshtaki, mshtakiwa, kushtaki
2. mrithi, mrithiwa, urithi, kurithi
3. majadiliano, kujadili
4. toba, kutubu
5. tisho, kutisha

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waunde vitenzi kutokana na nomino zilizopigiwa mistari katika sentensi zinazofuata.

**Kwa mfano:** ***Kinywaji*** hiki ni kitamu sana.

**Jibu:** (ku)nywa

1. ***Mtazamaji*** huyu anapenda vipindi vya watoto.
2. ***Mpenzi*** wake alichelewa kufika nyumbani.
3. Baba yangu ni ***mjenzi*** stadi sana.

4. Shangazi alipika ***<u>mlo</u>*** mtamu.
5. ***<u>Mkwezi</u>*** wa miti ile ya matunda ameumia.

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

1. tazama
2. penda
3. jenga
4. (ku)la
5. kwea

## 14.7 MAJIBU

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 118-119**

1. Wakurugenzi wa shule, mwalimu mkuu, naibu wa mwalimu mkuu, wazazi, walimu na wanafunzi.
2. Mwalimu wa Kiswahili.
3. Kwa kuwa kumekuwa na visa vingi vya utovu wa maadili vinavyowahusu baadhi ya wanafunzi.
4. *Heshima si utumwa*. Methali hii inamaanisha kuwa heshima inastahili kutolewa kwa mtu yeyote yule bila ya kuwa na vizingiti vyovyote.
5. Kufukuzwa shuleni au kufungwa jela.
6. Walimu wamewasaidia wanafunzi kadri ya uwezo wao.
7. Wizi, ubakaji na matumizi ya dawa za kulevya.
8. Kuwa na heshima, kuwa, mnyenyekevu, kuwa mkweli, kuwa mwaminifu, kuwa na nidhamu, kuwa na bidii, kuwajibikia shughuli unazopewa, kumcha Mungu na kutumia lugha yenye heshima.
9. Ili kuwasaidia wazazi wao siku za usoni na pia kujiendeleza wenyewe.
10. Kuwa mvivu, kuwa na wivu, wizi, ubakaji, kutozingatia usafi, kutumia dawa za kulevya, kutumia lugha chafu iliyojaa matusi, ubakaji, kutozingatia usafi, kuwa na kiburi, kuzua vita n.k.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 119**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati waliopatana nao katika hotuba waliyosoma.

**Kwa mfano:**

1. ***maadili -*** tabia njema zinazokubalika katika jamii
2. ***mwenendo -*** namna mtu anavyojiwasilisha katika hali yake ya kawaida

**Zoezi la 1, ukurasa 119**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati waliopatana nao katika hotuba waliyosoma. Pia, atathmini sentensi watakazotunga.

***Kwa mfano:***

1. ***wamejitolea mhanga -*** wameamua kufanya jambo fulani kwa mioyo yao yote
2. ***wamejikaza kisabuni -*** wametia jitihada sana
3. ***utovu -*** ukosefu wa
4. ***kesi -*** mashtaka yaliyofikishwa mahakamani
5. ***hofu -*** hali ya kuhisi woga fulani
6. ***kupindukia -*** kupita kiasi
7. ***elimu -*** mafunzo yanayotolewa na jamii kwa watu wake
8. ***ubakaji -*** tendo la kumwingilia mwanamke au mwanamume kingono kwa lazima
9. ***uaminifu –*** tabia ya mtu kuaminika kwa kusema ukweli
10. ***wizi -*** tendo la kuchukua mali ya mtu mwengine bila idhini yake

***Matumizi katika sentensi:***

1. Wazazi ***wamejitolea mhanga*** kutulipia karo ya shule.
2. Wanafunzi wa darasa letu ***wamejikaza kisabuni*** katika masomo yao.
3. Kuwatusi watu ni ***utovu*** wa nidhamu.
4. Uvutaji wa bangi ulimsababishia ***kesi*** mahakamani.
5. Nina ***hofu*** kuwa mtu yule ametoroka na pesa zangu.

6. Mwanafunzi aliyefukuzwa shuleni alikuwa amelewa ***kupindukia***.
7. Kila binadamu anastahili ***elimu*** bora.
8. Mwendawazimu yule alishtakiwa kwa kosa la ***ubakaji***.
9. Mwanafunzi bora alituzwa kwa ***uaminifu*** wake.
10. Matapeli wale walishtakiwa kwa ***wizi*** wa kimabavu.

**Zoezi la 2, ukurasa 120**

Mwalimu atathmini namna wanafunzi watakavyofupisha hotuba waliyosoma. Sharti wazingatie idadi ya maneno waliyoambiwa.

***Kwa mfano:***

*Kutokana na visa vingi vya utovu wa maadili, mkurugenzi aliteua mada kuhusu maadili. Maadili ni mwenendo au tabia njema inayokubalika katika jamii. Huhusu kuwa na heshima, kuwa mnyenyekevu, mwaminifu na mkweli. Wanafunzi wanahimizwa kuwaheshimu watu wote; wakubwa kwa wadogo. Mwanafunzi asiye na heshima huadhibiwa vikali. Mtu mwongo hana amani kwa kuwa ana hofu ya kugunduliwa. Kufuta alama kwenye karatasi za mitihani ni tabia ya uongo ambayo inafaa kukoma. Wanafunzi wanahimizwa kutia bidii masomoni kwa kuamka mapema na kudurusu ili waweze kufaulu na kuwasaidia wazazi wao siku za usoni. Wizi, ubakaji na matumizi ya dawa za kulevya huweza kusababisha mtu kufungwa jela au kufukuzwa shuleni. Kuzua vita na kuwanyanyasa wanafunzi wengine zimetengewa adhabu kali zaidi. Wanafunzi wanahimizwa kutambua kuwa hakuna mwanafunzi aliye bora zaidi kuliko mwengine. Mwisho, wanafunzi wanahimizwa kujenga msingi bora wa maisha yao na kutia bidii masomoni.*

**Zoezi la sarufi, ukurasa 121**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi, kwa mfano:

1. ‘*Mchezaji*’ ni nomino kwa sababu inaonyesha mtenda na ‘*cheza*’ ni kitenzi kwa sababu kinaonyesha kitendo.
2. ‘*Mlevi*’ ni nomino kwa sababu inaonyesha mtenda na ‘*lewa*’ ni kitenzi kwa sababu kinaonyesha kitendo.
3. ‘*Mvuvi*’ ni nomino kwa sababu inaonyesha mtenda na ‘*vua*’ ni kitenzi kwa sababu kinaonyesha kitendo.

4. ‘*Mkulima*’ ni nomino kwa sababu inaonyesha mtenda na ‘*lima*’ ni kitenzi kwa sababu kinaonyesha kitendo.

5. ‘*Mrina asali*’ ni nomino kwa sababu inaonyesha mtenda na ‘*rina*’ ni kitenzi kwa sababu kinaonyesha kitendo.

**Zoezi la 3, ukurasa 122**

1. ***jadili -*** mjadala, majadiliano, kujadili
2. ***adhibu -*** mwadhibu, adhabu, kuadhibu
3. ***samehe –*** msamaha, kusamehe
4. ***lima -*** ukulima, mkulima, kulima
5. ***vua -*** uvuvi, mvuvi, kuvua
6. ***andika -*** mwandishi, maandishi, mwandiko, kuandika
7. ***kunywa -*** mnywaji, unywaji, kinywaji
8. ***kimbia -*** mkimbiaji, ukimbiaji, mbio, kukimbia
9. ***pika -*** mpishi, upishi, kupika
10. ***chora -*** mchoraji, uchoraji, kuchora, mchoro

**Zoezi la 4, ukurasa 122**

1. *okoa* **-** mwokozi, uokoaji

   ***Mwokozi*** ametusamehe dhambi zetu zote.
2. *hariri* **-** mhariri, uhariri

   ***Mhariri*** alikifanyia kitabu cha riwaya uhariri.
3. *okota* **-** uokotaji, mwokotaji

   ***Uokotaji*** wa takataka jijini unasafisha eneo hilo.
4. *osha* **-** mwosha, uoshaji

   ***Mwosha*** amekamilisha kazi yake mapema.
5. *penzi* **-** mpenzi, mapenzi

   ***Mapenzi*** aliyopewa na mpenzi wake yalimpa furaha.

# Somo la 15: Mwongozo wa kuandika ufupisho

## Vipindi 51-53: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi kifungu cha hotuba kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kujadili mwongozo wa kuandika ufupisho.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha mwongozo wa kuandika hotuba;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 123;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linahusu hotuba kuhusu manufaa ya elimu. Mwalimu aandae vifaa vitakavyohitajika kufunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Katika kufanikisha somo hili, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila zoezi linalohusika.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu aanze somo lake kwa kuwaamkia wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha mazoezi waliyopewa katika kipindi kilichotangulia.

Baadaye, mwalimu aendelee na somo kwa kuwaomba wanafunzi katika

makundi ya wanafunzi watatu watatu watazame michoro iliyo kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 123. Mwalimu awachangamshe wanafunzi wake kwa kuwauliza maswali kuhusu michoro hiyo.

Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye michoro hiyo?* Mwalimu awaelekeze wanafunzi wake kuhusu namna ya kujibu swali waliloulizwa kwa kuwapa kitangulizi kama vile *"mimi ninaona…."* . Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu wao. Kwa mfano, *mimi ninaona wanafunzi wakipewa cheti.* Katika sehemu hii, ni vyema mwalimu awaelekeze wanafunzi wake ili wapate ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro husika huku wanafunzi nao wakifikiri na kugundua kile kinachoendelea katika michoro hiyo.

### 15.1 Kusoma na kufahamu: Hotuba kuhusu manufaa ya elimu

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya hotuba kuhusu manufaa ya elimu huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu hotuba waliyosoma ili kuhakikisha kuwa wameielewa. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza: *Kwa nini elimu ni muhimu?* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika hotuba husika. Kwa mfano: *Elimu humwezesha mtu kupata ajira*. Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha maswali ya ufahamu huku akitoa maelezo pale ambapo wanafunzi wanatatizika.

Hatimaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kusahihisha maswali hayo ya ufahamu.

## Tathmini ya vipindi 51-53

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kubainisha manufaa ya elimu.

## Vipindi 54-55: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati uiotumika katika hotuba husika;
- Kutumia msamiati wa hotuba husika katika sentensi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Kamusi ya Kiswahili;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 126;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu msamiati unaotokana na hotuba kuhusu manufaa ya elimu iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 123-125. Kwa kuwa hotuba hii inahusu manufaa ya elimu, ni vyema mwalimu alete vifaa vinavyoweza kurahisisha uelewa wa mada hii.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili kama vilivyobainishwa hapo juu. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza kuelewa somo hili. Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.

### 15.2 Ujifunzaji wa msamiati wa hotuba kuhusu manufaa ya elimu

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu na kuwaomba watafute maana za msamiati mpya kwa kurejelea jinsi ulivyotumiwa katika hotuba waliyosoma hapo awali. Mwalimu awaombe wanafunzi watumie kamusi ya Kiswahili pale wanapohitaji. Mwalimu azunguke darasani akiwaelekeza

wanafunzi wanaopata taabu katika kuitumia kamusi hiyo au kufafanua msamiati husika.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi kufanya zoezi la 1 ambapo wanahitajika kufafanua msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Baada ya wanafunzi hawa kukamilisha zoezi walilopewa, mwalimu awaombe wanafunzi kusahihisha kwa pamoja mazoezi hayo ya msamiati.

Ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wameelewa msamiati uliokuwa mpya kwao, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi wataje msamiati ambao hawakuelewa maana yake ili ujadiliwe kwa pamoja darasani kulingana na matumizi yake katika hotuba waliyosoma.

## Tathmini ya vipindi 54-55

Mwalimu atathmini iwapo malengo ya kufundisha msamiati wa hotuba kuhusu manufaa ya elimu yametimizwa.

## Vipindi 56-58: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kutaja mambo ya kuzingatia katika kuandika ufupisho kwa ujumla;
- Kujadili kuhusu vipengelee muhimu katika uandishi wa ufupisho.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Ufupisho ulioandikwa kwa kuzingatia mwongozo kamili na sahihi;
- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye mwongozo wa kuandika ufupisho;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 126;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya funzo hili, mwalimu atafute vifaa vitakavyoweza kurahisisha uelewa wa wanafunzi kama vile ufupisho mbalimbali zilizoandikwa kwa kuzingatia mwongozo kamili na sahihi pamoja na mambo muhimu ambayo hufaa kuzingatiwa katika uandishi wake. Kupitia vifaa hivyo, mwalimu aandae maswali mbalimbali yatakayowachochea wanafunzi kutambua mambo muhimu ya kuzingatia katika kuandika ufupisho.

## d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize wanafunzi maswali mepesi kuhusu waliyojifundisha katika kipindi kilichotangulia. Mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika majadiliano haya. Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

### 15.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano kuhusu mwongozo wa kuandika ufupisho

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wajadiliane kuhusu mambo ambayo yanafaa kuzingatiwa katika uandishi wa ufupisho. Wanafunzi wajadiliane kuhusu suala hili.

Baadhi ya hoja ambazo wanafunzi wanaweza kuzijadili ni:

1. *Kusoma taarifa waliyopewa kwa mfululizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.*
2. *Kusoma taarifa hiyo kwa mara ya pili huku wakidondoa hoja muhimu na kuziandika.*
3. *Kuchunguza iwapo kuna hoja ambazo zimesahaulika katika taarifa asilia.*
4. *Kunganisha hoja zao kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.*
5. *Kusoma hoja walizounganisha kuhakikisha zina mtiririko mzuri.*
6. *Kuhariri makala yao kuondoa makosa ya kisarufi.*
7. *Kuzingatia idadi ya maneno yanayostahili.*

Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao. Baada ya muda mfupi wa majadiliano, mwalimu awaombe wanafunzi wawasilishe mambo waliyojadiliana mbele ya wanafunzi wenzao.

Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kuelewa mambo muhimu ya kuzingatia katika uandishi wa ufupisho. Majadiliano katika makundi yatasaidia kuelewa jambo hili.

Mwalimu awahimize wanafunzi kufanya mazoezi zaidi kuhusu namna ya kuandika kwa hati nzuri inayoweza kusomeka kwa urahisi.

## Tathmini ya vipindi 56-58

Mwalimu atathmini iwapo malengo ya kufundisha mwongozo wa kuandika ufupisho yametimizwa.

## Vipindi 59-60: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kutunga hotuba yenye mada yoyote ile;
- Kufupisha hotuba husika;
- Kudondoa hoja muhimu za kuandikia ufupisho.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 127;
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji ujifunzaji na uangalifu maalum.

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Hotuba waliyosoma hapo awali itumiwe kuwaongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuweza kutunga hotuba. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kutunga makala kasha kuyafupisha kwa mwongozo kamili na sahihi.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi katika kuandika ufupisho.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie ufupisho alioandaa kutanguliza funzo hili.

### 15.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kufupisha hotuba

Mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha watunge hotuba kuhusu mada yoyote watakayochagua wao wenyewe. Iwapo wanafunzi hawataweza kujichagulia mada ya kuandikia hotuba, mwalimu anaweza kuwapa mada teule. Baada ya wanafunzi kutunga hotuba yao, mwalimu awaelekeze wafupishe hotuba hiyo kwa kutumia maneno themanini (80) pekee. Wanafunzi wahakikishe wanazingatia na kufuata taratibu za kuandika ufupisho. Wajihadhari wasipoteze ujumbe asilia wa hotuba yao katika mchakato wa kufupisha hotuba yao.

Baada ya zoezi hili, mwalimu ateue mwanafunzi wawili wawili kutoka kwa kila kundi wasimame mbele ya wanafunzi wenzake na wawasomee hotuba waliyotunga pamoja na ufupisho walioandika katika makundi yao. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi ya wanafunzi wakati wa mawasilisho yao. Wanafunzi wapewe fursa ya kujadili hotuba na ufupisho watakazosomewa kwa kuchunguza iwapo zimedhibiti mada umbo la hotuba pamoja na kuzingatia taratibu za kuandika ufupisho.

## Tathmini ya vipindi 59-60

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutoka kwa mawasilisho mbalimbali ya kila kikundi kuhusiana na uandishi wa hotuba pamoja na uandishi wa ufupisho wa hotuba hizo. Mwalimu athibitishe iwapo wanafunzi wamepata uelewa wa kuandika ufupisho kwa usahihi.

# Vipindi 61-62: Sarufi (Uundaji wa vitenzi jina)

## a) Malengo ya somo

- Kutambua maana ya vitenzi jina;
- Kuonyesha mifano ya vitenzi jina;
- Kuunda vitenzi jina:
- Kutunga sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi jina.

## b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha vitenzi jina mbalimbali;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 127;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Katika maandalizi ya somo hili, mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kubaini vitenzi jina katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, mwalimu atafute vifaa vya kufundishia somo hili kama vile: chati yenye kuonyesha vitenzi jina mbalimbali. Ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wote, mwalimu afikirie wakati mwafaka wa kuonyesha vifaa hadharani na kuwatumia wanafunzi wenyewe kuelewa somo hili.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Katika utangulizi, mwalimu awaamkie wanafunzi na kuwauliza maswali mepesi kuhusu kipindi kilichopita kuhusu sarufi ya uundaji wa nomino kutokana na vitenzi. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu aendelee kwa kuwashirikisha wanafunzi wote kusahihisha mazoezi waliyopewa katika kipindi kilichopita.

## 15.5 Uundaji wa vitenzi jina

Katika hatua hii, wanafunzi watapata fursa ya kufahamu mifano ya vitenzi jina vinavyopatikana katika lugha ya Kiswahili. Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awaelekeze kuchunguza maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika *Kitabu cha Mwanafunzi,* ukurasa 127-128. Wanafunzi wachunguze sentensi hizo kisha waelezane maneno yaliyopigiwa mistari ni ya aina gani na yameundwa kwa kutumia viambishi vipi. Wanafunzi wahakikishe kuwa wanajadiliana katika makundi yao. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaopata matatizo katika makundi yao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua kuwa maneno yaliyopigiwa mistari ni nomino zilizoundwa kutokana na mizizi ya vitenzi kuongezewa viambishi tamati.

***Kwa mfano:***

1. *kuchora – ku+chora*
2. *kuandika – ku+andika*
3. *kulia – ku+lia*
4. *kucheza – ku+cheza*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutambua kuwa ***vitenzi jina*** (kuchora, kuandika, kulia, kucheza) huundwa kwa kuongeza kiambishi awali ***'ku-'*** kwenye mzizi wa kitenzi pamoja na kiishio chake.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuhusu namna ya kufanya zoezi la 3 ambapo wanafunzi wanahitajika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi jina walivyopewa.

Baada ya kukamilisha zoezi hili, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kusahihisha zoezi hilo kwa kuwachochea kupata ujuzi ainasafu kama vile tafakuri tanduizi ambapo anaweza kuomba wanafunzi wengine kuchunguza majibu yanayotolewa na wenzao.

## Tathmini ya vipindi 60-61

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali hayo yaegemee hasa kwa kuchunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kutaja vitenzi jina mbalimbali na kuainisha viambishi vinavyoviunda.

Mwalimu pia ahakikishe kuwa wanafunzi wamepata maarifa ya kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi jina.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

- Taratibu za kuandika ufupisho:

1. Kusoma taarifa uliyopewa kwa mfululizo kuanzia mwanzo hadi mwisho.
2. Kusoma taarifa hiyo kwa mara ya pili huku ukidondoa hoja muhimu na kuziandika.
3. Kuchunguza iwapo kuna hoja ambazo zimesahaulika katika taarifa asilia.
4. Kuunganisha hoja zako kwa kutumia viunganishi mwafaka panapostahili.
5. Kusoma hoja ulizounganisha kuhakikisha zina mtiririko mzuri.
6. Kuhariri makala yako kuondoa makosa ya kisarufi.
7. Kuzingatia idadi ya maneno yanayostahili.

- Vitenzi vinapoambishwa kiambishi awali ***'ku-'*** huunda nomino zinazoitwa ***vitenzi – jina***.

***Kwa mfano:***

i) ku +ja = kuja

***Kuja*** *kwake hakukutarajiwa.*

ii) ku + tega = kutega

***Kutega*** kwake kuliifanya mitego yote kuteguka.

iii) ku + lima = kulima

***Kulima*** *kwa mkulima yule kuliwavutia wapitanjia.*

## 15.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada lifuatalo ambalo linalenga kuinua kiwango cha chini kwa wanafunzi wasioweza kuelewa kwa haraka kama wenzao.

*Ainisha vitenzi jina vifuatavyo kwa kuonyesha viambishi vyake mbalimbali.*

1. kuongoza
2. kusamehea
3. kuangamia
4. kuchotewa
5. kushonwa

**Kwa mfano: kujadiliwa**

**Jibu:** ***ku+jadili+w+a***

#### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

1. kuongoza = ku+ongoz+a
2. kusamehea = ku+samehe+a
3. kuangamia = ku+angami+a
4. kuchotewa = ku+chot+ew+a
5. kushonwa = ku+shon+w+a

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi tano sahihi kwa kutumia vitenzi jina.

***Kwa mfano:***

1. ***Kula*** kwa watoto wale kuliwashangaza wageni.
2. ***Kufagia*** kwa msichana huyu kunaridhisha.

**Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe vitenzi jina.

## 15.7 MAJIBU

**Maswali ya ufahamu, ukurasa 125**

1. Waziri wa elimu, afisa wa elimu wa Mkoa wa Kusini, wasimamizi wa shule mbalimbali, walimu wakuu wa shule mbalimbali, wananchi, wanafunzi, mabibi na mabwana.
2. Kujitambulisha, kuwatambua waliohudhuria pamoja na kutaja mada ya hotuba.
3. Elimu ya gumbaru ni mafundisho ya kimsingi yanayotolewa kwa watu waliopitisha umri wa kuwa shuleni.
4. Kila kitu katika ulimwengu wa sasa hufanyika kwa kuandika na kusoma. Kwa mfano: kusoma taarifa za magazeti, kusoma vitabu, maelezo ya bidhaa dukani kutumia teknolojia n.k.
5. Wafanyabiashara huweza kuendeleza shughuli zao kwa urahisi. Miradi huweza kudhibitiwa kwa urahisi pamoja na kuihusisha na teknolojia. Maarifa na namna ya kuepuka kupata hasara hupatikana kupitia elimu.
6. Wahalifu huwakosesha wananchi amani na kuwa kero kubwa kwa jamii.
7. Elimu imewasaidia wafanyabiashara kuendesha mitambo na mashine mbalimbali ambazo husaidia kurahisisha shughuli za kibiashara.
8. Ajira humwezesha mtu kupata mshahara wa kujikimu kimaisha kwa kupata chakula, mavazi na mahali pa kuishi. Elimu huwezesha nchi kupata wataalamu kama vile: madaktari, makarani, manahodha n.k.
9. Mtu asiyeelimika hana uwezo wa kusoma na kuandika na hivyo, mawasiliano na watu wengine hutatizika. Mtu huyu hupata ugumu wa kushiriki katika biashara na kufaulu kwa sababu ya matatizo ya kuwasiliana na wateja na wauzaji na pia kutodhibiti hesabu zake. Huwa vigumu kwa mtu huyu kupata ajira hasa zinazohitaji maarifa maalumu. Watu hawa huishia kuwa maskini na wengine hujiingiza katika uhalifu na kuwaathiri wananchi wengine.

10. Kwa kuwahimiza watu wote kufahamu kuwa elimu ina manufaa mengi, kuwahimiza watu wote kupata elimu na pia kuwashukuru wote waliohudhuria mkutano.

### Zoezi la msamiati, ukurasa 126

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati waliopatana nao katika usomaji wa hotuba waliyopewa.

**Kwa mfano:**

1. ***marubani -*** watu wenye ujuzi wa kuongoza ndege angani
2. ***elimu ya gumbaru -*** mafundisho ya kimsingi yanayotolewa kwa watu waliopitisha umri wa kuwa shuleni

### Zoezi la 1, ukurasa 126

Mwalimu atathmini maelezo ya msamiati pamoja na sentensi za wanafunzi.

***Kwa mfano:***

1. **jazila -** nyingi
2. ***Rabana -*** Mungu
3. ***masimulizi -*** maelezo yanayotolewa kama hadithi
4. ***tusife moyo -*** tusikate tamaa
5. ***anahisi -*** anapata fahamu kupitia viungo vyake kama vile: masikio, pua.
6. ***mshahara -*** malipo anayopata mtu mwishoni mwa mwezi baada ya kufanya kazi fulani
7. ***ajira -*** kazi ya kulipwa mshahara
8. ***wahandisi -*** watu wenye elimu na ujuzi wa kuhudumia mitambo, majengo na madaraja
9. ***waashi -*** mafundi wa kujenga nyumba kwa mawe au matofali
10. ***marubani -*** watu wenye ujuzi wa kuongoza ndege angani

**Matumizi katika sentensi:**

1. Mzungumzaji alitupa shukrani ***jazila*** kwa kuwa makini mkutanoni.
2. Tusisahau kumwomba ***Rabana*** kila siku.
3. ***Masimulizi*** ya bibi hutufurahisha.
4. Afisa wa elimu alituambia ***tusife moyo*** katika juhudi zetu za kila siku.
5. Mgonjwa ***anahisi*** maumivu kwenye tumbo.
6. Nitautumia ***mshahara*** wangu wa mwezi huu kununua runinga.
7. Maria amepata ***ajira*** ya kuwa karani wa wizara.
8. Tulifanya mkutano na ***wahandisi*** wawili pekee.
9. Hospitali kuu ya mkoa imejengwa na ***waashi*** maarufu.
10. Ndege zitakazowasafirisha wanajeshi zitakuwa na ***marubani*** wawili wawili.

**Zoezi la 2, ukurasa 127**

Mwalimu atathmini kila ufupisho ambao utaandikwa na wanafunzi katika makundi yao. Sharti wazingatie idadi ya maneno waliyoambiwa.

***Kwa mfano:***

*Elimu ni mafunzo ambayo hutolewa na jamii kwa watu wake, darasani au mahali pasipokuwa darasani. Enzi za mababu zetu, maarifa yalipitishwa kupitia masimulizi ya hadithi, vitendawili na misemo. Elimu humpa mtu uwezo wa kusoma na kuandika. Ni himizo kwa kila mtu kupata elimu hata wale waliopitisha umri wa kuwa shuleni wanahimizwa kuhudhuria kupitia mradi wa elimu ya gumbaru. Elimu pia humwezesha aliyeelimika kupata ajira ambayo humwezesha kupata mshahara wa kujikimu kimaisha. Shughuli za kibiashara huboreshwa na elimu kwani wafanyabiashara huweza kuendeleza biashara zao kwa urahisi na kuendesha mitambo au mashine mbalimbali ambazo husaidia kurahisisha shughuli za biashara. Elimu huwapa waandishi na watunzi maarifa ya kuandika tungo kama vile: riwaya, tamthilia na hadithi fupi, wakulima pia hupata maarifa ya kuendesha ukulima wao na pia uhusiano wetu na watu wa mataifa mengine huboreshwa. Madhara ya kutoelimika ni pamoja na: mtu asiyeelimika kukosa uwezo wa kusoma na kuandika, kupata ugumu katika kushiriki biashara, kukosa ajira na kuishia kuwa maskini wa kuombaomba kisha kujiingiza katika uhalifu. Ni himizo kwa wote kuwa elimu ina manufaa mengi.*

### Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 127

Mwalimu atathmini hotuba ambazo wanafunzi wataandika pamoja na ufupisho wa hotuba zenyewe. Ahakikishe kuwa wamezingatia mambo muhimu katika uandishi wa hotuba pamoja na ufupisho.

### Zoezi la sarufi, ukurasa 127-128

1. Neno '*kuchora*' ni nomino ya kitenzi-jina iliyoundwa kwa kiambishi awali '*ku-*' pamoja na kitenzi '*chora*'.
2. Neno '*kuandika*' ni nomino ya kitenzi-jina iliyoundwa kwa kiambishi awali '*ku-*' pamoja na kitenzi '*andika*'.
3. Neno '*kulia*' ni nomino ya kitenzi-jina iliyoundwa kwa kiambishi awali '*ku-*' pamoja na kitenzi '*lia*'.
4. Neno '*kucheza*' ni nomino ya kitenzi-jina iliyoundwa kwa kiambishi awali '*ku-*' pamoja na kitenzi '*cheza*'.

### Zoezi la 3, ukurasa 128

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***Kuchonga*** kwake vinyago hunifurahisha.
2. ***Kusafisha*** kwa mama huleta harufu nzuri.
3. ***Kulima*** kwa mkulima huyu ni kwa manufaa.
4. ***Kufuga*** kwake mifugo kumemsaidia sana.
5. ***Kukimbia*** kwa Gasimba kumemletea mali nyingi.
6. ***Kusali*** kwetu kumetuondolea balaa.
7. ***Kushona*** kwa fundi huyu hunipendeza.
8. ***Kutembea*** kwa wakimbizi kunashtua.
9. ***Kulala*** kwa mtoto mchanga ni kwa manufaa kwake.
10. ***Kula*** kwetu hapa ni muhimu.

**Majibu ya tathmini ya mada 3**

**Zoezi la 1 la kuandika, ukurasa 129**

Mwalimu atathmini hotuba ambazo wanafunzi wataandika kuhusu umuhimu wa kudumisha usafi wa mwili na mazingira.

**Zoezi la 1, ukurasa 129**

a) unguza
b) tembelewa
ch) lilia

**Zoezi la 2, ukurasa 129**

a) - lim-
b) -kuj-
ch) -end-
d) -tuli-
e) -on-

**Zoezi la 3, ukurasa 129**

1. a) uvuvi, mvuvi, kuvua
   b) upanzi, mpanzi, kupanda
   ch) upishi, mapishi, mpishi, kupika
   d) utabibu, tabibu, kutibu
   e) uchungaji, mchungaji, kuchunga
2. Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe nomino walizounda hapo juu.

***Kwa mfano:***

a) ***Uvuvi*** wa ***mvuvi*** huyu humletea pesa nyingi.
b) Huu ni msimu wa ***upanzi*** humu nchini.
ch) ***Mpishi*** wa shule yetu ameondoka.
d) ***Utabibu*** unahitaji umakini.
e) ***Mchungaji*** wa kondoo wetu ana jipu kifuani.

**Zoezi la 2 la kuandika, ukurasa 129**

Mwalimu atathmini hotuba ambazo wanafunzi wataandika ambazo watawasomea wanafunzi wenzao katika sherehe za siku ya wazazi shuleni mwao.

**Zoezi la 4, ukurasa 130**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

| Kitenzi (kauli ya kufanya) | Kauli ya kutendea | Kauli ya kutendeka | Kauli ya kutendesha | Kauli ya kutendewa |
|---|---|---|---|---|
| shona | shonea | shoneka | shonesha | shonewa |
| andika | *andikia* | *andikika* | *andikisha* | *andikiwa* |
| *ona* | onea | *oneka* | *onesha* | *onewa* |
| *pika* | *pikia* | pikika | *pikisha* | *pikiwa* |
| *onja* | *onjea* | *onjeka* | onjesha | *onjewa* |
| *tembea* | *tembelea* | *tembeleka* | *tembeza* | tembelewa |

**Zoezi la 5, ukurasa 130**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

1. ***a+me+nyw+eshw+a***

- '-a-' ni kiambishi ngeli
- '-me-' ni kiambishi cha wakati uliotimilika
- '-nyw-' ni mzizi wa kitenzi
- '-eshw-' ni kiambishi cha mnyambuliko
- '-a-' ni kiishio

2. ***u+me+m+kasiri+sh+a***

- '-u-' ni kiambishi cha nafsi
- '-me-' ni kiambishi cha wakati uliotimilika
- '-m-' ni kiambishi cha mtendewa
- '-kasiri-' ni mzizi wa kitenzi
- '-sh-' ni kiambishi cha mnyambuliko
- '-a-' ni kiishio

3. ***tu+ta+palili+a***
- ‘tu-’ ni kiambishi cha nafsi
- ‘-ta-’ ni kiambishi cha wakati ujao
- ‘-palili-’ ni mzizi wa kitenzi
- ‘-a’ ni kiishio

4. ***wa+li+zuru***
- ‘wa-’ ni kiambishi ngeli
- ‘-li-’ ni kiambishi cha wakati uliopita
- ‘-zuru-’ ni shina la kitenzi

5. ***wa+na+shereheke+a***
- ‘-wa-’ ni kiambishi cha nafsi
- ‘-na-’ ni kiambishi cha wakati uliopo
- ‘-shereheke-’ ni mzizi wa kitenzi
- ‘-a’ ni kiishio

## Zoezi la 6, ukurasa 130

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga.

**Kwa mfano:**

*1. Mama anamnywesha mtoto dawa.*

*2. Mwalimu alimketisha mwanafunzi kitini.*

*3. Shangazi amejishughulisha na kazi za pale nyumbani.*

*4. Nilimwandikisha barua kwa chifu.*

*5. Mwalimu alimsomesha mwanafunzi yule.*

Sura ya Nne

**Mada Kuu 4:** Ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo

**Mada Ndogo:** Midahalo na mijadala

## Uwezo upatikanao katika mada hii

Mwanafunzi aweze kuelewa mwongozo wa midahalo na mijadala na kushiriki katika kazi za majadiliano kwa kuzingatia mada zilizotolewa kujadiliwa; kujua jinsi ya kuchambua maneno ya Kiswahili kwa kutumia njia ya uambishaji.

## Malengo ya kujifunza

| Maarifa na ufahamu | Stadi | Maadili na mwenendo mwema |
|---|---|---|
| • Kutaja sifa au mwenendo unaofaa wakati wa kutoa hoja katika makundi.<br>• Kueleza mazingira ya mada na kuijadili bila upotovu wowote.<br>• Kutambua lugha inayofaa katika majadiliano.<br>• Kutafsiri mtiririko wa hoja au majadiliano ili kujiepusha na marudio ya wazo au fikira.<br>• Kuonyesha njia ya kutumia katika uambishaji wa maneno ya Kiswahili. | • Kutofautisha pande zinazoshiriki kwenye mdahalo au mjadala (utetezi au upinzani).<br>• Kutoa suluhisho katika majadiliano kwa kutetea hoja zinazomkera.<br>• Kutumia lugha sahihi na yenye kuvutia na kuridhisha.<br>• Kutumia ishara za mwili kulingana na hoja inayohusika. | • Kuonyesha moyo wa heshima wakati wa majadiliano.<br>• Kutokata tamaa na kutokasirika ovyo.<br>• Ushirikiano<br>• Urafiki<br>• Kujiamani |

## Maelezo kwa mwalimu

Mwalimu afahamu na awafahamishe wanafunzi kuwa mada hii inahusiana na masomo mengine yanayohusiana na kujenga mahusiano mema, kujenga tabia njema, umoja na ushirikiano, umoja na maridhiano, mapendo, adabu, siasa, dini, afya n.k.

Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanaelewa kuwa mazungumzo ni njia nzuri ya kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha. Kwa hivyo, mada hii inachukuliwa kama fursa muhimu ya kumsaidia mwanafunzi kukuza uwezo wake wa kuwasiliana na wengine na kujenga hoja kamili za kujitetea mbele ya wengine. Hivyo basi, mwanafunzi apewe nafasi kubwa na mazoezi ya kutosha ambayo huweza kumfaa katika kuongeza umahiri wa kujadiliana na kutoa maoni mbalimbali kwa kupinga au kutetea hoja za wengine na hata kufafanua jambo fulani linalohitaji ufumbuzi na uamuzi fulani. Mwalimu atafute namna ya kuwahimiza wanafunzi kushiriki katika midahalo na mijadala ya darasani na ile ya nje ya darasa ambapo wanafunzi wanaweza kuanzisha vilabu mbalimbali vinavyodhamiria kukuza uwezo wao kimaongezi kwa kutumia lugha ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi.

Katika mada hii, dhana za kisarufi pia zimejitokeza kuhusu uambishaji wa maneno ya Kiswahili.

## Masuala mtambuka

Baadhi ya masuala mtambuka ambayo yatashughulikiwa katika mada hii ni: *amani na maadili, elimu ya pamoja usawa wa kijinsia, pamoja na mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo wake.*

***Elimu ya pamoja*** itaendelezwa kupitia kwa wanafunzi wote kusoma pamoja kwa kuwashirikisha hata na wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali na matatizo mbalimbali iwapo wapo darasani. Elimu hii ya pamoja pia itahusisha wanafunzi wote kuwakubali wenzao na kushirikiana kwa pamoja na licha ya wao kutoka katika matabaka mbalimbali ya kijamii. Wanafunzi pia watafundishwa ***umuhimu wa mazingira*** yao na namna ya kuyahifadhi.

***Amani na maadili*** yatashughulikiwa kupitia kwa kushiriki katika mijadala na midahalo mbalimbali yenye kuendeleza maadili mema, uzalendo pamoja na ushirikiano miongoni mwa Wanyarwanda. Wanafunzi waelekezwe kutangamana kwa amani na upendo. ***Usawa wa kijinsia*** utatiliwa mkazo kwa kuwafahamisha wanafunzi kuwa wasichana pamoja na wavulana wana uwezo sawa wa kufaulu katika maisha yao licha ya jinsia zao tofauti.

## Uwezo wa jumla

Mwalimu ahakikishe kuwa katika ufundishaji wa somo hili wanafunzi wanapata uwezo wa kuwa na: *stadi za utafiti, utawala binafsi, usuluhishaji wa matatizo, mawasiliano katika lugha rasmi, ushirikiano na stadi za maisha, ubunifu na ugunduzi, tafakuri tanduizi pamoja* na *ujifunzaji wa muda mrefu.*

Mwalimu awaelekeze na awashirikishe wanafunzi wote katika kuwa na ***tafakuri tanduizi*** kwa kufikiri kwa undani zaidi kuhusiana na uandaaji wa mijadala na midahalo mbalimbali. Katika ufundishaji wa somo hili, utunzi mwingi na utoaji wa maelezo mengi utahusishwa. Ujuzi huu utawawezesha wanafunzi kuyajibu maswali yaliyo katika somo hili.

Kupitia kwa mazoezi ya kutunga na kushiriki katika utoaji wa hoja katika mijadala na midahalo mbalimbali, wanafunzi watahimizwa ***kuwasiliana kwa lugha rasmi*** pamoja na kuwa na ***utawala binafsi*** pamoja na kuzifahamu ***stadi mbalimbali za maisha na ushirikiano***. ***Stadi za utafiti*** zitakuzwa kupitia kwa wanafunzi kufanya utafiti kuhusiana na namna ya kushiriki katika mijadala na midahalo inayohusu masuala mbalimbali yanayowaathiri Wanyarwanda pamoja na kuendeleza ***ubunifu na ugunduzi*** wao. ***Ujifunzaji wa muda mrefu*** uendelezwe kupitia kwa wanafunzi kupata maarifa mbalimbali kuhusiana na kushiriki katika mijadala na midahalo mbalimbali darasani au hata nje ya darasa na katika maisha yao ya kila siku ili kuwa wazalendo kamili na kupata maarifa ya ***usuluhishaji wa matatizo***.

## Msamiati maalum

Msamiati maalum na muhimu ambao wanafunzi watapatana nao katika mada hii ni kuhusu ukuzaji wa matumizi ya lugha kimazungumzo nchini Rwanda kama vile:

| | Msamiati | Maana |
|---|---|---|
| 1. | mjadala | mazungumzo yanayohusu mada fulani ambayo hufanywa kwa kujenga hoja |
| 2. | mdahalo | mazungumzo maalum ambayo hufanywa na watu wenye mitazamo inayokinzana |
| 3. | mwenyekiti | mtu aliyechaguliwa kuongoza mkutano, chama au shirika kwa kipindi fulani |
| 4. | katibu | mtu anayeandika na kuhifadhi hoja katika mdahalo au mjadala |
| 5. | kujadili | kuzungumza kwa kutoa hoja aidha ya kuunga mkono au ya kupinga |
| 6. | mshiriki | mtu anayehusika katika shughuli fulani |
| 7. | hoja | maelezo ambayo huunga mkono au kupinga jambo linalojadiliwa |
| 8. | mtetezi | mtu anayeunga mkono hoja fulani katika majadiliano |
| 9. | mazungumzo | maongezi kati ya watu wawili au zaidi |
| 10. | mpinzani | mtu aliye na mtazamo tofauti na watu wengine anaoshindana nao |

## Usuluhishaji wa tatizo

Mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi yanayotakikana kisha awaombe wachunguze kwa makini michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 132 kuhusiana na mdahalo waliopewa. Wanafunzi pia wachunguze mada ya mdahalo waliopewa. Wanafunzi wote washirikishwe katika shughuli hii. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika makundi yao ili waweze kujibu maswali watakayoulizwa na mwalimu ili kuelewa kinachohitajika kujadiliwa katika mada mbalimbali watakazopewa. Kwa hivyo, mwalimu achochee uwezo wa wanafunzi wa kupata maarifa kuhusu ubunifu na ugunduzi na tafakuri tanduizi kwa kuchunguza mada mbalimbali za midahalo na mijadala iliyo katika vitabu vya wanafunzi.

## Ushirikishaji wa wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali

Ili kuwashirikisha kwa pamoja wanafunzi wenye ulemavu mbalimbali, ni vyema mwalimu awe na vifaa maalum vya kuwasaidia wanafunzi wa aina hii katika

kusoma na kujifundisha kwao. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona, mwalimu ahusishe matumizi ya breli pamoja na vifa vya kunasia sauti. Kwa wanafunzi wasio na uwezo wa kusikia, mwalimu ahusishe matumizi ya lugha ya ishara. Mwalimu anaweza kuwahusisha watafsiri wa lugha ya ishara. Haya yatawawezesha wanafunzi hawa kusoma kama wenzao bila vikwazo vyovyote. Nafasi ya wanawake katika shughuli kama vile za kushiriki katika midahalo na mijadala mbalimbali itiliwe maanani kupitia kwa michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi* ili kukuza usawa wa kijinsia na elimu ya pamoja kwa kudumisha ushirikiano na mienendo mizuri miongoni mwa wanafunzi.

## Orodha ya masomo na vipindi

| Mada ya somo | | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|
| **Somo la 16:** | Sifa za mdahalo | 16 |
| **Somo la 17:** | Mwongozo wa kuandika mdahalo | 16 |
| **Somo la 18:** | Mjadala | 15 |
| **Somo la 19:** | Mwongozo wa kuandika mjadala | 15 |
| | | **JUMLA: 62** |

## Somo la 16: Sifa za mdahalo

### Vipindi 1-3: Kusoma ufahamu

**a) Malengo ya somo**

- Kusoma kwa usahihi mfano wa mdahalo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutaja majina ya watu wanaoshiriki katika mdahalo.

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Mdahalo ulioandikwa;
- Mdahalo uliorekodiwa;
- Michoro ya wasemaji na wasikilizaji katika mdahalo;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 132;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Mdahalo ulioandaliwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mdahalo wowote. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa mdahalo kupitia wahusika wote wanaojitokeza katika mfano huu ili mwanafunzi apate picha kamili ya mdahalo mzuri na jinsi unavyofanywa. Kwa kuwa mdahalo huu unahusu athari za mavazi, ni vyema mwalimu alete vifaa vingine vinavyoweza kurahisisha uelewa wa mada hii kwa kurejelea mavazi yenye heshima. Katika hali hii, mwalimu anaweza kutafuta picha zinazoonyesha watu waliovaa mavazi yanayokubalika na jamii.

Hivyo basi, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kufundishia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kusoma na kuigiza mdahalo waliopewa. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza kuelewa somo hili.

Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake kisha awaulize maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu na hatimaye wasahihishe zoezi walilopewa kama kazi ya ziada.

Mwalimu atangulize somo hili kwa kuwagawa wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha awachangamshe kwa kuwauliza maswali kuhusu michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 132. Mwalimu awaelekeze kuelewa maana ya mdahalo na lengo lake la jumla. Mwalimu awaulize maswali kama vile: *Mnaona nini kwenye michoro hii? Watu hawa wanafanya nini?* Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa na mwalimu. Kwa mfano: *Mimi ninaona watu wakiwa katika shughuli ya kujadili mdahalo.*

Kutokana na mchoro kuhusu mdahalo, ni vyema mwalimu awaongoze wanafunzi kuelewa umuhimu wa kupanga na kutoa hoja kamili zenye kueleweka na wanaoshiriki katika mdahalo. Aidha, mwalimu aulize maswali kwa kuwataka wanafunzi waweze kugundua kile kinachoendelea katika michoro iliyopo ili

wakuze uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi na kuwasaidia kupata ujuzi katika ubunifu na ugunduzi, tafakuri tanduizi, usawa wa kijinsia kupitia wahusika wanaoshiriki katika mazungumzo na zile za wasikilizaji waliopo.

## 16.1 Kusoma na kufahamu

### Mdahalo kuhusu athari za mavazi ya kisasa

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya mdahalo ulio katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 132-135. Wanafunzi wasome kama wanavyoelekezwa na mwalimu. Baada ya kusoma huku, mwalimu awateue wanafunzi tofautitofauti ili wasome kwa sauti mdahalo huo. Katika shughuli hii, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wanajaribu kuiga mazungumzo huku wakizingatia kanuni zifaazo za kisarufi, utamkaji sahihi na kiimbo kinachotakiwa. Baadaye, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wote wameyaelewa mazungumzo waliyosoma kwa kuwauliza maswali kama vile: *Ni watu gani wanaozungumza katika kifungu hiki?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu.

Mwalimu achukue fursa hii kuwafafanulia wanafunzi utaratibu wa mdahalo ambapo watu wa pande mbili hujadiliana na kutoa hoja zinazotetea au kupinga wazo lililo katika mada inayozungumziwa huku akiuliza wanafunzi maswali kadhaa kuhusiana na yale waliyosoma. Mwalimu asahihishe makosa ya kimatamshi pindi yanapojitokeza.

Baadaye, mwalimu awashirikishe wanafunzi wote katika kujibu maswali ya ufahamu ambayo yatasahihishwa kwa pamoja kabla ya kumalizika kwa kipindi hiki.

## Tathmini ya vipindi 1-3

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kubainisha watu muhimu wanaohitajika katika mdahalo na kudhihirisha majukumu yao katika kuendeleza mdahalo.

Vilevile, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wanaweza kueleza utaratibu wa mdahalo na mambo muhimu yanayozingatiwa ili mdahalo uweze kufanyika

## Vipindi 4-6: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati unaotumika katika mdahalo;
- Kutaja majina ya watu wanaoshiriki katika mdahalo;
- Kutumia msamiati wa mdahalo katika sentensi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mdahalo uliorekodiwa;
- Michoro au picha za wasemaji na wasikilizaji katika mdahalo;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 135;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa mdahalo kupitia kwa wahusika wote wanaojitokeza katika mfano watakaousoma katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 132-135 ili mwanafunzi apate picha kamili ya mdahalo mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza kuelewa somo hili. Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.

## 16.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na mdahalo husika

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu ili wajadiliane kuhusu maana za msamiati mpya waliopatana nao huku wakitumia kamusi pale inapohitajika. Ili kuwaelekeza kupata uelewa wa msamiati huo, mwalimu awaongoze wanafunzi katika

kuchunguza matumizi ya msamiati huo katika mdahalo waliosoma. Wanafunzi wajadiliane na mwalimu azunguke darasani akitoa maelekezo kwa wanafunzi wanaotatizika.

Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajadiliane kuhusu zoezi la 1 la msamiati na ahakikishe kuwa wanafunzi wote wamejibu maswali yaliyopo. Mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanatunga sentensi zao wenyewe kwa kutumia maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi walizopewa.

## Tathmini ya vipindi 4-6

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti kwa kurejelea msamiati mahususi uliopatikana katika mdahalo waliosoma kuhusu athari za mavazi ya kisasa. Kwa hivyo, vifaa na picha zilizotumiwa kujifunzia somo hili zinaweza kutumiwa kuchunguza iwapo wanafunzi wanaweza kurejelea midahalo mbalimbali kuhusiana na namna ya kushiriki katika mdahalo katika kiwango cha utetezi na upinzani.

## Vipindi 7-9: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili sifa za mdahalo;
- Kutaja majina ya watu wanaoshiriki katika mdahalo.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- Mdahalo uliorekodiwa;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 136;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mdahalo ulioandaliwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mdahalo. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa mdahalo kupitia wahusika wote wanaojitokeza katika mfano huu ili mwanafunzi apate picha kamili ya mdahalo mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kushiriki katika mdahalo watakaopewa katika makundi yao.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

Mwalimu atumie mdahalo alioandaa kutanguliza funzo hili.

## 16.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za mdahalo

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu watatu wajadiliane kuhusu: *sifa bainifu za mdahalo.*

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili kuhusiana na sifa za mdahalo. Wanafunzi wanaweza kutoa hoja kama vile:

*Mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mitazamo tofauti huitwa **mdahalo**.*

***Sifa bainifu za mdahalo ni kama vile:***

1. *Mdahalo huhusisha pande mbili ambapo mtazamo wa kwanza hutoa hoja zinazotetea au kuunga mkono wazo kuu na mtazamo wa pili hutoa hoja za kupinga au kukataa wazo kuu.*
2. *Washiriki wa mdahalo huwa: mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi pamoja na wasikilizaji washiriki.*

*3. Mdahalo huhusisha mazungumzo.*

*4. Mdahalo huhusisha mada maalumu aghalabu inayohusu jamii.*

Wanafunzi wanaweza kurejelea mdahalo waliosoma na kuchunguza iwapo unadhihirisha sifa za mjadala walizojadiliana. Baadaye, mwalimu aombe kila kundi la wanafunzi lijitokeze mbele ya darasa na kuwaeleza wenzao matokeo ya majadiliano yake. Katika hatua hii, mwalimu arekebishe makosa ya kimatamshi pindi yanapotokea.

Katika zoezi la 2, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wasikilize mdahalo uliorekodiwa na kujibu maswali yafuatayo:

a) Sifa za mdahalo waliousikiliza darasani.

b) Waeleze mada ya mdahalo huo.

ch) Wajadili hoja zilizotolewa na wapinzani katika mdahalo huo.

d) Wajadili hoja zilizotolewa na watetezi katika mdahalo huo.

Mwalimu azunguke darasani na kutoa maelezo pale yanapotakiwa ili kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

## Tathmini ya vipindi 7-9

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kwa kurejelea sifa bainifu walizojifundisha kuhusu mdahalo huku wakirejelea wahusika wanaopatika katika mdahalo na majukumu yao katika kuendeleza mazungumzo yao.

## Vipindi 10-12: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kuigiza mdahalo husika;
- Kuongoza mdahalo;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mdahalo;

**b) Vifaa vya kujifunzia**

- Wanafunzi wenyewe;
- Mdahalo uliorekodiwa;
- Michoro na picha za wasemaji, mwenyekiti, katibu na wasikilizaji katika mdahalo;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 137;
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji ujifunzaji na uangalifu maalum.

**ch) Maandalizi ya somo**

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mdahalo ulioandaliwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuigiza mdahalo waliopewa kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 132-135. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kushiriki katika mdahalo kupitia kwa wahusika wote wanaohusika ili mwanafunzi apate picha kamili ya mdahalo mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kuigiza mdahalo waliopewa katika makundi yao.

**d) Utaratibu wa somo**

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie midahalo aliyoandaa kutanguliza funzo hili.

## 16.4 Kusikiliza na kuzungumza: Mdahalo

Sehemu hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kushiriki katika mdahalo husika kupitia kwa maigizo.

Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watano watano ili waweze kuigiza mdahalo waliosoma kuhusu athari za mavazi ya kisasa.

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao ambapo kila kundi litapewa muda wa kuigiza mdahalo husika. Kila kundi litateua mwenyekiti, katibu wa mdahalo, mtetezi na mpinzani na wanafunzi wengine watakuwa wasikilizaji. Ili kufanikisha maigizo ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaongoze waelewe utaratibu unaozingatiwa katika maandalizi na utekelezaji wa mdahalo.

Wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa, wapange viti kwa njia inayorahisisha mazungumzo yao halafu mwenyekiti afungue mdahalo na aongoze mazungumzo kwa kuzingatia muda uliopendekezwa kwa kila kundi. Wanafunzi wengine wafuate mazungumzo ya wenzao kwa kuandika kasoro na mafanikio yanayojitokeza katika mazungumzo yao. Hivyo basi, kila kundi la wanafunzi lizungumze na mwishoni wenzao wapewe muda wa kutoa mchango wao kuhusu jinsi ambavyo mdahalo huo ulivyoendelea. Mwalimu naye achukue muda wake kwa kusahihisha makosa ya wanafunzi pindi yanapotokea na awapongeze pale wanapofanikiwa huku akiomba makundi mengine kuwaiga wenzao na kusahihisha makosa waliyofanya ili wafanye mdahalo mzuri zaidi kuliko kundi lililotangulia.

Vilevile, mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi na achunguze iwapo wanafunzi wanatunga sentensi kamili zisizo na makosa ya kisarufi ili wapate uwezo wa kuwasiliana katika lugha fasaha.

## Tathmini ya vipindi 10-12

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kuongoza midahalo, kushiriki katika midahalo pamoja na kutoa hoja za aidha kupinga au kuunga mkono mada mbalimbali.

## Vipindi 13-16: Sarufi (Maana ya nomino)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua maana ya nomino;
- Kutumia nomino kutunga sentensi sahihi kisarufi;
- Kuunda nomino kutokana na vitenzi, vivumishi na nomino nyingine.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 137;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ambayo itawawezesha wanafunzi kutambua maana ya nomino ya Kiswahili. Mwalimu anaweza kuandika mifano kadha ya nomino mbalimbali za Kiswahili ambazo atawapa wanafunzi katika makundi yao ili wazijadili na kuziainisha katika kategoria zao.

## d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu aina za nomino wanazofahamu ambazo hutumika kuunda sentensi katika Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa. Wanafunzi wajikumbushe kuhusu aina mbalimbali za nomino wanazofahamu kwa mfano: *nomino za pekee, nomino za kawaida, nomino za wingi, nomino za dhahania* n.k.

## 16.5 Uundaji wa nomino

Katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wajaribu kuunda nomino kutokana na maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa kwenye vitabu vyao. Baada ya kuunda nomino hizo, wazitumie kutunga sentensi sahihi kisarufi.

**Kwa mfano:** *Mwalimu mkuu alimsamehe mwanafunzi aliyekuwa amekosa.*

Nomino zinazoweza kuundwa kutokana na kitenzi '*samehe*' ni *'msamaha'* na *'kusamehe'*.

Mfano wa sentensi yenye kutumia nomino hizi ni:

a) *Sisi sote tulipata **msamaha** kutoka kwa Mwenyezi Mungu.*

b) ***Kusamehe** kwa makosa yake kulimpa amani moyoni.*

Wanafunzi katika makundi yao waunde nomino kutokana na maneno waliyopewa kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia nomino hizo kama walivyoelekezwa na mwalimu. Mwalimu azunguke darasani kuwasadia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Baada ya hapa, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutambua kuwa nomino zinaweza kuundwa kutokana na maneno kama vile: vitenzi, vivumishi na hata nomino nyingine. Uundaji wa nomino huhusisha kuongeza viambishi awali na viambishi tamati kwenye mizizi ya maneno hayo.

***Kwa mfano:***

i) Kuunda nomino kutokana na vitenzi:

| **Kitenzi** | **Nomino** |
|---|---|
| samehe | msamaha, kusamehe |
| cheza | mchezo, kucheza, mchezaji, uchezaji |

ii) Kuunda nomino kutokana na vivumishi:

| **Kivumishi** | **Nomino** |
|---|---|
| -rembo | urembo |
| Safi | usafi |

iii) Kuunda nomino kutokana na nomino nyingine:

| **Nomino** | **Nomino** |
|---|---|
| mwandishi | kuandika, maandishi, andiko |
| chakula | mlo, kula, ulaji |

Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 ambapo wanahitajika kuunda nomino kutokana na maneno waliyopewa. Wanafunzi wajibu zoezi hilo na mwalimu awaombe wachunguze maelezo muhimu yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi ili wapate kuelewa zaidi kuhusu uundaji wa nomino kutokana na maneno mengine. Baada ya wanafunzi kukamilisha zoezi hili, mwalimu awaongoze katika kulisahihisha kwa pamoja huku akiwashirikisha wanafunzi wote kutambua makosa ya wenzao na kuyasahihisha.

## Tathmini ya vipindi 13-16

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kubainisha iwapo wanafunzi wamepata uelewa wa kutosha kuhusu uundaji wa nomino kutokana na vitenzi, vivumishi na nomino nyingine.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mitazamo tofauti huitwa ***mdahalo***.

- Mtazamo wa kwanza hutoa hoja zinazotetea au kuunga mkono wazo kuu.
- Mtazamo wa pili hutoa hoja za kupinga au kukataa wazo kuu.

Washiriki wa mdahalo huwa: mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi pamoja na wasikilizaji washiriki.

- Baadhi ya sifa za mdahalo ni: *huwa ni mazungumzo, huhusisha mitazamo miwili, huhusu mada maalum, mada yenyewe huhusu jamii* n.k.

Neno linalotaja mtu, kitu, jambo, hali au mahali huitwa ***nomino***.

### *Aina za nomino:*

1. Nomino za kawaida. Mifano: *mpira, kalamu, chakula* n.k.
2. Nomino za pekee. Mifano: *Mutoni, Jumapili, Kigali, Kiswahili* n.k.
3. Nomino za dhahania. Mifano: *uvivu, njaa, upendo, amani* n.k.
4. Nomino za jamii. Mifano: *thurea, baraza, tita, umati, bunda* n.k.
5. Nomino za wingi. Mifano: *maji, mafuta, marashi, maziwa* n.k.
6. Nomino za vitenzi-jina. Mifano: *kuimba, kula, kucheza, kuandika* n.k.

Uzalishaji wa maneno mapya kutokana na mizizi ya maneno mengine huitwa ***uundaji wa maneno***.

Nomino zinaweza kuundwa kutokana na mizizi ya vitenzi, vivumishi na nomino nyingine.

### *Kwa mfano:*

| | | |
|---|---|---|
| i) | **Kitenzi** | **Nomino** |
| | soma | somo, msomi, msomaji, kusoma |
| ii) | **Kivumishi** | **Nomino** |
| | mfupi | ufupi |
| iii) | **Nomino** | **Nomino** |
| | mtoto | utoto, toto, kitoto |

**FAHAMU:** Nomino huundwa kutokana na maneno mengine kwa kuongeza viambishi awali au viambishi tamati kwenye mzizi wa neno linalounda.

## 16.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waunde nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo.

**Kwa mfano:** osha

**Jibu:** kuosha, mwosho, uoshaji

1. jenga
2. lia
3. tazama
4. iba
5. okoa

### Majibu ya zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini nomino ambazo wanafunzi watatunda kutokana na vitenzi walivyopewa.

1. kujenga, majengo, jengo, mjenzi
2. kulia, kilio, mlizi, mliaji
3. kutazama, mtazamo, mtazamaji
4. kuiba, mwizi, wizi
5. kuokoa, mwokozi, mwokoaji, wokovu, uokoaji

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waunde nomino kutokana na nomino zifuatazo.

**Kwa mfano:** mlo

**Jibu:** chakula, mlaji, ulaji, mlafi

1. mtu
2. mfu
3. mrithi

4. mwandishi
5. mchoraji

**Majibu ya zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka**

Mwalimu atathmini nomino ambazo wanafunzi wataunda kutokana na nomino walizopewa.

1. watu, utu, kitu, jitu, kijitu
2. wafu, kifo
3. mrithiwa, urithi
4. mwandiko, kuandika, uandishi, maandishi
5. mchoro, kuchora, uchoraji

## 16.7 MAJIBU

**Maswali ya ufahamu 135**

1. *Shetani wa mtu ni mtu*: ni sawa na adui wa binadamu ni binadamu mwenzake. Methali hii inamaanisha kuwa anayemtendea binadamu mabaya ni binadamu mwenzake.
2. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi.
3. Uzinifu hupoteza utamaduni wa watu na umewafanya wasichana wadogo kujiingiza katika maisha ya kushiriki ngono wakiwa wachanga.
4. Uzinzi na uasherati ni tabia ya kupenda sana kufanya ngono.
5. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi.
6. Yamechangia katika uzinifu kwa kuwa wasichana wadogo wanazini na akina baba waliokomaa.
7. Serikali kupiga marufuku mavazi hayo ya kisasa.
8. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi.
9. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi. Kwa mfano: *utumiaji wa dawa za kulevya, shinikizo kutoka kwa marika, umaskini* n.k.
10. Mdahalo ni mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi wenye mitazamo tofauti kuhusu jambo fulani wanalozungumzia.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 135**

Mwalimu atathmini maelezo ambayo wanafunzi watatoa kuhusu msamiati uliotumika. **Kwa mfano:**

1. ***Uzinifu -*** tabia ya kupenda sana kufanya ngono
2. ***Mdahalo -*** mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi wenye mitazamo tofauti kuhusu jambo fulani wanalozungumzia

**Zoezi la 1, ukurasa 136**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati. Sharti uwe sahihi. Pia atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga.

***Kwa mfano:***

1. ***mdahalo -*** mazungumzo au majadiliano kati ya watu wengi wenye mitazamo tofauti kuhusu jambo fulani wanalozungumzia
2. ***uzinifu -*** tabia ya kupenda sana kufanya ngono
3. a) ***wapinzani -*** watu wanaopinga jambo fulani au maoni fulani

   b) ***hoja -*** maelezo ya kupinga au kuunga mkono jambo lililokwisha kusemwa
4. ***kikwazo -*** pingamizi, kizingiti au kizuizi cha mafanikio au utekelezaji wa jambo fulani
5. ***maadili -*** tabia njema na zinazokubalika katika jamii
6. ***sampuli -*** muundo wa kitu
7. ***sugu -*** -enye tabia isiyoweza kubadilika kwa urahisi
8. ***vibiritingoma -*** wanawake malaya
9. ***uasherati -*** tabia ya kupenda sana kufanya ngono
10. ***ushawishi -*** hali ya mtu kuvutika kutenda jambo fulani

**Matumizi katika sentensi:**

1. Leo tutakuwa na ***mdahalo*** kuhusu athari za teknolojia ya kisasa.
2. Watu wawili walihukumiwa kwa ***uzinifu***.
3. Katika mdahalo wa jana, upande wa ***wapinzani*** ulikuwa na ***hoja*** nyingi.

4. Uvivu ni ***kikwazo*** cha maendeleo.
5. Mwanafunzi mwenye ***maadili*** mema sharti atuzwe.
6. Sijawahi kuona mavazi ***sampuli*** hii.
7. Jambazi ***sugu*** alifyatuliwa risasi tatu.
8. Yusufu alionekana akizungumza na ***vibiritingoma*** kando ya mkahawa.
9. Mungu hapendi ***uasherati***.
10. Nilivutiwa na ***ushawishi*** wa mwenyekiti wa kampuni hii.

**Zoezi la 2, ukurasa 137**

Mwalimu aandae kanda yenye mdahalo uliorekodiwa kisha awape wanafunzi fursa ya kuisikiliza. Baada ya wanafunzi kuisikiliza kanda hiyo, awape fursa ya kujibu maswali yaliyo kwenye vitabu vyao katika makundi yao ya wanafunzi watatu watatu.

**Zoezi la sarufi, ukurasa 137-138**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi, kwa mfano:

1. Maneno '*ng'ombe*' na '*nyasi*' ni nomino za kawaida.
2. Maneno '*Akimana*' na '*Kiswahili*' ni nomino za pekee.
3. Neno '*Jumapili*' ni nomino ya pekee.
4. Neno '*kitanda*' ni nomino ya kawaida.
5. Neno '*kucheza*' ni nomino ya kitenzi jina na neno '*mwanafunzi*' ni nomino ya kawaida.
6. Neno '*nguo*' ni nomino ya kawaida.
7. Neno '*kikombe*' ni nomino ya kawaida.
8. Neno '*maziwa*' ni nomino ya wingi na neno '*wageni*' ni nomino ya kawaida (wingi).
9. Neno '*unga*' ni nomino ya wingi.
10. Neno '*duka*' ni nomino ya kawaida.

**Zoezi la 3, ukurasa 138**

Mwalimu atathmini namna wanafunzi watakavyoziainisha nomino na kuzitolea mifano.

***Kwa mfano:***

1. ***Nomino za jamii -*** hutaja vitu au watu katika makundi. Mifano: *umati, tita, furushi* n.k.
2. ***Nomino dhahania -*** hizi ni nomino ambazo hutaja vitu vya kufikirika tu. Mifano: *wema, uchovu, upendo* n.k.
3. ***Nomino za wingi -*** huonyesha nomino ambazo hupatikana katika wingi pekee. Mifano: *maji, maziwa, marashi* n.k.
4. ***Nomino za pekee -*** hizi hutaja mtu, kitu au mahali maalumu. Mifano: *majina ya watu, majina ya miji, majina ya mito, majina ya lugha mbalimbali, majina ya siku za wiki, miezi* n.k.
5. ***Nomino za kawaida -*** hujumuisha nomino za makundi ambayo hayabainiki waziwazi. Mifano: *kiti, kikombe, mpira* n.k.

**Zoezi la 4, ukurasa 138**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi.

**Kwa mfano:**

i) Sentensi zenye nomino dhahania:

1. ***Upendo*** wake kwa mamake ni wa dhati.
2. Nililala mapema kwa sababu ya ***uchovu*** mwingi.

ii) Sentensi zenye nomino za wingi:

3. ***Marashi*** yangu yameisha.
4. Yachemshe ***maziwa*** ya mtoto.

**Zoezi la sarufi, ukurasa 138-139**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi, kwa mfano:

1. Kutokana na kitenzi ‘*tubu*’ tunaweza kuunda nomino ‘*toba*’ na ‘*kutubu*’.

***Mfano wa sentensi:*** *Padri alikubali toba ya mfuasi wake.*

2. Kutokana na kitenzi '*jadili*' tunaweza kuunda nomino '*majadiliano*' na '*kujadili*'.

***Mfano wa sentensi:*** *Majadiliano ya wanafunzi yalihusu utamaduni wao.*

3. Kutokana na kitenzi '*tisha*' tunaweza kuunda nomino '*tisho*' na '*kutisha*'.

***Mfano wa sentensi:*** *Kutisha kwa sinema ile kulimfanya mtoto alie.*

4. Kutokana na nomino '*mrithi*' tunaweza kuunda nomino 'u*rithi*' na '*kurithi*'.

***Mfano wa sentensi:*** *Kaka yangu alipata urithi kutoka kwa baba yetu.*

5. Kutokana na kivumishi '*mrefu*' tunaweza kuunda nomino '*urefu*'.

***Mfano wa sentensi:*** *Urefu wa jumba lile ulishangaza.*

**Zoezi la 5, ukurasa 140**

1. Werevu

   ***Werevu*** wa Neza umemfikisha chuo kikuu.

2. Ufagio, mfagizi

   ***Ufagio*** wa ***mfagizi*** umepotea.

3. Mchoro, mchoraji

   ***Mchoraji*** aliyeuchora ***mchoro*** wa msitu ametuzwa.

4. Ubaya

   Mbaya ataadhibiwa kwa ***ubaya*** wake.

5. Mpenzi, mapenzi

   ***Mpenzi*** wangu ana ***mapenzi*** tele.

## Somo la 17: Mwongozo wa kuandika mdahalo

## Vipindi 17-19: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi mfano wa mdahalo kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;

- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mdahalo;
- Kuandika hoja muhimu zilizotolewa katika mdahalo.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mdahalo uliorekodiwa,
- Michoro ya mwenyekiti na wasemaji wengine katika mdahalo;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 141;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu athari za rushwa kwa wananchi na nchi kwa jumla. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kufikiria kuhusu changamoto zinazojitokeza katika sekta mbalimbali hasa sekta ya usafiri. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kuongoza mdahalo na kushiriki katika midahalo mbalimbali kwa kutumia lugha rasmi na sahihi kisarufi.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na mdahalo walioshiriki. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi kupata ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

Baadaye, mwalimu awachangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali kadhaa kuhusiana na michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 141. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye michoro hii?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kwa kueleza kile wanachokiona katika michoro hiyo. Kwa mfano: *"Mimi ninaona dereva anayempa askari kitu fulani. Mimi ninaona basi lililoanguka* na kadhalika.

Katika sehemu hii, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanapata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro hiyo huku akiwataka kufikiria na kugundua kile kinachoendelea katika michoro hiyo. Vilevile, nafasi ya wanawake katika mazungumzo nayo igusiwe kupitia kwa michoro iliyotumika.

## 17.1 Kusoma na kufahamu: Mdahalo kuhusu athari za rushwa

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya mdahalo uliopo huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mdahalo waliosoma ili kuhakikisha kuwa wameusoma na kuuelewa. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: *Taja majina ya wasemaji waliopo katika mazungumzo haya.* Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika mdahalo huo. Kwa mfano: *Wasemaji wanaopatikana katika mazungumzo haya ni Kawera, Bagirimana, Mukandayisenga na Birasa*. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wanashirikishwa katika shughuli hii.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuyajibu maswali ya ufahamu waliyopewa ambayo yatasahihishwa kwa pamoja darasani. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wanaopata matatizo katika makundi yao.

## Tathmini ya vipindi 17-19

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutokana na mdahalo waliousoma.

# Vipindi 20-22: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati unaotumika katika mdahalo;
- Kutaja majina ya watu wapatikanao katika mdahalo;
- Kutumia msamiati wa mdahalo katika sentensi sahihi.

**b) Vifaa vya kujifunza**

- Mdahalo uliorekodiwa;
- Michoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mdahalo;
- Wanafunzi wenyewe;
- Kamusi ya Kiswahili;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 144;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

**ch) Maandalizi ya somo**

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu msamiati unaohusiana na athari za rushwa na kuendeleza maisha mazuri ya wanajamii. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kuelewa maana ya msamiati unaohusiana na suala la ufisadi. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kuongoza mdahalo na kushiriki katika midahalo mbalimbali kwa kutumia lugha rasmi na sahihi kisarufi. Katika maandalizi ya somo lake, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta picha au michoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mdahalo ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi hasa wanafunzi wenye ulemavu au matatizo mbalimbali.

**d) Utaratibu wa somo**

***Utangulizi***

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na mdahalo kuhusu athari za mavazi ya kisasa na namna ya kuendeleza maisha mazuri ya wanajamii mbalimbali. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilolipewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi wapate ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

## 17.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na mdahalo husika

Baadaye, mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi watatu

watatu na awaombe watafute maana za msamiati mpya waliopatana nao katika mdahalo waliosoma. Ni vyema mwalimu awakumbushe wanafunzi wachunguze matumizi ya msamiati huo katika mdahalo waliosoma na kutumia kamusi pale inapohitajika. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 1. Wanafunzi wafafanue msamiati huo kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu awakumbushe wanafunzi wachunguze matumizi ya maneno hayo katika mdahalo waliosoma na watumie kamusi pale inapohitajika ili kukamilisha zoezi hilo. Aidha, mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Katika kufanikisha uelewa wa wanafunzi katika zoezi hili, mwalimu awaombe walisahihishe kwa pamoja huku akihakikisha kwamba utunzi wa sentensi zao umezingatia amani na maadili, usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, elimu kuhusu fedha; mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo na utamaduni wa kiusanifishaji.

## Tathmini ya vipindi 20-22

Katika hatua hii ya tathmini, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kutokana na mdahalo waliosoma huku wakirejelea wahusika wanaopatikana katika mazungumzo ya aina ya mdahalo na majukumu yao katika kuendeleza mazungumzo hayo.

## Vipindi 23-25: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili mwongozo wa kutunga mdahalo;
- Kutaja majina ya watu wapatikanao katika mdahalo;
- Kutambua msamiati unaohusiana na mdahalo.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha mwongozo wa kutunga mdahalo;
- Michoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mdahalo;

- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 145;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi zaidi kuhusu mwongozo wa kutunga mdahalo kwa kurejelea mdahalo waliousoma kuhusu athari za rushwa. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kumwezesha mwanafunzi kutunga mdahalo kwa kuzingatia mwongozo sahihi na kamili.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na msamiati wa mdahalo. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilolipewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi wapate ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

## 17.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Mwalimu azingatie kwamba katika hatua hii ya matumizi ya lugha ndipo anatakiwa kuwaelekeza wanafunzi kupata ujuzi unaotakikana kuhusu mwongozo wa kutunga mdahalo. Hivyo basi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuchunguza maelekezo yaliyotolewa katika sehemu hii ili waweze kugundua namna ya kutunga mdahalo kwa kuzingatia taratibu zifaazo. Wanafunzi wajadiliane katika makundi yao naye mwalimu azunguke kuwasaidia wanaotatizika katika makundi yao. Baadhi ya taratibu za kuzingatia katika utungaji wa mdahalo ni:

1. *Kuwepo kwa mada ya kujadiliwa*
2. *Kuwepo kwa pande mbili za majadiliano (upande wa utetezi na upande wa upinzani)*
3. *Mazungumzo yashamiri.*

4. *Hoja zihusishwe.*
5. *Kuwepo kwa wahusika kama vile: mwenyekiti, watetezi, katibu, wapinzani na wasikilizaji.*

Baadaye, kila kundi lipewe muda wa kuwasilisha matokeo ya majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao. Mwalimu ahakikishe kuwa anakosoa makosa ya kimatamshi wakati wa mawasilisho haya. Zoezi hili litawawezesha wanafunzi kupata ujasiri wa kusimama na kuzungumza mbele ya watu pamoja na kuzungumza kwa lugha sahihi na rasmi.

## Tathmini ya vipindi 23-25

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea taratibu za kutunga mdahalo walizowasilisha darasani. Wanafunzi waelekezwe kubaini nafasi ya mwenyekiti na wazungumzaji wengine wakati wa kuendeleza mdahalo na hata wabainishe mienendo mizuri inayotakikana katika mazingira ya mazungumzo ya mdahalo.

## Vipindi 26-28: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kuandaa mdahalo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mdahalo;
- Kuandika hoja muhimu zilizotolewa katika mdahalo;
- Kueleza majukumu ya wahusika wa mdahalo.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Mdahalo uliorekodiwa;
- Michoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mdahalo;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 145;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mdahalo ulioandaliwa au uliorekodiwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mada ya mdahalo waliopewa kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 145. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kutunga mdahalo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia. Kupitia kwa wahusika wote wanaohusika katika mdahalo, wanafunzi wapate picha kamili ya mdahalo mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili kama vilivyotajwa hapo juu ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi katika kutunga mdahalo waliopewa katika makundi yao.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie midahalo aliyoandaa kutanguliza funzo hili.

## 17.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga mdahalo

Katika hatua hii, ni muhimu mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni yake kuhusu mada mbalimbali na kuzungumza na wengine kwa kutetea hoja zake ili aweze kuungwa mkono. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watano watano ili waweze kuandaa mdahalo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na hapo baadaye kuuwasilisha mbele ya wanafunzi wenzao.

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao ambapo kila kundi litapewa muda wa kujadiliana kuhusu mada waliyopewa na kuandika hoja zao. Kila kundi likumbuke kuteua mwenyekiti na wasemaji wengine.

Ili kufanikisha mazungumzo ya wanafunzi katika makundi yao, ni vyema mwalimu awakumbushe utaratibu wa kutunga mdahalo.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa, wapange

viti kwa njia inayorahisisha mazungumzo yao halafu mwenyekiti afungue mdahalo na aongoze mazungumzo kwa kuzingatia muda uliopangwa. Wanafunzi wengine wafuate mazungumzo ya wenzao kwa kuandika kasoro na mafanikio yanayojitokeza katika mazungumzo yao ili, baadaye, waweze kutoa mchango wao kwa kuboresha mazungumzo yao katika midahalo mingine.

Mwalimu achunguze jinsi wanafunzi wanavyojadiliana na awaelekeze kutambua kasoro zilizopo huku akisahihisha matamshi ya wanafunzi na kuwasaidia kutunga sentensi kamili kwa kuchochea uwezo wao wa ubunifu na ugunduzi, tafakuri tanduizi na kudumisha uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi.

## Tathmini ya vipindi 26-28

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika sehemu hii ya kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kuongoza midahalo, kushiriki katika midahalo pamoja na kutoa hoja za kujenga mada katika mdahalo.

## Vipindi 29-32: Sarufi (Maana ya kivumishi)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua maana ya kivumishi;
- Kutaja mifano ya vivumishi mbalimbali;
- Kuunda vivumishi kutokana na maneno mengine.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 145;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ambayo itawawezesha wanafunzi kutambua maana ya kivumishi katika lugha ya Kiswahili. Mwalimu anaweza

kuandika mifano kadha ya vivumishi mbalimbali vya Kiswahili ambavyo atawapa wanafunzi katika makundi yao ili wavijadili.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu maneno mbalimbali ya Kiswahili ambapo miongoni mwa maneno hayo kuna vivumishi. Maneno haya mbalimbali ndiyo hutumika kuunda sentensi katika Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

## 17.5 Maana ya kivumishi pamoja na uundaji wake

Katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wawili wawili kisha wajaribu kueleza sifa za wenzao kwa kuzingatia wanavyoonekana au vitu walivyo navyo. Kwa mfano: *kuwa mrefu, kuwa mfupi, kuwa mrembo, kuwa na macho mazuri, kuwa na mkoba mwekundu, kuwa na viatu vipya* n.k. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kueleza majadiliano yao kuhsu wanavyoonekana wenzao au vitu vyao.

**Kwa mfano:** *Mutoni ana* ***macho mazuri*** *na* ***saa mpya***.

Kutokana na sentensi ambazo wanafunzi watatunga, mwalimu awaongoze kufahamu kuwa maneno waliyotumia kuelezea zaidi kuhusu nomino walizotaja (***mazuri, mpya***) yanaitwa ***vivumishi***.

Mifano zaidi ya sentensi:

*a) Mukandayisenga ana mkoba* ***mweusi*** *wa kubeba vitabu.*

*b) Kalisa ana sauti* ***nzuri*** *na ngozi* ***nyororo***.

*ch) Ngabo ana nywele* ***nyingi*** *na sare* ***safi***.

Wanafunzi waelekezwe kutambua aina mbalimbali za vivumishi kama vile:

1. Vivumishi vya sifa. Mifano: *-zuri, -ekundu, -baya, -refu* n.k.
2. Vivumishi vionyeshi/viashiria. Mifano: *huyu, huyo, hiki, lile, hapo* n.k.
3. Vivumishi vimilikishi. Mifano: *wangu, chako, lake, petu, zako* n.k.
4. Vivumishi vya idadi. Mifano: *wawili, vichache, kumi, wengi* n.k.

5. Vivumishi viulizi. Mifano: *gani, ngapi, yupi, upi* n.k.

6. Vivumishi vya pekee. Mifano: *-enyewe, -enye, -ingine, -ote* n.k.

Baada ya haya, wanafunzi katika makundi yao washirikishwe kuunda vivumishi kutokana na maneno mengine kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vivumishi hivyo kama walivyoelekezwa na mwalimu. Mwalimu azunguke darasani kuwasadia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Baada ya hapa, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutambua kuwa vivumishi vinaweza kuundwa kutokana na maneno kama vile: vitenzi na nomino. Uundaji wa vivumishi huhusisha kuongeza viambishi awali na viambishi tamati kwenye mizizi ya maneno husika.

***Kwa mfano:***

i) Kuunda vivumishi kutokana na vitenzi:

| **Kitenzi** | **Kivumishi** |
|---|---|
| cheka | mcheshi |
| remba | mrembo |
| saliti | msaliti |

ii) Kuunda vivumishi kutokana na nomino:

| **Nomino** | **Kivumishi** |
|---|---|
| ubaya | mbaya |
| urefu | mrefu |
| wembamba | mwembamba |

Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la 5 ambapo wanahitajika kuunda vivumishi kutokana na maneno waliyopewa. Wanafunzi wajibu zoezi hilo na mwalimu awaombe wachunguze maelezo muhimu yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi ili wapate kuelewa zaidi kuhusu uundaji wa vivumishi kutokana na maneno mengine. Baada ya wanafunzi kukamilisha zoezi hili, mwalimu awaongoze katika kulisahihisha kwa pamoja huku akiwashirikisha wanafunzi wote kutambua makosa ya wenzao na kuyasahihisha.

## Tathmini ya vipindi 29-32

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa

wanafunzi wa kubainisha iwapo wamepata uelewa wa kutosha kuhusu uundaji wa vivumishi kutokana na vitenzi na nomino.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

Mwalimu awaelekeze wanafunzi kutambua:

- **Aina za vivumishi:**

1. Vivumishi vya sifa. Mifano: *-zuri, -ekundu, -baya, -refu* n.k.
2. Vivumishi vionyeshi/viashiria. Mifano: *huyu, huyo, hiki, lile, hapo* n.k.
3. Vivumishi vimilikishi. Mifano: *wangu, chako, lake, petu, zako* n.k.
4. Vivumishi vya idadi. Mifano: *wawili, vichache, kumi, wengi* n.k.
5. Vivumishi viulizi. Mifano: *gani, ngapi, yupi, upi* n.k.
6. Vivumishi vya pekee. Mifano: *-enyewe, -enye, -ingine, -ote* n.k.

- Vivumishi vinaweza kuundwa kutokana na mizizi ya vitenzi na nomino.

***Kwa mfano:***

| | | |
|---|---|---|
| i) | Kitenzi | Kivumishi |
| | tukuka | mtukufu |
| ii) | **Nomino** | **Kivumishi** |
| | Ukubwa | mkubwa, kikubwa, kubwa n.k. |

**FAHAMU:** Kivumishi huundwa kutokana na maneno mengine kwa

## 17.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waunde vivumishi kutokana na vitenzi watakavyoteua kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vivumishi hivyo.

**Kwa mfano:** tukuka (*kitenzi*) – mtukufu (*kivumishi*)

**Matumizi katika sentensi:** Kiongozi ***mtukufu*** alihutubia wananchi wakafurahi.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini vivumishi ambavyo wanafunzi wataunda kutokana na vitenzi mbalimbali na kisha kuvitungia vivumishi hivyo sentensi sahihi. Sharti sentensi hizi ziwe sahihi kisarufi.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waunde vivumishi kutokana na nomino watakazoteua kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vivumishi hivyo.

**Kwa mfano:** ujinga (*nomino*) – mjinga (*kivumishi*)

**Matumizi katika sentensi:** Mwanafunzi ***mjinga*** amebadilika na kufaulu kwa kutia bidii.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mwalimu atathmini vivumishi ambavyo wanafunzi wataunda kutokana na nomino mbalimbali na kisha kuvitungia vivumishi hivyo sentensi sahihi. Sharti sentensi hizi ziwe sahihi kisarufi.

## 17.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 143

1. Mwenyekiti, Kawera, Bagirimana, Mukandayisenga, Birasa, mabibi na mabwana.
2. Ni chanzo cha siasa mbovu, hurudisha maendeleo ya taifa nyuma, hucheleweshа kutolewa kwa huduma au huduma hizo kukosa kutolewa kabisa.
3. Kwa sababu ya kupewa hongo.
4. Ili kupata huduma fulani kwa haraka kama vil*e:* kupata nafasi katika shule fulani au kuamuliwa kwa kesi bila kuzingatia haki.

5. Kamera zimewekwa barabarani ili kunasa na kurekodi matukio yote barabarani, wafanyakazi na viongozi katika vitengo balimbali wameelimishwa kuhusu athari za ufisadi na adhabu anayoweza kupata mtu yeyote atakayejiingiza katika shughuli za kiufisadi.
6. Rwanda imeorodheshwa miongoni mwa nchi zenye visa vichache mno vya ufisadi, serikali imejitolea kupigana na ufisadi hasa katika vitengo ambavyo ufisadi umeripotiwa. Kwa mfano: katika uchukuzi, kamera zimewekwa barabarani ili kunasa na kurekodi matukio yote barabarani. Wafanyakazi na viongozi katika vitengo mbalimbali wameelimishwa kuhusu athari za ufisadi na adhabu anayoweza kupata mtu yeyote atakayejiingiza katika shughuli za kiufisadi. Kumekuwa na kampeni kwenye redio ili kuwaomba wananchi wawe huru kuripoti visa vyovyote vya ufisadi kupitia kwa nambari za simu pamoja na anwani za baruapepe.
7. Ufisadi umekithiri yaani, umezidi.
8. Hongo, chai na kitu kidogo.
9. Kwa kutoshiriki katika shughuli zozote za kiufisadi kama vile kutoa au kupokea hongo.
10. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 144**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati waliopatana nao katika usomaji wao.

***Kwa mfano:***

1. ***Rushwa -*** pesa au kitu chochote cha thamani anachopatiwa mtu mwenye uwezo au madaraka katika jambo fulani ili amfanyie mtoaji hisani au upendeleo
2. ***Watetezi -***wanaotetea au wanaounga mkono jambo fulani

**Zoezi la 1, ukurasa 144**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati husika. Pia atathmini sentensi watakazotunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***hongo -*** pesa au kitu chochote cha thamani anachopatiwa mtu mwenye uwezo au madaraka katika jambo fulani ili amfanyie mtoaji hisani au upendeleo
2. ***waadilifu -*** wenye maadili mema au tabia zinazokubalika katika jamii
3. ***hazina -*** idara ya serikali ambapo shughuli zinazohusiana na fedha za serikali huendeshwa
4. ***huwapora -*** huwaibia
5. ***ubinafsi -*** tabia ya mtu kujali maslahi yake pekee na kuyapuuza ya wengine
6. ***takwimu -*** maelezo ya kihesabu yanayotumiwa kufafanua na kulinganisha ukweli wa matukio au jambo fulani
7. ***ufisadi -*** utumiaji mbaya wa mali ya umma, serikali, chama au shirika; tabia ya ubadhirifu
8. ***mikakati -*** mipango
9. ***asasi -*** shirika la kutoa huduma kama vile elimu au matibabu
10. ***huhodhi -*** hukusanya

**Matumizi katika sentensi:**

1. Abiria waliotoa ***hongo*** barabarani walinaswa na kamera za wizara ya uchukuzi.
2. Viongozi ***waadilifu*** hutenda kazi yao vyema.
3. Pesa za kuanzisha mradi wa kutoa chanjo kwa mifugo zitatolewa kwenye ***hazina*** ya serikali.
4. Wezi ambao ***huwapora*** wapitanjia wamekamatwa leo.
5. Gatete ana ***ubinafsi*** mwingi. Yeye alijinunulia jumba kubwa na akawaacha wazazi wake katika hali ya umaskini.
6. Kulingana na ***takwimu*** za hivi punde, wananchi wengi huhudhuria mikutano ya kisiasa.
7. Kuwapa jamaa zako pekee kazi na kuwaache watu wengine bila kazi ni ***ufisadi*** wa hali ya juu.
8. Mkuu wa mkoa amehakikisha kuwa kuna ***mikakati*** ya kuboresha elimu katika mkoa wake.

9. Huduma za elimu na matibabu hutolewa na ***asasi*** ya kijamii.
10. Baada ya wanasiasa kupata vyeo vyao, wao ***huhodhi*** kila kitu kilichotengewa wananchi.

**Zoezi la matumizi ya lugha, ukurasa 145**

Mwalimu atathmini namna wanafunzi watashiriki katika majadiliano kuhusu mwongozo wa kutunga mdahalo. Wanaweza kutaja mambo kama vile:

1. Kuwe na mada ya mdahalo.
2. Kuwe na pande mbili za mdahalo. Yaani, upande wa watetezi wa mada na upande wa wapinzani wa mada.
3. Mwenyekiti wa kuongoza mjadala sharti awepo n.k.

**Zoezi la 2, ukurasa 145**

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi yao ya uigizaji kisha awape fursa ya kuigiza mdahalo waliosoma na atathmini uigizaji wao.

**Zoezi la sarufi (Maana ya kivumishi), ukurasa 145**

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kueleza sifa za wanafunzi wenzao kama vile: *kuwa mrefu, mwembamba, mnene, mfupi, mkarimu, mchafu, mpole* n.k.

Wanafunzi wafahamishwe kuwa sifa hizo ndizo huunda ***vivumishi vya sifa***.

**Zoezi la 3, ukurasa 146**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi.

***Kwa mfano:***

1. Vivumishi vya idadi kamili: *moja, sita, saba, nane* n.k
   a) *Mukamunana alinunuliwa vitabu* ***sita****.*
   b) *Nitatumia kalamu* ***sita*** *muhula huu.*
2. Vivumishi vya idadi isiyo kamili: *chache, nyingi* n.k.
   a) *Niletee maji* ***machache*** *tu.*
   b) *Kurasa* ***nyingi*** *zimeraruliwa.*

3. Vivumishi vya sifa: *-fupi, -refu, -baya, -zuri* n.k.

   *a) Wanafunzi **wabaya** wamemwibia mwalimu.*

   *b) Nilipoteza rula **ndefu**.*

**Zoezi la utafiti, ukurasa 146**

Mwalimu atathmini majibu ya utafiti wa wanafunzi kuhusu aina mbalimbali za vivumishi.

**Zoezi la makundi, ukurasa 147-148**

A - 5

B - 4

CH - 2

D - 3

E - 1

**Zoezi la uundaji wa vivumishi, ukurasa 148 -149**

1. Nyumba ***ambayo*** mama aliiremba ilikuwa kwa ajili ya kupokea wageni.
2. Jumba ***refu*** linaogopesha.
3. Kwa nini una mtoto ***mwenye*** kulia.
4. Chumba ***kichafu*** hakikaliki.
5. Wewe ***mbaya*** umepoteza kazi.

**Zoezi la 4, ukurasa 149**

1. Mwerevu
   Mwanafunzi ***mwerevu*** ametuzwa.
2. Mcheshi
   Mwanasiasa ***mcheshi*** amewasili ukumbini.
3. –embamba
   Uzi ***mwembamba*** utatumika kushonea gunia.
4. –nene
   Watoto ***wanene*** wametibiwa.
5. –dogo
   Viti ***vidogo*** vitakaliwa na watoto.

## Somo la 18: Mjadala

## Vipindi 33-35: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi mfano wa mjadala kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kutaja majina ya watu ambao hushiriki katika mjadala;

### b) Vifaa vya kujifunza

- Mjadala uliorekodiwa;
- Michoro ya mwenyekiti na wasemaji wengine katika mdahalo;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 150;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili ni mwendelezo wa masomo mawili yaliyotangulia ambapo lengo kuu la mwalimu ni kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi katika kujadali, kutetea hadharani na kupanga hoja kwa kushawishi kuungwa mkono katika mada mbalimbali. Kwa hivyo, mwalimu aandae vifaa mbalimbali vinavyohitajika kama vilivyotajwa hapo juu ili kurahisisha ufundishaji wa somo hili.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi wake na kuwauliza maswali kuhusu somo lililopita. Wanafunzi wajibu maamkizi pamoja na maswali ya mwalimu. Mwalimu awaombe wanafunzi wasahihishe zoezi walilopewa katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wasahihishe zoezi hilo.

Baada ya shughuli hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili wajadiliane kuhusu kile kinachoendelea katika michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 150. Wanafunzi wachunguze michoro hiyo ili waelewe kinachoendelea au kinachoonekana katika michoro hiyo. Mwalimu azunguke darasani kuhakikisha kuwa wanafunzi wanajadiliana kama inavyotakikana.

### 18.1 Kusoma na kufahamu: Mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo

Katika hatua hii, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wasome kwa kimya mjadala waliopewa huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi wasome kwa kimya pamoja na kuandika msamiati huo mpya. Baadaye, mwalimu achunguze ikiwa wanafunzi wote wamesoma na kuelewa kama walivyoambiwa. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu mjadala waliosoma. Kwa mfano, anaweza kuuliza maswali yafuatayo: *Wazungumzaji katika mjadala huu walikuwa kina nani*? Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kuonyesha kuwa wamesoma mjadala huo na kuuelewa. Kwa mfano: *Wazungumzaji katika mjadala huu ni Birasa, mwenyekiti, Mugatara, Mutoni* na *uwase.*

Baada ya kupata picha ya uelewa wa jumla wa wanafunzi kuhusu mjadala waliosoma, mwalimu awachague wanafunzi kulingana na idadi ya wahusika waliopo katika mjadala husika na awaelekeze kusoma kwa njia ya maigizo na kwa kuzingatia matumizi ya alama za vituo vinavyopatikana katika mjadala huo. Ni vyema mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi pale wanapofanya makosa kwa lengo la kutambua herufi, silabi na sentensi zilizopo.

Hatimaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuyajibu maswali ya ufahamu waliyopewa na kuyasahihisha kwa pamoja darasani. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

## Tathmini

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kubainisha watu muhimu wanaohitajika katika mjadala na kudhihirisha majukumu yao katika kuendeleza mjadala.

Vilevile, mwalimu achunguze iwapo wanafunzi wanaweza kueleza utaratibu wa mjadala na mambo muhimu yanayozingatiwa ili mjadala uweze kufanyika kwa njia inayofaa.

## Vipindi 36-38: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati unaotumika katika mjadala husika;
- Kutaja majina ya watu wanaoshiriki katika mjadala;
- Kutumia msamiati wa mjadala husika katika sentensi.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Mdahalo uliorekodiwa;
- Michoro au picha za wasemaji na wasikilizaji katika mjadala;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 152;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa mjadala kupitia kwa wahusika wote wanaojitokeza katika mfano ulio kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 150-152 ili mwanafunzi apate picha kamili ya mjadala mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili kama vilivyotajwa hapo juu. Ikiwa kuna wanafunzi wasioweza kuona au kusikia, ni lazima mwalimu atafute namna ya kuwaelekeza kuelewa somo hili. Ni vyema pia mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wamejigawa katika makundi ya wanafunzi wanaotakikana kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwa kila shughuli ya wanafunzi iliyopendekezwa katika kitabu cha mwanafunzi.

## 18.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na mjadala husika

Katika hatua hii, mwalimu awagawe wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili waweze kujadiliana kuhusu msamiati mpya waliopatana nao katika usomaji wa mjadala husika. Mwalimu awaombe wazingatie matumizi yake katika mjadala waliosoma na watumie kamusi pale wanapoihitaji. Wanafunzi wajadiliane kama walivyoelekezwa naye mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi pale wanapotatizika. Hatimaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajibu maswali katika zoezi la 1 la msamiati ambapo wanahitajika kueleza maana ya msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia msamiati huo.

Wanafunzi watunge sentensi zao kwa kuzingatia jinsi maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa yalivyotumika katika mjadala waliosoma. Mwalimu azunguke darasani kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika na awashirikishe wanafunzi wote kusahihisha zoezi hilo mara moja wanapomaliza kujadiliana katika makundi yao. Hivyo basi, mwalimu aombe kila kundi liandike sentensi zao ubaoni na wanafunzi wengine wazichunguze na watoe mchango wao kuzikubali au kuzikataa na kuzisahihisha.

## Tathmini

Katika hatua hii, mwalimu ahitimishe kwa kuuliza maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Wanafunzi pia waulizwe maswali kuhusu msamiati unaohusiana na mijadala pamoja na shughuli zinazoonyesha umuhimu wa uzalendo kwa Wanyarwanda.

## Vipindi 39-41: Matumizi ya lugha

### a) Malengo ya somo

- Kujadili sifa bainifu za mjadala;
- Kutaja majina ya watu wanaoshiriki katika mjadala.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- Mjadala uliorekodiwa;

- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 153;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mjadala ulioandaliwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mjadala. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa mjadala kupitia kwa wahusika wote wanaojitokeza katika mfano waliopewa ili mwanafunzi apate picha kamili ya mjadala mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kushiriki katika mjadala watakaopewa katika makundi yao.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

Mwalimu atumie mjadala alioandaa kutanguliza funzo hili.

## 18.3 Matumizi ya lugha: Sifa bainifu za mjadala

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wanne wanne wajadiliane kuhusu: *sifa bainifu za mjadala*.

Mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kujadili kuhusiana na sifa za mjadala. Wanafunzi wanaweza kutoa hoja kama vile:

*Mazungumzo kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mtazamo mmoja huitwa* ***mjadala***.

- *Washiriki wa mjadala huwa: mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi pamoja na wasikilizaji washiriki.*

- *Baadhi ya sifa za mjadala ni: kuhusisha mazungumzo, kuhusisha mtazamo mmoja, kuhusu mada maalum, mada yenyewe kuhusu jamii n.k.*

Wanafunzi wanaweza kurejelea mjadala waliosoma na kuchunguza iwapo unadhihirisha sifa bainifu za mjadala walizojadiliana. Baadaye, mwalimu aombe kila kundi la wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa na kuwaeleza wenzao matokeo ya majadiliano yao. Katika hatua hii, mwalimu arekebishe makosa ya kimatamshi pindi yanapotokea.

Katika zoezi la 2, mwalimu awaombe wanafunzi katika makundi yao wasikilize mjadala uliorekodiwa na kujibu maswali yafuatayo:

*a)* *Wajadili sifa za mjadala huo waliousikiliza darasani.*
*b)* *Waeleze mada ya mjadala huo.*
*ch)* *Wajadili hoja zilizotolewa katika mjadala huo.*

Mwalimu azunguke darasani na kutoa maelekezo pale yanapotakiwa ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

## Tathmini

Mwalimu awaulize wanafunzi maswali tofauti tofauti kwa kurejelea sifa bainifu walizojifundisha kuhusu mjadala huku wakirejelea wahusika wanaopatika katika mjadala na majukumu yao katika kuendeleza mazungumzo yao.

## Vipindi 42-44: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kuigiza mjadala husika;
- Kuongoza mjadala husika;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mjadala.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Wanafunzi wenyewe;
- Mjadala uliorekodiwa;
- Michoro na picha za wasemaji, mwenyekiti, katibu na wasikilizaji katika mjadala;

- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 154;
- Chombo cha kunasia sauti na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji ujifunzaji na uangalifu maalum.

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mjadala ulioandaliwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuigiza mjadala waliopewa kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 150-152. Mwalimu aandae somo kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kushiriki katika mjadala kupitia kwa wahusika wote wanaohusika ili mwanafunzi apate picha kamili ya mjadala mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi wakati wa kuigiza mjadala waliopewa katika makundi yao.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kipindi kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie mjadala alioandaa kutanguliza funzo hili.

## 18.4 Kusikiliza na kuzungumza: Maigizo

Sehemu hii inalenga kumwezesha mwanafunzi kushiriki katika mjadala husika kupitia kwa maigizo.

Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi sita sita ili waweze kuigiza mjadala waliosoma kuhusu umuhimu wa uzalendo.

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao ambapo kila kundi litapewa muda wa kuigiza mjadala husika. Kila kundi litateua mwenyekiti, katibu wa mjadala, mtetezi na mpinzani na wanafunzi wengine watakuwa wasikilizaji. Ili kufanikisha maigizo ya wanafunzi katika makundi yao, mwalimu awaongoze waelewe utaratibu unaozingatiwa katika maandalizi na utekelezaji wa mjadala.

Wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa, wapange viti kwa njia inayorahisisha mazungumzo yao halafu mwenyekiti afungue mjadala na aongoze mazungumzo kwa kuzingatia muda uliopendekezwa kwa kila kundi. Wanafunzi wengine wafuate mazungumzo ya wenzao kwa kuandika kasoro na mafanikio yanayojitokeza katika mazungumzo yao. Hivyo basi, kila kundi la wanafunzi lizungumze na mwishoni wenzao wapewe muda wa kutoa mchango wao kuhusu jinsi ambavyo mjadala huo ulivyoendelea. Mwalimu naye achukue muda wake kwa kusahihisha makosa ya wanafunzi pindi yanapotokea na awapongeze pale wanapofanikiwa huku akiomba makundi mengine kuwaiga wenzao na kusahihisha makosa waliyofanya ili wafanye mjadala mzuri zaidi kuliko kundi lililotangulia.

Vilevile, mwalimu asahihishe matamshi ya wanafunzi na achunguze iwapo wanafunzi wanatunga sentensi kamili zisizo na makosa ya kisarufi ili wapate uwezo wa kuwasiliana katika lugha fasaha.

## Tathmini

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kuongoza mijadala, kushiriki katika mijadala pamoja na kutoa hoja kuhusiana na mada yoyote.

## Vipindi 45-47: Sarufi (Uundaji wa vitenzi)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua maana ya kitenzi;
- Kutaja mifano ya vitenzi mbalimbali;
- Kuunda vitenzi kutokana na maneno mengine.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 154;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ambayo itawawezesha wanafunzi kutambua maana ya kitenzi katika lugha ya Kiswahili. Mwalimu anaweza kuandika mifano kadhaa ya vitenzi mbalimbali vya Kiswahili ambavyo atawapa wanafunzi katika makundi yao ili wavijadili.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu maneno mbalimbali ya Kiswahili ambapo miongoni mwa maneno hayo kuna vitenzi. Maneno haya mbalimbali ndiyo hutumika kuunda sentensi katika Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

## 18.5 Maana ya kitenzi pamoja na uundaji wake

Katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wachunguze maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa ni ya aina gani. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kujadiliana katika makundi yao.

Ibainike kuwa, maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa ni vitenzi mbalimbali. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kutambua aina mbalimbali za vitenzi kutokana na waliyofundishwa katika viwango vya hapo awali.

Mwalimu awaongoze wanafunzi kufahamu kuwa:

- *Neno ambalo hueleza kuhusu kinachofanywa, kilichofanywa au kitakachofanywa huitwa **kitenzi**.*

#### *Aina za vitenzi:*

1. ***Vitenzi halisi:** Huchukua viambishi awali na viambishi tamati na hujisimamia vyenyewe. Mifano: anawahudumia, amefukuzwa n.k.*
2. ***Vitenzi visaidizi**: Hutumika pamoja na vitenzi vikuu ili kuwa na maana kamili. Mifano: **alikuwa** akila, **angali** anasoma n.k.*
3. ***Vitenzi vikuu:** Hubeba maana kuu ya katika sentensi na hutumika pamoja na vitenzi visaidizi. Mifano: alikuwa **akiimba**, anaweza **kusoma** n.k.*

4. ***Vitenzi sambamba:*** *Hutumika pamoja katika sentensi moja vikifuatana.*

   *Mifano: sikumwambia apike chakula, nilimwona akiiba n.k*

Hatimaye, wanafunzi waelekezwe kufanya zoezi la 3 katika makundi yao. Baada ya kukamilisha zoezi hili, mwalimu awashirikishe wanafunzi kulisahihisha zoezi hilo kwa pamoja.

Baada ya haya, wanafunzi katika makundi yao washirikishwe kuunda vitenzi kutokana na maneno mengine kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi hivyo kama walivyoelekezwa na mwalimu. Mwalimu azunguke darasani kuwasadia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Baada ya hapa, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutambua kuwa vitenzi vinaweza kuundwa kutokana na maneno kama vile: vivumishi na nomino. Uundaji wa vitenzi huhusisha kuongeza viambishi kwenye mizizi ya maneno husika.

### *Kwa mfano:*

i) Kuunda vitenzi kutokana na vivumishi:

| Kivumishi | Kitenzi |
|---|---|
| -safi | safisha, safishia, safishwa, safika, safishika |
| -fupi | Fupisha, fupika, fupishia, fupishwa |

ii) Kuunda vitenzi kutokana na nomino:

| Nomino | Kitenzi |
|---|---|
| mapenzi | penda |
| eneo | enea |
| mlezi | lea |

Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la 3 ambapo wanahitajika kuunda vitenzi kutokana na maneno waliyopewa kisha watunge sentensi sahihi kwa kutumia vitenzi walivyounda. Wanafunzi wajibu zoezi hilo na mwalimu awaombe wachunguze maelezo muhimu yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi ili wapate kuelewa zaidi kuhusu uundaji wa vitenzi kutokana na maneno mengine. Baada ya wanafunzi kukamilisha zoezi hili, mwalimu awaongoze katika kulisahihisha kwa pamoja huku akiwashirikisha wanafunzi wote kutambua makosa ya wenzao na kuyasahihisha.

## Tathmini

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kubainisha iwapo wanafunzi wamepata uelewa wa kutosha kuhusu uundaji wa vitenzi kutokana na vivumishi na nomino.

## Maelezo muhimu kwa mwalimu

Mazungumzo kati ya watu wengi ambao huzungumzia jambo moja maalumu na huwa na mtazamo mmoja huitwa ***mjadala***.

- Washiriki wa mjadala huwa: *mwenyekiti, katibu, wapinzani, watetezi* pamoja na *wasikilizaji washiriki.*
- Baadhi ya sifa za mjadala ni: *kuwepo kwa mazungumzo, kuhusisha mtazamo mmoja, kuhusu mada maalum, mada yenyewe kuhusu jamii* n.k.

Neno ambalo hueleza kuhusu kinachofanywa, kilichofanywa au kitakachofanywa huitwa ***kitenzi***.

### Aina za vitenzi:

1. ***Vitenzi halisi:*** Huchukua viambishi awali na viambishi tamati na hujisimamia vyenyewe. Mifano: anawahudumia, amefukuzwa n.k.
2. ***Vitenzi visaidizi:*** Hutumika pamoja na vitenzi vikuu ili kuwa na maana kamili. Mifano: ***alikuwa*** akila, ***angali*** anasoma n.k.
3. ***Vitenzi vikuu:*** Hubeba maana kuu ya katika sentensi na hutumika pamoja na vitenzi visaidizi. Mifano: alikuwa ***akiimba***, anaweza ***kusoma*** n.k.
4. ***Vitenzi sambamba:*** Hutumika pamoja katika sentensi moja vikifuatana.

***Mifano:*** *sikumwambia apike chakula, nilimwona akiiba* n.k

Vitenzi vinaweza kuundwa kutokana na mizizi ya vivumishi na nomino.

***Kwa mfano:***

| | | |
|---|---|---|
| i) | **Kivumishi** | **Kitenzi** |
| | nadhifu | nadhifisha, nadhifika n.k. |
| ii) | **Nomino** | **Kitenzi** |
| | eneo | enea, eneza n.k. |

**FAHAMU:** Kitenzi huundwa kutokana na maneno mengine kwa kuongeza viambishi awali au viambishi tamati kwenye mzizi wa neno linaloundwa.

## 18.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha chini katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waunde vitenzi kutokana na vivumishi watakavyoteua kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi hivyo.

**Kwa mfano:** -refu (*kivumishi*) – refusha, refushia, refushwa, refuka (*vitenzi*)

**Matumizi katika sentensi:** *Ukuta wa mji ule unazidi ku**refushwa**.*

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini vitenzi ambavyo wanafunzi wataunda kutokana na vivumishi mbalimbali kisha kuvitungia vitenzi hivyo sentensi sahihi. Sharti sentensi hizi ziwe sahihi kisarufi.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe waunde vitenzi kutokana na nomino watakazoteua kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia vitenzi hivyo.

**Kwa mfano:** ufagio (*nomino*) – fagia (*kitenzi*)

**Matumizi katika sentensi:** *Mama alitumia ufagio ku**fagia** nyumba.*

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mwalimu atathmini vitenzi ambavyo wanafunzi wataunda kutokana na nomino mbalimbali kisha kuvitungia vitenzi hivyo sentensi sahihi. Sharti sentensi hizi ziwe sahihi kisarufi.

## 18.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 152

1. Ni hali au fikira ya mtu kuipenda nchi yake kwa dhati.
2. Kupiga kura huhakikisha kuwa nchi inatawaliwa na viongozi waadilifu.
3. Mzalendo huijali nchi yake, huitetea na kuistawisha.
4. Ni wajibu wa raia kuilinda mipaka ya nchi yake, kuripoti wahalifu na washirika wao na kuepukana na vishawishi vya makundi ya kigaidi.
5. Uzalendo ni nguzo ya mshikamano wa kitaifa na umoja wa wananchi.
6. Anaweza kufundishwa wimbo wa taifa, mila na tamaduni, ushirikiano, kula pamoja na kuheshimu wazee.
7. Uchumi kuzorota, miundo msingi kukosekana na ile iliyopo kudhoofika kufanya gharama ya bidhaa muhimu kuwa ghali.
8. Viongozi wana wajibu wa kuleta amani, maendeleo, umoja wa nchi, kukua kwa uchumi na kustawi katika elimu na miundo msingi.
9. Wimbo wa taifa utawafanya kuipenda nchi, kuthamini uhuru wa nchi yao, historia yao na kutetea umoja wa nchi yao.
10. Mwalimu atathmini namna wanafunzi wataimba wimbo wao wa taifa.

### Zoezi la msamiati, ukurasa 152

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati waliopatana nao katika mjadala husika.

**Kwa mfano:**

1. ***mnafahamu -*** mnajua
2. ***umoja -*** hali ya kuwa na muungano au ushirikiano

### Zoezi la 1, ukurasa 153

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati waliopatana nao katika mjadala husika. Pia, atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi na zihusishe msamiati husika.

***Kwa mfano:***

1. ***umeimarika -*** umekuwa thabiti
2. ***ari -*** hamu ya kutaka kufanya jambo bila ya kushindwa
3. ***utu -*** hali ya kuwa na tabia nzuri ya kibinadamu
4. ***bomu -*** silaha ambayo imetengenezwa ili kutoa mlipuko na husababisha uharibifu mkubwa sana
5. ***mshikamano -*** hali ya kuwa na msimamo na ushirikiano katika kutimiza jambo fulani
6. ***uhalifu -*** tendo la kuvunja sheria za jamii
7. ***usalama -*** hali ya kutokuwepo hatari au fujo
8. ***dhahiri shahiri -*** wazi kabisa
9. ***ufisadi -*** utumiaji mbaya wa mali ya chama, shirika au serikali
10. ***miundo msingi -*** mfumo fulani labda wa ujenzi, uchukuzi n.k.

**Matumizi katika sentensi:**

1. Usalama ***umeimarika*** katika nchi yetu.
2. Wanafunzi wengi wana ***ari*** ya kusoma Kiswahili.
3. Wizi wa kimabavu ni ukosefu wa ***utu***.
4. Washambulizi hao walirusha ***bomu*** katika kanisa moja.
5. Wanajamii hii wana ***mshikamano*** wa kuonewa fahari.
6. Vijana wengi wanaotumia dawa za kulevya hujiingiza katika ***uhalifu*** bila kujua.
7. Wanajeshi hawa watashika doria ili kudumisha ***usalama***.
8. Ushahidi ulionyesha ***dhahiri shahiri*** kuwa mwizi huyo alinaswa na kamera za duka.
9. Viongozi wanaoshiriki ***ufisadi*** hawatapigiwa kura tena.
10. Ili kuimarisha ***miundo msingi*** yetu, waziri wa uchukuzi ametuahidi mambo mengi.

**Zoezi la 2, ukurasa 154**

Mwalimu awapange wanafunzi katika makundi yao kisha atayarishe kanda yenye mjadala uliorekodiwa na kuwapa wanafunzi hao fursa ya kusikiliza mjadala. Atathmini hoja za wanafunzi kuhusu maswali yaliyoandikwa vitabuni mwao.

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 154**

Mwalimu awape wanafunzi fursa ya kuigiza mjadala waliousoma. Ahakikishe kuwa wanazingatia ujasiri wa kusimama na kuigiza mbele za wanafunzi wenzao.

**Zoezi la sarufi, ukurasa wa 154**

1. Kitenzi halisi
2. Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu
3. Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu
4. Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu
5. Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu
6. Kitenzi kishirikishi kipungufu
7. Kitenzi kishirikishi kikamilifu
8. Vitenzi sambamba
9. Vitenzi sambamba
10. Vitenzi sambamba

**Zoezi la 3, ukurasa 155**

Mwalimu atathmini sentensi za wanafunzi. Sharti ziwe sahihi na zihusishe vitenzi vikuu na visaidizi.

***Kwa mfano:***

1. Mwalimu ***angali anafundisha***.
2. Mtoto ***alikuwa akiimba*** mama alipofika.
3. Sisi ***tutakuwa tukicheza*** uwanjani.
4. Mgeni ***amekuwa akibisha*** kwa muda mrefu.
5. Birasa ***angali anasafiri***.

**Zoezi la sarufi, ukurasa 155 - 156**

1. fagia
   Mutoni anafagia nyumba.
2. lea, leka, lelea
   Mama amemlea mtoto wa jirani.
3. safisha, safishwa, safishia, safishika
   Mwalimu ameniomba nisafishe ofisi.
4. chora, choreka, chorewa, chorwa, chorea
   Picha niliyochora imetundikwa ukutani.
5. fupisha, fupika, fupishia
   Zoezi la pili ni la kufupisha hotuba tuliyosoma.

**Zoezi la 4, ukurasa 156**

1. erevuka, erevusha
   Mtoto wake ***ameerevuka***.
2. chosha, choshwa
   Kazi ya kupaka ukuta rangi ***imenichosha***.
3. cheza, chezwa, chezea, chezeka
   Mpira wa vikapu ***utachezwa*** kesho.
4. nenepa, nenepesha
   Dawa alizonyweshwa dada yangu ***zimemnenepesha***.
5. fuga, fugwa, fugia, fugika
   Kanga ni ndege ***anayefugika***.

## Somo la 19: Mwongozo wa kuandika mjadala

## Vipindi 48-50: Kusoma ufahamu

### a) Malengo ya somo

- Kusoma kwa usahihi mfano wa mjadala kwa utambuzi wa herufi, silabi na sentensi;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mjadala;
- Kuandika hoja muhimu zilizotolewa katika mjadala.

### b) Vifaa vya kujifunzia

- Mjadala uliorekodiwa,
- Michoro ya mwenyekiti na wasemaji wengine katika mjadala;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 157;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, **wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).**

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu ugonjwa wa Ukimwi. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kufikiria kuhusu changamoto zinazojitokeza kuhusiana na ugojwa huu. Wanafunzi wataweza kujadiliana kuhusu namna ya kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi na jinsi mtu anavyoweza kuupata na asivyoweza kuupata. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kuongoza mjadala na kushiriki katika mijadala mbalimbali kwa kutumia lugha rasmi na sahihi kisarufi.

### d) Utaratibu wa somo

### Utangulizi

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na mjadala walioshiriki. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilopewa

katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi kupata ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

Baadaye, mwalimu awachangamshe wanafunzi kwa kuwauliza maswali kadhaa kuhusiana na michoro iliyo katika *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 157. Kwa mfano: *Mnaona nini kwenye michoro hii?* Wanafunzi wajibu maswali ya mwalimu kwa kueleza kile wanachokiona katika michoro hiyo. Kwa mfano: *"Mimi ninaona muuguzi na mgonjwa hospitalini. Mimi ninaona mwanamke anayemeza dawa. Mimi ninaona daktari na mgonjwa aliye kitandani* na kadhalika. Katika sehemu hii, mwalimu ahakikishe kuwa wanafunzi wanapata ujuzi kuhusu tafakuri tanduizi, ubunifu na ugunduzi kwa kuwaonyesha michoro hiyo huku akiwataka kufikiria na kugundua kile kinachoendelea katika michoro hiyo. Vilevile, nafasi ya wanawake katika mjadala nayo igusiwe.

## 19.1 Kusoma na kufahamu: Mjadala kuhusu ugonjwa wa Ukimwi

Mwalimu awaombe wanafunzi wasome kwa kimya mjadala uliopo huku wakiandika msamiati mpya wanaopatana nao. Wanafunzi nao wasome kwa kimya huku wakiandika msamiati huo mpya. Hatimaye, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mjadala waliosoma ili kuhakikisha kuwa wameusoma na kuuelewa. Kwa mfano, anaweza kuuliza swali lifuatalo: *Taja njia za kuambukiza ugonjwa wa Ukimwi*. Wanafunzi, kwa upande wao, wajibu maswali ya mwalimu kulingana na yale waliyoyasoma katika mjadala huo. Kwa mfano: *Baadhi ya njia za kuambukiza ugonjwa wa Ukimwi ni kupitia kwa kushiriki ngono ovyo bila kinga na mtu aliye na virusi vya Ukimwi, kupitia kwa mama mwenye virusi hivi kwa mtoto wake wakati wa kunyonyesha, kutumia vifaa vyenye makali na mtu mwenye virusi vya Ukimwi* miongoni mwa nyingine. Mwalimu ahakikishe kwamba wanafunzi wote wanashirikishwa katika shughuli hii.

Baadaye, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuyajibu maswali ya ufahamu waliyopewa ambayo yatasahihishwa kwa pamoja darasani. Mwalimu awaelekeze wanafunzi wanaopata matatizo katika makundi yao.

## Tathmini

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali mbalimbali kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha kutokana na mjadala waliousoma.

## Vipindi 51-53: Kujifunza msamiati

### a) Malengo ya somo

- Kubaini msamiati unaotumika katika mjadala;
- Kutaja majina ya watu wapatikanao katika mjadala;
- Kutumia msamiati wa mjadala katika sentensi sahihi.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Mjadala uliorekodiwa;
- Michoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mjadala;
- Wanafunzi wenyewe;
- Kamusi ya Kiswahili;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 161;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Somo hili linalenga kumpa mwanafunzi ujuzi zaidi kuhusu msamiati unaohusiana na ugonjwa wa Ukimwi na kuendeleza afya nzuri ya wanajamii. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kuelewa maana ya msamiati unaohusiana na sekta ya afya. Ni vyema mwalimu alenge kumsaidia mwanafunzi kupata maarifa ya kuongoza mjadala na kushiriki katika mijadala mbalimbali kwa kutumia lugha rasmi na sahihi kisarufi. Katika maandalizi ya somo lake, mwalimu ahakikishe kwamba ameleta picha au michoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mjadala ili kuwasaidia wanafunzi kuelewa kwa urahisi hasa wanafunzi wenye ulemavu au matatizo mbalimbali.

### d) Utaratibu wa somo

***Utangulizi***

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na mjadala kuhusu umuhimu wa uzalendo na namna ya kuendeleza maisha mazuri ya Wanyarwanda. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilopewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi wapate ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

## 19.2 Ujifunzaji wa msamiati kutokana na mjadala husika

Baadaye, mwalimu awapange wanafunzi katika makundi ya wanafunzi wawili wawili na awaombe watafute maana za msamiati mpya waliopatana nao katika mjadala waliosoma. Ni vyema mwalimu awakumbushe wanafunzi kuchunguza matumizi ya msamiati huo katika mjadala waliosoma na kutumia kamusi pale inapohitajika. Mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wachunguze msamiati uliopigiwa mistari katika sentensi walizopewa katika zoezi la 1. Wanafunzi wafafanue msamiati huo kisha watunge sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia msamiati huo. Ni vyema mwalimu awakumbushe wanafunzi wachunguze matumizi ya maneno hayo katika mjadala waliosoma na watumie kamusi pale inapohitajika ili kukamilisha zoezi hilo. Aidha, mwalimu azunguke darasani ili kuwasaidia na kuwaelekeza wanafunzi wanaotatizika. Katika kufanikisha uelewa wa wanafunzi katika zoezi hili, mwalimu awaombe walisahihishe kwa pamoja huku akihakikisha kwamba utunzi wa sentensi zao umezingatia amani na maadili, usawa wa kijinsia, elimu ya pamoja, elimu kuhusu fedha; mazingira, mabadiliko ya hali ya hewa na mwendelezo na utamaduni wa kiusanifishaji.

## Tathmini

Katika hatua hii ya tathmini, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea msamiati mahususi waliojifunza kutokana na mjadala waliosoma huku wakirejelea wahusika wanaopatikana katika mazungumzo ya aina ya mjadala na majukumu yao katika kuendeleza mazungumzo hayo.

# Vipindi 54-56: Matumizi ya lugha

## a) Malengo ya somo

- Kujadili mwongozo wa kutunga mjadala;
- Kutaja majina ya watu wapatikanao katika mjadala;
- Kutambua msamiati unaohusiana na mjadala.

## b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- Chati yenye kuonyesha mwongozo wa kutunga mjadala;
- Michoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mjadala;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 161;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

## ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi zaidi kuhusu mwongozo wa kutunga mjadala kwa kurejelea mjadala waliousoma kuhusu ugonjwa wa Ukimwi. Mbali na kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni muhimu katika uwanja huu, somo hili litasaidia pia kumwezesha mwanafunzi kutunga mjadala kwa kuzingatia mwongozo sahihi na kamili.

## d) Utaratibu wa somo

### *Utangulizi*

Mwalimu awaamkie wanafunzi na awaulize maswali kuhusu somo lililopita kuhusiana na msamiati wa mjadala. Wanafunzi wajibu maamkizi na maswali ya mwalimu. Mwalimu awashirikishe wanafunzi kusahihisha zoezi walilolipewa katika somo lililopita na awaelekeze wanafunzi wapate ufahamu wa mambo yaliyoonekana kuwatatiza.

## 19.3 Matumizi ya lugha: Majadiliano

Mwalimu azingatie kwamba katika hatua hii ya matumizi ya lugha ndipo anatakiwa kuwaelekeza wanafunzi kupata ujuzi unaotakikana kuhusu mwongozo wa kutunga mjadala. Hivyo basi, mwalimu awaelekeze wanafunzi kuchunguza maelekezo yaliyotolewa katika sehemu hii ili waweze kugundua namna ya kutunga mjadala kwa kuzingatia taratibu zifaazo. Wanafunzi wajadiliane katika makundi yao naye mwalimu azunguke kuwasaidia wanaotatizika katika makundi yao. Baadhi ya taratibu za kuzingatia katika utungaji wa mjadala ni:

1. *Kuwepo kwa mada ya kuzungumziwa.*
2. *Kuwepo kwa upande mmoja. Aidha upande wa utetezi au upande wa upinzani.*
3. *Mazungumzo yashamiri.*
4. *Hoja zihusishwe.*
5. *Kuwepo kwa wahusika kama vile: mwenyekiti, katibu na wazungumzaji .*

Baadaye, kila kundi lipewe muda wa kuwasilisha matokeo ya majadiliano yao mbele ya wanafunzi wenzao. Mwalimu ahakikishe kuwa anakosoa makosa ya kimatamshi wakati wa mawasilisho haya. Zoezi hili litawawezesha wanafunzi kupata ujasiri wa kusimama na kuzungumza mbele ya watu pamoja na kuzungumza kwa lugha sahihi na rasmi.

## Tathmini

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali mbalimbali kwa kurejelea taratibu za kutunga mjadala walizowasilisha darasani. Wanafunzi waelekezwe kubaini nafasi ya mwenyekiti na wazungumzaji wengine wakati wa kuendeleza mjadala na hata wabainishe mienendo mizuri inayotakikana katika kujikinga dhidi ya ugonjwa wa Ukimwi na katika mazingira ya mazungumzo ya mjadala.

## Vipindi 57-59: Kusikiliza na kuzungumza

### a) Malengo ya somo

- Kuandaa mjadala kuhusu manufaa ya ulezi bora;
- Kushiriki katika mazungumzo na kutoa hoja mbalimbali katika mjadala;
- Kuandika hoja muhimu zilizotolewa katika mjadala;
- Kueleza majukumu ya wahusika wa mjadala.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Mjadala uliorekodiwa;
- Michoro ya mwenyekiti, katibu na wasemaji wengine katika mjadala;
- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 162;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu ahakikishe amewagawa wanafunzi wake katika makundi ya wanafunzi yanayotakikana. Mjadala ulioandaliwa au uliorekodiwa utumiwe kuongoza wanafunzi na kuwapa mwelekeo kamili wa kuendesha mada ya mjadala waliopewa kwenye *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 157. Mwalimu aandae somo hili kwa namna ya kumwezesha mwanafunzi kupata ujuzi kuhusu utaratibu wa kutunga mjadala kuhusu manufaa ua ulezi bora. Kupitia kwa wahusika wote wanaohusika katika mjadala, wanafunzi wapate picha kamili ya mjadala mzuri na jinsi unavyofanywa.

Mwalimu ahakikishe kwamba ameleta vifaa vinavyohitajika kujifunzia somo hili kama vilivyotajwa hapo juu ili kuwaelekeza ipasavyo wanafunzi katika kutunga mjadala waliopewa katika makundi yao.

### d) Utaratibu wa somo

*Utangulizi*

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu. Mwalimu awaulize maswali mbalimbali kuhusu waliyosoma katika kilichotangulia. Wanafunzi wajibu maswali waliyoulizwa. Mwalimu atumie mijadala aliyoandaa kutanguliza funzo hili.

## 19.4 Kusikiliza na kuzungumza: Kutunga mjadala

Katika hatua hii, ni muhimu mwalimu alenge kumwezesha mwanafunzi kutoa maoni yake kuhusu mada mbalimbali na kuzungumza na wengine kwa kutetea hoja zake ili aweze kuungwa mkono. Kwa hivyo, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi wanne wanne ili waweze kuandaa mjadala kuhusu manufaa ya malezi bora na hapo baadaye kuuwasilisha mbele ya wanafunzi wenzao.

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao ambapo kila kundi litapewa muda wa kujadiliana kuhusu mada waliyopewa na kuandika hoja zao. Kila kundi likumbuke kuteua mwenyekiti na wasemaji wengine.

Ili kufanikisha mazungumzo ya wanafunzi katika makundi yao, ni vyema mwalimu awakumbushe utaratibu wa kutunga mjadala.

Baadaye, mwalimu awaombe wanafunzi wajitokeze mbele ya darasa, wapange viti kwa njia inayorahisisha mazungumzo yao halafu mwenyekiti afungue mjadala na aongoze mazungumzo kwa kuzingatia muda uliopangwa. Wanafunzi wengine wafuate mazungumzo ya wenzao kwa kuandika kasoro na mafanikio yanayojitokeza katika mazungumzo yao ili, baadaye, waweze kutoa mchango wao kwa kuboresha mazungumzo yao katika mijadala mingine.

Mwalimu achunguze jinsi wanafunzi wanavyojadiliana na awaelekeze kutambua kasoro zilizopo huku akisahihisha matamshi ya wanafunzi na kuwasaidia kutunga sentensi kamili kwa kuchochea uwezo wao wa ubunifu na ugunduzi, tafakuri tanduizi na kudumisha uwezo wao wa kuwasiliana katika lugha rasmi.

## Tathmini

Katika sehemu hii, mwalimu awaulize wanafunzi maswali kuhusu mambo muhimu waliyojifunza katika sehemu hii ya kusikiliza na kuzungumza. Maswali yake yachunguze uwezo wa wanafunzi wa kuongoza mijadala, kushiriki katika mijadala pamoja na kutoa hoja za kujenga mada katika mjadala.

## Vipindi 60-62: Sarufi (Maana ya kiwakilishi)

### a) Malengo ya somo

- Kutambua maana ya kiwakilishi;
- Kutaja mifano ya viwakilishi mbalimbali;
- Kuunda viwakilishi.

### b) Vifaa vya kujifunza

- Wanafunzi wenyewe;
- *Kitabu cha Mwanafunzi*, ukurasa 162;
- Chombo cha kunasia sauti, breli pamoja na vifaa vingine vinavyoweza kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji uangalifu maalumu (kwa mfano, wanafunzi wasioweza kuona, kusikia n.k.).

### ch) Maandalizi ya somo

Mwalimu aandae somo hili kwa namna ambayo itawawezesha wanafunzi kutambua maana ya kiwakilishi katika lugha ya Kiswahili. Mwalimu anaweza kuandika mifano kadhaa ya viwakilishi mbalimbali vya Kiswahili ambavyo atawapa wanafunzi katika makundi yao ili wavijadili.

### d) Utaratibu wa somo

#### *Utangulizi*

Mwalimu atangulize sehemu hii kwa kuwaamkia wanafunzi na kuwauliza maswali mbalimbali kuhusu maneno mbalimbali ya Kiswahili ambapo miongoni mwa maneno hayo kuna viwakilishi. Maneno haya mbalimbali ndiyo hutumika

kuunda sentensi katika Kiswahili. Wanafunzi wajibu maamkizi ya mwalimu pamoja na maswali waliyoulizwa.

## 19.5 Sarufi: Maana ya kiwakilishi pamoja na uundaji wake

Katika sehemu hii, mwalimu awaombe wanafunzi wajigawe katika makundi ya wanafunzi watatu watatu kisha wachunguze maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi walizopewa. Mwalimu awaelekeze wanafunzi katika kujadiliana katika makundi yao. Mwalimu awaelekeze wanafunzi kubaini kuwa maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi za kwanza ni nomino na maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi za pili ni viwakilishi vya nomino hizo. Mwalimu awaongoze wanafunzi kufafanua maana ya kiwakilishi. ***Kiwakilishi*** ni neno au kiambishi ambacho hutumika badala ya nomino katika sentensi moja. Wanafunzi wafahamu kuwa nomino na kiwakilishi chake haviwezi kutumika kwa pamoja katika sentensi moja.

Baada ya uelewa huu, mwalimu awashirikishe wanafunzi katika kutunga sentensi sahihi kisarufi kwa kutumia nomino kisha waziandike upya kwa kutumia viwakilishi vyao bila nomino zenyewe.

***Kwa mfano:***

***Sentensi yenye nomino:*** *Shangazi* anapiga nguo pasi.

***Sentensi yenye kiwakilishi:*** *Yeye* anapiga nguo pasi.

Kutokana na sentensi ambazo wanafunzi watatunga, mwalimu awaongoze kufahamu kuwa maneno waliyotumia badala ya nomino ni ***viwakilishi***.

Wanafunzi waelekezwe kutambua aina mbalimbali za viwakilishi, kama vile:

1. Viwakilishi vya sifa. Mifano: *-zuri, -ekundu, -baya, -refu* n.k.
2. Viwakilishi vionyeshi/viashiria. Mifano: *huyu, huyo, hiki, lile, hapo* n.k.
3. Viwakilishi vimilikishi. Mifano: *wangu, chako, lake, petu, zako* n.k.
4. Viwakilishi vya idadi. Mifano: *wawili, vichache, kumi, wengi* n.k.
5. Viwakilishi viulizi. Mifano: *gani, ngapi, yupi, upi* n.k.
6. Viwakilishi vya pekee. Mifano: *-enyewe, -enye, -ingine, -ote* n.k.
7. Viwakilishi vya nafsi. Mifano: *yeye, mimi, sisi, wao, wewe, nyinyi* n.k.

Baada ya haya, wanafunzi katika makundi yao washirikishwe kuunda viwakilishi kutokana na maneno mengine. Zoezi hili ni gumu kufanyika kwa sababu viwakilishi haviwezi kuundwa kwa kuambishwa kama inavyofanyika kwa maneno mengine ila vivumishi hutumika moja kwa moja katika sentensi kama viwakilishi.

***Kwa mfano:***

1. *Mama mrembo anatembea barabarani.* (Katika sentensi hii, neno '*mrembo'* ni kivumishi cha sifa kwa sababu linaeleza zaidi kuhusu nomino '*mama'*).
2. *Mrembo anatembea barabarani.* (Katika sentensi hii, neno '*mrembo'* ni kiwakilishi kwa sababu limetumika badala ya nomino '*mama'*).

Mwalimu azunguke darasani kuwasadia wanafunzi wanaotatizika katika makundi yao kuhusiana na matumizi ya viwakilishi katika sentensi.

Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya zoezi la 4 ambapo wanahitajika kutumia viwakilishi sahihi badala ya nomino husika katika sentensi walizopewa. Wanafunzi wajibu zoezi hilo na mwalimu awaombe wachunguze maelezo muhimu yaliyotolewa katika kitabu cha mwanafunzi ili wapate kuelewa zaidi kuhusu viwakilishi.

Baada ya wanafunzi kukamilisha zoezi hili, mwalimu awaongoze katika kulisahihisha kwa pamoja huku akiwashirikisha wanafunzi wote kutambua makosa ya wenzao na kuyasahihisha.

## Tathmini

Mwalimu ahitimishe somo kwa kuwauliza wanafunzi maswali tofauti kuhusu mambo muhimu waliyojifundisha. Maswali haya yatilie mkazo uwezo wa wanafunzi wa kubainisha iwapo wanafunzi wamepata uelewa wa kutosha kuhusu maana na matumizi ya viwakilishi.

**Maelezo muhimu kwa mwalimu**

- Neno au kiambishi ambacho hutumika badala ya nomino katika sentensi huitwa ***kiwakilishi***.

***Aina za viwakilishi:***

1. Viwakilishi vya nafsi. Mfano: *Mimi ninasoma kwa bidii.*
2. Viwakilishi vya ngeli. Mfano: *Kinasomwa na wanafunzi shuleni.*
3. Viwakilishi vya sifa. Mfano: *Mrembo anaimba vizuri sana.*
4. Viwakilishi vimilikishi. Mfano: *Langu limeuzwa kwa bei rahisi.*
5. Viwakilishi viulizi. Mfano: *Wangapi wamefika kwenye mkutano?*
   - Vivumishi vinaweza kutumika kama viwakilishi moja kwa moja katika umbo lao bila kuongeza viambishi awali au viambishi tamati.

***Kwa mfano:***

***Sentensi yenye kivumishi:*** Mtoto *mkorofi* amefukuzwa shuleni.

***Sentensi yenye kiwakilishi:*** *Mkorofi* amefukuzwa shuleni.

## 19.6 Mazoezi ya ziada

### i) Zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atoe zoezi la ziada lifuatalo ambalo linalenga kuinua kiwango cha chini kwa wanafunzi kwa kuwaomba watunge sentensi sahihi kisarufi zenye viwakilishi vyovyote.

**Kwa mfano:** *Ambavyo* vilinunuliwa vimevunjika.

#### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi dhaifu

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe viwakilishi vyovyote.

### ii) Zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Kwa wanafunzi wenye kiwango cha juu cha uelewa katika ujifunzaji wao, mwalimu awaombe watunge sentensi zilizo na vivumishi kisha waziandike sentensi hizo upya wakitumia vivumishi hivyo kama viwakilishi.

***Kwa mfano:***

***Sentensi yenye kivumishi:*** Maji *machafu* yamemwagwa nje ya nyumba.

***Sentensi yenye kiwakilishi:*** *Machafu* yamemwagwa nje ya nyumba.

### Majibu, zoezi la ziada kwa wanafunzi wenye uelewa wa haraka

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi na zihusishe vivumishi na viwakilishi kama walivyoagizwa.

## 19.7 MAJIBU

### Maswali ya ufahamu, ukurasa 160

1. Upungufu wa kinga mwilini.
2. Virusi vya ukimwi
3. Kushiriki ngono na mtu aliye na virusi vya Ukimwi, matumizi ya vifaa vyenye makali pamoja na mtu mwenye virusi vya Ukimwi, kupokea damu wakati wa matibabu na damu hiyo iwe iliyoambukizwa Ukimwi, kupitia kwa mama mwenye virusi kumnyonyesha mwanawe mchanga n.k.
4. Hauna tiba.
5. Kutoshiriki ngono kiholela, kutotumia vifaa vya makali pamoja wakati wa kutahiri au kukata kucha na mwanamke mjamzito kuhakikisha kuwa amepimwa ndiposa ajue hali yake na namna atakavyomnyonyesha mwanawe iwapo ana virusi vya Ukimwi.
6. Kudhoofisha kinga mwilini, mtu kukonda, kukosa nguvu mwilini, kukohoa sana na wengine hupata vipele mwilini.
7. Kwa kuwa kinga ya mwili huwa imepungua na kudhoofika.
8. Ugonjwa wa Ukimwi hutupora wafanyakazi wengi wenye elimu na ujuzi na kuirejesha jamii nyuma kimaendeleo na pia huongeza idadi ya mayatima na wajane.

9. Asife moyo kwa sababu kuna tembe za kupunguza makali ya virusi vya Ukimwi, ale lishe bora yenye matunda na mboga kwa wingi na awe na utulivu wa kiakili ili apate nafuu ya kumsogeza mbele kimaisha.
10. Mwalimu atathmini maoni ya wanafunzi.

**Zoezi la msamiati, ukurasa 161**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati waliopatana nao katika mjadala husika.

***Kwa mfano:***

1. ***tiba -*** kitu cha kuponya magonjwa
2. ***kuambukizwa -*** kupatwa na ugonjwa

**Zoezi la 1, ukurasa 161**

Mwalimu atathmini maelezo ya wanafunzi kuhusu msamiati uliopigiwa mistari. Pia atathmini sentensi za wanafunzi.

***Kwa mfano:***

1. ***hadhi -*** nafasi ya heshima anayopewa mtu katika jamii
2. ***silabi -*** tamko katika neno
3. ***kipindupindu -*** maradhi ya kuharisha na kutapika yanayosababishwa na uchafu
4. ***ukambi -*** ugonjwa wa vipele vidogovidogo wenye mwasho na unaosababisha mgonjwa kutoka na machozi na kamasi
5. ***kiholela -*** ovyoovyo
6. ***mwathiriwa -*** mtu anayepatwa na jambo linalomsababishia madhara au magonjwa
7. ***mayatima -*** watoto waliofiwa na wazazi wao
8. ***wajane -*** wanawake au wanaume waliofiwa na wake au waume wao
9. ***virusi -*** viini vinavyosababisha magonjwa
10. ***vipele -*** vivimbe vidogovidogo vilivyoenea mwilini

**Matumizi katika sentensi:**

1. Watu wa ***hadhi*** ya juu huheshimiwa sana.
2. Mwalimu ametuambia tuandike maneno manne yenye ***silabi*** mbili mbili.
3. Wagonjwa wa ***kipindupindu*** wamelazwa kwenye wodi moja.
4. Nilipokuwa mchanga niliugua ***ukambi***.
5. Msichana huyu amekuwa akishiriki ngono ***kiholela***.
6. ***Mwathiriwa*** wa ajali mbaya ya barabarani amepelekwa hospitalini.
7. ***Mayatima*** wengi huhitaji wafadhili wa masomo yao.
8. Mhubiri aliwaombea ***wajane*** wote.
9. ***Virusi*** vinavyosababisha Ukimwi havisikii dawa.
10. ***Vipele*** vilivyo mwilini mwangu vinasababisha mwasho.

**Zoezi la kusikiliza na kuzungumza, ukurasa 162**

Mwalimu atathmini hoja za mijadala ya wanafunzi kuhusu malezi bora. Sharti wazingatie muundo halisi wa mjadala.

**Zoezi la 3, ukurasa 162**

Mwalimu atathmini uigizaji wa wanafunzi. Ahakikishe kuwa wanazingatia ujasiri wakati wa kuigiza mjadala waliousoma pamoja na matumizi ya lugha rasmi na sahihi.

**Zoezi la 4, ukurasa 163-164**

1. ***Ki***lichoraruka kimeshonwa tena.
2. ***Ambaye*** alikuwa akilia amenyamaza.
3. ***Zote*** zimefuliwa zikawa safi na kuanikwa.
4. ***Mangapi*** yameagizwa kutoka ng'ambo?
5. ***Yake*** yamemwagika sakafuni.

**Zoezi la 5, ukurasa 165**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga. Sharti ziwe sahihi kisarufi.

***Kwa mfano:***

1. ***Mwekundu*** utatumika kushona nguo yangu.
2. ***Ndefu*** imekatika.
3. ***Safi*** yatanywewa na wageni.
4. ***Vyeusi*** vimepigwa rangi.
5. ***Vikali*** vitakata mboga.

**Majibu ya tathmini ya mada 4**

**Zoezi la 1, ukurasa 165**

1. Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi. Wanaweza kutaja majina ya: *miji, siku, miezi, watu, mito, milima, maziwa* n.k.
2.
   a) Nomino dhahania
   b) Nomino ya wingi
   ch) Nomino ya wingi
   d) Nomino ya kawaida
   e) Nomino ya pekee

**Zoezi la 2, ukurasa 165**

1. Mwalimu atathmini midahalo ambayo wanafunzi watatunga. Sharti ihusu usalama nchini.
2.
   a) mitamu
   b) vipi
   ch) kubwa
   d) hiki
   e) mzee

**Zoezi la 3, ukurasa 166**

1.

a) ***Vitenzi halisi:*** hivi huchukua viambishi awali na tamati. Kwa mfano: *ninatembea*.

b) ***Vitenzi visaidizi:*** hutumika pamoja na vitenzi vikuu. Hivi hubeba viambishi vya nafsi na wakati. Kwa mfano: *bidi, pasa, ngali, kwisha* n.k

ch) ***Vitenzi vikuu:*** hutumika pamoja na vitenzi visaidizi. Hubeba maana au wazo kuu linalowasilishwa. Kwa mfano: *Mtoto angali analala*.

d) ***Vitenzi vishirikishi vipungufu:*** huwa ni viambishi viwakilishi vya nafsi na ngeli vinapotumiwa kwa uamilifu wa vitenzi. Kwa mfano: *ni, si, ki, yu, m* n.k.

e) ***Vitenzi vishirikishi vikamilifu:*** hivi huweza kuwa vitenzi visaidizi vikitumiwa peke yake bila vitenzi vikuu. Mifano: *ndiye, ndiwi, ndisi, ndicho* n.k.

f) ***Vitenzi sambamba:*** ni vitenzi vya hadhi sawa vikitumika pamoja kwa kuwa ubavu kwa ubavu katika sentensi. Kwa mfano: *Mama anaimba akipika.*

2.

a) Kiwakilishi, kitenzi, kielezi

b) Nomino, kitenzi, nomino, kivumishi

ch) Nomino, kivumishi, kitenzi, nomino, kivumishi

**Zoezi la 4, ukurasa 166**

Mwalimu atathmini mdahalo na mjadala ambao wanafunzi wataandaa na kuuwasilisha mbele ya wanafunzi wenzao.

**Zoezi la 5, ukurasa 166**

Mwalimu atathmini sentensi ambazo wanafunzi watatunga kwa kutumia vivumishi visisitizi.

Kwa mfano:

1. *Kiti hiki hiki ndicho kitakachouzwa kesho.*
2. *Mbwa huyu huyu ndiye aliyebweka jana usiku.*
3. *Nguo hii hii ndiyo itakayofuliwa na mama.*

**Zoezi la 6, ukurasa 166**

Mwalimu atathmini majibu ya wanafunzi pamoja na sentensi ambazo watatunga kwa kutumia vitenzi watakavyotunga.

**Kwa mfano:**

1. *Mama amesafisha chumba cha wageni.*
2. *Mwanafunzi amejinadhifisha na anapendeza.*
3. *Mwalimu alimwerevusha mwanafunzi yule.*
4. *Mtoto amechafua nguo zake mpya.*
5. *Fundi wa nguo alifupisha rinda la dada yangu.*

## Vitabu vya Rejea


BAKITA (2015); *Kamusi Kuu ya Kiswahili*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Mbaabu I. (1992); *Sarufi ya Kiswahili*; Longman; Nairobi, Kenya.

Mdee J.S. , Njogu K., na Shafi A. (2011) *Kamusi ya Kiswahili ya Karne ya 21*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Ntawiyanga S. na Kinya J. (2015); *Kiswahili kwa Shule za Rwanda, Kidato cha 2*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Said A. Mohammed (1980); Riwaya ya *Utengano*; Longhorn; Kenya.

Timothy M. Arege (2009); Tamthilia ya *Kijiba cha Moyo*; Longhorn; Kenya.

TUKI (2009); *Stadi za Lugha ya Kiswahili*; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.

Waihiga G. na Wamitila K. W. (2013); *Chemchemi za Kiswahili, kidato cha 3*; Longhorn Kenya Ltd; Nairobi, Kenya.

Waihiga G. na Kagwa F. M. (2003); *Darubini ya Kiswahili*; Phoenix Publishers; Nairobi, Kenya.

Walibora K. (2002); Riwaya ya *Siku Njema*. Longhorn; Kenya.